ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Dole
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mpendae
30.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
31.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
34.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
35. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
36.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake

37. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
38.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
44.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
45.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
46.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
47.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
48.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
49.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
50.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
51.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
53.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
54.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini

59.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

61.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

62.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

66.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

67.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

68.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

70.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

71.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

72.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 17 Aprili, 2013

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwa heshima kubwa naomba kuweka mezani Hotuba ya Kuwasilisha Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kiliimo ya mwaka 2011/2012 naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (Kny. Kilimo na Maliasili): Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya mwaka 2011/2012, naomba kuwasilisha.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Fedha, Biashana na Kilimo ya mwaka 2011/2012, naomba kuwasilisha.

Mhe. Salmin Awadh Salmin (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Mhe. Spika, ruhusa yako naomba kuweka hati mezani Hotuba ya Muhtasari wa Ripoti ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 40

Kuhusu Bendera ya Zanzibar

Mhe. Salim Abdalla Hamad - Aliuliza:

Kwa kufuata na kutekeleza kifungu cha 3(2) ukurasa wa 1 wa Katiba ya Zanzibar ya 1984, Serikali ya Mapinduzi imekuwa na Bendera yake kama kielelezo cha serikali.

(a) Je, ile Bendera ndogo ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliyoko juu pembeni inamaanisha kitu gani.

(b) Kuna ulazima gani wa kuweko kwa Bendera ile ya Muungano kwenye Bendera ya Zanzibar.

(c) Kungelikuwa na athari/mapungufu gani kama Bendera ile ya Zanzibar ingekuwa inapepea katika Taasisi zote za Muungano

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 40 lenye sehemu (a), (b) na (c) kwanza naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mhe. Spika, Kifungu Nam. 3(2) cha Katiba ya Zanzíbar ya mwaka 1984 kinaeleza kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzíbar itakuwa na uwezo wa kuweka kitu chochote kitachokuwa kielelezo cha Serikali kama itakavyokubaliwa na Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi. Kwa kuzingatia kifungu hiki, Serikali ilifanya maamuzi ya kuwa na bendera yake ambayo itakuwa ni kielelezo cha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na itatumika katika shughuli mbali mbali.

Serikali ilipokwishafanya maamuzi hayo iliitisha zabuni za kampuni na watu binafsi walijitokeza katika kutengeneza bendera na serikali iliichagua aina ya bendera tulionayo sasa na bendera hiyo ilipitishwa na Baraza la Wawakilishi kwa kauli moja kuwa ndio kielelezo cha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzíbar. Hivyo, kuanzia mwaka 2004 Serikali ya Mapinduzi Zanzíbar alianza kupeperusha bendera na kuitumia bendera yake hiyo.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mheshimiwa kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kuwepo kwa Bendera ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pembeni mwa Bendera ya Zanzíbar ni kumaanisha kwamba Zanzíbar ni miongoni mwa nchi mbili zilizoungana na kuunda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(b) Mhe. Spika, kama nilivyokwishaeleza hapo awali kwamba serikali iliitisha zabuni kwa makampuni na watu binafsi kubuni bendera ambayo itakuwa kielelezo cha Serikali ya Mapinduzi ya Zanziabr na aina tofuati za bendera zilibuniwa. Serikali iliichagua aina ya bendera tuliyonayo sasa na bendera hiyo ilipitishwa na Baraza la Wawakilishi kwa kauli moja kuwa ndio kielelezo cha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzíbar.

(c) Mhe. Spika, Sheria iliopo ya Bendera ya Zanzibar ya mwaka 2004 kifungu cha 5 cha Kanuni yake imeeleza kwa uwazi maeneo ambayo bendera hiyo inatakiwa kupepea.

Hivyo Mhe. Spika, kwa faida ya Wajumbe naomba waipitie Kanuni hiyo ili waelewe maeneo husika yanayoruhusiwa kupepea kwa Bendera ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kwanza kwa majibu mazuri niliyoyapata kutoka kwa Mhe. Waziri nampongeza na la pili nashukuru swali langu limejibiwa vilivyo.

Mhe. Spika, mimi kwa suala hili nina swali moja la nyongeza. Kwanza ni kuwa Katiba ya Zanzibar iliundwa mwaka 1984, na Katiba hii imefanyiwa mabadiliko kadhaa na tokea kuundwa kwake kipengele hiki cha kuwa Zanzibar inaweza kuweka kitu chochote kuwa ni kielelezo cha serikali yake kiko. Lakini Mhe. Spika, ilipopitishwa sheria hii na Baraza la Wawakilishi na ikapatikana bendera hii tuliyonayo ambayo nimeulizia swali ni kuwa wakati ule Katiba ya

Zanzibar ilikuwa ikieleza kuwa, Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano na Katiba ya Jamhuri ya Muungano inaeleza mpaka leo kuwa Tanzania ni nchi moja na ni Jamhuri ya Muungano, ndio ukaona hata taasisi nyengine ambazo ni za Muungano wanakuwa na bendera yao na kibendera kidogo cha Muungano.

Lakini hivi sasa tuna katiba yetu ambayo imefanyiwa marekebisho na inasema Zanziba ni nchi na ina mipaka yake na kadhalika, na kwenye Muungano badala ya kusema ni sehemu imesema ni moja kati ya nchi mbili zilizofanya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa mabadiliko haya nakuipa hadhi nchi hii, hatuoni kuwa na sisi ni lazima tutoke kutoka kule Katiba ilivyoeleza kuwa Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano na hivi sasa kuwa Zanzibar ni nchi kamili na madaraka yake na kila kitu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, ni kweli kama ipo sheria inaendana na kinyume cha katiba basi sheria hiyo inapaswa kubadilishwa ili iendane na katiba. Lakini kwa bahati nzuri sheria iliyopo ya bendera Mhe. Spika, inakwenda sambamba na katiba iliyopo sasa, juu ya mabadiliko yaliyofanyika bado sheria hii ya bendera haigongani na katiba iliyopo sasa.

Kama nilivyosema kwamba katiba yetu inaeleza wazi kwamba Zanzibar ni miongoni mwa nchi mbili zilizounda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hivyo, kwa vyovyote vile Zanzibar ina haki yake ndani ya Jamnhuri ya Muungano wa Tanzania. Hivyo sisi ni wabia kwenye Muungano ule, tuna haki zetu na ndio maana tunazisimamia tuzipate. Kwa hivyo, kuweka ile Bendera ya Jamhuri ya Muungano bado inaonesha kielelezo kwamba Zanzibar ni miongoni mwa nchi mbili zilizounda jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa Zanzibar ni nchi na kwa kuwa bendera ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ipo na inapepea Zanzibar nzima kuanzia Makunduchi mpaka kufikia Nungwi, na kuanzia Mkoani mpaka kufikia Makangale. Je kuna ulazima gani wa kuweka kijibendera cha Jamhuri pale kwenye Bendera yetu ya Zanzibar. Kwa kufanya hivyo si kuifanya Zanzibar kama taasisi ya jamhuri ya Muungano kama ilivyo Jeshi la Polisi na bendera yake. Hilo la kwanza.

La pili, kwa kuwa Bendera ya Zanzibar ina kijipicha cha Bendera ya Jamhuri ya Muungano pale juu. Je, itakuwa dhambi gani ikiwa Bendera ya Zanzibar nayo ikabandikwa katika Bendera ya Jamhuri ya Muungano nayo ikawa kama ilivyo ya Zanzibar hivi sasa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, ni Baraza hili la Wawakilishi iliyoipitisha sheria ya bendera na ikaiwekea kanuni, na ikaeleza maeneo ya kupepea bendera hiyo. Kwa hivyo, ni uamuzi wa Baraza hili ndio unatekelezwa katika nchi yetu kwa kuona kwamba ulikuwepo umuhimu huo wa kufanya hivyo. *(Makofi)*

Kwa kufanya hivyo Mhe. Spika, huifanyi Zanzibar kuwa ni taasisi ya Muungao, Zanzibar inakuwepo inabaki kama Zanzibar na Zanzibar itaendelea kuwepo na ule ni uamuzi wa pamoja Mhe. Spika, tulioufanya. Kwa hivyo, ningependa tuelewane sana kwenye hili Mhe. Spika, kwamba serikali kupitia katiba hii ndio iliyoamua kuwa na kielelezo na kielelezo kile ndicho

tulichokipitisha sote kwa pamoja. Kwa hivyo, ikifika mahala kuona kwamba kielelezo kile kina kasoro inafaa tukizungumze hapa sio ku-*question* uamuzi ambao tumeshaufanya. Uamuzi ulikuwa halali, sahihi na ile ndio maamuzi yetu kwa pamoja. *(Makofi)*

Sasa Mhe. Spika, ni dhambi gani hili kidogo naomba alirudie.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ikiwa ni lazima Bendera ya Zanzibar ibebe kijinembo kidogo pale cha Bendere ya Jamhuri ya Muungano, itakuwa ni dhambi gani kwa Bendera ya Tanzania vile vile isiwe na kijibendera kidogo cha Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, nimefahamu. Bendera ile imepitishwa na Bunge vile vile limeridhia la Jamhuri ya Muungano na tuna wawakilishi wetu katika Bunge la Jamhuri ya Muungano na ipo na sheria yake, huwezi kujifanyia mambo kiholela. Huwezi Mhe. Mwakilishi ukakaa humu ndani umelala ukaamka tu ukasema tufanye hivi na hivi mambo yana taratibu zake za kisheria.

Kama kuna jambo lolote mnaona linahitaji haya mabadiliko katika Bendera ya Jamhuri ya Muungano basi Mhe. Mwakilishi zungumza na Mbunge wako umwambie kwamba kuna kasoro hii na hii akarekebishe, au wewe lete hoja hapa tutizame Baraza namna gani tunaweza kuifanyia kazi, mambo hayapelekwi kiholelaholela ukaamka nyumbani asubuhi unasema unavyotaka mwenyewe Mheshimiwa. Mambo tulioyapanga lazima tuyaheshimu yana sheria na lazima utaratibu uwepo.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kunipa fursa na mimi nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza. Kwa kuwa Bendera ya Zanzibar imo ndani ya Katiba ya Zanzibar na imeingizwa kisheria, na kwa kuwa siku za nyuma bendera hii ya Zanzibar baada ya kupachuliwa Bendera ya Afro Shirazi ilikuwa hatuna bendera ya Zanzibar baadae ikapitishwa kwenye Baraza la Wawakilishi na ikawa imo kwenye sheria.

Je, kuna sababu zipi za msingi kuwa Rais wetu akienda nje hapeperushi Bendera ya Zanzibar akajulikana kama ni Rais wa Zanzibar. Kama ndivyo hivyo, ni lini hasa serikali itaona kama kuna haja ya Rais wetu wa Zanzibar akienda nje akapeperusha Bendera ya Zanzibar kwa sababu imo kisheria na imo kwenye Katiba ya Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kama nilivyosema nchi inajiwekea utaratibu wake kwa mujibu wa Katiba na Sheria. Sisi Mhe. Spika, tulifanya maamuzi ya kuwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni maamuzi yetu Wazanzibari hayo tumeyafanya wenyewe. Na ile Bendera ya Jamhuri ya Muungano sisi ni *equal partner* ya bendera ile ni bendera yetu na huko nje tumekubaliana kabisa kwamba uwakilishi wetu nje uko chini ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa hivyo, Rais wetu anapokwenda nje ya visiwa vyeti hivi nje ya nchi bendera yake ile ya Jamhuri ya Muungano ni yake pia, ni haki yake hata wewe ni haki yako, hata sisi ni haki yetu, ni yetu huwezi kukataa chako ndio umekiunda, kama hukitaki sasa inabidi utafute utaratibu mwengine wa kukiondoa. Lakini utaratibu wa leo ni chetu pamoja na lazima tuheshimu tuendelee kuwa nao, kama kuna mabadiliko yoyote basi sasa hivi kwenye mchakato huu wa

mabadiliko ya katiba Mhe. Spika, wananchi watatwambia. Lakini hatuwezi kukataa letu, hatuwezi kukataa chetu, ni maamuzi yetu na yeyote anayesema si maamuzi yetu huyo ni muongo.

Nam. 86

Uharibifu wa Mazingira kwa Uchimbaji wa Kifusi

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:

Ujenzi wa majumba makubwa, ongezeko la mabarabara pamoja na upanuzi wa barabara za zamani na ujenzi wa viwanja vya ndege, ni miongoni mwa maendeleo ya nchi. Kwa kuwa miradi mikubwa ya ujenzi niliyoitaja hapo juu hupelekea Makampuni husika kuchimba kifusi, kupasua miamba pamoja na kuchota udongo jambo ambalo linapelekea uharibifu mkubwa wa mazingira, kwani eneo la Vitongoji Makaani kampuni kadhaa zimechimba hadi kutoka maji ya chumvi na hatimae ardhi ya maeneo hayo kutofaa tena kwa shughuli za kilimo.

Je, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kiasi gani inazilazimisha Kampuni hizo kuyafukia mashimo yao pamoja na kupanda miti.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais - Alijibu:

Mhe. Spika, kabla ya kujibu swali Nam. 86 la Mhe. Mwakilishi naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Udhibiti wa uvunaji na matumizi ya maliasili zisiozrejesheka zikiwemo mchanga, kifusi, mawe na udongo unasimamiwa na Wizara ya Kilimo na Maliasili kupitia Idara ya Misitu na Maliasili zisizorejesheka. Katika udhibiti huo, taasisi hiyo inatumia Kamati Maalum yenye Wajumbe kutoka taasisi mbali mbali ikiwemo Idara ya Mazingira kwa ajili ya kuidhinisha eneo linalofaa kuchimbwa maliasili hizo. Eneo la uchimbaji linapokubalika, taasisi hiyo hufanya makubaliano na kampuni inayohusika kutaka kuchukua rasilimali hiyo.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilsihi swali lake Nam. 86 kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzíbar kupitia taasisi ya Idara ya Misitu na Maliasili Zisizorejesheka inafunga mikataba na kampuni zinazoruhusika kuchimba maliasili zisizorejesheka na kuzipa masharti yakiwemo ya ufukiaji wa máshimo yaliochimbwa au kupanda miti na pia kina cha uchimbaji huo pia huoneshwa katika mikataba hiyo.

Hata hivyo, naomba nikiri kwamba katika kipindi cha miaka ya nyuma (kabla ya mwaka 2000) udhibiti wa shughuli hizi ulikuwa mdogo na hasa kwa Taasisi za Serikali, ambapo eneo la Vitongoji Makaani alilolielezea Mhe. Mwakilishi lilitumika kuchimba kifusi na kutengenezea kokoto, kwa ajili ya ujenzi wa barabara zikiwemo kama ile ya Mkoani – Chake, Vitongoji.

Katika kuongeza nguvu za udhibiti wa maliasili hizo, hivi sasa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imeshaandaa Kanuni za Matumizi Endelevu ya Maliasili Ziziorejesheka ambazo hivi sasa zipo kwa Mpiga Chapa wa Serikali (*Government Press*). Kanuni hizo pamoja na mambo mengine zitamtaka yeyote anayeomba ruhusa ya kuchimba maliasili isiyorejesheka kuwasilisha mpango wa jinsi gani atalirejesha eneo hilo mara atakapokamilisha kazi ya uchimbaji (*Rehabilitation Plan*).

Ni imani ya ofisi yetu kuwa Kanuni hizo zitasaidia kwa kiwango kikubwa uendelezaji wa máshimo yanayoachwa baada ya kuchimbwa maliasili zisizorejesheka za aina mbali mbali hapa nchini na kurudishia haiba ya maeneo hayo pamoja na kuruhusu wananchi kuendelea na shughuli zao.

Mhe. Saleh Nassor Juma: ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri aliyoyatoa Mhe. Waziri naomba niulize swali dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa kanuni za kudhibiti kwa mali isiyohamishika ndio kwanza iko kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali hivi sasa, na kwa kuwa ardhí ya Vitongoji tayari imeshaathirika na inaendelea kuathirika ardhi ambayo ilikuwa inatumiwa na wakulima wa Vitongoji kwa ajili ya kilimo cha tungule, mahindi, viazi vitamu, nyanya na kadhalika kiasi ambacho uharibifu huu umepunguza kwa kiasi kikubwa hali ya maisha ya kule na kusababisha wananchi kuwa masikini mno.

Je, ni hatua gani za dharura mtakazozichukua hivi sasa kuona kwamba watu wa Vitongoji wananeemeka baada ya madhara ambayo makubwa yameshasababishwa na Wizara hii ya Miundombinu na Mawasiliano pamoja na yale Makampuni yanayojenga barabara. Hilo la kwanza.

Pili, kwa kuwa suala la ujenzi sio linaathiri uhamishaji mali tu zisizohamishika, lakini hata kuathiri barabara ambayo Awamu ya Sita ya uongozi wa Zanzibar iliijenge ile ya Vitongoji/Mkaani Kwareni kule ikawa inateleza kama mgongo wa ngisi na hivi sasa imechafuliwa sana kwa sababu wamei-*over turn* jamaa wa *H Young* na makampuni mengine.
Mhe. Waziri ni hatua gani wizara yako kwa kushirikiana na Wizara ya Mawasiliano itakayowabana hawa kabla hawajahama kutoa fidia fulani ya kulifanyia *rehabilitation* ile barabara yetu pale.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, kwa hivi sasa ofisi yangu kupitia Idara ya Mazingira ikishirikiana na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, vile vile tukishirikiana na kikundi cha uhifadhi wa mazingira kilichopo Vitongoji tumeanza kuchukua hatua za kurekebisha eneo hilo.

Mhe. Mwakilishi kama atatembelea ataona kwa kiasi fulani kuna eneo kubwa limeanza kupandwa miti kwa kasi sana. Kwa hivyo, hatukukaa tu kusubiri kanuni ziweze kuwa tayari kwa sababu hizo zitatusaidia sasa na baadae, lakini tumeanza kuchukua hatua hizo. Na hatua nyengine tunayoifanya vile vile ni kuendelea kuvishajihisha vikundi vingine vya uhifadhi wa mazingira ambavyo kwa bahati nzuri tunavyo vingi kuweza kuvipatia nyezo na utaalamu wa jinsi gani kwa kushirikiana na sisi wenyewe wataalamu wetu, lakini vile vile panapohitajika msaada wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kuweza kulirejeshea eneo lile katika uasilia wake angalau liweze kutumika.

Swali lake la pili ameulizia kwamba, katika shughuli hizo pia barabara ya Vitongoji na Makaani imeweza kuathirika. Mhe. Spika, mimi naomba nikiri kwamba tarifa hii naisikia hapa kwa sasa na naomba nimuahidi kwamba tutashirikiana na wizara inayohusika ya mawasiliano kuweza kuliangalia sasa. Hivi anavyoshauri kwamba aliyehusika katika uharibifu wa barabara hii basi kama kuna hatua ambazo zitaweza kuchukuliwa ili irejeshewe katika uasilia wake na isiwe tumepata hasara iweze kufanyika hivyo.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kunipa fursa nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza. Kwa kuwa maswali anayouliza Mhe. Mwakilishi Mhe. Saleh Nassor yanalingana sana na mazingira ya Micheweni hasa ukizingatia kuwa Micheweni imeharibiwa zaidi kimazingira kuliko sehemu ya Mhe. Saleh. Kwa sababu Micheweni kuna mashimo mengi ya kifusi na bahati mbaya makampuni yanayokuja kiwango wanachowekewa kuchimba yanachimba zaidi mpaka kutoa maji ya baharí. Kwa hivyo, Micheweni imeharibika sana na bahati mbaya makampuni yana mikataba ya kuwa yakishachimba baadae yafukie, lakini makampuni haya yanaonekana hayatekelezi wajibu wao.

Sasa kwa kuwa wizara yako ndio dhamana ya uchafuzi wa mazingira. Je, Mhe. Waziri utachukua juhudi gani kuona makampuni yanayochimba ardhi zetu za Micheweni hasa ukizingatia kuwa Micheweni ina ardhi ndogo mno je, utachukua juhudi gani kuona makampuni haya yanatekeleza wajibu wao wa kufukia baada ya kwishakuchimba.

Kwa sababu barabara ya Micheweni imeharibika kama ya Mhe. Saleh. Je, utachukua juhudi gani ya kuona hii barabara wale wachafuzi wetu wanaoichafua wanairudisha katika hali yake ilivyo, kwa sababu Mhe. Karume alitujengea mgongo wa ngisi, sasa imechafuliwa yote haifai ni lini barabara mutachukua juhudi ya kuirudisha hali yake.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Kwanza wa Rais: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mhe. Mwakilishi ya nyongeza kama ifuatavyo.

Anavyozungumza kwamba nayo Micheweni imeathirika sana katika uchimbaji wa mali asili hizo na nini ofisi yetu itaweza kufanya. Naomba tushirikiane kufanya mambo mawili.

Ofisi yangu kupitia Idara ya Mazingira nitaituma kwenda katika jimbo lako eneo la Micheweni ili ikafanye tathmini kwanza ya maeneo hayo ambayo yameathiriwa sana katika uchimbaji wa raslimali. Inawezekana taarifa wanazo tayari.

Lakini la pili kuandaa mpango wa kuweza kuyarejesha katika hali yake kama ambavyo tunafanya katika maeneo mengine, mfano eneo la Uwandani hapo kunachimbwa matofali. Jitihada kubwa tunaifanya ya kuweza kupanda miti na kurejesha maeneo yale katika hali yake ya asili.

Lakini namuomba sana Mhe. Mwakilishi katika hili atusaidie kama hakuna vikundi ambavyo vinahusika na uhifadhi wa mazingira, basi aweze kuanzisha vikundi hivyo ndani ya eneo lake ili tushirikiane navyo katika kurejesha hali ya kawaida katika maeneo haya ambayo yameathirika.

Na kuhusu barabara ya Micheweni ambayo nayo imeharibika, hili naomba nilifanyie kazi sawa na lile la Vitongoji Makaani kama nilivyoeleza.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kuniona.

Mhe. Spika, napenda kumuuliza Mhe. Waziri kwa kuwa suala la uharibifu wa mazingira limekuwa wananchi wetu bado hawajalielewa na kwa kuwa uchimbaji wa mchanga ovyo hasa karibu na fukwe ndio tatizo kubwa linaloharibu suala la mazingira.

Je, Mhe. Waziri ni hatua zipi wizara yake itazichukua kwa wale ambao wanafanya kwa makusudi uharibifu huo wa mazingira.
Lakini la pili, Mhe. Waziri hebu tueleze tangu tumepitisha sheria hii ya mazingira ni watu wangapi ambao wamechukuliwa hatua ya uchimbaji wa mchanga, ukataji ovyo wa miti na pamoja na ukataji wa miamba. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Kwanza wa Rais: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya
Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:

Ni kweli kwamba kuna baadhi ya wananchi kwa makusudi na sio kutokuelewa wanavunja sheria za mazingira na wanavunja sheria ambazo zipo chini ya Idara ya Misitu na Mali Asili zisizorejesheka kwa kufanya uharibifu wa mazingira.

Nilichoeleza hapa ni kwamba kwa kiasi fulani tunakiri udhaifu ambao tuliokuwepo kama ni mapungufu kwamba usimamizi wa serikali haukuwa mzuri. Sisi kwa upande wetu Idara ya Mazingira ilikuwa na Kanuni hafifu na sheria ambayo haiwezi kuwabana moja kwa moja waharibifu hao wa mazingira na tulikuwa tunategemea moja kwa moja Idara ya Misitu na Mali Asili zilizorejesheka.

Hata hivyo nimeeleza katika jibu langu mama kwamba hivi sasa kutokana na sheria iliopo tumeandaa kanuni ambazo zitawabana zaidi waharibifu hawa wa mazingira ili kwa kushirikiana na Idara ya Misitu na Mali Asili zisizorejesheka ambao na wao wana sheria zao, basi tuweze kwenda vizuri.
Lakini kusimamia sasa utekelezaji wa kanuni hizo na sheria ambazo zitakuwepo.

Kuhusu suali la pili, Mheshimiwa ametaka kujua ni watu wangapi wamekamatwa kwenye uharibifu wa mazingira katika kukata miti, kuchimba mchanga ovyo labda na udongo. Naomba sana taarifa hii nimletee kwa maandishi kwa sababu inahitaji takwimu.

Nam. 95

Uendelezaji wa Dhana ya Utalii kwa Wote

(Mhe. Mjumbe aliyetaka kuuliza swali hili ameliondoa)

Nam. 53

Utengenezaji wa Bidhaa za Mwani

Mhe. Saleh Nassor Juma (Kny: Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza**:**
Kwa kuwa unga wa mwani umepanda bei kutoka shilingi 5,000 hadi shilingi 10,000 kwa kilo tangu kuanza kutumika kutengeneza vyakula na sabuni lakini wakulima wengi hawana mashine za kusaga mwani.

(a) Je, kwa kuwa bei ya unga ni kubwa kuliko bei ya mwani mkavu, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia mashine za kusaga mwani na kukausha wakulima wa zao hilo wakiwemo wa Jambiani.

(b) Kwa kuwa taasisi ya Sayansi za Bahari Zanzibar (IMS) tayari imetoa mafunzo ya kuzalisha sabuni na vyakula kwa kutumia unga wa mwani wakulima wangapi wamenufaika na mafunzo hayo.

(c) Kwa vile sabuni za mwani pia ni tiba ya ngozi na imepata soko kubwa katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Serikali imechukua hatua gani za kuwasaidia wazalishaji wake ili bidhaa zao wazalishe na kuzihifadhi katika ubora unaohitajika.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi - Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake Nam. 53 lenye sehemu (a), (b) na (c) lakini kabla naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika, kwanza naomba kuliambia Baraza lako tukufu kwamba nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba, wakulima wengi wa mwani hawana mashine za kusagia mwani juu ya kuwa bei ya unga wa mwani imepanda kutoka shilingi 5,000 hadi shilingi 10,000 kwa kilo moja.

(a) Mhe. Spika, Serikali kwa mashirikiano na wadau mbali mbali, inaendelea na juhudi za kuwaelimisha wakulima wa mwani njia bora za kuzalisha mwani ulio katika kiwango kizuri cha ubora. Pia kuunda vikundi vitakavyoweza kuvisaidia kwa urahisi kuweza kuingia katika utaratibu wa kusarifu mwani ikiwa ni pamoja na kutengeneza bidhaa mbali mbali.

Aidha, Serikali kwa kushirikiana na Jumuiya ya SERTA (*Social, Economical, Research and Training Association*) inaendeleza utaratibu huo katika vijiji kumi vya mfano. Vijiji hivyo ni:- Jambiani Kibigija, Bwejuu, Paje, Makunduchi Kiongoni na Mtende kwa Wilaya ya Kusini Unguja na vijiji vya Kidoti, Fukuchani, Matemwe na Pwani Mchangani kwa Wilaya ya Kaskazini "A" na kijiji cha Kiwengwa kwa upande wa Wilaya ya Kaskazini "B" kwenye jimbo kubwa la Mhe. Mshimba. Kuongezeka kwa mashine za kusaga mwani nchini utaendana na matumizi ya mwani hapa hapa nchini na kuufanya mwani kuwa na tija zaidi.

(b) Mhe. Spika, jumla ya wakulima wa mwani 17,124 kutoka katika vijiji 52 vya Unguja na Pemba wamenufaika na mafunzo ya kuzalisha sabuni na vyakula kwa kutumia unga wa mwani. Wanajamii wengi waliopatiwa taalum hiyo ni kutoka katika vijiji vingi vya Unguja na Pemba hapa Unguja.

(c) Mhe. Spika, kwa kushirikiana na washiriki wa maendeleo, Serikali inasaidia na kuendeleza juhudi za wazalishaji kwa kuwawezesha kuzalisha bidhaa zenye ubora unaohitajika. Serikali kwa kupitia Jumuiya ya *SERTA* inazifanyia matengenezo mashine zinazotumika kwa kuzalisha sabuni za mwani katika kikundi cha Tusife Moyo cha Kidoti na pamoja na Jumuiya hii inakusudia kutafuta wataalamu watakaotumika kutoa mafunzo zaidi ya matumzi na utunzaji wa bidhaa zilizo katika ubora unaohitajika na wananchi wetu.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri maswali madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa wizara imeshasaidia mashine katika maeneo mbali mbali ya vikundi vya mwani, nilitaka kujua ni mashine ngapi ambavyo wizara vimesaidia. Swali la pili vina thamani ya kiasi gani mashine hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe.Spika, kwa idhini yako naomba kujibu swali la nyongeza la swahiba wangu Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Kwahani kama ifuatavyo:

Ni mashine tatu mpaka sasa tayari zimeshatolewa na wizara yangu kwa vikundi mbali mbali hapa nchini vyenye thamani ya shilingi milioni ishirini.

Mhe. Salma Mussa Bilali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii kwa kumuuliza Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Naibu Waziri kwa kuwa bei ya mwani bado ni tatizo na kwa kuwa akinamama Mkoa wa Kusini Unguja wanatumia gharama kubwa za matayarisho hadi kupatikana huo mwani mkavu ambao hauna bei. Jee, serikali ni lini hasa itawapatia msaada wa vifaa na mashine za kuchukulia mwani huko pwani ili kuwapunguzia gharama na kupata faida hawa wanawake wa Mkoa wa Kusini.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe.Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mhe. Mwakilishi kama hivi ifuatavyo:

Serikali hivi sasa ina mpango madhubuti wa kushirikiana na Wizara ya Biashara ili kuona bei ya mwani inaongezeka na vile vile kwa utaratibu wa kushirikiana na asasi za maendeleo na jumuiya za wahisani wa maendeleo zipo katika hatua za kufanya mchakato wa kuweza kuwapatia wananchi vifaa mbali mbali vya kuzalisha mwani pamoja vile vile na kutengeneza mwani au usarifu wa mwani.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza.

Kwa kuwa hivi karibuni makampuni yanayonunua mwani yalisita kununua mwani Pemba na kusababisha mrundikano mkubwa wa mwani na wananchi kupata dhiki sana, na kwa kuwa suala la ulimaji wa mwani wananchi wetu wamehamasika sana na wanafanya kazi hiyo sana na mwani upo mwingi sana.

Ni lini serikali itaona haja ya kununua mwani ili kuwaondoshea matatizo na hasa ukizingatia haya makampuni kama yanasuasua.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika, serikali haina será ya biashara lakini serikali inajitahidi kushiriki na washirika wa maendeleo ili kutafuta soko zaidi kwa kushirikiana na Wizara ya Biashara ili kutafuta soko zaidi na makampuni zaidi mengi ili uweze kupata bei mwani wetu na wakulima wa mwani waweze kupata moyo jinsi gani serikali yao inavyowatafutia masoko nje ya nchi.

TAARIFA ZA SERIKALI

Ripoti ya Utekelezaji wa Kazi za Kamati ya Mawasiliano Na Ujenzi ya mwaka 2012/2013

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe jana shughuli hii haikuwahi kuwasilishwa na mawaziri pamoja na Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, na tulipanga na imani yangu kwamba Waheshimiwa Wajumbe munaelewa jinsi ya ratiba ya shughuli zetu ilivyotubana na ndio maana leo utakuta kwamba kuna shughuli mbili hizi zimepangwa zimalizike kama itawezekana, lakini nategemea tutazingatia hiyo ili shughuli hii zimalizike ilimuradi kwa namna ambavyo tulielezana ninafikiri tutafikia hivyo.

Hivyo niwaombe Waheshimiwa Wajumbe tujaribu kutumia muda wetu mfupi tulionao lakini shughuli zetu tujitahidi zimalizike, shughuli ambazo zimepangwa kwa mkutano huu na ni shughuli ambazo ni muhimu sana na vyema tukazimaliza kwa sababu ndio shughuli ambazo ni za usimamizi wa chombo hiki juu ya utekelezaji wa shughuli mbali mbali za serikali.

Kwa hivyo kazi iliyobaki ni kazi maalum za usimamizi wa Baraza kama ilivyo wajibu wa Baraza hili katika kuisimamia serikali. Ni vyema basi na ni muhimu kuona kwamba shughuli hizi tunazimaliza kwa muda mfupi lakini tukazimaliza tena kwa ufanisi.

Basi kwa kuwa Waheshimiwa Wajumbe waliokuwa hawakuwahi kuwasilisha ripoti za utekelezaji pamoja na kwamba kuna Wizara ya Fedha, kwa hivyo tumalize shughuli hii Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi na baadae ndio twende kwenye shughuli hiyo ya Kamati ya Fedha, Kilimo na Biashara.

Baada ya maelezo hayo basi naomba sasa nimkaribishe Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Pili wa Rais (Kny: Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati): Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Subhana Wataalla kwa kutujaalia kutuwezesha kutufikisha katika Baraza hili na kutupa hatua ya kusimama na kusema na kufikia yale yote tuliyokusudia kuyafanya kwa siku ya leo na inshaallah atuwezeshe na siku nyingi za mbele zijazo.

Mhe. Spika, vile vile nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha taarifa hii ya utekelezaji kwa upande wa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. Vile vile niwashukuru sana mwenyekiti wa kamati na wajumbe wake pamoja na wajumbe wote wa Baraza hili kwa namna wanavyotumikia na kutuelekeza ili serikali iweze kufanya wajibu wa msingi wa kuwahudumia wananchi.

Mhe. Spika, serikali imeamua kwa makusudi kabisa kuyapatia ufumbuzi matatizo mbali mbali yanayoikabili Wizara hii ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa nia ya kuwahudumia vyema wananchi wetu. Pia serikali imejipanga kuyapatia ufumbuzi masuala ya ardhi, maji, nishati na masuala mengine muhimu ya msingi kwa nchi yetu ili wananchi waishi kwenye hali iliyo bora zaidi.

Hivi sasa miradi mbali mbali imebuniwa ili kuhakikisha utekekelezaji unakuwa mzuri kwa manufaa ya watu wetu.

Mhe. Spika, túnalo tatizo kubwa la migogoro ya ardhi lakini serikali nayo imejipanga kutafutia tatizo hili ili wananchi wetu waepukane na bughdha hiyo na tuwe na mambo ambayo mengine muhimu ya kuyatekeleza badala ya kila wakati kushughulikia migogoro ya ardhi.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa kueleza hoja kama ambazo zilioneshwa na Kamati yetu hii.
Mhe. Spika, nianze na Idara ya Ardhi na Usajili. Agizo la kwanza Mhe. Spika, ilikuwa ni kamati inaishauri wizara ijitahidi katika utatuzi wa baadhi ya changamoto zilizopo ili kuwezesha wafanyakazi katika idara hiyo kufanya kazi zao kwa umakini.

Utekelezaji:
Ili kuwafanya watendaji kuwa makini katika kazi zao, idara imebuni mkakati wa kuwazungusha katika section na vitengo viliomo katika taasisi za ardhi ili kupata uelewa na kupata uzoefu.

Kuhusu kwa kuwa na wimbi kubwa na baadhi ya wananchi kuzigeuka eka zilizotolewa na serikali kwa ajili ya kilimo kuwa maeneo ya makaazi kwa wananchi na kujenga nyumba, kamati imeiagiza idara kusimamia na kudhibiti eka hizo hasa zile ambazo hazijavamiwa na kujengwa kwa makaazi.

Katika kudhibiti matumizi mabaya ya eka, idara inaendelea na mpango wake wa kuzitambua eka zote ziliopo sambamba na hilo na wale waliobainika kuhalifu matumizi ya eka watachukuliwa hatua za kuwanyang'anya ardhi hizo.

Tatu, kamati inashauri idara izidishe juhudi za kutoa elimu ya usajili wa ardhi na inakubaliana na wazo la idara la kuwashirikisha wanasiasa katika utoaji wa elimu hiyo. Katika suala hili la elimu

la usajili wa ardhi, idara kwa kushirikiana na Mrajis wa Ardhi imefanya mikutano na mikutano na vipindi kadhaa vya redio.

Aidha maagizo vipeperushi na vijarida vimetumika katika kufikisha ujumbe wa usajili wa ardhi. Maelezo ya ziada uzinduzi wa ardhi ulifanywa katika sherehe iliyohudhuriwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi hivi karibuni.

Nne, kamati inashauri suala la master plan lizidi kufuatiliwa kwa makini zaidi kuingiza maeneo ya vijijini katika mpango huu. *Master plan* na mpango wa matumizi ya ardhi unaendelea chini ya ufadhili wa *World Bank* na haya maagizo yatawekwa mkazo.

Tano, kamati inazidi kuweka msisitizo kwa idara kuepuka kutoa hati mbili kwa eneo moja na endapo ikitokea kutofahamiana kwa baadhi ya taasisi za serikali na idara au idara na mwananchi, na endapo kuna nafasi ya kukaa na kulipatia ufumbuzi suala hilo ni vyema likatatuliwa kwa makubaliano na kuepusha migororo inayopelekea kufunguliwa kwa kesi katika Mahakama ya Ardhi na kuongeza mrundikano wa kesi. Hatua zilizochukuliwa ili kuepuka utoaji wa hati mbili (*doublé allocation*), idara imebuni mkakati wa kuhakiki maeneo kwa umakini sana. Vile vile wakati wa kusaini hati wananchi wanaohusika huitwa wakati wa kufanyiwa usaini. Hivi sasa Mhe. Spika, ninapenda kuliarifu Baraza lako tukufu kesi za *doublé allocation* zimepungua kwa kiasi kikubwa.

Kuhusu agizo la sita, agizo la kufuatilia na kusaidia mawazo katika taasisi mbali mbali, kamati ilitembelea katika station ya Chake-Chake Pemba. Suala la *stand* ya Chake-Chake linashughulikiwa kwa karibu sana kupitia taasisi zetu za ardhi, mipango miji na vijiji, Afisa Mdhamini anaendelea vyema kulifanyia kazi jambo hili.

Kuhusu Idara ya Ardhi na Upimaji:
Kamati imeiagiza idara inapotangaza kufanya vipimo vya ardhi iharakishe kufanya zoezi hilo ili kuepusha usumbufu wa baadae ambapo kutokana na kuchelewa kwao wananchi wamekuwa wakivamia maeneo hayo.

Hatua za utekelezaji:
Idara imetoa mafunzo kwa wafanyakazi wake juu ya matumizi ya vifaa vya kisasa ili kufanikisha kazi ya upimaji kwa haraka kwa maeneo yanayoamulika kupimwa. Katika kufanikisha suala zima la upimaji kwa wakati idara pia imefanya semina mbili zenye madhumuni hayo Unguja na Pemba.

Wakati wa upimaji kamati imeiagiza idara kufanya mawasiliano ya karibu na wizara nyengine hasa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ili angalau katika maeneo zenye njia zisafishwe kwa *grader* ambapo njia hizo zitakuwa zinatenganishwa na kulinda ramani tunazozifanyia kazi.

Idara imefanya mazungumzo na taasisi nyengine kama Shirika la Umeme, Mamlaka ya Maji, Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano na kadhalika katika kupima maeneo na kushauriana katika kazi zinazohusiana na ramani.

Suala la tatu kamati inashauri idara husika ihakikishe kuwa inaliondoa kabisa la kupima kiwanja kimoja zaidi ya mtu mmoja ili kuepuka usumbufu na kusababisha matatizo makubwa kwa wananchi.

Idara imeziingiza kazi kongwe na mpya katika kompyuta ili kuepuka tatizo hilo na sasa tutahakikisha kwamba kiwanja kimoja kinatolewa kwa mtu mmoja na mfumo wa kutumia kompyuta unaingiza kumbukumbu za kupima taarifa nyengine za ardhi.

Kuhusu kamati kwa Kisiwa cha Pemba inaishauri idara kufanya mazungumzo na Wizara ya Kilimo ili kufuatilia suala lililokuwepo la tatizo la Tumbe ambapo limesababisha mgogoro mkubwa kati ya wizara hizi na kupelekea wananchi kulivamia eneo hilo.

Idara kupitia wizara tayari imefanya mazungumza na Wizara ya Kilimo na mafanikio yamepatikana na kubadilishana maeneo ili kufanikisha upimaji wa viwanja Tumbe.

Tano, kamati inaiagiza idara kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi kwa Wakuu wa Mikoa ambao baadhi yao huchukua jukumu la idara na kusababisha migogoro kati ya idara na wananchi. Idara imepanga mipango mikakati wa mawasiliano ili kutoa elimu kwa umma ili wananchi wote waweze kuelewa kwa kina utaratibu mzima na umuhimu wa sheria za ardhi.

Kamati inaiagiza idara iendelee na juhudi za kuwadhibiti baadhi ya watendaji wa idara ambao hutumia vifaa kupima baadhi ya maeneo na baadae kusababisha migogoro. Idara imeandaa utaratibu maalum wa kudhibiti vifaa vya upimaji. Kwa sasa kuna mfanyakazi maalum wa dhamana wa kuvihifadhi vifaa hivyo na endapo vifaa hivyo vitatumika kinyume na matakwa mfanyakazi huyo ndiye anayewajihishwe.

Aidha matumizi ya sare maalum kwa wafanyakazi wa upimaji yamekubalika ili kutofautisha wafanyakazi wetu na watu wanaofanya kazi hiyo kinyume na utaratibu.

Pia kamati imeiagiza idara itekeleze majukumu yake kwa mujibu wa sheria ili kuepuka matatizo yanayoweza kujitokeza na kusababisha migogoro na kesi zisizokuwa za ulazima. Idara imeipitia sheria na kanuni za upimaji na imependekeza wafanyakazi saba kuweza kukutana kwa ajili ya kuandaa taratibu za kazi za upimaji ili kuleta ufanisi wa kazi za kila siku na hatimaye kuleta mafanikio ya ardhi.

Maelezo ya ziada utaratibu wote unaokusudiwa kuletwa katika Serikali za Mitaa kwa ajili ya kukabili matatizo ya ardhi.

Kuhusu Idara ya Mipango Miji:
Kamati imeguswa na changamoto zote zinazoikabili idara na kuishauri wizara kufanya juhudi ya kuajiri angalau wataalamu sita wa fani zinazokwenda sambamba na matakwa ya idara ili kupunguza tatizo la wataalamu. Pia inashauri wizara kufikisha kilio cha maslahi ya wataalamu hao angalau wale wataalamu waliopo sasa na wenye nia ya kutaka kufanya kazi nchini wasikimbie nchi za wenzetu ambazo hupata maslahi makubwa zaidi.

Idara kupitia nafasi kumi za ajira iliyopatiwa kwa mwaka huu imeipatia nafasi mbili Idara ya Mipango Miji ili kuajiri watalamu wa fani ya mipango na usanifu wa majengo na hadi sasa usaili wa nafasi hizo umeshafanyika. Aidha wataalamu wa fani za ardhi sasa wanatambulika kama ni wataalamu adimu rare profesional, hivyo serikali inawapa kipa umbele na unawapa upendeleo maalum katika mishahara yao.

Kamati inasisitiza idara kusimamia ramani zake kwa kuhakikisha inafuatilia maeneo yote waliyopima na kuhakikisha kuwa maeneo mapya ambayo yanapimwa viwanja, njia zilizowekwa zinabakia kama ilivyo.

Idara inaongeza jitihada ya kufanya ukaguzi kwa kuhakikisha kwamba wananchi hawajengi katika maeneo ya wazi na njia. Kwa kufanikisha hilo idara inashirikiana na mikoa kutayarisha mpango ya kudhibiti wa ujenzi holela wa Mkoa wa Mjini/Magharibi pamoja na kushirikiana na Halmashauri kwa maeneo mengine.

Mhe. Spika, Kamati inaishauri idara kuharakisha kupima miji mipya ambayo haijapimwa na kuhakikisha kwamba maeneo mengine yanapimwa. Idara inafanya kazi ya agizo hilo, hivi sasa idara inatayarisha ramani za miji miwili mikubwa, Mji wa Zanzibar na Mji wa Chake Chake na vijiji vya Nungwi na Mgelema, idara itaendelea na hatua hii na kuhakikisha miji yote na vijiji vyote vinapimwa ramani za matumizi ya ardhi.

Kamati inaishauri idara katika mipango yake ishirikiane na idara nyengine kutafuta eneo ambalo litaweza kupangwa vizuri, ambapo eneo hilo ndio litakuwa mji wa Zanzibar. Agizo hilo limetekelezwa kwa kupitia mradi wa *Zanzibar Urban Service Project* ambapo Idara ya Mipango Miji inaendelea na maandalizi ya mpango mkuu wa matumizi ya ardhi katika Mji Mkuu wa Zanzibar *Master Plan*. Utaratibu wa kuandaa eneo la mpango, *Planning Area*, usimamizi wa mpango *Planning* na utaratibu wa kumpata mshauri elekezi vyote vimekamilika.

Kamati inashauri idara iandae utaratibu maalum wa kutoa elimu ya umma juu ya umuhimu wa kupanga miji yetu. Idara imezungumza na masheha wote wa Unguja na Pemba, kuhusu suala la matumizi ya ardhi. Hata hivyo, idara itazidi kutoa elimu ili suala la mipango miji lieleweke vizuri zaidi.

Mahakama ya Ardhi:
Agizo lilikuwa kama ifuatavyo. Kamati imeguswa mno na changamoto zote zinazoikabili mahakama ya ardhi na inaishauri Wizara kufanya juhudi za kuyatatua matatizo yanayoikabili mahakama, ili kurahisisha utendaji kazi wa taasisi hiyo. Juhudi zinachukuliwa ili mahakama iweze kutekeleza kazi zake za kupunguza wingi wa kezi ziliopo mahakamani hapa, ambapo mara tu baada ya kukamilika ukarabati wa ofisi ya Koani, mahakama itawapatia watendaji sambamba na hilo, juhudi za kuwapatia usafiri zinaendelea.

Mhe. Spika, Kamati inashauri kuendelezwa kwa tamko la Waziri kuwa zitafunguliwa mahakama tatu za ardhi ambazo zitasaidia kutatua matatizo yaliopo hivi sasa ya kurundikana kwa kesi katika mahakama ya ardhi, ambapo mahakama hizo hadi sasa hazijafunguliwa. Wizara tayari imeanza ukarabati wa majengo ya mahakama Mkoa wa Kusini liliopo Koani.

Vile vile Mhe. Spika, Kamati inashauri serikali kupitia Wizara kama imeshindwa kuendesha mahakama ya ardhi, basi ivunje na kuzipeleka kesi za ardhi katika mahakama ya kawaida.

Mhe. Spika, migogoro ya ardhi ni vyema ikaendelea kubakia kusikilizwa na mahakama ya ardhi, kama matakwa ya sheria nambari 7 ya mwaka 1994, wizara inajiandaa kufungua mahakama za mikoa na inatarajia kuwa na mahakimu wa mikoa na kutoa vitendea kazi ili mahakama hizo ziweze kufanya wajibu wake na kuondoa matatizo ambayo yanajitokeza sasa.

Mhe. Spika, Kamati inashauri wizara kufanya mazungumzo na Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, kuliomba jengo la Benki ya Watu wa Zanzibar liliopo Mwanakwerekwe litumiwe kwa mahakama ya ardhi. Wizara inafanya jitihada za kuwasiliana na Benki ya Watu wa Zanzibar, kutokana na muongozo wa Benki Kuu ya Tanzania, taasisi yoyote ya fedha inatakiwa iwe na sehemu ya kuhifadhia taarifa, *back up*. Hivyo jengo hilo halitoweza kupatikana kwa ajili ya mahakama ya ardhi kwa kuwa linatumika kama ni *back up* ya benki ya watu wa Zanzibar.

Mhe. Spika, Kamati inaagiza kwamba ukumbi uliopo chini ya jengo la idara ya upimaji ramani Pemba ambalo halitumiki likarabatiwe na litumiwe na mahakama kutokana na umuhimu wa shughuli hiyo. Ukumbi umefanyiwa matengenezo na kwa sasa unatumika kwa ajili ya kazi za mahakama ya ardhi. Kuhusu suala la usafiri wizara inajitahidi kuhakikisha kwamba wanapatiwa usafiri ili mahakama hiyo ifanye wajibu wake vizuri.

Kamati inaiagiza mahakama kuendeleza mradi wa kusajili ardhi, ili kuondoa tatizo liliopo hivi sasa ambapo migogoro ya ardhi imekuwa ikiibuka kwa wingi. Shughuli za usajili wa ardhi zimeanza rasmi kufuatia uzinduzi uliofanywa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na zinatekelezwa chini ya Idara ya Mrajis wa Ardhi.

Kamati inaiagiza mahakama ishirikiane na taasisi za ardhi katika utoaji wa hukumu zake, ili kuepusha kuwadhulumu baadhi ya wamiliki wa ardhi, ambao idara za ardhi huwa zina ushahidi wa kutosha katika suala zima la ardhi husika. Upo ushirikiano mkubwa wa idara husika na mahakama katika kuhakikisha inapata ushahidi ili iweze kutoa maamuzi yaliyo sahihi.

Kuhusu Idara ya Nyumba na Maendeleo ya Makaazi, kuzidisha usimamizi katika nyumba zote za serikali na kuendeleza juhudi za kutengeneza makaro ya nyumba hizo. Idara imeanza kwa kujenga *soak bit* moja kubwa Mombasa, kusafisha *septic tank* tano Michenzani na moja Mombasa. Imebadilisha bomba zilizochakaa Michenzani na Mombasa, hatua hii inaendelea kufanyiwa kazi ili kuhakikisha tatizo hili linaondoka.

Kamati inaunga mkono idara kuwekewa fungu la bajeti kwa kazi za matengenezo. Bado bajeti ni ndogo, lakini kadiri ya uwezo wa kifedha wa serikali utakavyowezekana, hali itafanywa hivyo ili kuhakikisha usumbufu unaondoka.

Vile vile Kamati inashauri wizara kukabiliana na mapendekezo mapya ya kodi za nyumba yaliyopendekezwa. Wizara imetayarisha mapendekezo ya bei mpya za kodi za nyumba na inatarajia kuziwasilisha Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, ili kutumika katika mwaka ujao wa fedha wa 2013/2014.

Idara ya Ujenzi

Agizo

Kamati inaiomba Wizara kufanya juhudi za kuwasiliana na Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ili wakubaliane kuwa halmashauri na vikosi vya SMZ vinavyotaka kujenga au kufanya maamuzi yoyote kuhusiana na mambo ya ujenzi kwa kuwaajiri au kuwakodi wataalamu wa mambo hayo, ili wafanye kazi hizo kitaalamu zaidi. Bodi zetu mbili tayari zimewasiliana za Wizara zote zinazohusika ili kuwaarifu utaratibu huo na kuhakikisha taratibu zinafuatwa.

Pia kamati imesikitishwa sana na taarifa kuwa fedha zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Mpapa zinataka kuchukuliwa, na kupelekwa Pemba kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Kengeja. Kwa hivyo, kamati inashauri kuliangalia upya suala hilo na kuziacha fedha hizo zitumike kwa ajili ya kumaliza nyumba za Mpapa.

Mhe. Spika, kuhusu fedha za ujenzi wa Pemba. Fedha za Mpapa hazikutumika kwa ujenzi wa jengo la Kengeja na jengo la Kengeja zimetengwa fedha zake maalum kwa kazi hizo kadiri ya uwezo wa serikali utakavyowezekana.

Kamati inashauri Wizara kuziangalia bodi za wataalamu na bodi za wakandarasi kwa kuzitengea fungu lake la bajeti, ili bodi hizo ziweze kufanya kazi zake. Katika bajeti ya mwaka ujao fedha za wizara zitajitahidi kadiri ya hali itakavyoruhusu kutenga fedha kwa ajili ya bodi hizi.

Mhe. Spika, kamati inaziagiza bodi zote mbili kuwachukulia hatua kali wale wote wanaokiuka sheria zilizopo ili iwe fundisho kwa wengine. Katika hatua za awali bodi imekuwa ikitoa taaluma kwa wakandarasi, ili kuwashajihisha kufuata taratibu za kisheria katika kutekeleza kazi zao. Bodi imeanza kufanya ukaguzi katika maeneo mbali mbali, ili kuangalia uhalali wa wakandarasi wanaojenga katika maeneo hayo. Pia bodi imeanza kwa hatua ya kuomba mtaalamu wa sheria, ambaye itamtumia kama mwendesha mashtaka kwa wale wote wanaohalifu sheria za usajili wa wakandarasi. Mtaalamu huyo tayari amepatikana.

Kuhusu Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe. Kufanya mazungumzo na Baraza la Manispaa kuhusiana na suala zima la *parking*, na suala la fedha za Bustani ya Forodhani ili kuondoa changamoto zilizopo hivi sasa.

Utekelezaji

Mamlaka imefanya kikao cha Bustani ya Forodhani chini ya uenyekiti wa bodi ya ushauri ya bustani hiyo, ambayo inawajumuisha maofisa kutoka taasisi hizi mbili, juu ya utekelezaji wa agizo hilo inayohusiana na utaratibu mzima wa utawala wa fedha, na suala zima la *parking* ya bustani hiyo na kutathmini juu ya njia za kukabiliana na changamoto ziliopo, kama vile matumizi mabaya ya bustani, wauzaji wa vyakula na kadhalika.

Mamlaka imepanga pamoja na uongozi wa sasa wa Baraza la Manispaa, kuwa na mashirikiano ya karibu sana na kukubaliana na utekelezaji wa hayo, kama kuna kikwazo kieleweke ili kupatiwa ufumbuzi, kuhakikisha kwamba bustani yetu inakuwa katika hali inayoridhisha kwa ajili ya manufaa ya watu wetu.

Pili, mamlaka izidishe juhudi za kusimamia bustani zake zote ili zisiharibiwe na baadhi ya wananchi. Mamlaka imeongeza juhudi ya kusimamia bustani zake, kwa kuweka kumbukumbu za kitaalamu *data base*. Aidha, tayari ramani mbili zimeshatayarishwa, moja ni nyuma ya *Africa House* na nyengine ni Malindi. Aidha, mamlaka inaendelea kujitahidi kuwatafuta wafadhili wa kuendeleza bustani hizo wakiwemo wananchi.

Maelezo ya ziada
Mamlaka inajiandaa kufanya taratibu ya namna nzuri ya kuendelezwa kwa bustani hizi, kutafuta njia bora ya mikataba itakayokubalika kisheria na serikali kuweza kushirikiana katika matengenezo makubwa ya bustani na mwananchi atakayejitokeza kufanya hivyo.

Tatu, Mamlaka izidishe kampeni ya kutangaza Mji Mkongwe na faida zake kwa wananchi na wageni wanaoitembelea Zanzibar. Mamlaka inachukulia kazi ya kampeni ya kuutangaza Mji Mkongwe na faida zake kwa wananchi, ni zoezi la kila siku katika kazi za kawaida za Mamlaka. Tunawashajihisha wananchi mbali mbali wanapowasilisha maombi yao ya ukarabati, wajenzi wanaoteuliwa na wasimamizi kupatiwa elimu kabla ya kuanza kazi. Wageni na wanafunzi wengi wa nje ambao wanafika mamlaka kufanya utafiti. Pia mamlaka inatoa elimu kwa watu wa nje ya nchi kupitia njia ya mtandao.

Maelezo ya Ziada
Viongozi na wafanyakazi wa mamlaka wanaposafiri kuhudhuria vikao mbali mbali vya urithi wa kimataifa, wanapata muda mzuri wa kutoa kampeni hizo. Pia ni njia nzuri ya kusaidia kuelimisha maendeleo ya Zanzibar kupitia Mji Mkongwe. Vile vile kutumia redio, magazeti vinatumika kwa kutoa elimu zaidi kwa wananchi wetu.

Mamlaka iandae utaratibu wa kutoa elimu kwa wananchi kuhusiana na umuhimu wa Mji Mkongwe kupitia vyombo vya habari. Mamlaka inalifanyia kazi jambo hilo, na itaendelea kuchukua hatua zifaazo ili kuhakikisha zinatoa taarifa sahihi.

Mamlaka ya Maji

Agizo
Kamati inaishauri mamlaka iwakopeshe wananchi hasa wasiokuwa na uwezo, kwa kuwasogezea karibu huduma ya maji, na watakapofungiwa huduma ya maji mamlaka ikate fedha inazowadai kwa utaratibu wa kidogo kidogo. Agizo hili tayari limeshatekelezwa na wananchi wanaungiwa huduma ya maji kwa njia ya mkopo, baada ya kujaza mkataba wa makubaliano ya mkopo baina ya mteja na mamlaka ya maji, na kukatwa deni hilo kidogo kidogo hadi linapokamilika. Mkopo huu ni kwa ajili ya wananchi wenye kipato cha chini tu.

Agizo jengine
Mhe. Spika, Kamati imeguswa sana na kilimo cha mamlaka ya uchache wa wafanyakazi hasa mafundi. Hivyo, kamati inashauri wizara ifanye utaratibu wa kuwaajiri mafundi watakaosaidia hasa waliopo sasa, ili kuondoa usumbufu wanaopata wananchi katika suala zima la maji.

Agizo hili limetekelezwa kwa kuzingatia nafasi za kazi katika fani ya ufundi, lakini kwa bahati mbaya matangazo yaliyojitokeza hawakujitokeza waombaji. Kwa hivyo mamlaka itachukua hatua ya kuzitangaza tena nafasi hizo.

Mhe. Spika, Kamati inaishauri Mamlaka inapotaka kufanya zoezi la kukata huduma ya maji, basi iandae utaratibu maalum wa kuyatambua maeneo ambayo wanakwenda kuondoa huduma ya maji, na sio kubahatisha na kuwakatia baadhi ya wananchi ambao hawana madeni.

Agizo hilo limetekelezwa, kwani zoezi hili huwa linafanywa kwa utaratibu maalum kwa kuyatambua maeneo ambayo yanahitaji kuondolewa huduma ya maji na kwa wale wote wenye madeni. Itachukua kila jitihada mamlaka ili kuhakikisha kwamba wale ambao hawana madeni jambo hilo halifanyiki yaani hawakatiwi maji, ili kuondoa usumbufu kwa wananchi, tutahakikisha kwamba wataalamu wetu wanafanya jambo hili kwa hadhari ya hali ya juu.

Mhe. Spika, Kamati inashauri mamlaka kujifunza kwa kupitia mamlaka nyengine zilizoko Tanzania Bara, ili mamlaka iweze kutoa huduma zake kwa ufanisi zaidi. Yapo mashirikiano makubwa kati ya mamlaka yetu ya *ZAWA* na mamlaka nyengine za maji za upande wa Tanzania Bara, hususan Arusha, na upo ushirikiano wa kutosha na mambo yanaendelea vizuri kwenye eneo hili.

Vile vile Kamati imeitaka Mamlaka na Wizara kwa ujumla izidi kusisitiza kuwa suala la ukosefu wa maji katika maeneo mengi ya Mkoa wa Mjini Magharibi, ni usumbufu mkubwa kwa wananchi. Kwa hivyo, kuna haja ya kuweka mpango mkakati wa kulipunguza au kuliondoa kabisa tatizo sugu la ukosefu wa maji ndani ya Mkoa wa Mjini Magharibi.

Mhe. Spika, suala hili limeshaanza kuchukuliwa hatua kwa kuchimba visima vitano, ili kuongeza wingi wa maji katika Mkoa wa Mjini Magharibi. Visima vitano hivyo ambavyo vimechimbwa vipo katika maeneo ya Chumbuni visima vitatu na Saateni visima viwili.

Lengo la mkakati huu ni kuchimba visima 9 na hatua mbali mbali Wizara inachukua, ili kuhakikisha jambo hili linafanyika ili kuhakikisha wananchi wanapata maji safi na salama katika mikoa yetu yote ya Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, pamoja na ufinyu wa bajeti uliopo hivi sasa na matatizo mbali mbali ambayo mamlaka inakabiliana nayo. Kamati inashauri mamlaka iwe na utaratibu wa kununua *spare* na vifaa vya akiba, pindi linapotokea tatizo katika mtandao wa maji, basi liweze kurekebishwa na kuondolewa usumbufu kwa wananchi katika upatikanaji wa huduma hii ya maji.

Agizo hilo linaendelea kufanyiwa kazi kwa kununua *spare* na vifaa mbali mbali vya maji, kama vile *pump*, *motor* na mabomba na kadhalika. Lakini kutokana na maharibiko ya mara kwa mara yapunguwe kwa *pump* na *motor*, tatizo ambalo linasababishwa na kupanda na kushuka kwa umeme na kupasuka kwa mabomba. Hali ambayo inasababisha kutumia fedha nyingi nje ya bajeti yetu tuliyojipangia.

Aidha, fedha ambazo zimepangiwa kwa ajili ya mradi wa usambazaji maji mijini na vijijini kutoka Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo huwa hazipatikani kwa wakati kiasi

kinachotakiwa. Hivyo, wizara itaendelea kufanya jitihada kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, kuhakikisha kwamba tunapata fedha za kutoa huduma hii ili kuondosha usumbufu kwa wananchi wetu.

Kuhusu Idara ya Nishati na Madini. Wizara kuweka wazi suala la mafuta hapa Zanzibar.

Utekelezaji
Suala bado limo katika mazungumzo baina ya serikali mbili kupitia Kamati ya kero za Muungano. Kimsingi Serikali ya Muungano kupitia kamati hiyo, imetoa kauli ya kukubali kufanywa marekebisho ili Zanzibar iweze kulisimamia suala hilo. Kamati maalum ya ufundi ikiongozwa na Wanasheria Wakuu wa upande wa Tanzania Bara na Zanzibar ndio wanaolifanyia kazi jambo hilo na *Inshaallah* litapatiwa ufumbuzi wa uhakika kwa maslahi ya nchi yetu.

Mhe Spika, kuharakisha hatua za kumalizika kwa sheria ya mafuta Zanzibar. Kazi hiyo imefika hatua ya ngazi ya Makatibu Wakuu na sheria hiyo itafikishwa Baraza mapema mwaka wa fedha 2013/2014. Hata hivyo, sheria ya kudhibiti biashara ya mafuta tayari imeshafanyiwa kazi na kupitishwa na Baraza la Wawakilishi tarehe 08/04/2013, ambayo itaanzisha mamlaka ya udhibiti wa mafuta yenyewe. Sheria ya *Zanzibar Petroleum Supply Act*, itasaidia mamlaka katika kutekeleza kazi hiyo. Kwa hivyo, kuwasilishwa kwa sheria hiyo mapema mwakani itakuwa bado wizara haijachelewa kufanya hivyo. Mchakato wa sheria hiyo unaendelea, ili kuhakikisha tunafikia lengo lililokusudiwa.

Mhe. Spika, kurudishwa kwa mashirikiano baina ya Idara ya Nishati na Madini na *ZASEA*. Idara tayari imefanya mawasiliano na *ZASEA* tokea mwaka jana 2012 kwa sasa taasisi hizo mbili tayari zimetiliana saini mkataba wa mafahamiano, *MOU* katika kutekeleza shughuli za nishati mbadala na hasa nishati ya jua. Idara imejipanga kwa kushirikiana na *ZASEA* katika utekelezaji wa baadhi ya shughuli za mpango wa kazi wa sera ya nishati.

Shirika la Umeme:
Mhe. Spika, kama ililiagiza shirika lizidishe juhudi katika kuhakikisha kuwa linawaunganisha wananchi wote wa Unguja na Pemba, na kuondoa malalamiko yaliopo kutoka kwa baadhi ya wananchi ili waweze kutumia huduma za umeme. Shirika hivi sasa linachukua hatua za haraka za kuwaunganishia umeme wananchi, mara tu baada ya kukamilisha taratibu za kulipia huduma hiyo. Utaratibu huu utakuwa endelevu ili kuhakikisha kwamba tatizo hili linaondoka kwa wananchi, hasa baada ya kupata umeme huu mpya kutoka Tanzania Bara, jambo ambalo ni kwa mashirikiano na ndugu zetu wa Japan, tumeongeza njia za umeme ili wananchi wetu waweze kufanikiwa vizuri zaidi.

Mhe. Spika, Kamati inashauri shirika kuwasogezea wananchi huduma ya umeme, hasa vijijini kwa wale wasiojiweza kuifuata huduma hiyo mbali, jambo ambalo linawaongezea wateja wa shirika hilo mzigo.

Ushauri umepokelewa, serikali imefungua kituo cha kuuzia umeme Mkokotoni Unguja, Mkoani na Wete Pemba. Vile vile litafungua vituo vya kutoa huduma ya kiufundi katika maeneo ya Makunduchi, Gamba Unguja na Wete kwa Pemba. Aidha, kazi ya kusambaza umeme mjini na

vijijini zinaendelezwa na shirika, kwa ujenzi wa *line* kubwa na ndogo za umeme kwa Unguja na Pemba, kwa kadri ya fedha zitakavyopatikana.

Mhe. Spika, Kamati inashauri katika baadhi ya maeneo ambayo hayana wasimamizi wa shirika na huduma ya umeme inapatikana, wawekwe wasimamizi japo mmoja ambaye atasimamia mambo yote ya shirika, yakiwemo ya ufundi. Kwa mfano, katika kisiwa cha Kojani, kamati inashauri awepo msimamizi ambaye atatambuliwa na shirika, na endapo likitokea tatizo basi wananchi waweze kumuona na kusuluhisha tatizo hilo lililojitokeza.

Kwa kuweka wasimamizi wa shirika kwenye baadhi ya maeneo yaliyopo mbali na mji na kutoa huduma. Shirika limefungua kituo cha huduma Makunduchi, Gamba Unguja na katika kisiwa cha Kojani ndugu Hussein Bwakame mfanyakazi wa shirika ameajiriwa kwa kutoa huduma kwa wananchi ndani ya kisiwa hicho. Shirika litaendelea na utamaduni wa kutoa huduma kwa haraka pale wananchi wanapopata usumbufu wa aina yoyote.

Mhe. Spika, Kamati inalishauri shirika kutoa taarifa za matatizo yote yanayojitokeza, ili kuepusha usumbufu unaojitokeza hivi sasa wa kukatika kwa umeme bila ya wananchi kupewa taarifa, jambo ambalo hupelekea usumbufu na kuunguza baadhi ya vifaa vya wananchi hao.

Shirika linakubaliana na Kamati kunakosababishwa miundombinu chakavu ya kusafirisha umeme kwa wananchi. Shirika limepata msaada kutoka Serikali ya Japan na tayari kazi ya kuimarisha miundombinu ya umeme inaendelea kutekelezwa hatua kwa hatua. Shirika litajitahidi kufanya marekebisho zaidi katika miundombinu ya umeme na kuhakikisha kwamba matokeo ambayo yanajitokeza, hayajitokezi siku za mbele.

Vile vile kwa kupitia redio Zanzibar, televisheni, *Cable Zanzibar* na vyombo vyengine vya habari, hatua zitachukuliwa kuhakikisha kwamba zinatolewa taarifa, ili wananchi waweze kujua pale ambapo pana tatizo na pale ambapo imetokezea kwa bahati mbaya Mhe. Spika, basi shirika linaomba radhi.

Mhe. Spika, Kamati inashauri shirika kuwa na utaratibu maalum, wa kuwatambua wadaiwa ambao wanastahiki kukatiwa umeme na sio kwenda kukata umeme kwa baadhi ya wananchi ambao hawana madeni, jambo ambalo husababisha usumbufu kwa wateja hao. Kamati inashauri shirika lichukue hatua zaidi kupunguza tatizo la kukatika kwa umeme mara kwa mara kisiwani Pemba.

Pia shirika limeandaa utaratibu mzuri wa kutoa *bill* kwa wateja na muda maalum wa kufanya malipo kabla ya kwenda kuwakatia huduma wananchi. Lakini itabidi kuchukua jitihada zaidi ili kuhakikisha kwamba utaratibu huu unakuwa mzuri zaidi, ili usilete usumbufu kwa wananchi, lakini wale ambao hawalipi madeni yao wanatarajiwa walipe madeni yao kwa wakati, ili kuepuka usumbufu huo usitokee kwa upande wao.

Mhe. Spika, Shirika la Umeme linalalamikiwa na Kampuni ya Zantel, kuwa mara nyingi yanapotokea matatizo katika vituo vinavyounganisha umeme, shirika limekuwa likichelewa kwenda kurekebisha matatizo hayo na kusababisha hasara kubwa kwa kampuni hiyo. Kwa hivyo, Kamati inaliagiza Shirika la Umeme na Kampuni ya Zantel, kuyaheshimu makubaliano

yaliyofikiwa tarehe 6/03/2012, katika kikao baina ya uongozi wa Shirika la Umeme, Kampuni ya Zantel na Kamati ambayo ilikuwa ni mashuhuda katika maazimio yaliyofikiwa katika kikao hicho, na kuzitaka taasisi hizo zaidi kushirikiana katika utendaji wao wa kazi, ziweze kufikia malengo ya kuwasaidia wananchi wanaohitaji huduma hiyo muhimu.

Shirika la Umeme na Kampuni ya Zantel zinaheshimu na kuendeleza makubaliano yaliyofikiwa mbele ya Kamati, na hivi karibuni tu Shirika la Umeme na Kampuni ya Zantel wamefikia muafaka wa kufanya biashara kwa pamoja, ya kuuza umeme kwa kutumia simu za mkononi, ili kuwasaidia wananchi kupata huduma kwa haraka zaidi.

Mhe. Spika, hayo ndio yalikuwa maagizo ya Kamati kwa upande wa Wizara hii. Kwa hivyo, kwa heshima kubwa Mhe. Spika na Waheshimiwa Wajumbe, naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, kueleza kwa ufupi kabisa kuhusiana na maagizo ya Kamati kwa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano na utekekezaji wake.

Kwanza namshukuru Allah kwa kutupa uhai, uzima na taufiq ya kufika hapa kuzungumza katika Baraza hili tukufu. Mhe. Spika, kwa niaba ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Wajumbe wote, kwa kufanya ziara mbali mbali kwa madhumuni ya kuona maendeleo na changamoto zinazotukabili.

Aidha, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru Wajumbe hao kwa michango na ushauri waliotupa, na wanaendelea kutupa kila tunapokutana katika mikutano inayohusiana na kazi zetu na ziara zao.

Mhe. Spika, maagizo yote yalikuwa ni 32. Mimi sitotaka kuyaeleza yote, kwa sababu tumetoa waraka ambao maagizo kwa wizara inapatikana katika ukurasa wa kwanza, usafiri na leseni unapatikana ukurasa wa 2 hadi wa 4, ujenzi na utunzaji wa barabara unapatikana katika ukurasa wa 5 hadi wa 7, Shirika la Meli inapatikana katika ukurasa wa 8, Shirika la Bandari linapatikana ukurasa wa 9 hadi wa 10, Mamlaka ya usafiri baharini ukurasa wa 11 hadi wa 13 na Mamlaka ya viwanja vya ndege ukurasa wa 14.

Mhe. Spika, baada ya kutoa hayo, napenda nieleze mambo kama manne makubwa ambayo yamejitokeza katika maelekezo ya Kamati. Suala la kwanza ni mikataba ya ujenzi wa barabara na ucheleweshaji wa kazi.

Mhe. Spika, shughuli hii kwa kweli ina nyanja nyingi, lakini kwa upande wetu sisi tatizo kubwa ilikuwa ni ulipaji wa fidia ili kuweka *corridor* kuwa safi kwa ajili ya mjenzi wa barabara. Kwa hivyo, baada ya kupata maelekezo ya Kamati na mengineyo, tumechukua hatua za dharura na tunaishukuru serikali kupitia Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, kwamba kuanzia Disemba hadi Machi mwaka huu tumeweza kulipa fidia ya kama bilioni 1.6, ili kupambana na tatizo la kucheleweshwa ujenzi wa barabara.

Mhe. Spika, tatizo jengine ni eneo la kuweka nafasi ya njia, yaani *road resolve*. Hili ni tatizo kubwa ambalo Kamati imelipendekeza kuwa liondolewe. Njia nyingi zinafanywa, lakini moja

wapo sasa hivi ni kurekebisha sheria ile ambayo ilikuwepo toka mwaka 1945. Kwa hivyo, katika kipindi kifupi kijacho tutaiwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu, marekebisho ya sheria hiyo, ili kuona sasa sheria ya *road resolve*, yaani mabakizi ya njia ya kuweza kutojengwa inakuja katika Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, tatizo jengine kubwa ambalo lilionekana ni juu ya utendaji na hali ya Karakana Kuu ya Zanzibar. Ni kweli Mhe. Spika, karakana kuu bado haijaweza kufikia kiwango chake na kwa hivyo, wizara imeliona hilo na inakubaliana na Kamati. Tupo katika mchakato mkubwa wa kumtafuta mbia ambaye tutaweza kushirikiana naye, ili kuiendesha kwa ufanisi na kutumia ile fursa iliopo ya zana na jengo ambalo lipo la kutosha. Kwa hivyo, hapa tunawashukuru Kamati vile vile kwa kuweza kulizindua suala hili.

Mhe. Spika, tatizo au pendekezo jengine ambalo limeonekana na Kamati ni namna ya usimamizi wa miradi ya ujenzi. Kwa kweli suala hili tunalihakikishia Baraza lako tukufu Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe pamoja na wananchi kwamba ujenzi wote wa barabara zote zinapata mshauri muelekezi (*consultant*) ndio kazi zinaanza. Kwa hivyo, baadhi ya matatizo yanayojitokeza ni kutokana na matatizo mengine ya kiufundi, lakini *consultant* anakuwepo.

Jambo jengine ambalo lililojitokeza ni juu ya ujenzi wa jengo jipya la kupokea abiria (*Terminal II*). Mhe. Spika, ni kweli kwamba hapa kuna tatizo lakini sisi kwa sababu kiwanja cha ndege, bandari ni masuala sio ya kitaifa tu, lakini ni ya kimataia.

Kwa hivyo, ili kuliona lile jengo linakamilika katika hali ya ufanisi na kuweza kufanya kazi, basi leo hii anaingia Mshauri Muelekezi kutoka Kampuni ya Ufaransa, ambaye ataanza kazi rasmi pamoja na timu yake ya watu wanne, kuona kwamba tatizo lile linatatuliwa kwa lugha ya Kiingereza wanasema *once and for all*, yaani moja kwa moja tunalitatua. Kwa maana hiyo, tunawahakikishia Waheshimiwa Wajumbe kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba kazi tunafanya nzito ya kuweza kuona kwamba jengo lile linapata mwelekeo mzuri, ili kuweza kukimu ile haja ambayo iliopo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya hayo mambo mengine mawili ambayo ni muhimu sana ni kuhusu suala zima la Shirika la Meli. Kweli kulikuwa na matatizo mengi katika shirika hilo ikiwemo kutowepo na hizo meli zenyewe, lakini hivi karibuni tulipitisha hapa katika Baraza lako tukufu Mhe. Spika, Sheria mpya ya Shirika la Meli na sasa tunaendelea na mchakato wa kuchapisha *Business Plan* ya kujiendesha Shirika la Meli itakayochukuana pamoja na kulirekebisha wenyewe shirika hilo liweze kujiendesha kibiashara. Kwa hiyo, hatua zinachukuliwa na si muda mrefu tutaweza kusikia kupitia vyombo vya habari mkataba utakaofungwa, ili kununua meli yetu mpya *Inshaallah*.

Jambo la mwisho kabisa Mhe. Spika, ambalo nataka kulisema hapa ni suala zima la marekebisho ya usafiri wa baharini kama Kamati ilivyopendekeza, ambayo yanapatikana kwenye ukurasa wa 11 mpaka 13 kama nilivyosema. Usafiri wa baharini umeimarishwa na tunahakikisha kwamba sheria zinafuatwa, lakini pia kuna mchakato wa kupata zile Kanuni ambazo zinahitajika na karibuni hivi niliweza kuletewa mimi kwa ajili ya kuzitia saini Kanuni hizo.

Mhe. Spika, kwa niaba ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano napenda nitoe shukurani za dhati kwa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kupitia Mwenyekiti wake mashuhuri aliyepewa jina la Jasiri wa Kiume jana na Msaidizi Mwanasheria Mkuu wa Baraza hili.

Kwa hivyo, napenda sana Waheshimiwa Wajumbe wote waitizame ripoti hiyo kama tulivyoitoa na watupe michango yao ya kufanya kuwa Wizara yetu iende vizuri zaidi, ili tuweze kumudu usafiri wote, kwa sababu wizara hii imebeba usafiri wote wa baharini, angani, nchi kavu na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Kwa hayo, machache nakushukuru tena Mhe. Spika, na naomba Waheshimiwa Wajumbe watuunge mkono na watupe michango ambayo ina muelekeo na inayoweza kutupeleka mbele zaidi.

Mhe. Spika, ahsante sana na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Waziri, ahsante sana kwa kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji kwa muda mfupi ukizingatia muda mfupi tulionao.

Sasa naomba nimkaribishe Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Mawasiliano na Ujenzi Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, karibu sana.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk (Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi): Mhe. Spika, kwa niaba ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, napenda kukushukuru wewe binafsi pamoja na Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa kuipa Kamati yetu ushirikiano mkubwa, uliotuwezesha kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi mkubwa. Lakini pia tunashukuru kwa kutupatia nafasi ya kueleza japo kwa muhtasari, ripoti ya Kamati inayotokana na kazi ambazo zimekuwa zikitekelezwa na Kamati kwa takriban mwaka mzima.

Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi imeundwa kwa mujibu wa kifungu cha Kanuni cha 106 (d) cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi toleo la mwaka 2012 na majukumu yake yametajwa katika kifungu cha (111).

Mhe. Spika, napenda kuchukua nafasi hii adhimu kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa mashirikiano yao, ambayo yamewezesha kufanya kazi zetu kwa ufanisi mkubwa. Wajumbe wenyewe ni hawa wafuatao:-

1. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk — Mwenyekiti
2. Mhe. Hassan Hamad Omar — Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu — Mjumbe
4. Mhe. Salma Mussa Bilali — Mjumbe
5. Mhe. Subeit Khamis Faki — Mjumbe
6. Mhe. Marina Joel Thomas — Mjumbe
7. Ndg. Aziza Waziri Kheir — Katibu
8. Ndg. Maryam Rashid Ali — Katibu

Mhe. Spika, Kamati ilifanya kazi zake kwa utaratibu wa kupokea taarifa za utekelezaji wa malengo ya wizara pamoja na taasisi zake na baadae kutembelea na kukagua utekelezaji wa shughuli zinazofanywa na taasisi hizo.

Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:

Mhe. Spika, Kamati yetu ilitembelea taasisi mbali mbali za wizara hii na kukagua miradi kadhaa inayotekelezwa na taasisi hizo. Baada ya kutembelea na kuona utekelezaji wa shughuli hizo, kamati ilitoa maelekezo na ushauri kwa wizara na taasisi zake kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utekelezaji.

Mhe. Spika, muhtasari huu unabainisha baadhi ya mambo ambayo kamati inaona kuwa ni muhimu sana kwa ajili ya kuisaidia serikali katika utendaji wake na wananchi kwa ujumla. Mambo yenyewe ni kama yanavyofafanuliwa hapa chini.

Mhe. Spika, ardhi ni miongoni mwa raslimali muhimu sana, na isipotumika inavyotakikana matatizo mbali mbali hujitokeza. Kutokana na udogo wa nchi yetu na matumizi ya ardhi kuwa ni makubwa, na kutokana na matatizo mbali mbali yaliyopo hivi sasa katika suala zima la ardhi.

Kamati inazielekeza idara zinazohusika na masuala ya ardhi, ambazo ni Idara ya Ardhi na Usajili, Idara ya Upimaji na Ramani na Idara ya Mipango Miji na Vijiji na nyenginezo kuyasimamia maeneo yote ambayo tayari yameshapimwa na kuhakikisha kuwa matumizi ya maeneo hayo yanalingana na mipango iliyopangwa na taasisi hizo. Aidha Kamati inazisisitiza taasisi hizo kufanya kazi pamoja, jambo ambalo litapelekea kupunguza baadhi ya kero zinazotokea katika jamii yetu.

Mhe. Spika, kamati yetu ilikagua katika eneo la Nungwi lililokuwa likimilikiwa na Kampuni ya *Spice Island*, ambapo maelezo iliyoyapata kutoka kwa wawakilishi wa kampuni hiyo na maelezo iliyoyapata kutoka katika Idara ya Ardhi na Usajili ni tofauti. Hivyo Kamati inapenda kushauri kuwa katika kesi kama hizo utoaji wa hukumu uzingatie uadilifu kwa kuzisikiliza pande zote zinazohusika.

Mhe. Spika, kamati yetu katika kazi zake imegundua kuwa kuna baadhi ya viongozi, ambao hawahusiki na masuala ya ardhi, lakini wamekuwa wakiyatumia mamlaka waliyonayo na kuamua baadhi ya mambo ambayo yapo nje ya mamlaka yao.

Aidha kuna baadhi ya viongozi ambao pia hutumia mamlaka yao kwa kutaka wauziwe maeneo, ambayo tayari yana umiliki wa wananchi au yameshauzwa kwa taasisi nyengine. Hivyo, kamati inapenda kutoa ushauri kuwa si jambo la busara kwa kiongozi mwenye kuheshimika kufanya kitendo kama hicho. Kamati inazishauri idara husika katika jambo la upimaji au uuzaji wa ardhi zisiwe na muhali kwa kumuangalia mtu kwa cheo chake, na badala yake haki itendeke kwa maamuzi yatakayokua hayana athari kwa mtu yeyote.

Mhe. Spika, masuala ya ardhi yamekuwa na malalamiko mengi hapa nchini na kusababisha mrundikano mkubwa wa kesi za ardhi katika Mahakama ya Ardhi. Hivyo Kamati inaishauri wizara kuisaidia Mahakama ya Ardhi kupata fedha kwa ajili ya ukarabati wa majengo ambayo

wamepatiwa kwa ajili ya kuyakarabati kuendeshea shughuli za mahakama. Kufanya hivyo kutasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza kesi nyingi zilizorundikana katika Mahakama ya Ardhi.

Pia Kamati inasisitiza kuwa suala la kuongezewa posho wazee wa Mahakama "*Assessors*" ni muhimu sana kutokana na kazi kubwa wanazozifanya wazee hao ambapo nyongeza hiyo itakuwa ni hamasa kwao kufanya kazi kwa badii zaidi.

Jambo jengine ambalo Kamati imeona ni vizuri kuliainisha hapa ni suala zima la upatikanaji wa huduma ya maji mijini na vijijini. Kamati ilitembelea miradi mbali mbali inayoendelezwa na Mamlaka ya Maji katika kutatua tatizo hilo hapa nchini. Pamoja na kukamilika kwa baadhi ya miradi na kuanza kufanya kazi kwa kutoa huduma hiyo kwa baadhi ya maeneo, kamati yetu inaendelea kusisitiza kuwa Mamlaka ina jukumu kubwa la kuwa na mpango maalum wa kulimaliza tatizo hilo hapa nchini.

Aidha Kamati inapenda kuwaomba na kuwasisitiza wananchi kuisaidia Mamlaka ya Maji kwa kuchangia kulipia huduma ya maji, jambo ambalo litasaidia kuondoa baadhi ya changamoto zilizopo katika Mamlaka na huenda ukawa ni msingi wa upatikanaji wa huduma ya maji kwa maeneo ambayo yanakosa huduma hiyo kwa muda mrefu.

Mhe. Spika, kamati yetu inaisisitiza serikali kulitilia mkazo suala la uanzishaji wa Shirika la Nyumba la Zanzibar, jambo ambalo kwa kiasi fulani litasaidia kupunguza kero zinazowakabili wananchi hivi sasa za ukosefu wa makaazi ya kudumu na ya uhakika. Aidha uanzishwaji wa shirika hilo pia utasaidia katika udhibiti wa kodi za majengo ya serikali.

Mhe. Spika, kamati yetu ilitembelea katika Nyumba za Maendeleo za Mpapa, ambapo iliridhishwa na hatua iliyofikia hivi sasa japokuwa fedha za mradi huo zimekua zikichelewa kuingizwa. Aidha juhudi zinazochukuliwa na Idara ya Ujenzi ni za kupigiwa mfano kutokana na kazi ngumu inazofanya katika mazingira magumu. Hivyo Kamati inapenda kuishauri serikali kuwa bajeti inayopitishwa kwa idara iingizwe kwa wakati na ipatikane kwa mujibu wa makisio yaliyowekwa.

Mhe. Spika, kamati yetu imesikitishwa sana na kitendo kilichofanywa na mkandarasi aliyepewa kazi ya kuliezeka jengo la *Beit-el-Ajaib*, ambapo mkandarasi huyo aliliezeka jengo hilo kwa mabati mapya lakini jambo la kushangaza aliweka lami katika mabati hayo, ambapo pamoja na uwekaji wa mabati mapya uliofanywa lakini mvua ikinyesha maji yote yanaingia ndani. *(Makofi)*

Hivyo Kamati ilipewa taarifa hiyo na Mamlaka ya Mji Mkongwe, ambapo Mamlaka hiyo imesema kuwa ni vyema kazi zote za *grade* ya juu za majengo yenye hadhi kubwa kwa mujibu wa sheria za Mji Mkongwe, zikapelekwa kwa Mamlaka na si vyema kazi hizo kupewa taasisi au mtu mwengine ambaye hana utaalamu wa kutosha kuhusiana na majengo hayo. Wazo hilo lilipokelewa na Kamati na tunaishauri serikali ilifanyie kazi mara moja. *(Makofi)*

Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano:
Mhe. Spika, katika wizara hii Kamati ilipata fursa ya kuzitembelea baadhi ya taasisi na kukagua miradi inayosimamiwa na taasisi hizo. Baadhi ya mambo muhimu ambayo Kamati iliyaona na kuyatilia msisitizo ni kama yanavyofafanuliwa hapa chini.

Kamati yetu ilitembelea katika Shirika la Meli na kuelezwa kuwa mkataba wa utengenezaji wa meli mpya bado haujasainiwa, hivyo kupitia ripoti hii Kamati inaomba kupatiwa maelezo ya kutosha juu ya suala la ununuzi wa meli na hadi sasa suala hilo liipofikia.

Mhe. Spika, kamati yetu ilipotembelea Shirika la Bandari ilipatiwa taarifa na kushuhudia kitengo cha '*Tower'* cha shirika kinakabiliwa na tatizo la ukosefu wa eneo muafaka kwa ajili ya kufanyia shughuli zake, ambapo eneo linalotumika sasa haliwawezeshi kuona maeneo yote kutokana na ujenzi wa eneo hilo kutoendana na mazingira ya kazi za kitengo hicho.

Kamati inaishauri wizara ilisaidie shirika na kufanya juhudi za makusudi za kupatikana eneo la kudumu ambalo litaweza kujengwa jengo litakalotumika kwa shughuli hiyo. Aidha Kamati iligundua kuwa bado shirika linakabiliwa na changamoto ya mrundikano wa makontena katika eneo la bandarini, kutokana na eneo la bandari hiyo kuwa dogo na mahitaji kuwa ni makubwa.

Kamati yetu inasisitiza umuhimu wa kupewa eneo liliopo mbele ya Hoteli ya Bwawani kwa ajili ya kuyaweka makontena hayo, ili kupunguza mrundikano huo ambao unazorotesha shughuli za kiutendaji katika bandari yetu na kutukosesha mapato mengi.

Aidha Kamati yetu inalielekeza shirika kuzidi kuziimarisha bandari zake ziliopo Pemba kwa kuharakisha upelekaji wa vifaa vya kupakulia mizigo katika bandari hizo kwa kufanya utanuzi wa Bandari ya Wete na matengenezo ya Bandari ya Mkoani. Kutokana na changamoto zilizopo katika Shirika la Bandari Kamati inaisisitiza serikali kufanya juhudi za makusudi za kulisaidia Shirika kupata wafadhili watakaosaidia fedha kwa ajili ya ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri, ambayo ndio itakuwa suluhisho la baadhi ya changamoto zilizopo hivi sasa.

Mhe. Spika, katika Mamlaka ya Usafiri Baharini Kamati ilielezwa changamoto nyingi zinazoikabili mamlaka hiyo ikiwemo ya ufinyu wa bajeti na ukosefu wa fedha za kuendeshea Mamlaka, hii ni changamoto ambayo inakwamisha mipango ya Mamlaka katika kutekeleza majukumu yake.

Kutokana na changamoto hiyo Kamati inashauri kuwa mamlaka iwezeshwe, ili iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi mkubwa, aidha kamati imelitaka Shirika la Meli kuyawasilisha mapato ya ndani ya mamlaka yanayotolewa na meli za kigeni, yawasilishwe kwa mamlaka, ili fedha hizo ziweze kusaidia kutatua baadhi ya changamoto zinazoikabili Mamlaka.

Vile vile inaishauri wizara iisaidie mamlaka kuikumbusha Wizara ya Fedha kuipatia Mamlaka Mhasibu na Msaidizi wake, ili mamlaka hiyo iweze kupatiwa fedha inazoziomba Wizara ya Fedha kwa wakati na kukabidhiwa akaunti yao ambayo hawajakabidhiwa na Wizara ya Fedha, kwa sababu ya kukosa Mhasibu na Msaidizi wake.

Mhe. Spika, kamati ilipotembelea katika Mamlaka ya Viwanja vya Ndege ilipewa taarifa kuwa ujenzi wa *Terminal* mpya ya uwanja wa ndege umesimama kutokana na matatizo yaliyojitokeza. Kwa hivyo, kupitia ripoti hii Kamati inaomba kupatiwa maelezo na wizara kuhusiana na suala hilo na hadi hivi sasa ujenzi huo umefikia hatua gani au maamuzi gani yaliyotolewa na serikali.

Aidha Kamati inazidi kusisitiza umuhimu wa uwanja wa ndege wa Pemba, ambapo uwanja huo unahitaji matengenezo makubwa, ili uweze kutumika kwa wakati wote kwa kuzingatia kuwa kwa sasa uwanja huo hautumiki wakati wa usiku kutokana na kukosa taa. *(Makofi)*

Kamati yetu iliagiza kupatiwa taarifa juu ya hatua za utekelezaji wa suala zima la taasisi ambayo inatoa huduma za uwanja wa ndege (*Ground Handling*). Ikumbukwe kwamba wakati wa bajeti serikali iliahidi kuondoa umiliki wa taasisi moja na kufungua milango ya ushindani, kupitia ripoti hii Kamati inataka kujua jee suala hilo limefikia wapi na kwa nini serikali haijatoa tarifa kwa kamati husika, ili wananchi wakaweza kuelewa nini kinaendelea kwa malengo ya wasiwasi, ambao baadhi ya wananchi wameupata.

Mhe. Spika, kamati katika Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara imeielekeza idara iandae mkakati madhubuti wa kuzilinda barabara zake kwa kuwachukulia hatua kali wale wote wanaoharibu miundombinu ya barabara, wakiwemo wale wote waliolipwa fidia na wakarudia tena kujenga pembezoni mwa barabara.

Aidha Kamati imesikitishwa na hatua zinazochukuliwa na baadhi ya wananchi wanaojenga matuta kiholela pasi na kufuata ushauri wa kitaalamu kutoka kwa idara. Kupitia ripoti hii Kamati inawaomba viongozi wote wa majimbo wakiwemo Waheshimiwa Wawakilishi kutoa elimu kwa wananchi kuhusiana na suala zima la matuta, endapo kukiwa na ulazima wa kuwekwa matuta katika maeneo hayo ni vyema kuwashirikisha wataalamu wa idara hii.

Mhe. Spika, kamati yetu inaamini kuwa Karakana ya Serikali endapo itatumika vyema inaweza kusaidia katika kukusanya mapato lakini pia kuokoa fedha nyingi za serikali. Kamati imesikitishwa sana na taarifa iliyopewa kuwa ni gari chache za serikali zinazoitumia karakana hii.

Kamati imeelezwa kuwa katika mwezi mzima ni gari kumi tu za serikali ndizo zinazopelekwa katika karakana hiyo kwa ajili ya kufanyiwa matengenezo. Kwa hivyo, kamati inapenda kuchukua nafasi hii kuzishauri wizara zote za serikali kuitumia Karakana ya Serikali kwa lengo la kuokoa fedha nyingi zinazotumika kulipia huduma za matengenezo katika magereji ya watu binafsi, na pia jambo hilo litaisaidia Karakana ya Serikali kujiongezea mapato yatakayotumika kuondoa baadhi ya changamoto zilizopo.

Hitimisho:

Katika kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar, Kanuni za Baraza la Wawakilishi na Sheria nyenginezo, Kamati imetoa maelekezo na ushauri wake ambao tunaamini kuwa utasaidia katika kuleta ufanisi kwenye utekelezaji wa majukumu ya Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano.

Maelekezo na maoni hayo yalitolewa na Kamati kwa dhamira ya kuwawakilisha vyema wananchi wa Zanzibar na kuona kuwa maslahi ya wananchi hao, kwa mujibu wa sheria, yanapewa kipaumbele. Kamati yetu inatumai kuwa maelekezo na maoni yaliyotolewa na Kamati kwa wizara hizo yatazingatiwa kwa lengo la kutoa huduma zilizotukuka kwa wananchi wa Zanzibar.

Mwisho, Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi inaushukuru Uongozi wa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati chini ya Waziri muhusika, Naibu Waziri, Katibu Mkuu wake pamoja na watendaji wote wa wizara hiyo. Vile vile tunamshukuru Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, Naibu Waziri, Katibu Mkuu wake pamoja na watendaji wake wakuu, kwa ushirikiano mkubwa walioupatia Kamati yetu katika kipindi chote cha kazi za Kamati kwa Unguja na Pemba. *(Makofi)*

Aidha Kamati pia inaushukuru Uongozi wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano chini ya uongozi wa Waziri wa wizara hiyo, Naibu Waziri na Katibu Mkuu wa wizara hiyo na watendaji wote wa wizara kwa ushirikiano mkubwa kwa Kamati yetu, ulioiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa. *(Makofi)*

Kamati inatoa shukurani za pekee kwa Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mhe. Pandu Ameir Kificho, Katibu wa Baraza la Wawakilishi na watendaji wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake vizuri, lakini zaidi kwa ushauri walioupatia kamati yetu katika kipindi cha utekelezaji wa majukumu yake.

Mwisho kabisa, kamati inawashukuru Makatibu wa Kamati hii kwa kutekeleza majukumu yao ya kuisaidia Kamati na Wajumbe wa Kamati, ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Lakini kwa mujibu wa Kanuni na mimi naomba nichangie kidogo.

Mhe. Spika, mimi nakwenda kwenye *points* zangu mbili ambazo ndio kubwa.

Kwanza tumetoa humu kuna kesi ile kubwa ya hawa ndugu zetu wa *Spice Island* wamekuja kuwekeza hapa Zanzibar kwa kuweka Hoteli ya *Five Stars*, ambapo tungezewa kuwasaidia wananchi wetu kupata ajira pamoja na kodi ya mapato kubwa sana. Lakini jambo la kusikitisha ni kwamba eneo hili viongozi wakuu walikwenda kuwanyang'anya na hawa watu walilipa, yaani walilinunua hili eneo kwa fedha nyingi sana.*(Makofi)*

Nashukuru katika zile siku zangu saba nilizosema kuna wengine wamejitokeza ku-*withdraw* kwangu mimi na amebakia mmoja tu mpaka hivi sasa bado hajaweza ku-*withdraw*, ambaye Mhe. Spika kama Kanuni au Sheria inaniruhusu nimtaje na kama nimfiche kwenye mabano naomba kupata ridhaa yako. Kwa kweli amebakia mmoja tu na kama huyu akishaondoa basi Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati na hili limetokana na mtendaji wake mmoja ndiye aliyeficha hati, Mhe Spika kama leo angekuwepo Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, basi tungesema Katibu wake hamfai kabisa na kama yupo ama ameondoka. *(Makofi)*

Kwa kweli leo sijui ilikuwaje Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa sababu leo ni siku adhimu na kama wapo Mawaziri wengine wameondoka basi Mhe. Spika hawakututendea haki, kwani leo hapa kuna kitu kinatolewa majibu, Mhe. Spika mara nyengine linda kikao chako kwa sababu hizi safari hazishi na wanakwenda Mawaziri wengi na hakuna tunachokifanya.

Kutokana na hali hiyo, ndio maana juzi nikasema kwamba jamani na wala sikuwa na mantiki ya kumuonea mtu choyo cha suti ya mtu, isipokuwa nilisema mawaziri tuvae suti za utendaji na wala sio suti za kujionesha na hicho ndicho nilichokisema na wala sikum-specialize mtu kumsema mtu fulani, kwa sababu suti sote tunazo jana nilikuja na ya Italy na leo nimekuja ya Uingereza, sasa kama ni suti utendaji basi na mimi nimevaa suti nitakuwa mtendaji na wala sikuwa na mantiki hiyo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba sana na nilipokuona umetikisa kichwa ukasema kuwa nisimtaje huyu mtu, lakini bado nitaendelea kutoa siku tatu za mwisho. Kwa hiyo, naomba sana ajiondoe mwenyewe na hawa wengine wameshafutwa, kwa sababu wazungu wako njiani wanakuja Waingereza, yaani ni watu wa kuheshimika. *(Makofi)*

Kwa kweli kwenye kadhia hii Mhe. Makamu wa Pili wa Rais aliifanya kazi nzuri sana, kwa sababu alikemea na alikwenda katika visite side aliona jinsi gani. Kwa hivyo, namuomba sana Makamu wa Pili wa Rais kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba kauli yake asiifute na wala asimuogope mtu na twende katika utendaji, kwa sababu wananchi wetu tunawadhalilisha kwa kutopata kazi. Mhe. Spika, naomba sana hili liweze kufadhilika.

Lakini Mhe. Spika, asili ya kupata sifa jana na mimi kuambiwa ni mmoja katika watu ambao na hii ni maajabu kwa sababu mwenzangu amepewa Marekani na mimi nimepewa Baraza la Wawakilishi tena na Mwakilishi mwenzangu kwa ule uchungu aliouona. Hali hii Mhe. Spika, ujiringie na hawa ni *UNDP*, kwa sababu wanatupa mafunzo na fedha zao tunazitumia kihalali na wala hatuzitumii kimagendo. *(Makofi)*

Sasa jana nilipewa sifa hiyo na kwa nini nilipewa sifa hiyo, kwa sababu kuna maeneo ambayo Mhe. Spika, tunataka kuwekeza mambo ya skuli. Mhe. Spika, naomba nikueleze ubabaishaji uliotokea, kwanza kile kiwanja kimepimwa mara mbili kwa tatu, na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na kusema futeni na ninaungana naye kwa asilimia mia moja na mimi niko pamoja tufute, kumbe hakukosea Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, lakini sijui alikuja kuogopa nini aka-*withdraw* kauli yake, nadhani ni vyema aikamate pale pale na wala hakukosea tena atamke kifua mbele kwamba hakukosea.

Mhe. Spika, ubabaishaji wa humu nitakwambia kwamba kiwanja kimoja kina namba 547 na kina hati tatu, hivi nani mwenyewe. Kuna jina moja Amina na maana yake jana Mhe. Spika nilicheka kwa sababu mimi nilichangia mwanzo, lakini Mhe. Wangu Shamhuna hakunitaja na nilishangaa sana kwa sababu mimi ndiye wa mwanzo katika kuchangia, lakini sikutajwa na wala sijui kwa nini na mimi sendi hivyo mimi nikishasema hapa yamekwisha.

Kwa hiyo, mtu ukiniuliza hali nitaitikia na kama hukuniuliza basi hiyo ni shauri yako mwenyewe, kwa sababu mimi ni wajibu wangu lazima niwatetee wananchi na wala tusiekeane nongwa au tusinuniane na kama unataka nongwa zisiwepo basi bora mtu ajiondoe.

Jambo la msingi ni mtu kufanya vizuri, ili tukupe *well done* kwa nini tusikusifu. Kwa mfano, namsifu Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora amefanya kitu kimoja kizuri sana katika viongozi wangu sita Mawaziri ninaowapenda mmoja na yeye ameingia wa saba, kwa sababu ameweka uwazi na ukweli jana kwamba watu wasifukuzwe kiholela

makazini, na hivyo ndivyo tunavyotaka. Mhe. Spika, twende kwa utaratibu na tuelimishwe hatua baada ya hatua. Mhe. Spika, na yule mtu wangu jana na yeye yumo katika wale Mawaziri saba ninaowapenda na yeye ameingia katika watendaji wazuri.

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kiwanja hichi kuna majina ya watu watatu kuna mtoto anaitwa Amina amepewa kiwanja hicho Amina Juma Shamhuna, kuna Katibu Mkuu wa Kilimo na Mifugo na Mazingira, kiwanja hicho hicho kapewa. Na kuna mwengine Mohammed Ussi Kheri kiwanja hicho hicho kapewa kiwanja hicho kimoja tu, sasa nani mwenyewe tujiulize. Balozi kafute nenda katangazeleo futa wananchi wajenge skuli wala usione tabu.

Pili kuna Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji sio mpya huyu mpya mtu mzuri bwana sie kabisa wala hana doa ee niseme ukweli hana doa hana chochote sie yeye huyu kaanza juzi tu wala ukimuuliza Zanzibar kuna viwanja vingapi yeye hajui. Kwa hivyo huyu sie nafuta hansard ikae safi huyu sie. Lakini nikiendelea tena kiwanja hicho hicho amepewa mtu mwengine lakini niseme hivi Mheshimiwa katika viwanja hichi kuna mama mmoja yeye kaona kuwa nimetoa siku 7 na ni mtu mzuri na mtu mwenye heshima kinamama nikupeni hongera uchungu wa mwana ulivyomuuma kwa kusikia inataka kujengwa skuli anaitwa mama Nachia Ali Haji yeye amekirudisha amesema niko *fair* kabisa nilipewa hidaya hii sasa nairejesha. Sasa hao wengine wanajitia sugu kuna Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Maji.

Mheshimiwa nataka nikwambie hawajachukua hati zao kazuie haraka sana kule hawajachukua wala hawaja-*sign* nyuma kule kwa sababu kule nyuma kuna *sign* ya makubaliano. Asha Ali Juma yeye haja-*sign* nyuma hati yake lakini hajachukukua ipo kule. Kuna Asha Ali Juma na kuna Amina Juma Shamhuna ambayo hii hapa hati zao yeye huyu keshachukua haraka haraka lakini wenzake hizi hati hawajazichukua bado zipo.

Mhe. Kuna Katibu Mkuu Afisi ya Waziri Kiongozi huyu *firster* keshachukua, sasa Katibu Mkuu niulize ni Wizara zenyewe au Katibu Mkuu jina la mtu hapo mimi ninaposhangaa na ninapojiuliza. Lakini kwa mujibu wa sheria na nilivyofaham na nilivyosomeshwa na Mwanasheria wangu mkuu hapa, hii inakuwa ni mali ya serikali sasa ni rahisi kwako kufuta, wala isikupe tabu Mheshimiwa wangu ni rahisi kwako kufuta kwa sababu kitu cha maendeleo cha jamii serikali ndio inavyotaka hivyo. Mhe. Makamo futa wala usiache sio amri kwa mujibu wa utaratibu namwambia tu futa Mheshimiwa wangu wala usibabaike wala hakuna mtu alokukera futa moja kwa moja.

Lakini nikimalizia Mhe. Wangu kwa kuokoa wakati maana yake nina mambo mengi Mhe. Spika, leo lakini kutokana na bajeti yako finyu itabidi mimi niendelee kusema.

Mheshimiwa hiki si kitu cha mzaha kwa sababu matajiri wapo wa kutujengea skuli, watu wameshajenga matenki tayari wamesimama, hivi kweli jamani tukose kwa kuwa mtu anataka kujenga nyumba ya starehe tu tukose elimu na eneo hilo wanavyopata tabu watoto wanakwenda skuli ni maili si chini ya moja mpaka mbili, wakipita pwani wanadhalilishwa wanapigwa na wawekezaji tunakwenda wapi viongozi tuwe na huruma jamani mambo mengine, maana yake leo nilikusudia Mhe. Spika, machozi yanitoke lakini basi tu yapo mbali tuwache hayo Mheshimiwa.

Lakini la pili tuheshimu matamko hapa tulisema kuwa mamlaka ziwe huru katika utendaji wake wa kazi, tusiziingilie mamlaka tuwape uhuru katika utendaji wake wa kazi. Tunapoziingilia mamlaka katika utendaji wake wa kazi tunafeli haiwezekani.

Mimi ninakupeni mfano jamani jana nilipiga kelele sana mimi kuhusu zile mashine za cancer lakini ninamshukuru babu yangu Juma kajibu vizuri sana nampa pongezi na yeye. Ile tenda alokwenda kupewa jamani si field yake hivi kweli chuma kikakwaruzike halafu kisifanye kazi ni jambo *imposible* haiwezekani kitu kama hicho, fedha za umma zile tunaambiwa hivi hivi tu vimekwaruzika, vinakwaruzika vipi chuma semeni vile vitu vimeletwa havikukamilika visu vyengine hakuna kavisa tuseme hivyo ukweli. Wamedanganywa, Makamo wa Pili kadanganywa, Makamo wa Kwanza kenda kadanganywa ukweli hatutaki kuwaambia.

Makamo nataka nikwambie bwana pesa zimeibiwa pale, kawatie ndani wale pesa zimeibiwa pale zimeliwa fedha, mashine zimeshindikana Mheshimiwa sasa na hii tujaribu kutafuta watu ambao wenye field zao tusiokote okote, uwanja wa Amaan mpaka leo ule pale mtu kaambiwa akajenge hoteli kaletwa pale hatimae mpaka leo anaingia mitini kajenga chumba kimoja tu cha kupumzikia tunakwenda wapi?

Sasa na hii mamlaka naomba sana Mhe. Waziri uje kutujibu vizuri hapa suala hili, umeitisha *tender* lakini mpaka leo hakuna jibu lililotokea kwa nini, mambo mengi tuna *delay time* ndio tunapokosa mambo mengi. Mhe. Waziri hii kesi ya *Spice Island* alikuwa afute vyote tuanze utaratibu, lakini Mhe. Waziri atafuta anaweka kwenye *briefcase* yake tunachelewa. Tunakwenda wapi jamani, naomba sana, hawa waliobakia nawapa tenda kwa muda wa siku tatu Baraza linalokuja hapa tena sina haya sina aibu.

Mhe. Spika, kutokana na wakati wako naiunga mkono hii ripoti yangu niliyoisema kwa asilimia mia moja ahsante sana kwa kuwasiliza.

Mhe. Spika: Ahsante sana, sasa tunaendelea na uchangiaji wa jumla, naendelea kuhimiza tutumie muda mfupi ili shughuli hii tuimalize kipindi cha asubuhi ili jioni twende na nyengine.

Mhe. Salma Mussa Bilal: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia ripoti ya kamati au utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Wizara hizi mbili. Mhe. Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii, halafu niwashukuru Mawaziri kwa kutoa maelezo yao ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati.

Mhe. Spika, mimi nisipoteze muda nianze katika suala zima la migogoro ya ardhi. Nitasema kwa ufupi kwa sababu tayari yameshazungumzwa na kwa kujali muda nitataka ufafanuzi mdogo tu. Suala la migogoro ya ardhi limekuwa ni kubwa mno kama taarifa inavyosema. Na kesi nyingi zimekuwa zikilundikana sana katika Mahakama ya Ardhi. Hii inatokana na kwamba hii mahakama ni moja ambayo Zanzibar nzima inategemea mahakama hiyo tu ambayo ndio inashughulikia afisi hizi.

Mhe. Spika, katika ziara zetu tumepata taarifa kwamba na tumetembelea hasa baadhi ya majengo kwamba yamependekezwa kuwa Mahakama ya Ardhi kwa Mkoa wa Kaskazini na Mkoa wa

Kusini. Kwa Mkoa wa Kaskazini tulitembelea eneo la Gamba Majenzi pale kuna jengo ambalo linatarajiwa kuwekwa Mahakama ya Ardhi. Kwa upande wa Mkoa wa Kusini ni eneo la Koani.

Mhe.Waziri nilikuwa nataka anifafanulie au anipa taarifa kwamba hatua za matengenezo hasa ya yale majengo yamefikia wapi na lini Mahakama zile zitaanza kutumika ili kupunguza mrundikana wa makesi katika mahakama moja ambayo ilikuwepo Vuga.

Mhe. Spika, je, katika mahakama zile kuna wazee wale wa Mahakama, wazee ambao weanafanya kazi nzuri, wanafanya kazi ngumu lakini posho zao ni chache sana. Na hili nilisisitiza kwamba wazee wale waongezewe posho kwa kazi ngumu ambazo wanazifanya ili waweze kufanya kazi kwa moyo na ari zaidi.

Mhe. Spika, suala jengine naenda kwenye suala la Mamlaka ya Maji. Tatizo la maji au kero ya maji bado kwa Zanzibar ni tatizo kubwa ingawa Mamlaka imejipanga vizuri, tunakwenda kule tunapata taarifa nzuri, lakini kila ambapo visima vya maji vinaendelea kuchimbwa lakini na matatizo ya maji katika maeneo mbali mbali yanazidi kuwa tatizo kubwa.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa naomba tu kwamba mamlaka izidi kujipanga vizuri kwa hili. Tulipata nafasi ya kutembelea mamlaka ya maji Mkoa wa Arusa, *AUSA*. Tulikwenda kule kwa bahati nzuri tulikutana na watendaji wa Idara ya maji, tumekwenda, tumesoma, tumetembea, tumeona jinsi gani wenzetu wamejipanga mpaka kuondoa tatizo la huduma ya maji katika Mkoa wa Arusha. Mimi ninachokiomba kwamba Mamlaka ya Maji izidi kujipanga vizuri zaidi ili kuweza kupunguza tatizo la upatikanaji wa maji katika nchi yetu.

Kubwa ambalo tumejifunza kule Mamlaka ya Arusha imejipanga vizuri na siri ya mafanikio yao ni ule utaratibu waliouweka wa kutoa huduma za maji. Wamejipanga kwamba kila mwananchi ambaye anapata huduma ya maji kwanza wamemfundia mita ya maji. Mimi ningeiomba Mamlaka ijipange kwa kuwa tulivyokwenda kule tulikwenda na watendaji kuiga jambo zuri na si dhambi. Kwa hiyo na wao wajipange vizuri ili kuweza kutoa ufanisi katika upatikanaji wa maji.

Pia ningeomba mamlaka ijipange vizuri katika kuhakiki wale wote ambao wanapata huduma hii ya maji, waweze kulipia huduma hii ili fedha zile ziweze kusaidia katika kuendeleza mamlaka hii kwa ufanisi. Hivi sasa kuna wananchi wengi wanapata maji, kuna maeneo mengi yanaungwa maji kiholela. Lakini kwa kuwa mamlaka bado ina upungufu wa wafanyakazi una upungufu wa watendaji inashindwa kufatilia hili. Kwa hivyo mimi ningeomba mamlaka ijipange vizuri katika kufatilia wale wote ambao wanapata maji, walipe maji na wale wote ambao wanaunga maji kiholela bila ya kupata taarifa au kupata uthibitisho wa mamlaka waweze kuwatambua na waweze kupitia katika njia za kisheria na baadaye kufanya malipo ili shirika liweze kujiendesha.

Mhe. Spika, niende katika Wizara ya Miundombinu, mimi naanza katika Shirika la Bandari. Sote tunajua kwamba bandari ni shirika ambalo tunalitegemea sana katika kupata mapato ya nchi yetu. Lakini bado bandari kuna tatizo la mrundikano wa makontena pale bandarini. Mlundikano ambao unasababisha makontena mengine yasiweze kuingia na halafu pia kupunguza kile kipato cha mfululiza cha upatikanaji wa nafasi ya kuingiza makontena. Tatizo hili tumelizungumza siku nyingi na tunakwenda tunalikuta, lakini bado halijapatiwa ufumbuzi.

Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri, wakati alipokuwa Makamo Mwenyekiti nadhani suala hili na yeye pia alikuwa analizungumzia sana lakini sasa ameshakuwa Waziri basi namuomba Mhe. Waziri kwa kushirikiana na Mhe. Waziri wa Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi mshirikiane ili kuliomba eneo la Bwawani ili Shirika la Bandari liweze kupewa lile eneo ili kupunguza mrundikano wa Makantena kule Bandarini yawekwe pale ili na mengine yaweze kuingia ili shirika liweze kujiendesha na kupata faida na makontena yaweze kupungua pale katika eneo la bandari.

Halafu pia Mhe. Waziri alisema kuhusu Bandari ya Mpigaduri, mimi ningeomba ziongezeke juhudi za maksudi ili wafadhili waweze kupatikana ili yaanze maandalizi ya Bandari ile ya Mpigaduri ili kupunguza mrundikano na matatizo mengine katika Bandari hii yaliyokuwepo sasa hivi.

Mhe. Spika, suala langu la mwisho nilikuwa nataka kumuuliza Mhe. Waziri kuhusu mradi wa *Post Code* nilikuwa nataka kujua mradi huu kwa hapa Zanzibar umefikia hatua gani. Kwa sababu kule kwa wenzetu Tanzania Bara mradi huu ulianza kwa majaribio katika Mkoa wa Dodoma na Arusha. Nadhani Mhe. Spika, sisi tulikwenda Dodoma kuangalia ule mradi na tumeona jinsi ulivyokuwa unaendelea vizuri. Kwa hiyo kwa upande wetu wa Zanzibar kwa maelezo ya Mkurugenzi wa *TCRA* hapa anasema huo mradi hapa tayari matayarisho yake yamekwisha kuanza kuandaliwa na fedha zipo za mradi huo na tayari walikwisha kuandaa *pallets area* mbili kwa Mkoa wa Mjini Magharib nadhani ni Mombasa na Chukwani.

Lakini nilikuwa nataka kujua mradi huo umefikia wapi au umekwama wapi kwamba mpaka leo bado katika hizo shehia ambazo zimekwisha kupangwa kwa majaribio kwa Zanzibar hazijaanza kazi. Kama nilivyosema kwa taarifa ya Mkurugenzi amesema kwamba hizo fedha zipo na zinakaribia kurejeshwa kwa sababu hadi leo huo mradi bado haujawa na matayarisho mazuri na haujaanza. Kwa hiyo nilikuwa nataka kujua Mhe. Waziri kwamba suala hili limefikia wapi kwamba mpaka leo halijakamilika ili tuweze kuanza mradi huo katika nchi yetu hii ya Zanzibar.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa na hayo tu ya kusisitiza na namuomba Mhe. Waziri anitolee ufafanuzi mzuri wakati wa kutoa maelezo yake. Mhe. Spika, nakushukuru ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa ajili ya kuchukua kumbukumbu vizuri Waheshimiwa Wajumbe nilikuwa naomba wanapotoa michango wazungumze karibu na spika, kwani inakuwa hatusikii halafu matokeo yake tutakuwa hatuwezi kuja na majibu sawa sawa. Naomba tufanye hivyo.

Mhe. Spika: Nafikiri majibu ni sahihi ili Waheshimiwa Wajumbe mpate kusikika na Waheshimiwa Mawaziri kwa kuja kutoa ufafanuzi hapo baadaye wakati unapofika.

Mhe. Marina Joel Thomas: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii ya kuchangia. Mimi nitachangia katika Idara ya Ujenzi. Katika idara hii tulivyotembelea tulikuta changamoto ambayo watendaji au wafanyakazi katika kitengo hicho kulikuwa na tatizo la mafunzo. Kitengo hicho ukiangalia Mhe. Spika, ni kitengo kipya, kinahitaji watendaji wenye ujuzi na uwezo. Kwa hapa nilikuwa nashauri kwa Mhe. Waziri kuwapatia mafunzo ili kuleta ufanisi zaidi katika kutekeleza majukumu yao.

Mhe. Spika, nije katika Idara ya Upimaji wa ramani, hapa katika kutembelea tulikuta kuna tatizo la kukosa mashirikiano katika ngazi ya Shehia, Wilaya ya Mikoa. Wakati wafanyakazi wa upimaji wanapokwenda katika zoezi la kukata viwanja walitueleza kuwa wanakosa mashirikiano katika ngazi ya Shehia, Wilaya na Mikoa na hatimaye wanafika hadi kufukuzwa. Kwa hivyo hapa ningemuomba Mhe. Waziri akae na hizo taasisi husika ili kuliondoa tatizo hili.

Mhe. Spika, katika kitengo hicho hicho cha Idara ya Upimaji na Ramani, kulikuwa na tatizo la uchakavu wa magari ya kufanyia kazi za upimaji. Kwa hiyo na hili vile vile Mhe. Waziri namuomba suala hili aliangalie kwa jicho la huruma ili kuwasaidia hawa wafanyakazi ambao wanakwenda katika maeneo na usafiri wao unakuwa wa matatizo.

Jengine Mhe. Spika, nitakwenda katika Idara ya Ujenzi nitazungumzia suala la majango ya Mpapa. Kwanza hapa napenda kuipongeza serikali kwa dhati kabisa kwa hatua iliyopiga kwa kuwapatia wananchi majengo hayo. Pia hapa nilikuwa na ushauri kwa Wizara au Serikali kupatia fedha hizo ili majengo hayo yakamilike ili yaweze kuwasaidia wananchi wetu.

Mhe. Spika, jengine ni msisitizo katika Shirika la Bandari. Shirika la Bandari kama ilivyoeleza ripoti kutokana na ukosefu wa eneo katika kitengo kile cha TAWA. Eneo walilokuwa nalo sasa hivi ni la kuazima tu. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri aisaidie wizara kupatiwa eneo la kudumu la kuweka TAWA hizo.

Mhe. Spika, nije katika Mamlaka ya Usafiri Baharini, katika kitengo hicho pia tumekuta tatizo la kutokuwepo kwa kuhasibu. Jambo ambalo linapelekea fedha kutopatikana kwa wakati. Hapa pia nilikuwa namuomba na namshauri Mhe. Waziri kuwapatia mamlaka ya usafiri muhasibu ili Mamlaka iweze kupata fedha wanazoziomba kwa wakati na kuweza kutekeleza majukumu yao.

Jengine nitakwenda katika Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara. Hapa Mhe. Spika, nitanzungumzia suala la ujenzi wa matuta. Tulivyokuwa katika Kamati yetu katika eneo la Kaskazini tulikuta matuta mengi yamejengwa kwa karibu sana, kwa hiyo nilitaka maelezo kwa muhusika wa utunzaji wa barabara walisema kwamba matuta hayo waliyajenga wenyewe wananchi. Hapa nilikuwa na ushauri, kwa sababu matuta ni muhimu yanasaidia kuepusha ajali, na hasa sehemu zile zenye huduma ya vituo vya afya, skuli yanasaidia sana. Lakini matuta hayo hayo kama yatajengwa pasipokuwa na vipimo maalum pia yanaweza yakasababisha ajali. Kwa sababu anaweza mtu akajenga tuta lakini sio kiwango kile ambacho kinatakiwa, litajengwa tuta kubwa na pengine mtu atakuja na gari kwa speed matokeo yake badala ya kukinga tunasababisha ajali.

Mhe. Spika, nilikuwa naomba hata Waheshimiwa Wawakilishi wenzetu kwenye majimbo yao pindipo ikiwa kuna haja ya kujenga matuta katika sehemu zangu nilikuwa nawashauri washirikiane na taasisi husika ili matuta hayo yajengwe katika viwango vinavyokubalika.

Mhe. Spika, jengine niende kwenye Shirika la Umeme. Umeme ni nishati muhimu sana katika kuendesha maendeleo ya nchi yetu. Lakini tulikuta tatizo la madeni katika taasisi mbali mbali. Hapa nilikuwa namuomba tu Mhe. Waziri kuna baadhi ya taasisi za serikali zina madeni

makubwa na hawalipi kwa wakati. Namuomba Mhe. Waziri alisaidie hili Shirika la Umeme kusimamia taasisi hizo ili ziweze kulipa madeni haya kwa wakati.

Kwenye Mamlaka ya Maji tulitembelea kisima cha Kitongwe eneo la Kiashange, hapa tulikuta kuna tatizo la kumwagika kwa maji mengi na tuliambiwa tatizo ni *air valve*, lakini yale maji yanayomwagika yalikuwa ni mengi mno ukilinganisha na ile gharama ya kifaa. Nilikuwa namuomba Mhe. Waziri likitokea tatizo kama hili ni vyema kuwasiliana na watendaji ambao ni wahusika wa kule ili kuliondoa tatizo hilo na kuepusha ile hasara ambayo imetokea.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, naunga mkono kwa asilimia mia moja, ahsante.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa fursa kuweza kutoa mchango wangu katika ripoti hizi zilizowasilishwa hivi asubuhi.

Kwanza niwapongeze mawaziri wote wawili na pongezi kubwa nimpe Mwenyekiti wa Kamati kwa ujasiri wake wa kuwasilisha ripoti yake na tumeweza kuielewa. Mimi ningakuwa na michango kama sita katika wizara zote mbili, nikianza na Wizara ya Mawasiliano nije kwenye sehemu ya Bandari.

Mhe. Spika, Bandari ni sehemu ambayo inayotutilia fedha katika nchi yetu na ni eneo muhimu sana. Lakini pamoja na jitihada zote wanazozifanya bado wana changamoto ambazo lazima serikali iweze kutafuta mbinu ya kuweza kuwasaidia. Kabla sijataja changamoto nimpongeze mfanyabiashara aliyejenga jingo la abiria pale bandarini ambalo hivi sasa limependeza sana. Na kwa kweli wazalendo kama hawa wanatupa moyo katika nchi yetu kwa sababu kaweka kitu ambacho kila atakakwenda pale basi anaweza akaona kafanya nini. Na nasikia lile jingo linachukua si chini ya watu 300 kwenda mbele kwa wakati mmoja. Tunampongeza sana kwa hilo.

Lakini pia nilitaka kujua kwamba majengo kama yale wanayojenga wafadhili huwa wanakabidhi bandari au huwa wanaliendesha wao wenyewe. Nataka Mhe. Waziri akija atwambie kama limekabidhiwa na bandari basi lazima tulifanyie usafi wa hali ya juu ili liweze kupendeza kama alivyofanya jitihada muwekezaji Yule.

Mhe. Spika, nije kwenye changamoto bandari sasa hivi kuna makontena mengi sana na hivi sasa wameyahamisha wanayaweka njia ya kwendea Bwawani. Mimi kwa upande wangu sikuvutiwa sana kwa sababu mji wetu ni mdogo halafu haiba ya kila pahala tukiweka vitu ambavyo havieleweki ile haiba yake inapotea, tangu hapo hauna haiba nzuri. Nakumbuka siku za nyuma kwamba bandari walinunua eneo kwa Mtipura kule na wakalisafisha ili kuweka makontena nyuma ya maghala ya akiba. Sasa sijui eneo lile walilonunua linafanyiwa kazi gani hivi saa. Lakini bado makontena ni kero lakini na wafanyabiashara wote bidhaa wanaleta kwa makontena.

Kwa hivyo naomba wizara kupitia serikali ifanye jitihada itafute eneo la kuweza kuka makontena katika hali ya usalama ili wafanyabiashara waridhike na biashara wanayoifanya.

La pili katika taarifa wameeleza kwamba bado tatizo jengine la changamoto la bandari kwamba upande wa magharibi kusini bandari inaanza kuzama yaani nadhani inaingia mchanga. Kwa

hivyo kina cha maji kinapungua, nadhani hili ni tatizo kwa sababu meli ndio zinapofikia na pahala panaanza kupungua kina cha maji. Sasa ikiwa itazama mpaka mwisho itakaa ngalawa tu biashara itakuwa inaharibika. Sasa tunataka wizara itwambie inachukua jitihada gani ili kuweza kuliondosha tatizo hili.

Jengine kwenye taarifa pia imeeleza kwamba bandari inadai taasisi za serikali na moja Wizara ya Fedha, KMKM, Shirika la Meli, jumla ya fesha ni US$ wanadai milioni 3.3 fedha za Tanzania wanadai milioni 190.3 taasisi tatu ni pesa nyingi sana. Naomba pia waziri akija atwambie kachukua jitihada gani kudai madeni haya ili iweze bandari kufanya kazi zake vizuri.

Lakini pia katika taarifa kulikuwa na taarifa kwamba bandari ya Mkokotoni nayo hivi sasa inashusha bidhaa nyingi kutoka Tanga, kuanzia vitanda, meza, makabati, mbuzi, ng'ombe na vitu vyengine kadhalika. Na walisema kwamba wana mkakati wa kuweza kuitengeneza bandari ile ili iweze kutia tija kwa hapa Zanzibar, baada ya bandari ya Malindi halafu ifuatie bandari ya Mkokotoni. Je, na hii imefikia hatua gani ambayo bado hivi sasa kazi inafanywa kubwa na mapato mengi yanaingia.

Mhe. Spika, tuliambiwa kwamba watu wanaohusika na mapato wapo lakini bado jitihaa za bandari kufanya lolote hakuna. Kwa sababu hata ukitaka kushuka ama kupanda chombo basi unashuka maji ya kifua au maji ya kiunoni na mabegi umejitwika kichwani. Sasa hiyo si bandari kwa kweli. Ningeliomba wizara ikatwambia imefika jitihada gani gasi angalau ikaweka jet ikaweza kunusuru hata muda wa kujenga bandari ukafika.

Mhe. Spika, jengine pia katika bandari upande wa Pemba kuna bandari tatu, Mkoani, Chake na Wete, hizi mbili kidogo ni nzuri ambayo ya Mkoani na Wete lakini bandari ya Wesha nayo inashusha bidhaa nyingi sana lakini bado haijatizwamwa na Shirika la Bandari. Sasa ningeliomba watwambie wanampango gani kuikuza bandari ya Wesha ambayo inatia pesa nyingi sana. Halafu kimazingira ya Pemba imekaa mahala pazuri maana ipo kati kati ya kisiwa baina ya Mkoani na Wete. Sasa naomba na hili akija Mheshimiwa atwambie kwamba wamechukua jitihada gani ya kuweza kuitengeneza bandari hii kwa kuweza kuleta tija.

Upande wa Mawasiliano nimeishia michango yangu hiyo mitatu sasa nije Wizara ya Ardhi na Makaazi. Suala la kwanza niishukuru serikali kwa jitihada kubwa inayofanya ya kuweza kuondosha tatizo la maji, lakini bado halijatatuka. Katika jimbo la Mfenesini, jimbo la Kitope na jimbo la Bumbwini tumebahatika kupata mradi unaoitwa AKRAA.

Mradi huu ulifunguliwa na Mhe. Rais mwanzoni mwa mwaka huu kwenye visima vilivyochimbwa Mfenesini na tangi likajengwa Kama. Cha kusikitisha baada ya kwisha kuondoka Rais usinduzi wa maji yale yameendelea mwezi mmoja sasa hivi yamepotea kabisa. Mradi umepoteza pesa nyingi, tukafunza vikundi mbali mbali kila shehia ya kutengeneza mabomba yaliyoharibika, ya kukusanya mapato kutokana na maji yaliyopatikana lakini kwa bahati mbaya maji hakuna, sasa hivi mwezi wa pili.

Mhe. Spika, mimi nimefatilia matatizo yako mawili kwa matatu. Tatizo la kwanza tangi lililojenga ni jipya lakini kwenye kozi nne zilizojengwa maji yakifika kwenye kozi ya pili tu yanavuja. Kwa hivyo inakuwa wapiga maji hawapigi tena wanaacha kozi mbili tu. Maji ya

kwenye kozi mbili kwenye tangi yakenda kwenye Jimbo moja jimbo jengine hayapa. Kwa hivyo naomba shirika likaangalie ujenzi wa tangi lile halipo katika hali ya umadhubuti. Waliojenga nadhani waliripua tu au kama limevuja kwa bahati mbasi waende wakaangalie ili liweze kurekebishwa.

Lakini suala la pili wizara na wizara hazikutambuana. Wizara ya Miundombinu imechimba misingi katika barabara lakini mabomba yote ya AKRAA kuanzia Mfenesini kwendea meli 10 wameyafukua yapo nje, mabomba ya nchi 6. Hiyo peke yake ni hatari na maji yayende vizuri kwa vile kumefukuliwa basi kwenye viungo maji mara kwa mara yanavuja. Kwa hivyo naomba wizara hizi mbili zikae zishauriane iyende ikarekebishe tatizo hili. Mabomba yako nje tena ya plastiki, kwa hivyo kikianguka kitu kizito tu kinavunja lile bomba na wenzetu wemetoa pesa nyingi.

Lakini jengine kutoka kwenye tangi bomba la nchi 6 linapeleka maji jimbo la Bumbwini na linalokuja Chuwini yote yanavuja na urefu lilipo hilo tangu mpaka barabara inafikia nusu kilomita lakini maji yanatoka tangu kwenye tangi mpaka barabarani na wataalamu wanaona na mafundi wanaona. Naona na hili wizara ingekwenda ikatizama ikarekebisha. Kwa sababu zile nguvu za wenzetu wakaona tumezithamini katika kuwasaidia wananchi. Mradi ni mzuri lakini mpaka hivi sasa usimamizi wake ni mbaya. Kwa hivyo naomba sana wizara na serikali iliangalie suala hili ili yale mafanikio yaweze kupatikana.

Lakini pia hapa mwanzo mjini palikuwa na mradi wa Majapani ambao walichimba visima zaidi ya saba kianga na maji yakawa yanaletwa Welezo, wamejenga matangi mawili makubwa. Maji yale yalizinduliwa lakini hadi hivi sasa bado hayajasambaa mjini kwa matatizo mbali mbali. Tatizo moja walilolitambua wataalamu kwamba visima vipya, matangi mapya lakini ule mtandao wa kupeleka majini ni ule ule mkongwe, wanawasiwasi kama kuna baadhi ya mabomba yamepasuka na habari haipo kwa hivyo maji yanakwenda katika sehemu ambazo hazikusudii. Tuliambiwa kwamba mtandao utajengwa mpya na mabomba ya zamani taachwa, lakini hadi leo jambo hilo halijafanywa na ikawa shida ya maji bado mjini haijesha. Naomba na hili serikali kupitia wizara wakalifatilia ili ule msaada wa wenzetu Wajapani ukaweza kufanikiwa na wananchi wakapunguza shida ya maji kwa maeneo ya mjini.

Mhe. Spika, nije kwenye tatizo la ardhi SELEM. Kwanza nimpongeze sana Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwa jitihada kubwa aliyofanya, tunamshukuru kwamba eneo kubwa sasa hivi limeshapimwa. Lakini tunamuomba muda mkubwa umepita wananchi hawajagaiwa maeneo hayo. Kwa hivyo itakuwa ni yale yale pamepimwa lakini masikitiko yapo kwamba watu hawajapewa. Kwa hivyo namuomba Mheshimiwa kupitia taasisi zinazohusika lile eneo lilikwishakupatikana basi ligaiwe, watakaobahatika kupata watapata na wengine watasubiri maeneo mengine.

Mhe. Spika, juzi hapa waziri baada ya kujibu maelezo au masuala alisema kwamba bado kuna viongozi wengine wamepewa heka nyingi pale, wengine 26, wengine 20, kwa hivyo alisema kwamba hawa watapunguziwa ili waweze kupewa wananchi kuondosha tatizo. Kwa hivyo naiyomba serikali kupitia wizara kauli zile zitekelezwe ili kuondosha tatizo. Tatizo lilikuwa wazi, limezungumzwa tumelisikia, kwa hivyo kwa wale waliokuwa na maeneo makubwa zaidi

basi yapunguzwe ili waweze kupewa wananchi. Kwa hivyo nadhani hilo limeeleweka niwaachie wizara waweze kulifuatilia.

Nije kwenye Idara ya Nyumba na Makaazi, naipongeza sana wamejitahidi katika hali mbali mbali ya kuweza kuziangalia nyumba zake. Lakini bado tatizo kubwa lipo kwenye nyumba za Michenzani. Nyumba za Michenzani nadhani idadi kubwa inayokaa ya watu ndio inashindwa kujiendesha. Kwa sababu utaona mwanzo ilikuwa nadhani jumba Nam. 5 karo zake zimejaa, sasa hivi maji yanakaribia Miembeni, yamefata Jumba yamemaliza yamepinda yanaingia Miembeni. Na upande wa huku Nam. 4 kwenye minazi inayowaka taa usiku limeanza pale mpaka maji yanapinda kuja Bwawani. Sasa nadhani wahusika wanaona na ule ndio mji wetu, maji machafu, gari zinapita zinawarushia watu wanapita mjini. Kwa hivyo kwa kweli hatutambui kama ni mji au vijijini.

Ningeshauri ama Shirika ama taasisi inayohusika wangejaribu kuyafanyia utaratibu kama makaro yale ya zamani yameshakuwa hayahimili watu waliokuwemo mle basi wangechimba makaro mapya kusaidia kwenye makaro ya zamani. Kwa sababu ukisema ushushe watu wanaokaa Michenzani jumbe lile moja basi Miembeni nzima itafurika na wengine watabaki. Watu wanakaa wengi lakini makaro ni madogo ya kutoa huduma ya maji taka yanavyoitwa hivi sasa. Kwa hiyo naishauri serikali iongeze makaro ili kuondosha kero hilo. Na hili sasa hivi halitaki tocchi, ukenda sasa hivi Michenzani utakuta ma-*block* niliyotaja mawili maji bado yanamwagika na mengine yamefanya mwani gari zinawekwa humo humo, halafu tunasema mji wetu mkuu na majengo ya kisasa. Kwa kweli bado tuko mbali naomba serikali na shirika liweze kusaidia kuweka uzuri matatizo haya.

Lakini wenyewe wamesema changamoto yao kubwa hayo yote wangeyakabili lakini wana ukosefu wa fedha, fedha wanazopata, wanazokusanya zinaingia Mfuko Mkuu wa serikali. Mimi ningeshauri kuwa kazi hii ya sasa hivi angalau miezi mitatu wangeachiwa wakarekebisha matatizo yaliyokuwepo. Pamoja na uchafu huo lakini majumba yetu yamezeeka sana, nadhani sasa hivi ni miaka 40 basi angalau rangi kupakwa nje inashindikana. Sasa ningelishauri huu mfuko wote wanaokusanya sasa hivi waachiwe kutia rangi na kujenga makaro mapya ili yale majumba yaweze kupendeza.

Nikiendelea nije mchango wangu wa mwisho katika Wizara hii nije kwenye Mamlaka ya Mji Mkongwe. Mamlaka ya Mji Mkongwe imeelezwa humu kwamba mji huu uliorodheshwa na *Unesco* mnamo mwaka 2000 kuwa miongoni mwa miji yenye urithi katika dunia. Umekuja kuangaliwa na sifa zake kubwa ni majengo yake na wakaazi wa mule. Lakini sasa hivi kumezuka changamoto ambazo nadhani wenyewe Mji mkongwe wameshindwa kuzisimamia pamoja na taasisi nyengine. Na changamoto kubwa sasa kumezuka wimbi la nyumba za makaazi kugeuzwa hoteli. Kule kulikuwa na hoteli mbili kwa tatu. Tembo, Serena na Africa House. Lakini sasa hivi ukienda kuhesabu kuna hoteli zaidi ya 20, watu wanapewa vilemba wanahama wanatengeneza hoteli.

Ningeliomba taasisi zinazohusika nadhani hoteli zipo fukwe nyingi tu wawekezaji wapelekwe wakajenge tuone uwezo wao. Sio wachukue majumba yetu wapake rangi wafanye mahoteli halafu wanatutoa kwenye Mji mkongwe. Mimi nadhani kama hatujalisimamia hili basi huu urithi wa kimataifa karibu tutaukosa. Kwa sababu tutatoka katika sifa zile ambazo zilikuwa

zimependekezwa. Kwa hivyo nashauri kabla hatujatolewa na tunapata faida kubwa basi kwanza ujenzi wa mahoteli usitishwe halafu na mengine ya kurekebishwa yarekebishwe.

Lakini changamoto nyengine kubwa ambayo pia inashindwa kusimamiwa Mji mkongwe kupitishwa magari makubwa ya tani ambazo haziruhusiwi na bado yanakwenda kule yanapita na yanaharibu majengo. Kwa hivyo naomba na hili serikali na taasisi zinazohusika zingesimamia ili tukaweza kuondosha tatizo ambalo linakabiliwa na Mji Mkongwe. Wana matatizo mengi lakini hayo ndiyo makubwa. Kwa hivyo naishauri Wizara kupitia serikali ingesimamia matatizo haya ili tukaweza Mji mkongwe ukabaki kwenye urithi kama wenzetu wa *UNESCO* waliopendekeza hilo.

Mhe. Spika, baada ya mawazo yangu machache naunga mkono ripoti hizi kwa asilimia 100 kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Mfenesini. Nashukuru sana.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia ripoti hii ya Mawasiliano na Ujenzi. Mhe. Spika, kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Ujenzi kwa utekelezaji wake mzuri wa ripoti yake aliyotuletea nzuri sana ina maelezo mazuri sana nashukuru sana. Mhe. Spika, pia nimpongeze sana Mwenyekiti makini wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kwa ripoti yake nzuri sana ina maelezo ya kila kitu kuhusu Kamati hii.

Mhe. Spika, nisipoteze muda sana nianze na hii taasisi muhimu sana kwa nchi yetu kwani ndio vyanzo vya mapato vyetu vikuu hapa Zanzibar. Mhe. Spika, nianze na Wizara ya Mawasiliano, Shirika la Bandari. Kwanza nimpongeze sana Mkurugenzi wa Bandari kwa jitihada zake kubwa alizochukua kuhakikisha Bandari yetu ya Zanzibar kuwa makini na kufanya kazi vizuri sana.

Mhe. Spika, nianze na Bandari yetu ya Malindi. Mheshimiwa bandari yetu ya Malindi Zanzibar ina matatizo mengi hasa upungufu wa vifaa. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, bandari yetu ina matatizo makubwa ya vifaa kama *tug*. Kamati yako ilikwenda kuangalia na kusikia changamoto zao, lakini tatizo lao kuwa *tug* ya kuingiza meli kubwa. Naomba Mhe. Spika, kupitia Wizara ya Mawasiliano ifanye jitihada zote katika bajeti yao kupata hii *tug* kubwa ya kuingiza meli katika Bandari yetu ya Malindi.

Mhe. Spika, kama tunavyojua bandari yetu hali yake ndogo na ufinyu wa sehemu ya kuwekea makontena. Lakini pia kuna tatizo moja kubwa mfanyabiashara mmoja ambaye kaleta unga, unga ule upo pale kwa muda mrefu Mheshimiwa na Mwenyekiti wa Kamati alielezea kwa muda mrefu suala hili lakini mpaka leo unga ule uko pale bila ya pato lolote la serikali kupata na unga ule haurejeshwi ulikotoka. Kwa kweli Mheshimiwa tatizo hili ni kubwa sana katika nchi yetu na hasa madhara ya wananchi wetu wanaofanya kazi pale, ule unga harufu yake mbaya na unaathiri kwa kweli maisha ya binaadamu. Kwa hivyo naomba Mhe. Spika, suala hili lipatiwe ufafanuzi haraka sana kupitia Wizara ya Mawasiliano.

Mhe. Spika, kamati yako pia ilitembelea katika Ofisi ya *Tower* iliyoko pale Kinazini lakini cha kusikitisha zaidi Mheshimiwa eneo lile ni dogo na huwezi kuona pande zote mashariki, kusini, kaskazini huwezi kuona. Kwa hivyo wale wanaoingiza meli wafanyakazi wetu wanajitahidi sana nawapongeza, lakini kwa ugumu wa kazi wanashindwa kufanya kazi zao vizuri Mheshimiwa

kwa ajili ya eneo linaona upande mmoja tu wa mbele tu nyuma huoni, pembeni huoni. Mheshimiwa hili tatizo sana kwa meli zetu zinazokuja kutoka nchi za nje inakuwa huwezi kuzifanyia kazi vizuri sana kwa eneo hilo.

Mhe. Spika, pia Kamati yako iliangalia suala kubwa la kupata wafadhili, hili suala la kupata wafadhili ni suala muhimu sana kutujengea Bandari yetu ya Mpiga duri. Kwa sababu kama tunavyojua bandari ni ndogo sana na kama uwezo wa serikali yetu ni ndogo tunaomba kupitia Wizara hasa Waziri kutafuta wafadhili kutujengea hii bandari yetu ya Mpiga duri ili tuweze kufanya kazi kwa ufanisi mzuri kabisa.

Mhe. Spika, nitakuwa mwizi wa fadhila kama sijampongeza mfanya biashara mkubwa sana wa maendeleo makubwa aliyoyafanya katika bandari yetu ya Malindi kwa kujenga eneo la abiria, kwa kweli ninampongeza sana, mfanyabiashara huyu Bakhressa kwa kujenga eneo zuri la abiria kuwaondoshea tatizo kubwa wananchi wetu hasa wanaokwenda Tanzania Bara, Pemba na kuja Unguja. Kwa hivyo ninamshukuru sana mfanyabiashara huyu kwa nia yake nzuri ya kuisaidia Zanzibar. Lakini cha kusikitisha zaidi Mheshimiwa, mfanyabiashara huyu anataka eneo apewe kwa ajili ya Ofisi zake za Azam Marine lakini mpaka leo hakupewa Ofisi yoyote. Kwa hivyo Mheshimiwa naomba mfanyabiashara huyu asaidiwe apate eneo zuri ili na yeye apate moyo zaidi kutusaidia katika nchi yetu hii ya Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa suala la Bandari kwa kweli linasikitisha hawa wafanyakazi wetu wanafanya kazi kubwa masaa 24 au masaa kumi na mbili zaidi, lakini wanakuwa hawapewi hata posho. Kwa hivyo kitu hiki Mhe. Spika, naomba Wizara iwaangalie sana wafanyakazi wetu angalau wajaaliwe posho ili kuwapa motisha zaidi na kufanya kazi zao kwa vizuri kabisa. Kwa sababu hawajali muda wao wanakuwa usiku, mchana wanaendelea na kazi zao.

Mhe. Spika, sasa nigusie kidogo Mamlaka ya Uwanja wa Ndege. Kama tunavyojua Mamlaka ya Uwanja wa Ndege ni chanzo kikubwa sana kupata vyanzo vya fedha kwa serikali yetu. Kwanza nimpongeze sana Mkurugenzi wa Mamlaka ya Airport kwa juhudi yake kubwa aliyochukua. Lakini cha kusikitisha zaidi

Mhe. Spika, Kamati yako ilikwenda kuangalia maeneo mbali mbali ya maeneo ya Mamlaka ya Airport lakini tukakuta matatizo makubwa yapo hasa hasa ukitizama suala la X Ray *machine, detector machine*, hivi vifaa vichache kama *X Ray machine* iko moja tu pale kwa ajili ya mizigo iliyokuja wageni wetu, lakini inakuwa matatizo na msongomano mkubwa sana kwa wageni wetu.

Kwa hivyo naomba kupitia Wizara suala hili lifanyiwe haraka kwa sababu ni muhimu sana kama tunavyojua dawa za kulevya zinaweza zikapitishwa pale, mambo ya ugaidi anaweza akafanyia pale. Kwa hivyo vifaa kama tukivipata vitatusaidia kwa nchi yetu kuwa na usalama zaidi na kujipanga vizuri sana kwa ajili ya watu ambao hawaitakii mema nchi yetu.

Mheshimiwa pia Kamati yako imeangalia sana suala la vifaa vya moto *fire tender improvement* vifaa hivi pale *airport* viko vichache sana sana, hata likitokezea suala la moto basi itakuwa mtihani mkubwa kuweza kufanikisha suala hili au kuweza kulitatua suala la moto. Kwa hivyo naomba kupitia Wizara Mheshimiwa naomba suala hili pia lifanyiwe ufumbuzi haraka sana.

Mheshimiwa tatizo kubwa pia la Mamlaka ya Airport wale wafanyakazi wetu kwa kweli sekta hii inatakiwa taaluma kubwa hasa huu uwanja wa ndege kwa sababu mambo yote yanatakiwa kwenda kwa utaalamu, *computerize* kila kitu, kwa hivyo hawa wafanyakazi wetu hawapati masomo kwenda kusoma kuongeza taaluma zao. Bado wapo kwenye hali ile ile ya miaka kumi ya nyuma. Kwa hivyo naomba Mhe. Spika, kwa kupitia Wizara ya Mawasiliano, Mamlaka ya Uwanja wa Ndege, hawa vijana wetu wapelekwe kupata taaluma zaidi ikiwa nje ya nchi, japo Tanzania Bara wakaongeze taaluma ya hii kuendesha Mamlaka ya Uwanja wa Ndege.

Mhe. Spika, hili suala la baadhi ya wananchi kwa upanuzi wa *airport*, kuna baadhi ya wananchi wanalalamika sana sana hawajapata mafao yao ya kulipwa kwa ajili ya mradi huu mpya wa *airport*. Kwa hivyo wanaomba Mhe. Waziri kidogo hili aliangalie hawa wananchi wanalalamika sana kwa ajili ya mafao yao ili walipwe tuendelee na mradi wetu mkubwa huu wa *airport*.

Mhe. Spika, la kusikitisha sana sana suala la *airport* ya Pemba, kama ripoti inavyoeleza ripoti makini haijaficha kitu humu, suala la *airport* ya Pemba Mhe. Spika, iko hali mbaya, ukiangalia ubovu wa trekta, majengo, *fence* hata taa ya kurukia ndege Mhe. Spika, haziwaki wakati wa usiku. Kwa hivyo hili Mheshimiwa ni tatizo kubwa. Ukiangalia pia katika miundombinu ya umeme au nishati utakuta hata jenereta pia hamna kwenye uwanja wa ndege ule. Kwa hivyo inakuwa ndege zinazokwenda usiku itakuwa hali gani pale Mhe. Spika.

Kwa hivyo naomba Wizara ichukue juhudi kubwa sana kuhusu suala la airport yetu ya Pemba, kwa sababu *airport* nayo muhimu, hasa katika eneo la jioni Mhe. Spika, katika eneo la Pemba mwenyewe nishakwenda nishakaa, kwa kweli jua linakupiga mpaka pale unapokaa sehemu ya kuondokea abiria pale unapigwa na jua kweli kweli. Kwa hivyo Mheshimiwa hili ni tatizo kubwa kwa wananchi wetu na kama unavyojua nchi yetu imeguswa sana na vianzio vya utalii, watalii wengi wanakuja kutembelea Visiwa hivi. Kwa hivyo ninaiomba Wizara ifanye kila njia na bajeti yake iongezwe ili tuweze kufanikisha haya masuala.

Mhe. Spika, Kamati yako pia ilitembelea Mamlaka ya Uwanja wa Ndege kuna tatizo kubwa Mheshimiwa kwa kipaza Sauti kwa abiria wanaoondoka hamna, utakuta wanakaa pale hakuna chombo kinachotangaza muda huu tayari wa kusafiri basi masikitiko makubwa na kitu ambacho kidogo sana kwa nchi ziloendelea, na hasa sisi tunopiga hatua kubwa kwa kuendelea kwa nchi yetu hii, kwa hivyo naomba suala hili kwa sauti kwa *airport* lifanyiwe ufumbuzi ipatikane kwa haraka Mhe. Spika.

Mhe. Spika, cha kusikitisha zaidi pia suala *terminal* mpya *airport*, *terminal* ile Mheshimiwa haifai na imefeli kabisa. Sasa Mheshimiwa naomba kupitia Wizara tunapotia mikataba na hawa wakandarasi hebu tuangalieni vizuri kwa sababu wafadhili wanaotupa hizi pesa, hawatokuja tena mara ya pili kusema nakupeni pesa nyengine. Kwa hivyo fedha zimepotea Mheshimiwa na lile jengo halifai sasa. Sasa unakuta tatizo kubwa kwa nchi yetu ya Zanzibar Mheshimiwa hawa wafadhili hawatokuja kila mara kutusaidia kama tutakuwa tunapoteza pesa kwa wakandarasi waongo na waliokuwa si wa kweli kazi kuja kutafuta fedha za watu wanyonge katika nchi hii.

Mhe. Spika, na hili nalo nataka nisisitize kidogo wafanyakazi wa *airport* pia wapatiwe posho muda wanaofanya kazi ni mkubwa hauna masaa, saa nyengine usiku mchana kwa hivyo naomba Mamlaka kupitia Wizara iangalie suala la posho kwa wafanyakazi wetu wananchi wetu.

Mhe. Spika, kwanza nilipongeze sana Shirika la Meli, nimpongeze Mkurugenzi, kwa utekelezaji wake mzuri. Mheshimiwa Shirika la Meli na Uwakala lina tatizo moja kubwa sana Mheshimiwa. Mheshimiwa tunajua karibuni tulisema tutanunua meli mpya kwa kuondosha usumbufu wetu wa hapa Zanzibar na Pemba, usafiri wa wananchi wetu lakini cha kusikitisha zaidi Mhe. Spika, ule mkataba mpaka leo haujasainiwa. Na ukienda katika Taasisi za Serikali unaambiwa bajeti yote ishakatwa kwa ajili ya ununuzi wa meli. Sasa Mhe. Spika, hizo pesa ziko wapi na kama hizo pesa zipo zishakatwa hiyo meli mkataba huo haujasainiwa. Naomba Mhe. Waziri hili anipe ufafanuzi wa kina kabisa kwa faida yangu na faida ya wananchi wangu wa Jimbo la Bububu.

Mhe. Spika, niingie kidogo kwenye Idara hii ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Wizara yake kwa ujumla kwa kilio kikubwa kwa wananchi wangu wa Jimbo la Bububu pale kwa Hanzar walikuwa kilio chao cha siku nyingi walikuwa wanataka kifusi lakini ninashukuru Mhe. Waziri kwa sasa na Wizara yako kwa ujumla, ile kazi ya kifusi ishaanza kutiwa pale na jana nilikwenda kuangalia Mhe. Waziri nikaona kazi inaendelea na wananchi wamefurahi sana na wamenipa pongezi zao rasmi kabisa nikuletee kwa Baraza hili tukufu kukwambia wanashukuru sana kwa kazi yako nzuri na ambayo itawaondoshea usumbufu mkubwa.

Lakini Mhe. Spika, nigusie kidogo suala la misingi hii inayojengwa Kijichi njia ya kwenda Polisi kwenda Kijichi Juu. Mhe. Spika, masikitiko makubwa ile misingi imejengwa sijui kwa madhumuni gani, sasa kama hizo fedha zipo tayari za kujenga misingi ile au bado, lakini kwa kweli misingi imejengwa, hamna maendeleo yoyote, kwa kweli wananchi wanapata shida sana kwa misingi ile hata gari kuingia eneo la Kijichi haiwezekani. Sasa kweli Mhe. Spika, hili suala naomba Mhe. Waziri katika Wizara atuangalie vizuri kabisa kwa sababu wananchi wanalalamika kwa suala hili, kweli tunawatengenezea miundo mbinu lakini wamalizie tuwapatie urahisi kupita kwenye njia zile bila ya usumbufu wowote.

Mhe. Spika, niingie kwenye Wizara ya Ardhi. Kwanza niipongeze Wizara na watendaji wote wa Wizara kwa umeme mpya na wa uhakika. Mhe. Spika, Shirika la Umeme Shirika hili ni muhimu sana kwa miundombinu yetu ya hapa Zanzibar. Lakini Mhe. Spika, Shirika hili lina upungufu; wafanyakazi ni wachache, ukitizama hata zile kazi sasa zinazorota kutokana na wafanyakazi wanakuwa kidogo kutenda zile kazi zao kwa haraka haraka kwa sababu Shirika lina wafanyakazi kidogo. Kwa hivyo naomba Mhe. Waziri hili waliangalie waongeze wafanyakazi kwa sababu kazi hii inataka taaluma, kazi ya umeme sio kazi ya mchezo mchezo ni kazi ambayo inataka watu ambao wanaoijua na wanaoifahamu vizuri kazi hii.

Mhe. Spika, pia cha kusikitisha Kamati yako ilikwenda kwenye Shirika la Umeme ikaona vifaa vya kutendea kazi pia kidogo. Tukitizama kama gari za kufanyia kazi, viatu vya kupandia nguzo za umeme juu viatu hamna. Vipuri ukitizama kasoro hasa ukitizama suala la *transformer* utakuta ikiharibika *transformer* hamna ya ku-*replace* nyengine. Kwa hivyo Mheshimiwa hili naomba kwa kupitia Wizara, Waziri kuangalia suala hili vizuri sana kwa sababu ni muhimu kwa nishati yetu hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, baadhi ya Taasisi kama Wajumbe wengine wamegusia kidogo Shirika la Umeme limekuwa na malalamiko makubwa sana ya madeni ya Taasisi za Serikali. Hizi Taasisi za

Serikali zinakuwa nyingi hawawalipi hawa Shirika la Umeme. Kwa hivyo Mhe. Spika, na kama watakuwa hawalipi na huduma zitazorota lakini taasisi kubwa sana ambayo inadaiwa pesa nyingi kwa sasa ni hii Mamlaka ya Maji *ZAWA*, hawa wanadaiwa pesa nyingi Mhe. Spika. Kwa hivyo naomba kupitia Waziri, Wizara ilishughulikie suala hili kwa sababu kuna sehemu za vianzio vya maji unakuta hata huo umeme hamna wana madeni makubwa kwa hivyo unakuta kazi inakuwa inakwenda vibaya kidogo kutokana na madeni yao waliyokuwa nayo mengi.

Mhe. Spika, vituo vya kuuzia umeme, vituo ni kidogo sana kwa Zanzibar, kwa hivyo wananchi wanapata usumbufu mkubwa, nilikuwa naomba kupitia Wizara, Waziri vituo viongezeke kidogo kutokana na watumiaji wa umeme wako wengi kwa sasa.

Mhe. Spika, pia kamati yako ilipata baadhi ya malalamiko kutoka Kisiwa chetu cha Pemba, wafanyakazi wa Pemba taaluma yao iko chini sana au ndogo hawapati mafunzo ya kila muda kwenda kusomea kuongeza taaluma hii. Kwa hivyo naomba Mhe. Waziri hii taaluma wafanyakazi wa Pemba wapewe taaluma nzuri ya umeme kwa sababu Pemba kuna umeme wa uhakika kabisa kama sisi tulivyokuwa nao hapa. Kwa hivyo naomba wafanyakazi wetu wa Pemba pia wapewe taaluma nzuri na wapewe nafasi za masomo.

Mhe. Spika, sasa niingie kwenye Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. Kwanza nimpongeze sana Mkurugenzi wa Mji Mkongwe kwa jitihada yake anayofanya kubwa anajitahidi kwa kuuweka mji wetu kama tunavyojua sasa mji wetu uko sasa katika *UNESCO*. Mheshimiwa kama tunavyojua sasa hivi Mji mkongwe umevamiwa sana sana nyumba zinafanywa hoteli, kila nyumba sasa hivi imekuwa ya biashara na ule mji kama tunavyojua Mhe. Spika, ni mji ambao wa kitalii kwa hivyo tukibadilisha nyumba zote zikiwa za hoteli zile, ninafikiri hata ule uhalisia wake ule Mji mkongwe utaondoka.

Kwa hivyo naomba Wizara husika inayotoa vibali vya kulaza wageni viangalie kwa kina kama nyumba hii kweli inastahiki au vipi, kama haistahiki basi naomba Mhe. Spika, suala hili la kutoa vibali mpunguze sana kwa Mji mkongwe, kwa sababu Mji mkongwe ni mji wa hifadhi wa dunia kama tunavyojua *UNESCO*. Kwa hivyo tukiuharibu mji huu tutakosa mapato hata katika sekta ya serikali ambayo tunategemea sana Utalii.

Mhe. Spika, suala la Bustani ya Forodhani. Suala la bustani ya Forodhani kamati yako ilitembelea na iliangalia na ilifanya ziara nzuri kabisa na wafanyakazi wote na wafanya biashara. Kwa kweli bustani hii Mheshimiwa kama ninavyojua ni ufadhili wa *Agakhan foundation* kwa pesa nyingi sana, lakini cha kusikitisha sana Mhe. Spika, bustani hii hata majani sasa hivi yanakauka. Ukitizama usafi umekuwa mdogo sana. Mhe. Spika, hata hawa wafanyakazi au wafanyabiashara wa hapa eneo hili la bustani ya forodhani wanashindwa kutoa kodi kutokana na wao wanalalamika kwamba hawapati maji.

Sasa kwa vile hawapati maji hata biashara zao zinakuwa ngumu kuzifanya Mheshimiwa. Kama tunavyojua hawa wananchi wetu wafanyabiashara ndogo ndogo ndio wapiga kura wetu Mheshimiwa, kwa hivyo tuwaangalie na wao kuwapunguzia hizi gharama, kuwapunguzia kodi, ukiangalia tangu Mhe. Rais anategemea kura za hawa wafanyabiashara wadogo wadogo mpaka Mhe. Diwani. Kwa hivyo kama hatujawaangalia vizuri hawa wafanyabiashara wadogo wadogo Mheshimiwa na malalamiko yao itakuwa hatuwatendei haki. Kama kuna uwezekano Mamlaka

ya Mji Mkongwe kupitia bustani ya forodhani wapunguziwe hata kodi wanalalamika pia kodi kubwa hawa wafanyabiashara sasa hivi.

Mhe. Spika, niingie kidogo nigusie Wizara ya Ardhi Makaazi, Maji na Nishati, Mamlaka ya Maji *ZAWA*. Mheshimiwa kama ninavyojua sekta hii ya maji au suala hili la maji kweli ni tatizo kubwa sana kwa Zanzibar. Kwa kweli kila pahala unapokwenda sasa hivi malalamiko makubwa ni maji. Kama tuanzie vianzio vyetu vya maji vikubwa nitoe mfano hiki kimoja kilikuwa chemchem ya Mwanyanya. Mhe. Spika, chemchem ya Mwanyanya mimi nilikwenda kule kuangalia nikasema kwa nini wananchi wangu hawapati maji eneo la Mwanyanya itakuwaje chemchem iwe hapa na maji yasipatikane Mwanyanya.

Kwa kweli Mheshimiwa nilipoenda nikaona yale maji yako chini sana na hayatoshi kwa kuhudumia wananchi wa pale. Lakini tu nimeambiwa kwa maji haya Mheshimiwa yanakwenda Saateni na kuwahudumia watu wa Mji Mkongwe. Kwa hivyo tukisema tuyachukue na maji haya tuwape na wananchi wako wa Mwanyanya kwa kweli hili suala gumu. Kwa hivyo tumeridhika Mheshimiwa haya maji yanakwenda Saateni na kuwahudumia wananchi wa Mji Mkongwe.

Mhe. Spika, kamati yako tulikwenda ziara moja sehemu inaitwa Kishangwe. Kwa kweli Mheshimiwa sehemu hii tulipokwenda ilikuwa na maji mengi sana, lakini la kusikitisha zaidi kuna sehemu ilikuwa kuna *spare* ndogo tu ya *air vague* gharama yake kama laki sita lakini ilikuwa hakuna *spare* ile ya kufungwa kubadilishwa kwa sababu tatizo kubwa ilikuwa hakuna *radio call* pale ya kuwasiliana mjini, hakuna usafiri kama gari kwa kweli Mhe. Waziri hilo tuliangalie sana kutokana na vifaa vyetu hivi muhimu sana kwa usafiri kwa ajili ya vyanzo vya maji kupata usafiri na wananchi wetu wapate huduma nzuri sana.

Mhe. Spika, nimalizie kidogo muda unakwenda mbio kidogo. Mhe. Spika, kamati yako ilipata safari ya kwenda Arusha.Kwa kweli Mheshimiwa nilifarijika sana na kwenda Arusha kuangalia vyanzo vyao vya maji, lakini tukisema tuwaige wenzetu pia kwa sababu wenzetu kisima kimoja wanachimba kwa milioni mia mbili. Kwa hivyo inakuwa shida kubwa na serikali yetu hii kwa sasa kufanya visima hivyo kwa milioni mia mbili kuvipata sio rahisi, lakini cha kumshukuru Mungu, Mwenyezi Mungu kutusaidia kwa visima vyetu hivi vinatusaidia hapa na pale vya kupata maji sio mengi lakini yanakuwa ya kutosha kidogo. Lakini naomba suala la maji Mhe. Waziri ni sekta muhimu na litiwe uzito mkubwa sana katika nchi yetu.

Mheshimiwa kwa kuokoa muda sijamaliza yote lakini kwa kuokoa muda nakubaliana na hotuba hii asilimia mia juu ya mia pamoja na wananchi wangu wa jimbo la Bububu. Ahsante.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, awali ya yote ninamshukuru muumba wetu kwa kutujaalia kuwa hai na uzima tukiwepo Barazani hapa tukiendelea na shughuli ambazo wananchi wa Zanzibar wametuleta kwenye fani. Nikushukuru na wewe Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia ripoti hii ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi na vile vile nimshukuru Mhe. Mwenyekiti wa Kamati hii jana kapewa sifa na cheo cha kuwa mwanamme jasiri ili aambatane na Mhe. Fatma Fereji kwamba yeye mwanamke jasiri, na Baraza hili mwanamme jasiri Mhe. Makame Mshimba Mbarouk kwa ripoti yao.

Mhe. Spika, kwa sababu ya muda naomba moja kwa moja niende katika mambo ambayo nataka kuyachangia. La jumla niipongeze Kamati kwa ripoti yao nzuri kabisa na katika Kamati ambazo zimeweka viwango vya ripoti zake basi moja ni Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi. Hata ripoti yao ya mwaka jana ukiitizama inapokwenda Idara kwa Idara inachambua maeneo ya msingi ambayo inayaona na kutoa maoni na ushauri kadiri inavyohitajika.

Sasa Mhe. Spika, yapo maeneo ambayo yapo ndani ya ripoti lakini yapo vile vile ambayo tumeyazungumza katika kipindi cha bajeti mwaka jana naomba vile vile niyachangie.

La kwanza Mhe. Spika, naomba nianze na Jimbo langu la Mji Mkongwe. Mhe. Spika, katika kushajiisha maendeleo serikali kwa nia nzuri kabisa ilianzisha mifuko ya maendeleo ya Jimbo kwa Wabunge na Wawakilishi. Mhe. Spika, kwa upande wa Mji Mkongwe mfuko wa maendeleo ya Jimbo hasa kwa upande wa Mbunge katika eneo hili, ilitoa shilingi milioni arubaini kuipa Wizara ya Mawasiliano na Miundombinu ili vibarabara vichache vya Mji Mkongwe viweze kutengenezwa.

Mhe. Spika, Mji Mkongwe ndio sura ya Zanzibar kwa sababu ndio makao makuu ya serikali, lakini ndio kituo kikubwa cha harakati za kiuchumi ukiwemo utalii tunaoutegemea sana kwa mapato yetu. Serikali kwa jumla ilikuwa sote tunapiga dana dana tu, tukiwaambia Wizara ya Mawasiliano wanasema barabara hizi wanaohusika ni Baraza la Manispaa. Mwisho mfuko wa Jimbo ukaamua kuchangia gharama si ndogo milioni arubaini ili barabara zile zijengwe. Ilikuwa pamoja na maeneo yaliyokubaliwa ni barabara ya Mkunazini; kipande kidogo tu kile, barabara ambayo imeanzia maeneo ya Muembetanga kuteremkia Mtendeni, Vikokotoni hadi ilipo Benki ya Barclays. Lakini pia baadae katika mazungumzo yangu na Uongozi wa Wizara nikaomba ajumuishe na akakubali kipande kidogo kile cha kutokea Malindi kwa Tausi hadi pale ilipokuwa Malindi *cinema*.

Mhe. Spika, nasikitishwa sana kwamba ule ustaarabu wangu labda au wetu wa Mji Mkongwe unatuponza. Kwa sababu suala hili na wewe mwenyewe shahidi sijalileta nikalipigia kelele sana kwa sababu nilikuwa nazungumza na wakubwa wa Wizara hii. Na katika jimbo ambalo limeweka rekodi kwa kutoa kiwango kikubwa cha fedha Mheshimiwa kuchangia masuala ya ujenzi wa barabara, tunajua barabara inajenga serikali lakini msaidie zile gharama ndogo ndogo basi ni Jimbo la Mji Mkongwe. Lakini tunasikitika Mhe. Spika, kwamba sijui kwa sababu linawakilishwa na Ismail Jussa na Mhe. Sanya au vipi, kwamba kuna majimbo wamechangia milioni tano lakini barabara zao zimejengwa barabara hizi hizi ndani ambazo si barabara kuu. Lakini sisi ambao tumetoa milioni arubaini, inaonekana kuna hujuma ya makusudi dhidi ya Jimbo la Mji Mkongwe.

Sasa nataka kuwaambia tu tunawakumbusha, nimepewa ahadi nyingi Disemba, Januari kabla ya Aprili, juzi Naibu Waziri Mhe. Gavu ananambia liachie kabla ya bajeti nikamwambia siliachii kwa sababu tumeshasema sana Mhe. Waziri ajue nimeshawahi kumwambia akanambia tunasubiri lami ije, kile kipande cha Mkunazini kimejengwa lakini tumeachiwa mashimo kwenye makaro mpaka leo yanasababisha mpaka ajali kwa watembeaji wa vyombo mle ndani. Lakini nasema kwa nini tusimaliziwe mbona kuna Majimbo mengine yametoa shilingi milioni tano Mhe. Spika wamemaliziwa barabara zao. Nawaambia kabisa kuwapa ilani, hapa tunawapa miezi

miwili kama hatukuziona barabara zinakamilishwa ikifika Juni/Julai wakati wa bajeti patakuwa hapatoshi katika wizara hii, nawaambia kabisa.

Kwa sababu tumetoa muda muda wa kutosha miaka miwili na nusu na mifano ipo wengine ambao wamejengewa. Hili haturidhiki kabisa Mhe. Spika, tunataka kuja kuona mambo haya yanakamilishwa ndani ya muda huu wala hatupokei ahadi nyengine yoyote ikifika mwezi wa Juni na Julai.

La pili Mhe. Spika, naomba nichangie eneo la Mamlaka ya Viwanja vya Ndege. Kwanza kuna jengo lile la abiria. Mhe. Spika, leo nimesikia kauli mpya ya Kiingereza ya Mhe. Waziri, kasema tutalimaliza *once and for all,* nikasema hii nafikiri imeondoka kutoka katika kuwa vile *be serious* sasa tunakwenda katika *once and for all*.

Lakini tunachosema Mhe. Spika, kwamba hata hili tangu Baraza hili limeapishwa baada ya Uchaguzi Mkuu uliopita suala hili limekuwa moja katika linalozungumzwa sana hapa, kwa hivyo ahadi zimeshatuchosha sasa hivi tunasema wakati wa bajeti tupewe ripoti hapa ya suala hili. Leo Mhe. Waziri katwambia kwa maelezo ya jumla jumla tu, tunataka tuje tuone hasa hatua gani zinachukuliwa, ule usanii wa kwamba sijui kuna *Design and Build* ambao mahodari sana wakubwa wa wizara hii kuja kutusomesha hapa tunawaambia tutawarejeshea wenyewe ikifika Juni na Julai kama hatukuona hasa kunachukuliwa hatua gani juu ya jengo lile na hasara ambayo wamewatia wananchi wa Zanzibar kwa sababu fedha ile ni ya mkopo inabakia katika shingo za wananchi wa Zanzibar wao waweze kulilipa kwa miaka mingi.

Mhe. Spika, katika Mamlaka ya Viwanja vya Ndege vile vile kuna suala la ujenzi uanoendelea pale, ukienda pale Mhe. Spika, hata wale wanaotumia huduma wanakwambia, kwamba ujenzi ule namna unavyofanyika unaacha maswali mengi sana. Kwanza hakuna kutolewa zabuni katika ujenzi ule, kuna ujenzi wa watu wako mifukoni ndio wanaopewa kazi ile, lakini matokeo yake nini, matokeo yake ujenzi unakuwa chini ya viwango.

Kuna vile vishirika vinavyotoa huduma za ndege zile ndogo ndogo wamehamishwa walikuweko yamejengwa majengo hapa mbele ukiingia kwenye barabara. Lakini Mhe. Spika, siku moja nilikwenda pale kulikuwa kuna mvua wala si kubwa maji yote yamo ndani ya ofisi zile, nikasema basi hata kuongezwa hiki kipaa, wakasema wee acha tu hapa wakubwa wana watu wao ndio waliopewa *tender* matokeo yake ujenzi ndo wa aina hii ambaoumejengwa.

Lakini sio huo tu Mhe. Spika, siendi jambo moja moja wakati wa bajeti ukifika tutakuja kuyazungumza kwa urefu lakini tuseme kuna masuala ambayo yanahitaji majibu katika ujenzi unaoendelea pale, kwamba taratibu gani zinafuata kunatolewa *tender*, viengo vinahakikishwaje, na hii nadhani hata Kamati ya *PAC* wanapaswa waje waliangalie kwa undani kabisa.

Mhe. Spika, tumewahi kusema mara nyingi hapa kwamba Mamlaka ya Viwanja vya Ndege sio uwanja wa ndege mmoja tu, kuna na uwanja wa ndege ulioko Pemba. Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano alikuwa ni mmoja katika mtetezi mkubwa alipokuwa upande wetu sisi huku, sasa leo ana dhamana. Na mwaka jana wakati wa bajeti aliahidi kwamba angalau lile la taa atalifanyia kazi binafsi, sasa tunataka tulisikie kwamba Mamlaka hiyo ya Viwanja vya

Ndege mbona imeshughulika hapa au hapa ndio penye ulaji kule hakuna kitu kwa hivyo kumeachiwa kama kulivyo. Tunaomba maelezo katika hilo Mhe. Spika.

Mhe. Spika, eneo jengine katika Uwanja wa Ndege ni suala la fidia katika upanuzi ule unaoendelea. Tuliwahi kulizungumza hili mwaka jana na tukaahidiwa na uongozi wa wizara kwamba utalifanyia kazi, lakini bado yako malalamiko ya wananchi na mimi naomba wizara ilifuatilie hili. Mimi ninayo barua hapa ya watu wawili, Yakoub Moh'd na Farida Abdalla Moh'd, wameandika barua kwa Makamu wa Pili wa Rais kulalamika na kutoridhika na utendaji wa kamati ambayo iliteuliwa kutathmini kwamba hapakuwa na uwazi.

Mhe. Spika kuna watu na wametoa mfano humu, naomba nimsomee kifungu kimoja tu kinasema, "kwa mujibu wa makadirio yetu shamba letu linaweza kukatwa takriban viwanja vya nyumba 30, ikiwa kuna watu kwa mfano Sadifa, Aziz Juma wamelipwa shilingi milioni kumi kwa kiwanja kimoja au wengine waliolipwa zaidi yetu. Kwa mfano, Bi Hidaya shilingi milioni thamanini, Ali Mwinyi shilingi milioni sabini na tano, wakati kiwanja chetu ni kikubwa ukilinganisha na vyao". Wao wamepewa shilingi milioni arobaini tu eneo ambalo linaweza kutoka viwanja 30.

Kwa hivyo, naseme bado kuna malalamiko mengi juu ya suala zima la fidia katiak hili naomba vile vile waziri atapokuja kufanya majumuisho anipatie maelezo.

Mhe. Spika, eneo jengine ambalo limenigusa katika ripoti ya kamati ni suala la Idara ya Leseni na Usafiri, agizo nambari tano ambalo liko katika ukurasa wa 122. Mhe. Spika, katika ripoti ya kamati agizo nambari moja, kamati imeeleza kuwa kuna changamoto kwa baadhi ya vijana ambao wazazi wao wana nyadhifa serikalini, huzitumia nafasi hizo wanapokwenda kufanya mitihani kwa ajili ya kuomba kupata leseni kwa kutoa kauli zisizoridhisha kwa wafanyakazi wanaosimamia shughuli hiyo.

Mhe. Spika haya nadhani yachukuliwe hatua, si mambo ambayo yanapendeza kuwa mpaka leo kuna watu wanatumia wazee wao kwa sababu ni wakubwa kuweza kufanya wanavyotaka. Lakini isitoshe kuna suala la ukusanyaji wa mapato, ukisoma ripoto ya waziri ukurasa wan ne kifungu nambari tano, kuna kutokuelewana pale inaonekana baina ya *ZRB* na Idara ya Usafiri na Leseni juu ya nani mwenye mamlaka ya kutoa leseni na kukusanya mapato. Hebu hili serikali ituwekee wazi hapa, nani hasa muhusika. Kwa sababu *ZRB* ni mamlaka ya serikali, Idara ya Usafiri na Leseni ni idara ya serikali, kwa nini hakuna kuelewana katika serikali moja juu ya nani hasa mwenye kuhusika. Suala hili nilikuwa naomba maelezo.

Mhe. Spika, eneo jengine ambalo sikulisikia maelezo yake humu haliwemo katika kamati, lakini tulipokua tukichangia tulililotolewa hoja hapa na nakumbuka nilikuja na mchanganuo kabisa hapa kwamba kuna ufisadi wa hali ya juu katika ujenzi wa barabara hasa kutokana na gharama zake ambazo zinakuwa zinaongezwa. Nikaja na mfano wa barabara hasa kutokana na gharama zake ambazo zinakuwa zinaongezwa. Nilikuja na mfano wa barabara hasa ile ya Amani – Mtoni. Sasa nilitegemea nione hatua zimechukuliwa kiasi gani kwa suala lile, lakini nilichokiona katika ripoti hii Mhe. Spika, nimesikitishwa kila pahala ushauri umepokelewa, kamati imepokea ushauri, wizara itafanyia kazi ushauri. Sasa nikasema hii ndio ripoti ya utekelezaji ya wizara.

Kwa hivyo, Baraza lako Mhe. Spika, kazi yake kushauri na serikali kujibu kwamba ushauri umepokelewa ndio mwisho wa hadithi huu si utendaji mzuri Mhe. Spika, hauoneshi *seriousness* ile Mhe. Waziri aliyokuwa akitwambia hatuioni katika majibu ya hoja za kamati kwa mwaka uliopita.

Mhe. Spika, la mwisho katika Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano niliikuwa naomba maelezo vile vile. Mwaka jana katika ripoti lilitajwa na mwaka huu limetajwa na Wajumbe wako wengi tulihoji katika bajeti, katika kujadili ripoti ya mwaka jana, kuna mamlaka hizi za Muungnao ambazo zinasimamiwa na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. Kuna mamlaka ya Shirika la Posta (*TPC*), kuna Kampuni ya Simu (*TTCL*) kuna Mamlaka ya Usafiri wa Anga (*TCAA*), kuna Mamlaka inayosimamia Mawasiliano (*TCRA*) tunataka kujua tumehoji mara ngapi, mapato ya Zanzibar yako wapi kutoka mamlaka hizi.

Hapa Mhe. Spika, niseme kidogo kamati imenisikitisha, imetoka katika kudai haki za Zanzibar mara hii sikuwafahamu wanakuja wanataka mamlaka hizi zisaidiwe na serikali. sasa ripoti hii ni kwa ajili ya Serikali ya Zanzibar najiuliza kamati katika Serikali ya Zanzibar baada ya kupewa haki zake sasa bado itoe hicho ilichokuwa haipewi tunachokusanya wenyewe pia iwapelekee mamlaka hizi kusaidia shughuli zao? Mimi sikuelewa Mhe. Spika. Kwa hivyo, bado nataka tupewe maelezo hapa kuna mapato na ni mapato mengi.

Katika eneo moja ambalo linachangia mapato makubwa katika Serikali ya Muungano ni Mamlaka ya Mawasiliano (*TCRA*). Ninaamini vile vile katika Mamlaka ya Usafiri wa Anga, *share* ya Zanzibar iko wapi Mhe. Spika, au ndio kama kawaida punda afe mzigo wa bwana ufike? Kwa sababu Wazanzibari kila siku tunaambiwa tunabebwa lakini kusema kweli inaonekana sisi ndio tunaowabeba Watanganyika kuchukua mapato sisi tukaendelea kuambiwa wewe suburi tu iko siku utanyonya tumekuwa kama watoto wa kuku. Naomba kuelezwa mapato ya mamlaka hizi Zanzibar tumefikia wapi katika kupata haki zetu.

Mhe. Spika, haraka haraka niende katika Wizara ya Ardhi, la kwanza ni suala la mafuta liko katika ukurasa wa 35 wa ripoti ya waziri ambayo kaisoma Kaimu Waziri. Mhe. Spika, imesema wizara kuweka wazi suala la mafuta hapa Zanzibar, serikali imetujibu kwamba mazungumzo yanaendelea. Kamati Maalum ya Ufundi ikiongozwa na Wanasheria Wakuu wa SMZ imeteuliwa katika kufanya matayarisho hayo.

Sasa mimi sina matatizo na mazungumzo ya Kamati Maalum ya Ufundi kuendelea, nasikitika tu kwamba bado ile heshima ya chombo hichi ambacho kilifanya maamuzi mazito, makubwa chini ya uongozi wako Mhe. Spika, mwaka 2009 bado leo mwaka wa nne hakuna ambalo tumelipata bado yanaendelea mazungumzo tu. Mazungumzo, mazungumzo, na wenzetu hodari wa kusema linazungumzika. Ukishasikia Tanganyika unaambiwa hili linazungumzika ujue ndiop tena limekaliwa kitako hilo kwa maneno ya Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika.

Mhe. Spika, mimi nataka kujua kwamba wakati haya mazungumzo yanaendelea nini kinaizuwia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuleta zile sheria ambazo tumetaka ziletwe katika Baraza hili. Sheria ya Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta Zanzibar na Sheria ya Kuanzisha Mamlaka itakayosimamia leseni na uendeshaji au *regulation* ya sekta hii ya mafuta.

Vile vile matayarisho mengine ya kiujenzi wa taasisi hizi yamefikia wapi hatupati chochote kama *feedback* kwa Baraza hili, hatupati maelezo kwamba lile vuguvugu la kimapinduzi hasa lililokuweko mwaka 2009 na kwamba limepozwa hivi hivi hakuna chochote unachokisikia katika Baraza lako juu ya utekelezaji. Mhe. Spika, maelezo haya bado ni *very shallow*, hayana uzito yanayoweza kuridhisha Baraza hili kwamba kweli serikali inasimamia maamuzi yale ya mwaka 2009. Tunataka kusikia tumefikia wapi.

Mhe. Spika, na hili nalisema kwa sababu hivi tunavyozungumza Rais wa Jamhuri ya Muungano yuko Uholanzi na tunajua kwamba Waziri wetu wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ni sehemu ya ujumbe huo, tusije tukasikia tena katika kuchukuliwa huko ikawa ni katika kwenda kutafutwa maneno mengine kuja kupewa lugha nyengine kuwa mazungumzo yanaendelea tunataka kuona hatua mazungumzo yashatutosha.

Mhe. Spika, niende maeneo mengine, la kwanza ni viwanja katika Idara ya Ardhi na Idara ya Upimaji na Ramani. Mhe. Spika, kuna malalamiko mengi sana ya wananchi kwamba wanaomba viwanja wengine mimi katika jimbo langu ninao wameniletea nakala niliwahi kuzipeleka katika wizara, wameomba tangu 1980 Mhe. Spika, mpaka leo hawajapewa viwanja na viwanja vinagawiwa.

Lakini unaweza kukuta mtu mmoja au wawili wao wanaendelea kujilimbikizia viwanja tu, na wengine kuna mtindo katika idara hii watendaji wenyewe pale na wafanyakazi kujigawia viwanja halafu baadae ndio vikawa vinafanywa biashara mitaani huko, lakini wananchi ambao wameomba tangu 1980 mpaka leo hawajapewa. Nataka maelezo kutoka katika wizara juu ya suala hili.

Lakini vile vile naomba maelezo kuna watu ambao walipewa nyumba za maendeleo za Michenzani na Marehemu Mzee Karume na ninayo barua ya mmoja wao hapa. Suala hili uongozi wa wizara huko nyuma uliwahi kuunda kamati chini ya Mkuu wa Mkoa kutathmini ili baadae kuzitambua wepi hasa ambao walipewa na Mzee Karume, mpaka leo suala hilo limeachwa njiani halikumalizwa. Tunaomba maelezo kutoka katika serikali suala hili limefikia wapi.

Mhe. Spika, la mwisho kabisa naomba nizungumzie Mamlaka ya Mji Mkongwe kwa ufupi tu. Hii Mhe. Spika, inahusu hasa Jimbo langu imetajwa katika ukurasa wa 118 na 119 ya ripoti hii. Mhe. Spika, kwanza nayaunga mkono mapendekezo takriban yote ambayo yametolea na kamati kuhusiana na suala hilo. Lakini naomba nisisitize kwa ufupi tu, kwanza suala la usafi katika Mji Mkongwe, inatia aibu inatia kinyaa, tumeshasema mpaka tumechoka katika Baraza hili, tunaahidiwa maneno mengi lakini Baraza la Manispaa limeshindwa kazi katika suala la kutunza usafi katika eneo ambalo ni uso wa Zanzibar.

Mhe. Spika, tunazungumzia utalii, sehemu kubwa za harakati za utalii kwa upande wa mjini ziko Mji Mkongwe, lakini mgeni anayekuja akakuta kila pahala kuna limbikizo la mataka, uvundo unatoa harufu anakuwa Balozi gani wa Zanzibar kwenda nje, tukiuliza hapo tutaambiwa wawakilishi watusaidie, mimi sikusanyi kodi. Watu wanatozwa kodi, maduka yanatozwa kodi mpaka shilingi elfu 29, tozo ya kusafisha mji, mahoteli yanalipa, nyumba za watu binafsi

zinalipa na Mji Mkongwe kama nisemavyo imekuwa kama ni ngo'mbe anakamwa anakamwa mpaka sasa hatoki maziwa tena anatoka damu, lakini ukija katika huduma uchafu umezagaa kila pahaka watu wa Mji Mkongwe wanataka kujua hizi kodi zao zinakwenda wapi, na kama Baraza la Manispaa limeshindwa basi watwambie.

Mimi kama Mwakilishi niko tayari kuwa-*organize* watu wakafanya usafi kama inavyotokea katika barabara ile ya sasa hivi ukipita safi, usiku kutoka Darajani mpaka Kilimatinde pale, barabara ya Mchangani. Lakini basi wakubali eneo lote la Mji Mkongwe tulisimamie wenyewe tukusanye sisi hayo mapato, sio wao wanakusanya mapato lakini huduma hawatoi lakini wananchi wakajitolea. Wananchi hawawezi wakajitolea wakati unamkamua pesa Mhe. Spika, watupe dhamana waone kama kutakuwa na uchafu Mji Mkongwe.

Mhe. Spika, nije katika Bustani ya Forodhani. Mhe. Spika inasikitisha, sasa hivi ukiona angalau inatizamika yale majani kwa sababu ya mvua hizi zilizokuja za masika, lakini ilikuwa majani yashapiga njano kabisa kwa sababu hata kule kumwagilia maji tumeshindwa, uchafu umerudi vile vile usimamizi wa zile kanuni ambazo zimeanzishwa na taasisi ambayo ilipewa mwanzo Mamlaka ile ya Aghakan kuwa wale watoa huduma pale kuvaa vizuri, wakavaa makoti meupe yale yote yameondoka. Tusiwalaumu watu au kulaumu wafanyabiashara si kweli, usimamizi kama mwananchi humsimamii hawezi kuwa na motisha ya kufuata sheria.

Lakini Mhe. Spika, pametajwa pia hapa, kwamba huwezi kutegemea yale yale, kwamba hao wanatozwa kila mwezi na kila siku wanapita watu kukusanya mapato kutoka katika vyanzo vyetu, lakini huduma za usafi wanaambiwa wafanye wenyewe. Sasa Mhe. Spika, huwezi kumtoza mtu pesa ukamwambia kwamba hii ni ya huduma za usafi halafu usafi afanye mwenyewe, ama umwachie afanye mwenyewe au ukikusanya fedha basi utoe hizo huduma.

Mhe. Spika, la mwisho katika Mji Mkongwe limetajwa katika kamati vile vile ni suala la maji. Kamati inasema kuwa Mamlaka ya Mji Mkongwe ishirikiane na *ZAWA*. Kama tunavyosema eneo ambalo ndilo linalotoa sehemu kubwa ya mapato katika nchi linapaswa lipewe kipaumbele. Hatukatai huduma za maji zilivyokuwa miaka ya nyuma kuna *improvement* fulani na tunapongeza hatua iliyochukuliwa. Lakini nadhani kuna haja ya kuangalia miundombinu hasa ya mabomba ya maji, kwa sababu kinachoonekana Mhe. Spika, unaweza ukakuta kwa mfano, kuna baadhi ya maeneo kama Mchangani unaweza kukuta maji ya zamu ya kima siku nne yanafika, lakini kunamaeneo kama mitaa ya Mbuyuni huku maji hayafiki, ukanda ndio ule ule.

Michenzani ukija wewe *block* nambari 8 kila baada ya siku nne tunapata maji na mimi naishi pale pale, lakini *block* nambari 6 kuna tatizo la maji na Mji Mkongwe ukienda ndio hivyo hivyo maeneo ya Mkunazini. Kwa hivyo, kunaonekana kuna tatizo, kuna maeneo yanapata na kuna maeneo hayapati, nadhani kuna haja ya kuangalia upya ule mfumo wa mabomba ya maji ambayo yapo pale.

Mhe. Spika, kuna mahoteli pale yanatoa huduma, eneo kama la Baghani kuna mahoteli mengi tu pale lakini kuna tatizo kuu la maji. Kwa hivyo, naiunga mkono hoja ya kamati kwamba kuna haja ya kuliangalia tatizo la maji katika Jimbo la Mji Mkongwe ili tuone kwamba hatua zinachukuliwa.

Mhe. Spika, nakushukuru na naikumbusha Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano nataka majibu ya uhakika kuhusu shilingi milioni arobaini tulizowapa na barabara zetu katika Mji Mkongwe. Nakushukuru sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kuna majina manne zaidi ya Mhe. Hamza Hassan Juma ambao sitamudu kuweza kuwapa muda kutokana na ufinyu wa muda wetu. Kwanza niombe radhi lakini pili kama kuna mambo yaliyo mazito na muhimu basi wawaandikie Waheshimiwa Mawaziri ili wapate kutoa ufafanuzi hapo baadae pamoja na Mwenyekiti wa Kamati.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwanza nakushukuru kunipa nafasi hii nikazungumza angalau mawili matatu katika kuchangia Ripoti ya Kamati. Mhe. Spika, mimi kwanza nataka niikubali moja kwa moja Ripoti ya Kamati na yale mapendekezo yao sina pingamizi nayo.

Mhe. Spika, kwanza nataka nianze moja kwa moja katika kuchangia ripoti hii kwa kumalizia pale alipomalizia Mhe. Ismail Jussa. Mhe. Spika, hata katika kamati yangu tulilishauri Baraza la Manispaa, Mhe. Spika sasa hivi mji mchafu na mchafu kweli kweli. Sasa tuliwashauri kwamba angalau zile siku za Jumamosi na Jumapili kutokana na upungufu wa mabari waliyokuwanayo waazime magari ya taasisi nyengine ambapo operesheni kama hizo zilikuwa zikifanyika katika kipindi kilichopita.

Kwa hivyo, tunaomba sana Mhe. Spika, suala la uchafu sio Mji Mkongwe tu kwenye majaa, sasa hivi majaa yameshawashinda Manispaa na wamekiri katika kamati kwamba kutokana na upungufu na uhaba wa magari waliokuwanayo hawana uwezo wa kuweza kuzitoa taka zote. Wametwambia wanaweza kuzoa asilimia 30 tu ya taka kwa kila siku je, hali ya mji wetu itakuwa vipi. Kwa hivyo, tunamuomba sana Mhe. Waziri ajaribu kuzungumza na taasisi nyengine ambao wanayo yale magari makubwa ili Jumamosi na Jumapili waweze kusaidia Baraza la Manispaa kwa ajili ya kuondoa taka katika mji wetu.

Mhe. Spika, baada ya kuunganisha hapo nataka nije moja kwa moja katika hoja. Mhe. Spika, mimi nataka nianze Barabara ya Amani – Mtoni. Hapa nataka Mhe. Waziri na pia Mhe. Waziri wa Fedha aje atusaidie jawabu vile vile. Katika bajeti iliyopita ya mwaka 2012/2013 tuliidhinisha shilingi bilioni moja kwa ajili ya kumalizia barabara ile ya Amani – Mtoni. Fedha hizi tuliziidhinisha kwa shingo upande, hasa baada ya kuona kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilitoa fedha kwa ajili ya kumalizia barabara ile tena ilikuwa mwaka 2009, mwaka 2010 tumeingiza fedha na hivi karibuni tumeidhinisha shilingi bilioni moja kwa ajili ya kumalizia barabara ile na wakatuhakikishia kwamba fedha hizo zikiingizwa wataweza kupatiwa.

Mhe. Spika, leo barabara imeshakwama, tumejaribu kufuatilia mmekwamba kitu gani wanasema fedha hawana. Je, tunauliza Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano aje atwambie zile shilingi bilioni moja tulizozipitisha katika bajeti hii tuliokuwa nayo mmeshapewa? Kama mmeshapewa imekwenda wapi?

Mhe. Spika, yaani leo barabara hii ya Amani - Mtoni imekuwa kama hadithi ya mkahawani, nenda, rudi, nenda, barabara miaka mitatu kilomita sijui tano tu pale aibu. Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri wa Fedha kama atakuwepo nae atwambie je hizi fedha hajawaingizia mpaka leo?

Mhe. Spika, nikimalizia suala la barabara ya Amani – Mtoni nakuja katika barabara ya Kwaabasi Hussein – Mboriborini. Barabara hii nimezuwia bajeti mara mbili na nikaahidiwa safari hii katika Mfuko wa Barabara. Hivi karibuni nimekwenda na watendaji wa *UUB* bado tatizo inaonesha fedha hawajaingiziwa.

Mhe. Spika, naomba sana kama alivyosema Mhe. Jussa sisi kwetu kupitia Mfuko wa Jimbo tulipeleka shilingi milioni tano tunashukuru tumetiliwa kifusi, lakini vifusi kama vile tumeshatia zaidi ya mara tano, lakini leo tunatia kifusi mwakani tunarudi tena, tumeomba basi angalau kile kijipande kidogo, tena tumepima juzi na watendaji wake wa UUB ni kama mita mia tano tu, basi hizo mita mia tano kututilia lami angalau hiyo nyengine mkaja mkatumalizia awamu nyengine pia inashindikana. Mhe. Spika, naomba hili mhe. Waziri najua analijua vizuri na Naibu Waziri analijuwa zaidi naomba sana Mhe. Spika, ili tena kwenye bajeti huko tuje tupongeze utendaji wa wizara hii.

Mhe. Spika, nakuja katika Mamlaka ya Uwanja wa Ndege. Wananchi leo katika vyombo vya habari walikuwa wanatutathmini je, Kamati za Baraza la Wawakilishi zinavyofanya kazi kuna *impact* gani? Wananchi wamesema wameanza kutuita *comedy*, yaani hapa kazi yetu kuja kusema tunapigiana makofi halafu hakuna kinachotekelezeka.

Mhe. Spika, tulizungumzia suala zima la Mamlaka ya Uwanja wa Ndege madudu yaliyoonekana katika Ripoti ya Kamati Teule, tumekaa na Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais tukazungumzia namna *ethics* za uongozi zinavyotaka, mpaka leo bado hatujaona chochote kinachoendelea. Mhe. Spika, naomba sana pamoja na utendaji mzuri wa Mamlaka ya Anga lakini kwa yale mambo ambayo miko ya uongozi hayaruhusu naomba sana Mhe. Spika, serikali iweze kuyashughulikia ili kujenga nidhamu ndani ya serikali yetu katika utendaji.

Lakini nakuja katika *terminal*. Mhe. Spika, kwenye *terminal* imeelezewa katika majibu ya waziri lakini imekuja vile vile katika ripoti ya kamati. Sasa hivi tumeambiwa kuna mshauri mwelekezi amekuja kuja kuangalia nani mkosa, hii ni aibu, fedha zimeshakwenda *airport* jengo lile halina kiwango, hivi sasa tunaambiwa jengo ile *floor* iko chini kuliko ile *run away*, jamani hawa wajenzi wanatoka wapi ina maana kweli hawa wajezi tuliowapata walikuwa *competent*. Sasa Mhe. Spika, huyu mshauri mwelekezi anayekuja kutoka Ufaransa tunaambiwa tayari ameshaingia ataanza kazi wakati wowote, huyu ina maana ni mzigo mwengine wa kodi ya wananchi tunakuja kumlipa pesa tena vile vile. Mhe. Spika, kwa kweli hii ni aibu tena ni aibu kubwa sana kwa serikali.

Mhe. Spika, kabla ya bajeti tunataka suala la Uwanja wa Ndege tuje tupewe jawabu kamili, tumeshaambiwa kila siku mata ujenzi ule unakwenda kwa *designing and building*, *designing and building* mambo yenyewe ndio yale kumtafuta mshauri mwelekezi. Mhe. Spika, kwa kweli hii ni aibu sana na kitu ambacho kinatutia uchungu sna ni hizi kodi za wananchi. Mhe. Spika, lakini vile vile ni deni la taifa, hili vizazi vyetu vinakuja kurithi katika kuja kulipa madeni haya ambayo kila siku tunaendelea kuyapigia kelele.

Mhe. Spika, nikiendelea katika mchango wangu nije Shirika la Meli. Mhe. Spika, tulipitisha hapa sheria nadhani ile mamlaka mpaka leo bado ile Bodi haijatangazwa, tunaomba sana iundwe hii

Mamlaka ya Shirika la Meli. Sasa hivi kuna tatizo kubwa sana la usafiri baina ya Unguja na Pemba, na kitu ambacho serikali ilikuwa ikifanye cha usafiri wa uhakika wa kwenda Unguja na Pemba. Leo ndugu zetu wanaanza kutulalamikia, wanasema sasa hivi ule usafiri wa siku zote umekuwa haupo, wiki mara tatu. Mhe. Spika, kwa kweli hili ni suala linalouliza sana.

Sasa mimi nataka nishauri, alikuja mfanyabiashara mmoja kutoka Marekani, huyu ni *President* wa *Real Estate of America.* Alikuja Mhe. Spika, kutokana na uchungu wetu wa maendeleo tukampeleka mpaka kwa Makamu wa Pili wa Rais akaonananae. Huyu yeye amekubali akasema kama Zanzibar ina taasisi ya serikali kama mfano Shirika la Meli wako tayari kuingia nao mkataba kuwapa meli hata kama tano, sita, saba hizi *speed boat* kwa ajili ya kuondoa tatizo la usafiri kwa upande wa Zanzibar, sasa hili Shirika la Meli linafanya kazi gani Mhe. Spika. Tunaomba sana serikali yetu ianzishe hii mamlaka ili waweze kufanya *joint venture* na hawa wafanyabiashara wengine.

Mhe. Spika, kama hii Mamlaka ya Shirika la Meli itaweza kuundwa kabla ya mwezi wa Septemba mwekezaji huyu amekubali kuwaalika katika Mkutano wa *Chamber of Commerce of Africa* ambao utakaofanyika Ghana katika mwezi wa Septemba, ili waende wakakae nao hawa wafanyabiashara wenzao kuangalia namna gani wanaweza wakaingia *joint venture* kwa ajili ya kuondoa tatizo la usafiri kwa upande wa Zanzibar.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, nilikuwa naomba sana hili Shirika la Meli tuweze kuliundia hayo Mamlaka yake na mamlaka tumeshaunda mimi nafikiri iweze kutangazwa hii Bodi na hili Shirika kwa ajili ya kuweza kufanya hiyo kazi.

Mhe. Spika, nakwenda haraka haraka naona unaangalia muda, lakini jengine nilikuwa nataka kuzungumzia kwa upande wa Idara ya Ardhi. Mhe. Spika, mimi naomba wizara inayoshughulikia masuala ya ardhi katika maeneo ya nyumba Mhe. Spika, naomba tuunde Shirika la Nyumba. Tumeona wenzetu Tanzania Bara sasa hivi wameanzisha Mamlaka ya Shirika la Nyumba sasa hivi wanafanya kazi nzuri, wanajenga majumba wanawakopesha wananchi, wanawauzia wananchi. Mhe. Spika, kupitia mfanyabiashara huyu, huyu ni *President* wa *Real Estate of America* wao sasa hivi wameshajenga nyumba laki nne na nusu Marekani wako tayari kuingia mkataba na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar aidha kwa *guarantee* ya aina yoyote, kutoa mkopo kwa ajili ya kujenga mji katika nchi yetu.

Mhe. Spika, amekuja ametembea, amekagua amesema Zanzibar ni sawa sawa na almasi ambayo iko juu ya jabali ambayo haijasafishwa. Mhe. Spika, kama tutaweza kuingia mkataba na hili Shirika la *Real Estate* tutaweza kupatiwa fedha na tutaweza kuwakopesha wananchi wao wamesema kwamba mkopo wao wanachukua miaka 40, wana uhakika kwamba wafanyakazi wote wa serikali pamoja na wananchi wakakopeshwa pesa hizo wakajenga nyumba wakalipa kwa muda wa miaka 40. Mhe. Spika, mimi naomba sana, hii Idara ya Nyumba naomba tukishatoka hapa niwape ile *E-mail* ya yule mfanyabiashara au yule mwekezaji ambae wanaweza wakakanae wakaweza kuangalia ni namna gani wataweza kuingia mikataba kama wanavyoingia wenzetu Tanzania Bara sasa hivi.

Mhe. Spika, wafanyakazi wengi wa serikali sasa hivi fedha zao nyingi wanaumia katika kujenga nyumba, leo wakipata mkopo wa ujenzi wa nyumba kwa muda wa miaka 40 kwanza kodi au malipo yatakuwa madogo wataweza kufanya kazi hii kwa vizuri.

Mhe. Spika, sijui nisme wapi kutokana na muda, sasa labda niseme tu kwamba katika bajeti inayokuja nitatoa shilingi mia katika mshahara wa waziri, najua kwa mujibu wa tataribu zetu kwa katiba siwezi kuzuia bajeti kutokana na Katiba yetu inavyotufunga, hatuwezi tukamuadhibu waziri mmoja mmoja. Lakini tutaizuwia, tutaondoa shilingi katika mshahara wa waziri mpaka tujue kama Ripoti ya Kamati Teule ya Shirika la Umeme serikali imechukua hatua gani.

Mhe. Spika, kwa taarifa tuliokuwanayo tunasikia wale wafanyakazi waliotuhumiwa na ubadhirifu wamepewa fomu, lakini wakati wanapewa fomu zile wanaambiwa hii tunatengeneza *formality* tu hakuna chochote kitakachofanyika.

Mhe. Spika, tumepata mafunzo kupitia *UA*, mradi wa *UNDP* tumeambiwa kama unashindwa kuzuia bajeti unaondoa mshahara wa Waziri, tukiondoa mshahara wa Waziri mimi nadhani Waziri atakuwa hawezi kufanya kazi. Kwa hivyo Mhe. Spika, naomba serikali ripoti ya Kamati Teule wale wote ambao walioshughulika na ubadhirifu wa fedha za umma katika Shirika la Umeme kabla ya bajeti inayokuja serikali ituletee ripoti vyenginevyo Waziri wa Maji atakuwa hana mshahara.

Baada ya hayo machache Mhe. Spika, ninaunga mkono ripoti ya kamati lakini yale mengine ambayo sikupata nafasi ya kuchangia nitajitahidi niwaandikie kwa maandishi japo kwa muda huu sijui kama nitawahi kuwaandikia ili waweze kunijibu. .Mhe. Spika, ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Mhe. Hamza nakushuru. Ninataka niwaombe Waheshimiwa Wajumbe kwamba muda wetu ni mfupi mno, shughuli hii tuimalize katika kipindi hiki cha mchana huu kabla ya jioni. Kwa hivyo Mhe. Waziri unifanyie kazi mbili.

Moja tuwaombe Waheshimiwa Wajumbe tumalize kazi hii kipindi hiki kwa kuomba kuongeza muda lakini pili ufanye majumuisho kumsaidia Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

Karibu Mheshimiwa.

KUONGEZWA MUDA WA BARAZA

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu, lakini pia nipokee maagizo yako. Nianze na kazi ya kwanza Mhe. Spika, wakati nasimama hapa kwamba kwa kuwa muda ulio mbele yetu hautoweza kutosheleza waziri muhusika naye kuja kutoa maelezo mbali mbali kwa niaba ya kamati pamoja na mwenyekiti wa kamati kutoa maelezo, hivyo niliombe Baraza lako Mhe. Spika, likubali kuwa basi leo tutengue muda ule wa Kanuni ili tuweze kumaliza shughuli iliyo mbele yetu kwa mchana huu.
Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, naafiki**.**

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Mhe. Waziri endelea na kazi ya pili.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, niendelee tena kukushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie hoja ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ambayo iliwasilishwa na mwenyekiti na vile vile nitoe baadhi ya ufafanuzi kutokana na maelezo ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili ambao wameeleza.

Kwa sababu ya muda Mhe. Spika, sitopenda kuwataja majina ya Waheshimiwa wala sitopenda kuyarudia yale ambayo nitakuwa nayaeleza. Mhe. Spika, kwanza nianze na suala la migogoro ya ardhi. Mhe. Spika, ni kweli tatizo la migogoro ya ardhi na nia ya serikali ni kuliondosha tatizo hili na kwa kiasi kikubwa tatizo hili linasababishwa na udogo wa ardhi yetu na mahitaji yenyewe yalivyo makubwa kwa shughuli mbali mbali za maendeleo kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, Zanzibar ni ndogo ukilinganisha na ukuaji na uingiaji wa wananchi na wageni mbali mbali kutokana na maendeleo ya kiuchumi wa nchi yetu. Kwa hivyo tatizo la ardhi linakuwa kubwa siku hadi siku. Lakini mkakati wa serikali kwenye hili ninafikiri kwa kiasi kikubwa utaondoa matatizo.

Kwanza kwa hatua zinazochukuliwa za kufanya usajili wa ardhi tunategemea mpaka mwaka 2015 tutakuwa kwa asilimia 50 tumeweza kusajili ardhi yote ya Zanzibar. Lakini vile vile hatua zinazochukuliwa katika kutayarisha master plan ili kuongoza matumizi bora ya ardhi, nalo jambo hili litatusaidia sana. Lakini kwa kiasi kikubwa pia kuzipitia na kuzifanyia marekebisho sheria za ardhi ili ziendane na wakati wa leo ili tuepuke mengi ambayo yanajitokeza. Lakini kubwa zaidi ni sera Mhe. Spika, badala ya kujenga kwa mtanuko basi tujenge kwa kwenda juu ili tupunguze eneo kubwa la matumizi ya ardhi. Kadri tutakavyojenga nyumba za ghorofa nina hakika kabisa Mhe. Spika, zitatusaidia sana kupunguza mahitaji ya ardhi.

Na mpango wa serikali katika kujenga *low cost houses* utatusaidia sana katika kupata ufumbuzi wa matatizo ya ardhi. Najua kwamba tatizo ni kubwa na kubwa zaidi ni kwamba mkakati wa serikali ni kuwachukulia hatua wale wote ambao watakuwa ni chanzo cha matatizo ya ardhi. Hatua zimeanza na zitaendelea kuchukuliwa kali sana. Naamini kabisa Waheshimiwa Wajumbe wataridhika na hatua zimeanza kuchukuliwa.

Kubwa zaidi Mhe. Spika, kwa pamoja sote kusimamia na kuheshimu sheria zetu, kwa sababu na sisi wananchi tunapaswa kuheshimu sheria ya ardhi. Mhe. Spika, kujenga kiholela, kuharibu mazingira na kadhalika ni sehemu kubwa kabisa ya kuvunja utaratibu mzuri wa ardhi jambo ambalo linatupa matatizo sote kwa pamoja.

Suala la kuimarisha Mahakama ya Ardhi Mhe. Spika, kitaaluma, vifaa, majengo, kiusafiri ndio nia ya serikali, tutafanya kila jitihada kuhakikisha kwamba hilo linafanyika ili Mahakama ya Ardhi ifanye kazi yake na wajibu wake mzuri kupunguza matatizo mengi ambayo yamejitokeza.

Kuhusu eneo la Nungwi Mhe. Spika, na Kampuni ya *Spice Islanders.* Utaratibu wa ufutaji wa hati, kwa hivyo hatua hii itafanyika bila ya matatizo yoyote tutahakikisha kwamba haki inatendeka katika masuala haya na kila mmoja anapata haki yake kwa utaratibu mzuri.

Agizo la Makamu wa Pili wa Rais hatua zinaendelea kuchukuliwa ili kuhakikisha kwamba matatizo haya yanandoka. Lakini vile vile suala la kutoa hati mara mbili Mhe. Spika, hivi sasa tunajitahidi na suala hilo na tutahakikisha kwamba utaratibu unafanyika na hakuna hati zinazotolewa mara mbili na kama nilivyosema asubuhi hii kwamba sasa hivi yule anayepewa hati huitwa kwa kusailiwa ili kujulikana mwenyewe ni huyu.

Na utaratibu wa baadhi ya watendaji kujikumbuzia idadi kubwa ya viwanda, hatua za kufanya tathmini zinachukuliwa. Aidha wale wote watendaji katika wizara husika au viongozi waliojilimbikizia viwanja kinyume na utaratibu, hivyo viwanda vitachukuliwa na serikali na vitapewa wananchi ili kukidhi mahitaji. Kwa hivyo hatua mbali mbali zitachukuliwa kuhakikisha kwamba tunachukua taratibu ambazo zitasaidia kuondoa migogoro na mizozo hii ya ardhi.

Kuhusu suala la maji Mhe. Spika, ni kweli tunalo tatizo la maji na tatizo hili linasababishwa na upungufu wa maji nchini. Tuna tatizo kubwa la upungufu wa maji nchini. Moja katika tatizo letu kubwa ni kutokuheshimu masuala mazima ya kulinda mazingira yetu. Tunakata miti ovyo, tunapoharibi mazingira, tunapojenga kiholela linasababisha sana hili tatizo kuwa gumu. Kwa hivyo ningependa kutoa wito kwa wananchi tuendelee kuheshimu sheria zetu, tuendelee kuheshimu matumizi bora ya ardhi, tuendelee kuheshimu raslimali zetu ambazo Mwenyezi Mungu ametujaalia hasa hasa za misitu ili zitusaidie katika kuhakikisha kwamba zinatupa manufaa sisi na vizazi vijavyo.

Hatua mbali mbali Mhe. Spika, zimeanza kuchukuliwa na wizara husika. Kwanza kuna hatua hii ya mradi huu wa *ADB* ambao karibu bilioni 67 zitatumika katika kuimarisha masuala ya maji nchini. Suala la ukarabati wa miundombinu mibovu, hilo ndilo tatizo kubwa. Hivi sasa tayari kupitia *African Development Fund* tunapata karibu Dola milioni 21, mkataba umeshasainiwa kwa nia ya kukarabati miundombinu ambayo hiyo ndio tatizo kubwa.

Kwa kweli ndio tatizo hasa linalosababisha ule mradi mkubwa wa maji wa Japan ambao umefanyika vizuri lakini sasa kuwafikia maji walengwa katika maeneo yao, kwa maana ya zile *feeder pipes* kutoka eneo la kwenye *main pipe* kwenda zile pipe ndogo ndogo zinazowafikia wananchi katika kupata maji ndio tatizo kubwa na hapo njiani maji huwa yanapotea. Kwa hivyo suala zima sasa la ufumbuzi wa suala hili linakuja katika ukarabati wa miundombinu mbali mbali itakayotumika kwa ajili ya kuimarisha miundombinu ya maji nchini ili wananchi waweze kupata maji ya uhakika.

Vile vile ndugu zetu wa *Ras el Khaima* wametupa ahadi ya kutusaidia kujenga visima 50 vya maji jambo ambalo vile vile litapunguza tatizo, msaada wa China wa visima 32unaoendelea utapunguza matatizo ya maji, na jitihada zitafanywa kuhakikisha kama tunaondoa tatizo la miundombinu mibovu ili maji yawafikie wananchi tukiamini ni huduma muhimu kwa wananchi wetu pia hatua hizo zitachukuliwa.

Ni kweli lipo tatizo la makaro Mhe. Spika, maji yanasambaa ovyo mabarabarani, yanaudhi na kukera kila mmoja wetu. Hatua zimeanza kuchukuliwa na ushauri tunaupokea ili tuzidi kuufanyia kazi lakini jitihada zinaendelea za kusafirisha makaro kwa kushirikiana na mafundi wa Manispaa, na mwaka huu wa fedha tutapanga bajeti kubwa zaidi tutafute namna ambayo ya kuondoa tatizo hili ili msingi wetu mkubwa ni kuhakikisha kwamba maeneo yale yanakuwa katika hali nzuri inaondosha matatizo ya hali mbaya ya namna ile.

Ni kweli mji wa Michenzani ule kuwa katika hali ile haipendezi na miji mengine ya Wete, Machomanne na kadhalika. Kwa hivyo Mhe. Spika, tutafanya jitihada kuhakikisha kwamba hali yetu inabadilika ili makaro yale yaweze kuondoa usumbufu kwa wananchi.

Kuhusu tatizo la Mji Mkongwe. Nia yetu ni kuleta maendeleo katika Mji Mkongwe na ni kweli Mji Mkongwe unahitaji Mhe. Spika, uwe safi, uwe kivutio, maana ndio raslimali ya mapato katika nchi hii. Kwa hivyo jitihada ni lazima zifanywe kuona usafi wa mji wetu. Hata suala letu la kukuza utalii, linategemea sana na usafi wa nchi yetu.

Chanzo kikubwa cha mapato kinatokana na utalii. Kwa hivyo kuweka mkazo maalum wa usafi wa Mji Mkongwe ni jambo la hekma na ni ushauri sahihi. Tunapenda tuwahakikishie Waheshimiwa kwamba tutalifanyia kazi jambo hili. Ni jambo ambalo linahitaji mashirikiano mazuri kati ya wizara yangu, wizara inayohusika pia na Tawala za Mikoa kuona kwamba usafi katika hali hiyo unafanyika na unatosheleza. Si vyema kabisa kabisa kuona hali kama ile ni ya kuvunja moyo Mhe. Spika.

Kwa hivyo tutachukua kila jitihada kuhakikisha kwamba usafi unapatikana katika Mji Mkongwe. Pia tatizo la maji lipo kwenye Mji Mkongwe kwa sababu siku hizi maji ya Mji Mkongwe Mhe. Spika, pipes zinapita utafikiri waya za umeme, kitu ambacho kinasikitisha sana. Lakini kwa sababu ya matatizo yenyewe, hivyo kipa umbele kitawekwa kuhakikisha kwamba maji katika eneo la Mji Mkongwe yanapatikana. Ni jambo la msingi sana kwa sababu hatuwezi kuendelea kuona wananchi wetu wanateseka wakati ni wajibu wetu kuchukua hatua zinazofaa kuondosha matatizo ambayo yanajitokeza.

Mhe. Spika, kuhusu suala zima ni kwa nini SMZ inashindwa kuanzisha taasisi zinazohusika na mambo ya mafuta ili mambo yaende vizuri zaidi katika suala zima la kumaliza mchakato wa mafuta kuwa hili suala litolewe katika mambo ya muungano. Hakuna atakayetuzuia Mhe. Spika, katika kutengeneza sera, sheria na kuanzisha utaratibu wa kuwa na taasisi. Haya mambo yameanza, sera imeanza kushughulikiwa na naamini tu tutakapopitisha sera, vile vile taratibu za awali za kuweka sheria hiyo zitafanyika na muundo wa kuwa na taasisi ambayo itasimamia mambo ya mafuta ni mchakato ambao utakuwepo. Kwa hivyo hakuna ambaye ataweza kutuzuia kwa jambo hili.

Suala la msingi hapa ni kwamba kulimaliza tatizo la mambo ya mafuta kwa mujibu wa kulitoa katika mambo ya muungano ambayo Wanasheria wetu Wakuu wa upande wa Zanzibar na upande wa Tanzania Bara wanakaa kulitatia ufumbuzi wa kitaalamu na wa kisheria ili jambo hili litoke katika mambo ya muungano, na mara litakapotoka hizi taasisi zitakapokuwa zimeekwa tayari itakuwa rahisi katika utekelezaji. Kwa hivyo mambo mengine haya yanawezekana na yatafanyika na hakuna haja ya kila mara kurudia tatizo hili kwa hili.

Mhe. Spika, kuhusu tatizo la upatikanaji wa viwanja kwa wananchi. Ni kweli lipo tatizo la upatikanaji wa viwanja kwa wananchi, kwa sababu mahitaji ni makubwa kuliko uwezo wenyewe wa kutoa viwanja vinavyohitajika kwa wananchi wetu. Kwa hivyo utaratibu mzuri ni ule sera ya kufikiria sasa badala ya kujenga nyumba ndogo ndogo nyingi za chini, tuanze kujielekeza katika kujenga nyumba za ghorofa kutokana na ufinyu wenyewe wa ardhi, lakini hatua zitachukuliwa kuhakikisha kwamba wale wanaoomba viwanja wanaomba mwanzo wapate mwanzo, asiwe amekuja mtu baadae akakoseshwa wa mwanzo. Hilo linasikitisha, kwa hivyo taratibu tuende zaidi katika hili na tuweke utaratibu mzuri na uwe utaratibu wa wazi.

Kwa sababu wananchi wote wana haki ya kupata viwanja, asiwe mmoja ananung'unika. Kwa hivyo manung'uniko nayo yanavunja moyo sana. Kwa hivyo tutafanya jitihada hizo tuone namna gani tuweke utaratibu mzuri zaidi kuhakikisha wananchi wetu wale wenye mahitaji ya viwanja wanavipata. Lakini tatizo kubwa Mhe. Spika, kama nilivyosema kuwa ardhi yetu ni ndogo, kwa hivyo tunahitaji kuchukua hatua nzuri zaidi zitakazohakikisha kwamba tunaliondoa tatizo hili.

Kuhusu kwa nini wananchi wenye haki ya kupata nyumba za Michenzani kwa muda mrefu mpaka leo hawajapata. Ni utaratibu wa serikali kuwapa wale wote ambao wamekosa haki hiyo. Hivyo tutaendelea kushauriana tutizame ni namna gani nani na nani wale ambao haki hii hawajaipata na wana wajibu wa kuipata waipate. Kwa sababu wale wote walioahidiwa kupewa nyumba zao baada ya kuvunjwa nyumba zao ni wajibu na haki yao kupata nyumba hizo. Kwa hivyo tutalifanyia kazi suala hilo. Ni gumu na ni zito lakini kwa njia moja au nyengine linahitaji kupata majibu. Kwa hivyo ninawaomba Wajumbe kuvuta subra tulishughulikie kwa upana wake ili tuone ni namna gani tunaweza kulitatua tatizo hili. Lakini ni nia ya serikali kuhakikisha kwamba wale wananchi wote ambao wameikosa haki hiyo basi wanapewa haki yao.

Kuhusu uanzishwaji wa Shirika la Nyumba. Hili Mhe. Spika, halina tatizo. Nia ni kuelekea huko kwa sababu tunaamini kabisa kabisa kuanzishwa kwa Shirika la Nyumba kutasaidia sana kuleta mabadiliko makubwa katika usimamizi mzima wa nyumba zetu tulizonazo, kujenga nyumba nyengine za kisasa kwa maendeleo ya wananchi wetu. Hivyo ushauri mzuri tunaupokea na umeshaanza kufanyiwa kazi na utaendelea kufanyiwa kazi ili kuhakikisha kwamba tatizo hili la nyumba katika nchi yetu tunaliondoa.

Kuhusu suala la Kamati Teule ya Shirika la Umeme. Wahusika ambao wataonekana wamefanya makosa hapana shaka yoyote hatua zitachukuliwa kwa mujibu wa sheria na hatupo tayari kumoonea mtu yeyote na wala hatupo tayari kumpendelea mtu yeyote, wale waliofanya makosa basi kwa mujibu wa taratibu ziliopo watachukuliwa hatua na kuhakikisha kuwa utendaji katika shirika unakwenda vizuri.

Lakini hapa Waheshimiwa ningependa sana niombe kwamba na wale wanaofanya kazi vizuri wakapikiwa majungu na kuharibiwa majina yao, lazima mambo pia tunayaone, tusiwavunje moyo watendaji wetu ambao wanafanyakazi kwa bidii kubwa sana. Shirika la Umeme tulitazame lilivyokuwa miaka mitatu minne nyuma na tulitazame leo. Yapo mabadiliko, kwa hivyo wanaofanya kazi uzuri tuwape pongezi, wanaofanya makosa tuwaweke pembeni. Lakini tusiwachanganye wote hata wale wanaofanya vizuri wakafanywa na wao wana makosa, tutakuwa hatukutenda haki. (*Makofi*).

Mimi nakubaliana kabisa kwamba wenye makosa hatua zichukuliwe za kinidhamu, za kisheria na wale ambao wanaofanya kazi vizuri tuwapongezeni na tuanze humu ndani kuwapongeza, tuseme fulani unafanya kazi nzuri hongera, tuwape moyo hawa kwa sababu ikiwa sisi kazi yetu kuwalaumu tu watendaji na wale wanaofanya vizuri tutaendelea kuwavunja moyo.

Kwa hivyo Mhe. Spika, kwa haya ambayo kwa ufupi yale yote mengine tunayopokea tukayafanyie kazi tuhakikishe kuwa wizara yetu inafanya kazi kwa kukidhi matakwa ya wananchi na hoja mbali mbali zinazotolewa na Wajumbe hapa ili ufumbuzi upatikane, tufanye mambo mazuri yatakayowaridhisha wananchi wetu na huduma bora zitolewe kwa maana ya umeme, maji, viwanja na mengine yote yenye matatizo yapatiwe ufumbuzi.
Kwa maelezo haya Mhe.Spika, nakushuru sana na naunga mkono hoja iliyowasilishwa na kamati husika. Ahsante sana. (Makofi).

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, napenda nikushukuru asubuhi ya leo na tukiingia mchana tena kunipa fursa hii. Vile vile kwanza nimshukuru Allah kwa kutubakisha hai na kuweza kutekeleza majukumu yetu.

Mhe. Spika, napenda niwashukuru wote ambao wamepata fursa hii ya kuchangia na wale ambao hawakupata fursa lakini walikuwa na nia basi wasione taabu kutuelekeza wakati wowote katika kipindi hiki cha utekelezaji wetu.
Waheshimiwa waliochangia ni:

1. Mhe. Makame Mshimba Makame
2. Mhe. Salma Mussa Bilali
3. Mhe. Marina Joel Thomas
4. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu
5. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
6. Mhe. Hamza Hassan Juma
7. Mhe. Ali Salum alileta kwa maandishi.

Mhe. Spika, mambo yaliyojitokeza ni kama yafuatayo na baadhi ya maelezo yake.

Kwanza tukianza na Shirika la Bandari. Ni sahihi kwamba uwezo wa bandari ya Malindi umekuwa ni mdogo kutokana na maendeleo ya ile bandari yenyewe, kwa sababu meli zinazokuja sasa ukilinganisha na miaka hata miaka mitano iliyopita ni kubwa zaidi na zinachukua makontena mengi zaidi. Kwa hivyo kumetokezea kitendo cha maendeleo bandari inaonekana ni finyu na jitihada kubwa tunachukua katika kuona kwamba bandari ile inakimu au inakidhi haja.

Kuna maeneo hivi sasa yanaekwa floor ambayo alikuwa hayawezi kuekwa makontena tayari inapatikana. Muda si mrefu tutakuwa na ujenzi wa ofisi ambayo itaondoka sehemu ile ya maghala na kwa hivyo eneo litapatikana. Lakini pia serikali imetoa kwa muda eneo la Bwawani

ambalo tayari sasa linaekwa makontena matupu ili kupunguza shehena za makontena ndani ya gati au ndani ya bandari.

Mhe. Spika, ni dhahiri kwamba serikali imepania katika kuona kwamba tunapata ujenzi wa bandari ya Mpigaduri. Lakini kama tulivyosema kwanza kwamba shughuli hii inafanyika kwa taratibu na kwa mujibu wa maslahi ya Zanzibar. Tayari wawekezaji wengine wameshajitokeza lakini inapimwa nini mahitaji yao, nini masharti yao na vipi Zanzibar itafaidika. Kwa hivyo serikali ipo katika jitihada kupitia wizara yetu ili kuona kwamba bandari hiyo ya Mpigaduri inapatikana.

Jengine lililoulizwa katika bandari ni uingiaji wa mchanga kutokana na bandari sio ya mvungu. Hii tayari imeshafanyiwa utafiti wa kina na karibu hivi itatolewa tenda kama sio tayari kwa ajili ya kuondolewa ule mchanga. Kwa sababu athari yake ni kwamba bandari inapungua kina na meli zetu zinazokuja hivi sasa ni kubwa zaidi, kwa hivyo kama hatukufanya mapema ina maana zinaweza zikashindwa meli zile kuingia. Kwa hivyo hilo limeshashughulikiwa na lishajulikana kima chake na ukubwa wake.

Baada ya hapo Mhe. Spika, kuna suala la mwisho la uimarishaji wa bandari za Pemba pamoja na ya Mkokotoni. Hili tayari linashughulikiwa katika kipindi kifupi kijacho tutapata msaada ambao utafanya study au utafiti wa kuzijua mahitaji yake na maendeleo yake. Kwa hivyo ni bandari ya Mkoani, Wete na Mkokotoni.

Ama kuhusu bandari ya Wesha bado kidogo kwa sababu…

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe mnaotoka nje kwa dharura mbali mbali tuelewe kwamba muda mfupi kutoka sasa tutapitisha ripoti hii, hivyo nawaomba turudi si muda mkubwa kutoka sasa kwa sababu kazi hii tunataka tuimalize punde tu. Quorum yetu hapa kwa hivi sasa haitoshelezi kumaliza. Kwa hivyo tuendelee lakini walioko nje waingie ndani ili tumalize kazi hii. Mhe.Waziri endelea.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Masuala mengine yaliyojitokeza ni Mamlaka ya viwanja vya Ndege. Kwanza tunaanza na *terminal two*.

Mhe. Spika, mkataba wa ujenzi wa *terminal two* ni *design and built* lakini katika hiyo *design and built* wanaotakiwa kushirikiana ni mjenzi na mjengewa; yaani *client* na *contractor*. Sasa huyu mshauri mwelekezi tuliyemleta si kuja kusema nani ana kosa, ni kutusaidia sisi kuona kwamba jengo lile tutaweza kuliendeleza vipi.

Kwa hivyo *consultant* anayekuja anakuja kutoa ushauri wa kiufundi namna gani ya kulimaliza jengo lile ili liweze kutumika katika ile shughuli ambayo tuliyokusudia. Kwa hivyo huyu atakuwa ni mshauri mwelekezi kwa upande wetu sisi; sisi ndiye atakayetushauri. Akitazama michoro ya mjenzi na hali ilivyo atatushauri nini kitakachoendelea na hiyo ndio idea tokea mwanzo ambayo ilikuwepo. Kwa sababu yule mjenzi katika ujenzi wa aina hii anatakiwa awe na ujuzi wake, sasa kama hana ujuzi anaweza akachukua mshauri mwelekezi ambaye yeye ndiye atamsaidia ile kutoa maelekezo.

Timu ya watu wanne inatarajiwa kufika leo ambayo itaanza kazi mfululizo kwa muda wa wiki sita kuona kwamba hali itakwenda kitu gani. Kwa hivyo ninaamini kabisa kabisa kwamba kabla ya bajeti yetu hali halisi ya jengo lile itaweza kupatikana na tutaweza kuendelea.

Suala la uendelezaji wa Uwanja wa Ndege Pemba, kama utaangalia bajeti mara hii katika 2013 ilitengwa shilingi milioni mia nne kwa ajili ya utiaji taa na milioni mia tano kwa ajili *feasibility* study ya kiwanja. Napenda niwahakikishie kwamba shughuli ya utiaji taa ipo kwenye tenda sasa, sio ile ndoto tena kwa sababu Mhe. Spika, wewe ni shahidi, mimi binafsi ndiye niliyekuwa champion wa kutetea utiaji taa wa Uwanja wa Ndege Pemba.

Sitoweza kurejesha ulimi wangu waswahili wamesema, halafu nikawa sio tena wa kulishughulikia suala lile. Na kwa hivyo sidhani kama yupo anayenishinda kwa kuona kwamba Uwanja wa Ndege Pemba unataka kutiwa taa, kwa sababu nililitetea pale ambapo hajasema mtu yeyote. Kwa hivyo kila atakayelisema achukue kwangu mimi.Lakini nawashukuru sana wale waliochukua kwangu wakali-*transfer* wakaanza kunirushia mimi, hao ninawashukuru sana. Kwa sababu walikuwa wakifanya kazi ya kunikumbusha.

Jengine Mhe. Spika, ni suala la fidia. Ni kweli kwamba kiwanja cha ndege katika utanuzi wake na kujengwa ukuta kulikuwa na kuingiliana na majengo ya wananchi na mashamba ya wananchi. Fidia imelipwa kadri ambapo thamani ilikuwa ikikisiwa. Malalamiko Mhe. Spika, ni sahihi kwamba yapo lakini uzuri wa malalamiko hayo ni kwamba yanashughulikiwa, hakuna lalamiko linalodharauliwa. Lakini tatizo letu tunalinganisha kitu ambacho hakiwezi kulinganishika. Wakati mwengine mtu tu anasikia tu kwamba huyu kapewa milioni fulani analinganisha na chake. Sasa haiwezekani kwamba watu wote walipwe aina moja. Lakini ushahidi upo wa wazi kwamba wale waliopeleka malalamiko yao na yakalingana na ile hali ilivyo, wamepewa nyongeza zao. Lakini sio kila atakayeleta lalamiko ni kweli kwamba atapewa kile ambacho anakihitaji yeye, atapewa kwa mujibu wa ile hali ambayo imeonekana kuwa ni sahihi au sio sahihi.

Kwa hivyo, tunawaomba wananchi wote kwamba wale ambao walikwishakupewa fedha zao waendelee na shughuli zao na juu ya hivyo umepita ubinadamu wa kwamba mtu kapewa pesa za nyumba yake, lakini kaachiwa achukuwe kila kitu ambacho anacho katika nyumba ile hata tofali lake. Kwa hivyo, serikali ilijitahidi na itaendelea kujitahidi kuona kwamba ulipaji wa fidia unafikia katika kiwango kizuri bila ya manung'uniko. Tunawashukuru sana wale walioanza kazi hii na sisi tunaendelea nayo.

Kuhusu huduma za uwanja wa ndege zinazoitwa *ground handling services,* mchakato bado unaendelea, mshindi wa *tender* bado hajatangazwa, kwa hivyo tusubiri wakati hali inaendelea atatangazwa mshindi wa *tender* ambaye atakuwa na mshirika pamoja na *ZAT,* katika kuendesha shughuli za kiwanja cha ndege chetu cha kimataifa.

Mhe. Spika, nikija kwenye Mamlaka ya Usafiri Baharini, kulikuwa na masuala mawili. Kwanza kulikuwa na lalamiko kutokana na kamati kwamba kuna ufinyu wa bajeti. Suala hili tumelipokea, lakini ufinyu wa bajeti kama tujuavyo ni kila pahala. Kwa hivyo, tutajitahidi ili tuweze kufikia.

Hatua ya pili ambayo ilitajwa katika kamati ni mchakato wa kuikuza ile mamlaka. Kwa kupitia Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo tayari Mkurugenzi wa Fedha ameshapatikana na mchakato wa kufungua *account* yake tayari umeshaanza. Kwa hivyo, hatua hiyo ambapo pengine kamati ilipopita ilikuwa bado, sasa hivi tayari imeshafikiwa.

Mhe. Spika, baada ya hapo tunakuja Idara ya Mawasiliano. Ni kweli kwamba mradi wa *Post Code* umewekwa pote, yaani maeneo yale tengefu yamewekwa kwa Bara na Zanzibar. Lakini kwa upande wa Zanzibar, ramani tayari imeshakamilika, hiyo ndio hatua ambayo iliyofikia. Uchoraji wa ramani katika maeneo yale tayari umeshakamilika.

Vile vile liliulizwa swali kwa njia ya maandishi kuhusu uondoshaji wa mnara wa Wireles Kikwajuni. Hili tayari vile vile lishakabidhiwa kuna kamati maalum ya serikali iliyoundwa, ikiongozwa na wizara yetu, Zantel pamoja na Mji Mkongwe. Zantel ndio iliyopewa jukumu hili na tayari wamo katika mchakato wa kushughulikia, muda sio mrefu tutatangazia hapa hapa katika Baraza kwamba mnara ule tayari unaangushwa, lakini ni kwa ajili ya kukingwa na ajali yoyote. Nashukuru kwa yule mjumbe ambaye aliliuliza swali, kwa hivyo wote wananisikia.

Kuhusu Idara ya *UUB* Mhe. Spika, yalitolewa malalamiko kuhusu mkakati wa kuzilinda barabara na ujenzi wa matuta kiholela. Mambo mawili hayo tayari yote yanashughulikiwa. Kama nilivyosema mwanzo katika utangulizi wangu, kwamba sheria ya kuzilinda barabara yaani kuweka *road resolve* tayari imo katika mchakato na sio punde hivi italetwa katika Baraza lako tukufu. Pia kuna matangazo mengi yanatolewa sasa hivi ambayo yanaelezea kuhusiana na tahadhari kwa wananchi, juu ya namna ya kujenga katibu na barabara hasa ujenzi ambao ungehatarisha maisha ya watu wengine.

Mhe. Spika, kuhusiana na ujenzi wa matuta kiholela. Suala hili tayari linashughulikiwa, kuna baadhi ya maeneo hasa Kaskazini Unguja, baadhi ya wananchi wanajenga matuta bila ya ruhusa ya *UUB* au kupitia wizara yetu. Kwa hivyo, tunaandaa kikao pamoja na wakuu wa Mikoa, Halmashauri ili kuweza kuona suala hilo linashughulikiwa vipi, kwa sababu njia ikiwa itakuwa na matuta tu itakuwa sio njia tena, ni lazima kuwe na utaratibu maalum naungana mkono na wajumbe hawa kwamba kuwe na utaratibu maalum wa kuweka matuta katika barabara, ili kuweza kuzilinda kwa usalama, lakini pia kuweza kundoa tatizo la usafiri.

Mhe. Spika, kuhusiana na barabara ndogo ndogo za Mji Mkongwe na fedha zilizotolewa na Wabunge na Wawakilishi na hasa Wabunge. Hili suala tulipanga kulizungumza pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Mjini Magharibi, ili kuona kwamba je, kuna tatizo gani ambalo limekwamisha kupatikana kwa fedha hizo, kwa sababu bado hazijaingia katika wizara yetu.

Pia napenda kusema kwamba bado tuna ukosefu wa lami. Kwa hivyo, barabara nyingi ambazo zilikuwa zimeshakuwa *pointed* kuwa zitiwe lami zimezuilika, mpaka hapo lami itakapopatikana.
Mhe. Spika: Kuhusu utaratibu Mhe. Ismail Jussa Ladhu.

UTARATIBU

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, naomba nimsaidie Mhe. Waziri kwamba hizo fedha zimeshaingia, kwa sababu liko jibu la Naibu Waziri wake katika Baraza hili hili, akithibitisha juu

ya kupokewa kwa shilingi 40 milioni na serikali zilizotoka katika Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo la Mji Mkongwe. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, nimelisikia na nitalifuatilia. Nitalifuatilia kwa kina Mhe. Spika, ndani ya wiki hii na tutampa jibu rasmi, yeye pamoja na hao waliotoa tutawaalika rasmi katika kikao, ili tuweze kulizungumza kwa kina *Inshaallah.*

Mhe.Spika, liliulizwa swali jengine kuhusu barabara ya Amani Mtoni. Serikali kupitia Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Mfuko wa barabara imetoa shilingi milioni 500 tu za ujenzi kwa barabara hiyo kwa mwaka huu. Kwa hivyo, pesa zilizotolewa ni shilingi milioni 500 na sio shilingi milioni moja kama ilivyodaiwa na zimeshatumika katika ujenzi wa barabara. Bado zinahitajika tena shilingi milioni 500 kwa ajili ya kulipa fidia ambazo mchakato wake unaendelea.

Kwa hivyo, tunawaomba Waheshimiwa Wajumbe kuona kwamba hali halisi ni hiyo.

Jengine Mhe. Spika, ni kuhusiana na Idara ya Usafiri na Leseni liliulizwa swali moja kuhusiana na mkanganyiko baina ya *ZRB* na Idara ya Leseni. Hakuna mkanganyiko isipokuwa kila mmoja anajukumu lake katika ile leseni wenyewe. Kwa hivyo, hapa kilichopo ni ushirikiano katika idara mbili hizi ili kuona kwamba mambo yanakwenda sawa sawa.

Mwisho Mhe. Spika, nakuja katika Shirika la Meli. Kwanza tunashukuru sasa hivi kwamba usafiri wa Pemba na Unguja umetengenea baada ya kuwa na meli tatu ambazo zinakwenda kwa kawaida, zikiwemo Azam Sea link, MV Maendeleo na MV Serengeti. Tunashukuru sana na tunamuomba Mwenyezi Mungu ajaalie kwamba viende kwa usalama na kurudi kwa usalama. Isipokuwa kuna tatizo la boti za kwenda kwa kasi bado hakuna zinazokwenda kwa hivi sasa.

Mhe. Spika, suala nyeti la ununuzi wa meli, mimi ningesema kwamba meli ununuzi wake ni wa uhakika, kwa sababu tunahitaji kupata meli iliyokuwa na hadhi ya Zanzibar, iliyokuwa na hadhi ya kupakia abiria, tukashindana na tukawashinda vyombo vya usafiri vya binafsi. Kwa hivyo, pamoja na kuchelewa kutiwa saini huo mkataba, lakini tunakuhakikishieni kwamba zile fedha zilizotengwa kutokana na ombi rasmi la Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, kwa ajili ya ununuzi wa meli yote, itakwenda kulipia asilimia fulani ya ununuzi wa meli. Ujuwe kwamba ununuzi wa meli ni ghali, lakini ile fedha yote ambayo ni shilingi 17.4 bilioni itakwenda kulipia asilimia fulani ya ununuzi wa meli na meli hiyo ndani ya miezi 18 ijayo itaweza kukamilika na kuja Zanzibar. Lakini siku ya kutiwa saini mtasikia nyote wala hakuna anayemdanganya mtu, meli tayari imeshapatikana, tumeshaiona kwa *electronic pictures* tayari imeshapatikana ya meli na sisi bado kuanguka tu kwa kuweka saini kwa ajili ya ununuzi wa meli.

Mhe. Spika, tunawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa usikivu wao, naomba nimalizie hapa ili tuweze kutoa nafasi kwa mambo mengine, ahsante.

UTARATIBU

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, nilikuwa namuomba Mhe. Waziri kulikuwa na swali niliuliza, kuhusu bilioni moja tuliyoitenga katika umaliziaji wa barabara ya Amani Mtoni, fedha zile hazijaingia kwa sababu ile barabara imeshakwama. Hebu tungepata jawabu. Tumetenga bilioni moja ya kumalizia barabara ya Amani Mtoni kwenye bajeti, hubu tupate maelezo kidogo.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, alizungumza Mhe. Hamza Hassan. Mimi nilisema kuwa zilidaiwa kwamba zimetolewa shilingi bilioni moja kwa ujenzi wa barabara ya Amani Mtoni, lakini zilizotolewa na Mfuko wa Barabara ni shilingi milioni 500 na zimeshatumika kujenga mpaka kiwango kile kilichopo. Bado kuna deni la bilioni 500 la fidia kwa wananchi. Kwa hivyo, zilizotolewa na Mfuko wa Barabara kwa mwaka huu wa 2013 mpaka sasa hivi ni shilingi milioni 500 na sio shilingi bilioni moja kama ilivyodaiwa. Hivyo, ndivyo nilivyojibu. Kwa hivyo, namuomba sana mheshimiwa achukuwe huo ndio usahihi wenyewe.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, angetusaidia ufafanuzi, tumetenga katika bajeti ya serikali shilingi bilioni moja kwa kumalizia barabara ya Amani Mtoni. Mhe. Waziri anasema kwamba zimetolewa shilingi milioni 500, tena anasema ni za *compaciation*. Sasa ina maana hizo shilingi milioni 500 ni za *compaciation*. Hebu atufafanulie, kwa sababu kama shilingi bilioni moja ilikuwa kwa kumalizia ujenzi ule wa barabara, kama shilingi milioni 500 tayari zimeshatoka, barabara ile imetengenezwa pahala padogo na imeshaganda sasa hivi. Sasa hiyo shilingi milioni 500 ikitolewa itakwenda kwenye *compaciation* au kwa kumalizia barabara. Hebu angetuwekea sawa, hii barabara imeshakuwa ni miaka minne tena inajengwa.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, ni kwamba zilizotolewa mpaka sasa hivi, kwa sababu mpaka bajeti haujamaliza, hatuzungumzi bajeti sasa hivi. Tunazungumza kazi za kamati, hatuzungumzi kipindi cha bajeti. Nilizosema zimetolewa mpaka sasa hivi ni shilingi milioni 500, kwa hivyo pale ilipofika ni shilingi milioni 500 zilizotolewa. Pamoja na ujenzi huo kuna shilingi milioni 500 nyengine zinatakiwa za kulipia fidia. Sasa nini kitaendelea baadae ni maamuzi yatafikiwa. Lakini nilichokisema ni kwamba hicho kilichotumika sasa hivi na hapo unapoiona barabara ilipofika ni shilingi milioni 500 zilizotolewa na tukumbuke kwamba mwaka wa bajeti haujamaliza, kwa sababu hatuzungumzi bajeti sasa hivi.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:(Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi): Mhe. Spika, kwanza niwashukuru wale wote waliochangia na niwape hongera sana kwa ufanisi wao waliochangia. Lakini Mhe. Spika, kabla sijawataja wale waliochangia michango yao ile ilitusaidia sisi pamoja na serikali, kwanza kwa ruhusa yako naomba nitowe indhari.

Mhe. Spika, suala la mwisho hapa lilikuwa ni suala la meli na tulitoa mapungufu mengi sana katika wizara kutokana na kuwapunguzia utendaji wao, ili ipatikane meli na wananchi waweze kutumia fursa yao kupata meli ile bila ya kupata matatizo ambayo huwa yanatokezea.

Mhe. Spika, nasema meli inachelewa kupatikana na yeyote ambaye anasababisha kuchelewa meli kwa kutaka asilimia 10, sheria ipo ole wake. Sheria tumepitisha hapa na kila siku tunaambiwa mikataba, lakini haiishi mikataba hiyo. Tunasema kinywa kipana sheria tumepitisha hapa, basi nitaandamana na yeye sitomuacha katu. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika, waliochangia ni watu 4 au 6 ambao ni:

1. Mhe. Salma Mussa Bilal
2. Mhe. Marina Joel Thomas
3. Mhe. Ali Abdalla Ali
4. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu
5. Mhe. Ismail Jussa Ladhu na
6. Mhe. Hamza Hassan Juma

Mhe. Spika, wote hawa walizungumzia suala la migogoro. Hii migogoro kila siku ardhi, ardhi iliyokuwa haijesha kwa nini, tunaoneana haya tuseme ukweli, hatuambizani ukweli.

Mhe. Spika, Mhe. Rais wa Zanzibar Dk. Shein alisema kuwa migogoro yote tuimalizie katika mikoa, wilaya halikadhalika katika wizara husika. Mhe. Spika, ni sawa lakini naona kama tunaipa mizigo. Mkoa tunaupa mzigo, wilaya tunaipa mzigo. Lakini nani hasa wa kuweza kumaliza migogoro hii ni wizara husika peke yake hakuna mwengine. Kwa nini wizara ina uwezo wa kufuta na kukupa wewe, isiweze kuondoa tatizo hili hakuna sababu. Msimuonee haya hata Mshimba mtoweni tu mnamuonea haya nini, mfuteni tu kama yuko katika ubadhirifu. Lakini Mwenyezi Mungu kanijaalia Alhamdulillah safii sipo.

Mhe. Spika, Mhe.Waziri amelikubali suala hilo na amesema kuwa hatua zimeanza kuchukuliwa kwa wale wote ambao wanakiuka utaratibu. Lakini najiuliza Mhe. Spika, kila siku itakuwa ni hatua hiyo hiyo. Mhe.Spika, kuna mambo mengine tuyakubali kuwa tunaweka muda na tunayakosesha mapato serikali kwa huku kupoteza muda.

Ulilizungumzia suala la *Spice*. Pana kauli nzito hapa, kuna kauli ya mwenyewe Mhe. Makamu wa Pili wa Rais nani asiyejua kuwa ni mtendaji mkuu wa serikali hii, kwa nini tunaidharau. Wallah nasikitika siku zote, kauli iheshimike ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, akisema hapana basi ni hapana. Sasa hivi akisema hapa kuwa, Spika, natoa amri vunja Baraza atasahau kanuni lakini pale tutaitii amri kwanza, baadae tutatafuta kanuni si ndio sheria ilivyo. Kwanza tutaitii amri kasha baadae Mhe. Mwanasheria atasema jamani hee utaratibu, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwanza hapo umeteleza, itabidi twende na kanuni yetu ili twende sawa. Lakini kwanza timiza wajibu.

Mheshimiwa ameshakwenda na *Benz* lake huo sehemu yenyewe mkienda hizi gari zetu zinaweza zisifike, lakini Mheshimiwa kaenda na *benz* lake ndani huko kafika, hakwenda kuuza sura kule kenda kuangalia matatizo ya mwekezaji ambaye anataka kuwekeza katika nchi yetu mpaka leo tuna-*delay* tunaogopa nini. Naomba sana Mhe. Waziri hayupo leo lakini Katibu Mkuu naye ni mtendaji tunaomba sana hili suala litekelezwe haraka sana mwekezaji mwenyewe apewe haki yake. Mhe. Kaimu Waziri yupo *take action*, mara moja hili suala lifatiliwe kutokana na ile kauli ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais.

Lakini vile vile Mhe. Spika, nikienda katika sura nyengine ambayo Waheshimiwa wengi walizungumzia ni masuala ya matatizo ya maji. Matatizo ya maji kweli yapo nakubaliana nayo kwa asilimia kubwa kabisa. Kwa sababu kwanza tatizo na sisi wenyewe tunajenga kiholela, nalo hilo tuliangalie sana kwa sababu vianzio vya maji vinazidiwa kutokana na nyumba havipati rutba

ya ile mimea, kama tungekuwa na mimea mingi ambayo tunapanda basi hata vile vianzio vingeweza kujaa maji. Sasa na hili ni tatizo ambalo linatufanya kuwa hatupati maji, kila siku tutawagomba hawa watu wa *ZAWA*, lakini tatizo letu na sisi tunajenga kiholela hatujengi kwa *plan* ambayo ipo kwa mujibu wa utaratibu.

Vile vile tuseme na hivyo vianzio ambavyo viko tayari vimeshafanywa basi wajitahidi wawafikishie maji wananchi, tujitahidi sana tusilipishe pesa pale pasipokuwa na maji, tulipishe pale pahala penye maji, lakini leo unakwenda kumlipisha mtu hata maji hayaoni. Nalo hili tuliangalie kabisa ambalo linaleta mzigo kwa wananchi kupiga kelele, mpe raha msogezee maji ili aweze kufanya kazi zake vizuri.

Mhe. Spika, tukija katika hoja ya matatizo ya Mji Mkongwe waziri amesema kuwa atayafanyia kazi haya mambo ya kawaida.Mhe. Hamza Hassan anasema kila siku itakuwa ni hivyo hivyo tu, mwisho Baraza litageuka la *comedy* hili. Ni kweli nakubaliana nayo, imekuwa kila siku tunasema haya haya tu jamani. Mhe. Spika, mimi husema kwa namna moja tu, kama inawezekana hebu nipeni mfano mimi, kama inawezekana Wallahi Laazim sisemi masihara nasema kwa kutaja jina la Mwenyezi Mungu kwa sababu nimeshasoma sana nimeona udhaifu uko wapi, kama inawezekana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais hebu niombee siku moja tu nipewe uwaziri kwa dakika au kwa muda wa mwenzi mmoja, haki ya Mungu na Mtume utaona kitu gani. Kwa sababu ni mambo ya kufuatilia, Mhe. Hamza anasema ni mambo ya kufuatilia kila siku tutafanya, tutafanya, mpaka lini?

Mhe. Spika, inasikitisha wananchi wetu tunawaumiza, fanya mfano siku moja tu tena si mchezo nakwambia muda wa mwezi mmoja tu tena unipe wizara maalum, sio unipe wizara ambazo ngumu, tena nitakwambia wizara zenyewe wala sioni tabu. Wizara ya Afya nipe utaona, wizara ya majenzi nipe, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, wizara nyengine naziacha. Kwa sababu zote hizo nimeshazipitia na nazielewa tatizo liko wapi, sio siri na suti hii ukaniapishie hii hii.*(Kicheko)*

Mhe. Spika, kuna tatizo ambalo sasa hivi limejitokeza suala la kuwafutia wananchi viwanja vyao, ningeomba sana kuna wengine hali zao ngumu hebu tuwape angalau miaka mitano ndio wafutiwe kwa sababu hali zao ni ngumu na wengine wanapelekea kwenda kuuza vile viwanja, usifikirie wanauza kwa kutaka wanauza kwa lile suala ambalo limewakifu hapa na kusikia tangazo la ufutaji. Ninawaomba sana watendaji wakuu mfikirie hilo.

Mhe. Spika, tatizo la upatikanaji wa viwanja kwa wananchi, viwanja Mhe. Waziri ameshasema vimeshapimwa, lakini wananchi bado havijawafikia kuwapelekea wenyewe hebu tufanyeni haraka sana. Kuna watu Mhe. Ismail Jussa anasema miaka nenda miaka rudi hatujawafikiria kuwapa. Ninaomba sana Mhe. Spika, maeneo ambayo yazaanza kupimwa hebu tufanye utaratibu tuwakabidhi wenyewe wananchi ili kufanya shuguli zao za kuleta maendeleo na ili waweze kuondokana na mambo ya kodi.

Mheshimiwa nakwenda mbio mbio ili kuumega wakati wetu sisi huu mana sio wa Baraza nimalizie kwa suala la Shirika la Nyumba. Shirika la Nyumba tulikwenda sisi wenyewe kule *National House*, Dar es Salaam kwa kweli limetutia huruma sana. Kwa sababu kututia huruma kwenyewe tumeona choyo, wanatwambia sasa hivi tuna *one trillion* tunatafuta *two trillion.* Kwa

nini wakafanya hivyo wanasema, serikali haiwatilii mkono imewapa kibali cha kwenda kukopa pesa benki wanavyotaka wao wenyewe,wamekwenda kukopa benki fedha kama shilingi bilioni tano lakini wamechukua shilingi bilioni mbili tu hivi au tatu.

Sasa mimi naomba sana Mhe. Spika, mamlaka hizi jamani tuziachie fursa tuipe mikono, serikali iondoe mikono yao kuwaingilia ingilia ili wapate fursa, mamlaka jamani ni kitu cha muhimu sana, wanakwenda kutuonesha jumba Upanga pale kubwa sana, kwa kila *flat* moja wanasema ni shilingi milioni mia tatu na kitu hivi mtu kanunua, milioni mia tatu, hebu tuone faida yake ilivyokuwa na anasema kuwa halina nafasi limeshajaa kabisa ghorofa 15 hizo, fanya hesabu jumla ni ngapi. Halijaanguka bado liko imara kabisa wala sio la makandarasi wa ovyo ovyo, wanawatafuta wakandarasi waliokuwa ni muhimu kabisa. Sisi tunasema jamani mamlaka zetu tuzipe fursa kabisa tena ambazo zenye uwezo tuwatanulie ili watuletee neema, tuna uwezo wa kuwaambia.

Mhe. Spika, kuna suala ambalo wengi wamelizungumza Mhe. Ismail Jussa kazungumza, Mhe. Hamza Hassan kuhusu hii *terminal* yetu. Mhe. Spika, kwa kweli uwanja wetu unasikitisha sana, ambapo ni sehemu ya kutupatia mapato, sisi tunazifanyia masihara. Mhe. Spika, niseme ile *terminal* moja kwa moja wala sioni haya haifai, hilo tuseme tusifichane, wala tusije tukamdanganya Rais halafu baadae tukaja kuuwa pale, kwa sababu hujui sio, huwe kujua wakati wowote lile linaweza likakatika mara moja ukauwa. Tulikwenda pale tukaangalia zile *bolt* zimeshaota kutu, utaniambia kutu ni kitu cha kawaida, kutu ni kitu cha kawaida, hizi pepo zinazokuja za kila aina ambazo hazitabiriki.

Mimi naomba Mhe. Spika, kwamba tusidanganye, hatuna fedha tuliache tutastahamili, tumestahamili miaka mingapi, kwani lile hatukulitumia. Mimi jengo lile la Uwanja wa Ndege tangu sijazaliwa tumelitumia na bado unaliona mpaka leo hii, kwa nini tufanye jambo la haraka. Tutafute fedha serikali. Mhe. Waziri wa Fedha usinitizame, tutafute fedha tulijenge jengine tumalizie. Lakini Mhe. Spika, mamlaka ni mamlaka, mamlaka tuipe huru kutokana na utendaji wake. Tumesema tunataka *International Airport, ZAT* peke yake hawawezi kufanyakazi tukasema lazima watafutwe na wengine. Mhe. Waziri hili utujibu.

Mhe. Spika, *tender* imeitwa na mtu ambaye kama yupo kwa mujibu wa utaratibu ameshakubalika unangoja nini. Mhe. Waziri, leo nilisema nikungoje nikumalizie na mimi, badala ya waziri wa ardhi kaambiwa shilingi ya mshahara inatolewa, basi mimi nasema ilikuwa nitowe shilingi tatu badala ya shilingi moja na mimi nikunyang'anye mshahara wako, kwa sababu hukunipa jibu mimi. Kwa hivyo, naomba sana Mhe.Spika, *tender* imetoka tufuate utaratibu, mamlaka itowe uwamuzi wake, yule mkandarasi aliyekubalika kwa mujibu wa sheria akubalike, twende na wakati, uwanja wa ndege tupate vitu vya kisasa kabisa. Tusitafute mkandarasi anauza gari tunakwenda kumuweka pale, tumepondwa na maji. Tuwe waangalifu jamani, mimi sasa hivi sina mchezo.

Mhe. Spika, namalizia kwa kusema kuwa bado nina waraka huu hapa. Mhe. Spika, nasema tena kwa unyenyekevu, nilisema kuwa kuna mama alikubali kutoa mwenyewe, akasema mimi jamani na-*withdraw* hiki kitu ambacho nimekiona kina maslahi. Watu wengine wakasema pengine na Mshimba yumo, ndio mama wenyewe huyu kajitoa kwa taarifa yenu. Ni mama watoto amepewa kiwanja kile kwa jina la Mhe. Mshimba, amesema mimi sikitaki. Kwa hivyo, na wengine

wajitokeze waseme hatutaki, tusione tabu tunajenga maendeleo, hapa kuna maendeleo. Sehemu hii imekuwa ni ya maendeleo, skuli ipo tangu zamani sio jana na leo hii skuli, tunaona tabu ya nini. Kwa taarifa yako Mhe. Balozi watu wameshauza shilingi milioni 80 sijui kama hivi, kimeshauzwa kile kiwanja tulichosema. Kimeshauzwa shilingi milioni 80 na kauziwa mzungu.

Sasa na mimi sikufichi nakuambia wazi kuwa keshauziwa mzungu bwana wala usipate shida katika maamuzi yako. Kwa hivyo, kwa kumalizia nasema Kiwengwa Kairo mheshimiwa kawahalalishe, ili tujenge skuli ya ghorofa pale ili mchezo umalizike. Vyengine vyovyote hatukubali, usimuogope nani wala nani, kwa sababu hapa kuna majina tofauti sirudii tena, ndio yale yale. Cha msingi ni kwamba nione au nikupe hii karatasi, waite watu wapo kule waliofanyakazi, waambie kuwa bwana nyinyi mlinidanganya au hamkunidanganya, lakini kumbe mambo tayari mimi nimeshafanya utafiti kama ni mwenyekiti mwenyewe.

Mhe. Spika, kwa hayo machache niwashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri wawili kwa utendaji wao mzuri na niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe waliochangia, kwa kweli wamechangia vizuri sana. Vile vile nimesema kwamba pale panapo matatizo basi serikali itafanya kazi.

Mhe. Hamza Hassan Juma alifungia hapa na kusema ah! Kama wapo watu wabadhirifu katika *ZAWA*, basi wachukuliwe hatua. Lakini Mhe. Waziri amesema kuna wengine hupikiwa majungu na kweli barua zipo tunazo sisi, ambazo sisi wenyewe Kamati tulipikiwa majungu na tukaambiwa Mshimba kala nguzo 10, kumbe vile nguzo zile amenunua Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kupeleka ofisi yake na hakujua yule jamaa na wala hakutafautisha Mbunge na Mwakilishi ni nani, sasa ile peke yake ilikuwa tayari fika ni fitina.

Sasa tulipomwita kwenye Kamati akasema aa! Maana yake Wajumbe wengi walirushiwa *message* humu, huyo anayesimama hivi sasa Mshimba muongo ameshakula nguzo 10, yaani wengi walirushiwa *message* humu. Mhe. Spika, nilipokuja kumkamata kwenye Kamati alisema mimi sio namba yangu ya simu na tulipopiga simu ililia kwenye ukumbi na mwenyewe ameshangaa maana yake iliingia baharini.

Kutokana na hali hiyo, basi alitufuata na kusema jamani tafadhalini nistirini, basi sisi tukasema kwamba tukustiri kaombe radhi na kaandike barua, huyo mtu akaandika barua na ipo na wanamlea wao wenyewe, ili kuomba radhi lakini hatimaye alipokuja Mhe. Rais akaenda kusema mengine ya uongo kuliko yale.

Mhe. Spika, ukweli tuuseme wazi kwamba wengine ni mafatani wana kazi yao kufanya ufitina, lakini wengine wako *right* kabisa, kwa hiyo wale waliokutwa wezi basi tia pingu na mimi simtetei hata siku moja kabisa tia pingu. Vile vile nimesema kuwa wizi wa mashine ya kuchunguzia kensa kama fedha zimeibiwa basi tia pingu hakuna kuacha. Mhe. Spika, tunaendelea na wakataokula fedha za meli tia pingu hakuna kuacha. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ahsante sana na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa majumuisho hayo. Waheshimiwa Wajumbe, niwahoji wale wanaokubaliana na Ripoti za Utekelezaji pamoja na Ripoti mpya ya Mwenyekiti

wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla hatujaakhirisha kikao kuna taarifa mbili. Kwanza Mnadhimu wa upande wa Wawakilishi wa CCM anaomba kuonana na Wawakilishi wa CCM mara baada ya kuondoka humu ndani wakutane hapo juu kwa muda mfupi kidogo kuna mazungumzo, ili kuweka mambo vizuri.

Taarifa ya pili nimeombwa na Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo niwatangazie kwamba Msanii wetu Maarufu amefariki dunia. Kwa hivyo, naomba mupokee taarifa hiyo kama alivyonituma Mhe. Waziri.

Baada ya hayo naakhirisha kikao hichi mpaka saa 11:00 jioni

(Saa 7:35 mchana Baraza liliakhirishwa mpaka sasa 11:00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

TAARIFA ZA SERIKALI

Ripoti za Wizara za Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Fedha Biashara na Kilimo 2011/2012

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwanza kabisa napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia tukiwa wazima wa afya njema. Aidha napenda pia kukushukuru wewe binafsi Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi hii ya kutoa taarifa juu ya utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa na Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo.

Mhe. Spika, napenda pia kutoa shukurani za kipekee kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati inayosimamia Ofisi ya Rais, Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo chini ya uongozi wa Mwenyekiti wao Mhe. Salmin Awadh Salmin Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Magomeni kwa kuisaidia sana Ofisi yangu katika kutuongoza na kutushauri kwa nia ya kufanikisha utekelezaji wa majukumu mbali mbali ya Ofisi yangu na serikali kwa ujumla kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Spika, nachukua fursa hii kuwashukuru pia Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kutuongoza katika kufanikisha majukumu yetu ya kila siku. Aidha ninawashukuru kwa kuchangia hotuba na taarifa mbali mbali zilizokuwa zikitolewa kwa lengo la kusaidia utekelezaji wa shughuli za ofisi yangu na serikali kwa ujumla. Nakuombeni sana muendelee kuipatia

miongozo Ofisi ya Rais, Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo, kwani kufanya hivyo ni pamoja na kutekeleza majukumu yenu kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, serikali kupitia Ofisi yangu haitasita katika kuhakikisha kuwa uchumi wa nchi yetu unakua na hatimaye kupatikana mapato zaidi yatakayotuwezesha kuendeleza ujenzi wa miundombinu pamoja na kukuza ustawi wa wananchi wetu. Aidha suala la kukaribisha wawekezaji katika kusukuma maendeleo yetu pamoja na upatikanaji wa ajira kwa wananchi wetu, litaendelea kupewa msukumo wa kipekee na serikali yetu.

Mhe. Spika, mnamo mwezi wa Aprili, mwaka 2012 Mhe. Salmin Awadh Salmin Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha Biashara na Kilimo alisoma taarifa kwa niaba ya Kamati yake na kuchangiwa na Wajumbe wa Baraza lako tukufu, maelezo ya kamati pamoja na michango mbali mbali ya Wajumbe tuliichukua na kuifanyia kazi kadri ya uwezo wetu.

Aidha kwa mujibu wa kanuni za Baraza kifungu 108 kifungu kidogo 15 kinamtaka kila Waziri kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu taarifa ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati. Na mimi nikiwa ni miongoni mwa Mawaziri nina wajibu pia wa kutoa taarifa juu ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati.

Mhe. Spika, kutumia kifungu hicho cha kanuni nimesimama mbele ya Baraza lako tukufu kutoa taarifa ya utekelezaji wa maagizo kumi na tano yaliyotolewa na Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, agizo la kwanza ambalo Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ilitoa kwa Ofisi yangu ni kwamba serikali zote mbili ile ya Mapinduzi ya Zanzibar na ile ya Muungano zisimamie utekelezaji wa utaratibu wa kuhakikisha kuwa kodi ya mapato kwa wafanyakazi wa Jamhuri ya Muungano Tanzania wanaoishi Zanzibar, kodi yao ya mapato *PAYE* iwe inakusanywa Zanzibar kupitia Bodi ya Mapato kama wakala.

Mhe. Spika, utekelezaji katika agizo hili kwa kuwa suala hili ni la Muungano kikatiba, serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia wakala wake *TRA* ndio wanaokusanya kodi hii. Aidha kuanzia Julai, 2012 tumekuwa tukipokea jumla ya shilingi bilioni 1.75 kwa mwezi ikiwa ni kodi ya mapato *PAYE* kwa wafanyakazi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanaofanya kazi Zanzibar.

Mhe. Spika, agizo la pili ni kwamba utaratibu wa ukusanyaji wa kodi wa *visa* ubadilishwe kwani utaratibu unaotumika hivi sasa hauoneshi uasilia wa mapato halisi sambamba na idadi ya wageni wanaoingia nchini.

Utekelezaji, Mhe. Spika, Wizara inafanya *study* kuangalia mfumo utakaotumika wa kukusanya kodi za *visa* kutoka kwa wageni wanaoingia. Aidha *study* hii iko katika hatua za mwisho kukamilika.

Agizo la tatu Mhe. Spika, lilikuwa ni suala la magendo ya mafuta linahitaji msukumo wa pamoja kati ya vyombo vya ulinzi Bandarini na wananchi kwa ujumla, wavuvi na wale wanaotumia bandari zisizo rasmi. Utekelezaji wake ni kwamba matayarisho yanafanywa kuona kuwa kero hii

nayo inaondoshwa kama ilivyokuwa kero ya magendo ya karafuu ambayo serikali iliweka mkakati maalum wa kuwezesha kuondoshwa kero hiyo.

Agizo la nne Mhe. Spika, ilikuwa elimu itolewe kwa wafanyabiashara ikiwa ni msisitizo wa kuhakikisha kuwa kila mfanyabiashara anatoa risiti bila hata kuombwa na mteja au kuweka masharti ya kupunguza bei iwapo mteja hatapatiwa risiti. Utekelezaji wa agizo hili Mhe. Spika, ni kwamba elimu inaendelea kutolewa kwa wafanyabiashara na kwa wananchi kwa ujumla kupitia vipindi vya redio na televisheni mbali mbali.

Mbali na utayarishaji wa vipindi hivyo mikutano mbali mbali imefanywa inayowashirikisha walengwa ambao huzungumziwa na kuelimishwa umuhimu wa utoaji stakabadhi wakati wa mauzo, kwa madhumuni ya kupata usaidizi katika usimamizi, kiliandaliwa kikao baina ya uongozi wa Jeshi la Polisi, ngazi za Wilaya zote na *ZRB* chenye lengo la kuelimisha aina ya nyaraka zinazohitajika kuwa nazo kwa anayesafirisha bidhaa na hata kwa raia mmoja mmoja ili kumthibitisha uhalali wa kumiliki bidhaa hiyo. Hivi sasa unafikiriwa kuwepo utaratibu wa kuwawekea mashine Wizara za biashara zitakazowawezesha kupatikana kwa taarifa zao za mauzo na kuonekana moja kwa moja katika Taasisi zinazohusika na usimamizi wa kodi.

Mhe. Spika, agizo la tano lilikuwa utaratibu uandaliwe kuanzisha mfumo wa utoaji risiti uliounganishwa na mtandao *electronic receipt* ambao utamuwezesha kila mfanyabiashara kuwa na risiti. Kama tulivyogusia katika agizo namba 4, suala la utoaji wa risiti kwa kutumia utaratibu uliounganishwa na mtandao jambo hili limeshaanza kufikiriwa na namna ya utekelezaji wake kupitia mfumo wa *e-revenue*.

Agizo la sita Mhe. Spika, lilikuwa kuwe na udhibiti mzuri wa ukusanyaji wa kodi za mahoteli ili kuwe na uwiano ulio na idadi sawa ya wageni wanaoingia Zanzibar na kulala hotelini na mapato yanayokusanywa. Aidha mapato yanayokusanywa yaendane na viwango vya mahoteli yenyewe.

Mhe. Spika, utekelezaji wa suala hili ni kuwa suala la kupata uwiano wa wageni wanaoingia nchini na ile ya idadi ya wageni wanaolala katika mahoteli linaendelea kufanyiwa kazi baada ya kubainika kuwepo kwa kasoro kubwa ya kitakwimu katika mahoteli kuwiana na viwango vya hoteli, ni kuwa suala hili nalo limeshaanza kufanyiwa kazi kwa kuitaka Kamisheni ya Utalii kuhakikisha ukamilishaji wa kuziwekea daraja hoteli zote za Zanzibar.

Kuwepo kwa daraja za mahoteli itakuwa ni msingi utakaowezesha kueleweka viwango vya kutozea huduma zinazotolewa katika hoteli hizi, jambo ambalo hivi sasa linakosekana na kusababisha kutowepo kwa uwiano wa uchangiaji wa mapato.

Agizo la Saba Mhe. Spika, lilikuwa ni *TRA* Zanzibar iangalie sana malipo ya ushuru unaotolewa ili kuwe na malipo ya tofauti ya ushuru huo, ili kusiwe na malipo tofauti ya ushuru huo iwapo bidhaa itasafirishwa kupelekwa Tanzania Bara. Mhe. Spika, utekelezaji wake ni kwamba serikali inazingatia kuangalia kwa kina wazo la kutumia *centralized imports and exports valuation data base* kwa kuangalia faida za kiuchumi, kisiasa na kijamii ili kuepuka malipo ya tofauti ya ushuru kwa bidhaa zinazosafirishwa Tanzania Bara. Suala hili tuna Kamati tumeunda na tunalifanyia kazi kati ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Muungano kupitia vyombo vyetu vya *TRA* na *ZRB*.

Mhe. Spika, agizo la nane ni kwamba sheria namba 6 ya mwaka 1996 ya ushuru wa stempu ifanyiwe marekebisho ili kuwe na uwezekano wa kuweka kiwango maalum cha kodi ya mapato badala ya makisio. Hapa Mhe. Spika, nataka kusema kwamba kuna kodi mbili hapa zimejichanganya. La kwanza ni suala zima la ushuru wa stempu, huu ni ushuru ambao hapo awali ilikuwa tunatoza asilimia moja kwa wale wote ambao wanakwenda kutaka kukopa kupitia mabenki. Kutokana na kwamba hiyo asilimia moja tumeiona ni kubwa sasa hivi tumepunguza na tumesema kwamba haitazidi shilingi laki moja kwa mkopo wowote ule ambao utakaokopwa na mabenki, haitazidi shilingi laki moja.

Lakini la pili hapa ni kodi ya mapato, Mheshimiwa kodi ya mapato *income tax* kwa maana *PAYE* na *corporate tax* sasa hivi *PAYE* kila mshahara una kodi ya aina yake na hizo tumezipitisha katika *finance bill* ambayo tuloisoma mwezi wa Julai wakati tunamaliza bajeti. Lakini vile vile tumegundua kwamba *corporate tax* asilimia 30 ni kubwa nayo vile vile tunaifanyia marekebisho ili tuweze kuwapunguzia wafanyabiashara wetu na kuendelea kulipa.

Agizo la Tisa Mhe. Spika, serikali iweke kipaumbele wa ujenzi kwenye miundombinu katika maeneo huru ya uchumi ili iwe kivutio kwa Wawekezaji. Utekelezaji ni kwamba serikali imeweka kipaumbele katika ujenzi wa miundombinu katika maeneo huru ya kiuchumi hii itategemea na zaidi juu ya uwezo wa serikali. Lakini hata hivyo tayari tumeanza kufanya mawasiliano na Wawekezaji mbali mbali ili tuweze kuingia nao ubia katika ujenzi na uendeshaji wa maeneo huru ya kiuchumi.

Agizo la kumi lilikuwa ni mamlaka inayosimamia utoaji wa huduma za bima *TIRA* iangalie vyema kanuni zake hasa ile inayohusiana na umiliki wa mali zisizohamishika *fixed asset* ili kampuni zinazotoa huduma za Bima ziweze kumiliki wenyewe majengo ya Ofisi badala ya kukodi. Mhe. Spika, na mimi nakubaliana na agizo hili. Lakini kwa nini kifungu hiki kimewekwa chini ya *TIRA*, utaratibu huu unaotumiwa na *TIRA* una lengo la kuwalinda wateja hasa ukizingatia fedha ambazo zitatumika ni za wateja.

Kwa hivyo mimi nakubali kwamba tuwe na majengo yetu, lakini vile vile lazima tuangalie jinsi ya kuwalinda wateja kwa sababu tukiruhusu ujenzi wanaweza wakamaliza fedha za wateja kwa ujenzi na halafu bahati mbaya ikitokea kama ilivyotokea kwa Shirika la Bima la Taifa wateja wanataka pesa zao lakini pesa hawana ikabidi Shirika la Bima la Taifa auze majengo.

Agizo la kumi na moja Mhe. Spika, Shirika la Bima la Zanzibar likamilishe taratibu zake za kuanzisha bima inayoendana na maadili ya kiislam; *takaful*. Shirika la Bima la Zanzibar tayari limeshafanya matayarisho ya kuanzisha Bima inayoendana na maadili ya kiislam, tunachokisubiri sasa hivi ni kibali tu kutoka *TIRA* ili tuweze kuanzisha shughuli hiyo.

Agizo la kumi na mbili Mhe. Spika, serikali izitumie kikamilifu takwimu zinazotolewa na Mtakwimu Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuweka vipaumbele vya miradi na mipango mengine ya maendeleo. Serikali inatumia na itaendelea kutumia takwimu zinazotolewa na Mtakwimu Mkuu wa Serikali katika kuyatarisha mipango ya maendeleo ya taifa na kutoa vipaumbele. Ni muhimu kwa sekta binafsi nayo pia kusaidia kutekeleza mipango hiyo.

Agizo la kumi na tatu Mhe. Spika, ni kwamba bado wananchi wanashindwa kufahamu kwa undani madhumuni ya takwimu na suala zima la kuhesabiwa yaani sensa, hivyo elimu zaidi inahitajika kutolewa kwa wananchi ili waweze kutoa taarifa kwa usahihi kabisa.

Mhe. Spika, hatua zilizochukuliwa ni kwamba mafunzo yametolewa na wananchi wengi waliotufahamu wameweza kushirikiana na sisi katika kutoa taarifa wakati wa kipindi cha sensa. Lakini kwa sababu sensa ni kila baada ya miaka 10 basi tutaendelea kutoa taarifa, tutaendelea kutoa mafunzo, tutaendelea kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa kutoa taarifa kwa ajili ya sensa. Takwimu za sensa sasa hivi ziko wazi, takwimu za sensa sasa hivi zimeshaanza kutumika, na kwa kweli tumeshuhudia asilimia 46.6 ya watu wanaoishi Zanzibar wapo katika Mkoa wa Mjini Magharibi. Hiyo ni muhimu kwa takwimu katika mipango yetu inaonesha kwamba asilimia 50 ya mipango yetu tuielekeze katika Mkoa huu kwa sababu karibu nusu ya watu wetu wanaishi katika Mkoa huo. Kwa hivyo huo ndio umuhimu wa kutumia takwimu katika mipango.

Mhe. Spika, agizo la kumi na nne, Kamati inaagiza Bodi ya Mapato Zanzibar ihakikishe kuwa inawatambua na kuwasajili wafanyabiashara wote wakubwa na wadogo. Nataka nikubaliane na Kamati kwamba ni vizuri kuwatambua na kuwasajili. Bila ya kuwatambua na bila ya kuwasajili hawa hawatalipa kodi hawa. Kwa hivyo tunachokifanya sasa hivi hii ni shughuli endelevu na tunashirikiana sana sana na Mamlaka ya Leseni ili kuweza kuona kwamba hawa wafanyabiashara wote wanasajiliwa na hatimae wanalipa kodi.

Tatizo tulilonalo sasa hivi ni wale wafanyabiashara tunaowaita tupa tupa jua kali, machinga ndio tatizo letu. Lakini na wao tunaanza kuwatafutia dawa ili na wao kwa sababu wanafanya biashara waweze kushiriki katika ulipaji wa kodi, *of course* wao watakuwa kidogo tafauti na wale wengine wakubwa. Lakini wanalazimika na wao kuchangia katika ulipaji wa kodi, hili nimefarajika sana na agizo hili na tutaendelea kulifanyia kazi na tutakuwa tunatoa taarifa kupitia kwenye bajeti zetu kila tutakaposoma bajeti.

Agizo la kumi na tano Mhe. Spika, na ni agizo la mwisho. Kamati inaagiza kuwa wafanyabiashara wote kuwa wanafanya mauzo katika maeneo ya biashara na wanatoa ankara za kodi kwani hivi sasa walipa kodi wengi hawatoi risiti wanapofanya mauzo. Utekelezaji wake ni sawa na agizo la nne na agizo la tano. Ukitaka kufanya biashara lazima uwe na eneo la kufanyia biashara ndipo utapoweza kulipa kodi. Tatizo kubwa tulilonalo ni hawa wafanyabiashara wanaotembea tembea na hasa wale wa jua kali waliopo Darajani. Tukifanikiwa na wao kuwawekea pale eneo tukijenga *mole* pale Darajani na wao tukawatafutia eneo ndani ya *mole* lile wakafanya biashara zao, mimi nina imani kubwa sana wataweza kuchangia na wao katika maendeleo yetu.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo ni matumaini yangu kwamba nimetoa ufafanuzi kadri ya uwezo wangu na pale ambapo Kamati itaona bado hawajapata ufafanuzi, ofisi yangu iko wazi na ofisi zao najua ziko wazi basi tuitane tu tuweze kutoa ufafanuzi na tujenge heshima ya serikali yetu na nchi yetu.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:(Kny. Waziri wa Kilimo na Maliasili) Mhe. Spika, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia tena kutuwezesha kukutana tena hivi jioni na kuendelea katika shughuli za Baraza. Aidha nikushukuru wewe Mhe. Spika, niwashukuru na Wajumbe wa Kamati yetu hii ya Kilimo, Maliasili na Wajumbe wa Baraza hili tukufu kwa namna ambavyo wanavyojitahidi kusaidia, kushauri na maelekezo ili kufanikisha shughuli za serikali.

Mhe. Spika, taarifa hii inahusu utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa na Kamati ya Kilimo, Fedha na Biashara ya Baraza la Wawakilishi baada ya ziara zake katika Wizara ya Kilimo na Maliasili na kutembelea miradi mbali mbali kwa ajili ya malengo ya bajeti kama inavyoainishwa katika vikao vya Kamati za kudumu za Baraza la Wawakilishi ya mwaka 2011/2012.

Mhe. Sekta za kilimo na maliasili bado zinaendelea kuwa ni mhimili mkuu wa uchumi wa Zanzibar ambapo inatoa mchango wa moja kwa moja katika kujikimu kimaisha kuwa na uhakika wa chakula lishe na afya za wananchi walio wengi vijijini na mjini, na kwa hivyo ina jukumu kubwa katika maisha yetu. Kwa mwaka wa fedha 2011/2012 sekta hizi zilichangia asilimia thalathini ya pato la taifa na inakadiriwa kuwa zaidi ya asilimia 70 ya wananchi wanategemea sekta hii kwa kuwapatia ajira na mapato yao ya kila siku.

Mhe. Spika, kufuatilia malengo ya utekelezaji wa malengo ya bajeti za Wizara ya Kilimo na Maliasili ya mwaka 2011/2012 Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Fedha Biashara na Kilimo ilitoa maagizo na ushauri kwa Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa lengo la kuongeza ufanisi na katika utekelezaji wa kazi za Wizara.

Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo na Maliasili inaomba kuwasilisha utekelezaji wa ushauri, maoni na maagizo yaliyotolewa na Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi kwa mwaka 2011/2012 kama hivi ifuatavyo:

Mhe. Spika, agizo namba moja sheria na kanuni zinazohusiana na makosa ya uharibifu wa misitu na maliasili na nyengine zipitiwe upya kwani inaonekana adhabu zilizowekwa ni ndogo kiasi cha kutomtia khofu anayetenda makosa.

Utekelezaji Wizara ya Kilimo na Maliasili imetekeleza agizo hilo kwa kufanya mambo muhimu yafuatayo:

a) Kufanya mapitio ya sera ya misitu, rasimu mpya ya sera ya misitu imetayarishwa na itakamilishwa mara baada ya kukamilika kwa sensa ya miti inayoendelea kufanyika Unguja na Pemba kwa ufadhili wa ubalozi wa Norway.

b) Utayarishaji wa kanuni mpya yenye kuonesha viwango vipya vya faini na adhabu mbali mbali kwa makosa ya matumizi mabaya ya maliasili, kanuni hiyo tayari imechapishwa katika gazeti rasmi la serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

c) Utayarishaji wa kanuni ya kudhibiti matumizi mabaya ya msumeno wa moto tayari imekamilika, kanuni hiyo imechapishwa katika gazeti rasmi la serikali na inaendelea

kutumika kwa mafanikio makubwa. Changamoto ya matumizi ya msumeno wa moto ni kubwa sana na zinahitaji mashirikiano makubwa.

d) Kanuni za viwango vipya vya bei na huduma mbali mbali za maliasili imekamilishwa, utaratibu wa ruhusa wa bei hizo Wizara ya Fedha itaendelea kuichapisha katika gazeti rasmi. Maelezo ya ziada usimamizi bora wa maliasili unahitaji ushiriki mkubwa kati ya sekta husika na wananchi na vyombo vya dola.

Agizo la pili upandaji wa mikarafuu mipya uwe ni mkakati wa makusudi kwa Wizara na isimamie kwa karibu zoezi hili hasa katika makuzi ya mikarafuu hiyo kila mwaka tuwe na takwimu halisi inayoonesha idadi iliyopandwa, iliyokua vizuri, maeneo yaliyoonesha kiwango kizuri cha ukuaji na yale ambayo hayakufanikiwa pamoja na sababu ya kitaalamu ya matokeo hayo.

Utekelezaji, Wizara ya Kilimo na Maliasili inaendelea kuratibu upandaji wa mikarafuu na maendeleo ya jumla ya zao la karafuu kwa lengo la kuongeza uzalishaji na kuinua uchumi wa jamii na taifa kwa jumla kama ifuatavyo:

a) Kuotesha miche milioni moja kila mwaka ambapo kwa mwaka 2012/2013 jumla ya miche laki saba imeoteshwa. Aidha miche hiyo imetolewa kwa wananchi bila ya malipo.
b) Kutengeneza daftari la wakulima wa mikarafuu Zanzibar kwa lengo la kujua wale wote ambao wanachukua miche na kuwapatia huduma mbali mbali.
c) Kufanya tathmini ya miche ya mikarafuu iliyopandwa kwa kila mwaka kwa lengo la kujua wastani wa miche iliyostawi na kuendelea kukua vizuri.

Aidha mwaka 2011/2012 wastani wa miche laki tano ishirini na mbili elfu imepandwa na asilimia 51 imeota vizuri kwa Pemba na kwa Unguja wastani wa asilimia 36 kwa mwaka 2011/2012.

Wizara imejipanga kutoa elimu zaidi na kuwahamasisha wakulima katika kuhakikisha uzalishaji wa karafuu unaongezeka. Maelezo ya ziada Wizara ya Kilimo na Maliasili imejipanga kuongeza mabwana shamba na mabibi shamba ili kuongeza elimu na huduma bora za mikarafuu.

Agizo la tatu Chuo cha Kilimo Kizimbani kizidi kuendelezwa ili kiwe miongoni mwa vyuo vya kilimo vinavyotoa elimu hiyo kwa kiwango cha shahada yaani degree. Malengo ya muda mrefu ya Kituo cha Kilimo Kizimbani ni kutoa wahitimu wa degree katika kutekeleza lengo hilo kuanzia mwaka 2012 chuo hiki kimeanza kufanya mageuzi makubwa na kuanzisha *course* za diploma za aina tatu ambazo ni kama ifuatavyo:

1) Uzalishaji wa mazao wa kilimo, *diploma in crop production*.
2) Uzalishaji wa mifugo *diploma in animal production*
3) Kilimo cha majumuisho *diploma in general agriculture*

Uanzishwaji wa kozi hizi umewezekana kutokana na juhudi zilizofanyika za kukiimarisha chuo katika Nyanja zifuatazo:

1) Kukisajili Chuo kwenye Baraza linalosimamia vyuo vya ufundi Tanzania *NACTE*, kutokana na usajili huu Chuo kinaruhusiwa kutoa mafunzo hadi ngazi ya *degree* katika Nyanja za kilimo, mifugo na maliasili.
2) Ujenzi wa dakhalia mpya kwa ajili ya kuongeza makaazi ya wanafunzi.
3) Uimarishaji wa kitengo cha sayansi ya mifugo kukipatia maabara, vifaa na mifugo ya kisasa kwa ajili ya kazi za kufundishia.
4) Ununuzi wa vifaa vya kisasa kwa ajili ya kufundishia kama vile *projectors*.
5) Mafunzo kwa walimu juu ya mbinu ya kufundishia.
6) Uimarishaji wa maktaba ya Chuo kwa kuipatia vitabu na vifaa vya *electronic* kama vile *photocopy*, *scanners*, *computer* na huduma ya mtandao *internet*.

Kazi za kuimarisha chuo ambazo bado zinaendelea ni kama zifuatazo:

1) Kutayarisha mpango mkakati wa Chuo.
2) Ujenzi wa dakhalia mpya la ghorofa 4 kwa ajili ya kuongezea makaazi ya wanafunzi.
3) Kuviimarisha vitengo vya sayansi ya mifugo na sayansi ya mazao kwa kuimarisha mafunzo kwa njia ya vitendo na maonesho ya ufugaji ng'ombe na mbuzi wa maziwa na ukulima bora wa mazao ya mboga na viungo.
4) Mafunzo kwa walimu 10 ngazi ya digirii ya pili yanafanyika.
5) Uimarishaji wa Maktaba kwa kuipatia vitabu.

Agizo la nne, wakulima wapatiwe mbegu bora za mpunga zinazozalishwa kwa wakati ili wawahi msimu wa kilimo cha mpunga.

Utekelezaji. Kwa mujibu wa kitabu cha bajeti ya Wizara ya Kilimo, Wizara iliahidi kuwapatia wakulima mbegu bora na kwa wakati jumla ya tani 322 zilizotolewa msimu wa mwaka 2011/2012 kwa wakulima. Mbegu ya *BKN super* ilizalishwa makusudi kwa hadhari pindi ikitokea baadhi ya wakulima kuharibikiwa na kulazimika kupanda tena ili wawahi wakati. Shabaha hiyo ilifanikiwa kwa kuwapatia wakulima walioharibikiwa msimu huu kutokana na jua kali. Jumla ya tani 74 za *BKN super* zimetolewa hapa Unguja na tani 20 zimetayarishwa kwa wakulima wa Pemba.

Agizo la tano, Wizara itayarishe maombi ya fedha serikalini mapema ili fedha hizo zipatikane kwa wakati wa msimu unaoendana na kilimo.

Utekelezaji. Kwa kawaida maombi yote ya fedha za utekelezaji wa kazi za Wizara huwa yanawasilishwa Wizara ya Fedha kwa wakati kwa mujibu wa bajeti ya serikali inayoanzia mwezi wa Julai wa kila mwaka.

Aidha, Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa mwaka wa fedha 2011/2012 kwa kupitia Idara ya Kilimo kwa kipindi cha Julai hadi Juni 2012, Idara imepata jumla ya Tanzania shilingi bilioni moja, milioni kumi na tisa laki tisa na saba mia tisa sitini na tatu sawa na asilimia 19.9 ya fedha zilizotengwa.

Agizo la sita wakulima wapatiwe huduma ya matrekta mapema kwa ajili ya kuchimba na kuburuga.

Utejekezaji. Wizara ya Kilimo ilipanga kutengeneza matrekta 37 Unguja na Pemba kwa msimu wa mwaka 2011/2012 ili kuanza kuingia mabondeni mapema. Mpango huu ulianza kupeleka matrekta na kuanza kuchimba mapema kama ilivyopangwa. Hivyo kwa upande wa wakulima pia kunahitajika juhudi za kuhamasishwa wakulima kujitokeza kwa wakati na kwa pamoja hapo ndio kazi itakuwa rahisi zaidi katika kuendeleza kilimo nchini.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba kuwasilisha na nawaomba Wajumbe waichangie ili tupate muongozo wa ziada tuweze kutekeleza vizuri wajibu wetu wa kuimarisha kilimo nchini.

Mhe. Waziri wa Afya: (Kny. ya Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko) Mhe. Spika, ninakushukuru sana kwa kuniruhusu kusoma kwa niaba ya Waziri wa Biashara maelezo ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi, kuhusu biashara, viwanda na masoko.

Mhe. Spika, naomba kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia sote kuwa na afya njema na uzima uliotuwezesha kufika hapa leo na kuweza kutekeleza majukumu yetu ya kitaifa tuliyopewa. Aidha, naomba kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kutoa maelezo ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kuhusu utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa mwaka 2011/2012.

Mhe. Spika, naomba kumshukuru Mwenyekiti, Mhe. Salmin Awadh Salmin pamoja na Wajumbe wake wa Kamati. Maendeleo makubwa yanayopatikana katika Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa sehemu kubwa yanatokana na ushauri pamoja na miongozo inayochangiwa na Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo. Ushirikiano wetu baina ya kamati na wizara ni mzuri sana na ndio unaotufanya kuweza kutimiza majukumu yetu ya kuendeleza biashara, viwanda na kuwasaidia wazalishaji na wajasiriamali kwa ujumla.

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa napenda kuwapongeza na kuwashukuru Wajumbe wenzangu wote wa Baraza la Wawakilishi kwa jinsi wanavyonipa ushirikiano wa dhati kwangu, mimi binafsi pamoja na watendaji wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Tunaamini kwamba maelekezo ya Baraza hili tukufu ni sehemu kubwa ya wizara yangu kupata mafanikio katika utekelezaji wa malengo yake. Ninawaomba Waheshimiwa Wajumbe waendelee kushirikiana na wizara yangu ili tuweze kuimarisha na kutelekeza majukumu yetu kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Spika, baada ya kutoa maelezo hayo ya shukurani naomba kueleza kwamba katika Ripoti za Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi Zanzibar kwa mwaka 2011/2012, wizara iliagizwa kutekeleza maagizo 13. Naomba sasa uniruhusu kutoa maelezo ya utekelezaji wa maagizo hayo kwa njia ya bangokitita kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, Agizo la Kwanza. Kuna haja ya kuwaelimisha wakulima umuhimu wa kuwepo kwa wachukuzi na majukumu yao ili ipatikane njia muwafaka itakayoondosha mgongano kati yao.

Utekelezaji:
Wakulima wanaendelea kufahamishwa kwamba jukumu la kulipia gharama za uchukuzi wa karafuu kutoka katika gari kuja kituoni ni la mkulima. Kwa kuwa karafuu hizo zinakuwa bado hazijanunuliwa na shirika.

Agizo la Pili, Kamati inazishauri Serikali za Wilaya kuwa na uwiano wa bei za vyeti vya mazao kati ya Halmashauri moja na nyengine.

Utekelezaji:
Kwa kuwa cheti hicho kinachoelezwa ni kwa ajili ya mazao yote ya kilimo na si karafuu peke yake, wizara yangu inashauri suala la kufanyiwa kazi kwa ujumla wake na taasisi zinazohusika ikiwemo Wizara ya Kilimo na Maliasili na Tawala za Mikoa.

Agizo la Tatu, Kamati inalishauri shirika kuangalia uwezekano wa kununua aina nyengine ya menzani ya kisasa zaidi (*digital*), ili kuondosha wasi wasi wa baadhi ya wakulima wanaouza karafuu juu ya uwezo wa menzani zilizopo sasa.

Utekelezaji:
Shirika limeshanunua menzani kumi za kisasa (*digital*), kwa ajili ya kupimia karafuu zinazosafirishwa. Aidha, shirika limo katika utaratibu wa kununua menzani nyengine 33 kwa ajili ya ununuzi wa karafuu katika vituo.

Ununuzi wa menzani katika vituo unakwenda sambamba na ukarabati wa vituo na uwekaji wa umeme katika vituo hivyo.

Agizo la Nne, suala la kusafirisha karafuu kutoka Wilaya moja kwenda nyengine zikiwa mbichi au kavu, kamati inashauri bado serikali iliangalie kwa makini na iandae utaratibu mzuri wa kutoa vibali ili vibali hivyo visitoe fursa ya upelekwaji wa karafuu mahali pasipostahiki.

Utekelezaji:
Wizara yangu imelizingatia suala hili na tayari sheria na kanuni zinazohusika na uhamishaji wa karafuu zinafanyiwa marekebisho katika mapitioi ya sheria ya karafuu ya mwaka 1985 yanayoendelea.

Agizo la Tano, kamati inashauri kufanyiwa matengenezo majengo ya vituo vya ununuzi wa karafuu pamoja na ujengwaji wa vyoo.

Utekelezaji:
Shirika limepanga kufanya ukarabati wa vituo vyote 32 vya kununulia karafuu. Katika kipindi hiki ukarabati wa vituo vitano umefanyika na linaendelea na hatua za kufanya matengenezo ya vituo vingine vitano. Aidha, katika matengenezo hayo yanajumuisha uwekaji wa vyoo, huduma ya maji na sehemu ya kupumzikia.

Vituo vilivyojengwa ni Mzambarautakau, Chonga, Kinyasini, Raha na Mkanyageni. Awamu inayofuata vitajumuisha vituo vya Gando, Bwagamoyo, Chanjaani, Chambani na Wambaa.

Agizo la Sita, bado hakuna uwiano wa bei za bidhaa hasa za vyakula zinazouzwa katika sehemu moja. Hivyo wizara haina budi kufanya ukaguzi wa mara kwa mara ili kuhakikisha kwamba yale makubaliano ya bei kati yao na wafanyabiashara yanatekelezwa kama walivyokubaliana.

Utekelezaji:
Wizara huwa na utaratibu wa kukutana na wafanyabiashara kwa ajili ya kuweka bei za bidhaa muhimu kila inapotokezea mahitaji ya kufanya hivyo. Mahitaji hayo ni pamoja na mabadiliko ya bei za unuuzi katika soko la dunia, kiwango cha kubadilisha fedha za kigeni.

Hivi sasa bidhaa muhimu zinauzwa kwa mujibu wa makubaliano ambapo kilo moja ya mchele inauzwa shilingi elfu moja mpaka elfu moja na mia moja, kilo ya sukari inauzwa shilingi elfu moja mia nne mpaka elfu moja mia tano na unga wa ngano shilingi elfu moja na mia moja. Gharama za usafiri, gharama za utoaji wa mizigo. Aidha, wizara hufanya ukaguzi kila siku kwa ajili ya kuhakikisha kwamba bei zilizokubaliwa zinafuatwa.

Agizo la Saba, juhudi za makusudi zifanyike ili kujua idadi sahihi ya maghala na maduka yanayouzwa bidhaa kwa ujumla na rejareja.

Utekelezaji:
Wizara inaendelea kufanya tathmini maalum kwa ajili ya kutambua idadi kamili ya maghala na maduka yanayouza jumla na rejareja. Utafiti huo utajumuisha pia idadi ya mabekari na mezani za kupimia bidhaa kwa wateja.

Agizo la Nane, zabuni kwa ajili ya matayarisho ya Uwanja wa Kimataifa wa Maonesho ya Biashara itangazwe mapema ili matumizi na gharama za eneo hili zifahamike na walengwa.

Utekelezaji:
Kutokana na gharama kubwa na utaalamu unaohitajika katika kuendeleza mradi huu, serikali imeamua kuishirikisha sekta binafsi. Katika hatua za awali za utekelezaji, wizara imeshatayarisha nyaraka za zabuni kwa ajili ya kutafuta mwekezaji pamoja na mshauri mwelekezi. Hatua hizo zinatujumuisha matayarisho ya upembuzi yakinifu, mpango wa matumizi wa eneo hilo pamoja na gharama za ujenzi.

Agizo la Tisa, ukarabati wa maghala ya kuhifadhia chakula cha hakiba ya nchi pamoja na matayarisho mengine yanayohusiana na uhifadhi huo kwa mujibu wa sheria ufanyike haraka ili angalau mwakani maghala hayo yaweze kutumika kwa kuhifadhia chakula cha hakiba.

Utekelezaji:
Suala hili la maghala ya hakiba ya chakula linasimamiwa na Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa mujibu wa sheria Nam. 5 ya chakula cha hakiba na lishe ya mwaka 2011.

Agizo la Kumi, wizara isimamie suala la uhifadhi wa mafuta ya nchi kwa ajili ya mafuta ya dharura.

Utekelezaji:
Suala hili la hakiba ya mafuta ni muhimu kwa nchi. Hata hivyo, wizara haijapewa mamlaka ya kisheria ya kusimamia hakiba ya mafuta.

Agizo la Kumi na Moja, wizara iharakishe kufanya marekebisho ya Sera ya Viwanda ili iendane na wakati na iwe na vivutio kwa wawekezaji katika Sekta ya Viwanda.

Utekelezaji:
Wizara ya kwa kushirikiana na *UNIDO* na SMT inaendelea na matayarisho ya Sera ya Viwanda na awamu mbili zimeshakamilika kati ya awamu nne za utayarishaji wa sera. Awamu zilizokamilika ni matayarisho ya Mpango Kazi na Ripoti ya Ushindani wa Viwanda. Hatua zinazofuata ni matayarisho ya mkakati na Sera ya Viwanda.

Agizo la Kumi na Mbili, kamati inaagiza wizara kuajiri wafanyakazi wa ukaguzi wa bidhaa wenye ujuzi wa kutosha na kuwapatia vitendea kazi.

Utekelezaji:
Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara imeomba wafanyakazi watano wenye kiwango cha elimu ya shahada ya kwanza na kuendelea katika sehemu ya ukaguzi na imeruhusiwa kuajiri watatu. Kwa upande wa vifaa, wizara imenunua vifaa vya ukaguzi vikiwemo *mask*, makoti ya ukaguzi, *prove* kwa ukaguzi wa bidhaa ya ujazo wa mafuta, vifaa vya bidhaa zilizofungashwa na vifaa vya mezani.

Agizo la Kumi na Tatu na la mwisho Mhe. Spika, elimu zaidi inahitajika kwa wajasiriamali ili waweze kutengeneza bidhaa zitakazoweza kukabiliana na ushindani katika masoko.

Utekelezaji:
Suala la kuwafundisha wajasiriamali ni mtambuka ambalo linatekelezwa na taasisi za serikali na watu binafsi. Kwa upande wa wizara imetoa mafunzo kwa wajasiriamali yanayohusu mpango wa biashara, njia bora za uzalishaji, ufungishaji wa bidhaa na utafutaji wa masoko.

Mhe. Spika, baada ya kueleza hayo kwa heshima na taadhima naomba kuwasilisha na wenzangu wapate nafasi ya kujadili.

Mhe. Salmin Awadh Salmin (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Mhe. Spika, ufuatao ni muhtasari wa Hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi kuhusu Ripoti ya Kamati ya mwaka 2013/2014.

Mhe. Spika, awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru Allah kwa kutuwezesha siku hii ya leo kuwasilisha mbele ya Baraza lako Tukufu muhtasari wa ripoti ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo na maoni ya Kamati juu ya ripoti hiyo.

Aidha, napenda kuitumia nafasi hii kwa niaba ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, kukushukuru wewe Mhe. Spika, Katibu wa Baraza la Wawakilishi na watendaji wako wote kwa kuiwezesha kamati kufanya kazi zake zote bila ya matatizo katika kipindi chote cha miaka miwili na nusu, tunakushuru sana.

Mhe. Spika, napenda kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati hii ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa mashirikiano yao. Katika utekelezaji wa kazi zao za Kamati, ushirikiano ambao umeniwezesha kuingoza Kamati katika kipindi chote bila ya matatizo yoyote nawashukuru na kuwapongeza sana.

Mhe. Spika, kabla ya kutoa maoni ya Kamati, napenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri, Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, Mhe. Omar Yussuf Mzee, Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Mhe. Nassor Ahmed Mazrui pamoja na Naibu wa Wizara hio Mhe. Thuwaybah Edington Kisasi. Waziri wa Kilimo na Maliasili, Mhe. Suleiman Othman Nyanga pamoja na Naibu Waziri Mhe. Mtumwa Kheri Mbarak kwa mashirikiano makubwa waliotupa katika kipindi chote cha Kamati hii ambayo kipindi hiki inamaliza muda wake kwa mujibu wa Kanuni ya 107(4) Kanuni ya Baraza la Wawakilishi la Zanzibar Toleo la mwaka 2011.

Mhe. Spika, pia niwashukuru Makatibu Wakuu wao wa Wizara hizo, Manaibu Makatibu Wakuu. Wakurugenzi, Makamishna, Wakuu wa Vitengo mbalimbali ikiwa ni pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara hizo bila ya kuwasahau Wakuu wa Taasisi mbali mbali zinazosimamiwa na Wizara hizo, kwa mashirikiano makubwa waliotupa wakati wote tulipokuwa tukifanya nao kazi, tunawashukuru sana.

Mhe. Spika, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ilikuwa na Wajumbe wafuatao:-

1.	Mhe. Salmin Awadh Salmin	Mwenyekiti
2.	Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Makamo Mwenyekiti
3.	Mhe. Mahmoud Moh'd Mussa	Mjumbe
4.	Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Mjumbe
5.	Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Mjumbe
6.	Mhe. Rufai Said Rufai	Mjumbe
7.	Mhe. Hamad Masoud Hamad	Mjumbe
8.	Mhe. Raya Suleiman Hamad	Mjumbe
9.	Ndg. Shemsa Maabad Moh'd	Katibu
10.	Ndg. Khamis Hamad Haji	Katibu

Mhe. Spika, katika mkutano huu wa Kumi na moja wa Baraza la Wawakilishi, Baraza lako Tukufu limepokea taarifa ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati, maagizo yaliyotolewa kwa serikali katika ripoti ya mwaka uliopita 2011/2012. Hii ni kwa mujibu wa Kanuni ya 108(15) ya Baraza la Wawakilishi la Zanzibar Toleo la mwaka 2011.

Utaratibu huu ni mpya, lakini ni mzuri kabisa, kwani utaliwezesha Baraza lako Tukufu kuelewa namna serikali inavyowajibika kwa wananchi lakini pia inavyowajibika katika chombo hiki kwa mujibu wa katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, Ibara ya 43(5) ambapo Katiba imeeleza bayana kuwa:

> "Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Mamlaka ya Rais ndiyo itakuwa na uwezo wa kufanya maamuzi juu ya sera za Serikali kwa ujumla, na Mawaziri chini ya Uongozi wa Makamo wa Pili wa Rais watawajibika kwa pamoja katika Baraza la Wawakilishi kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar".

Mhe. Spika, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo katika ripoti yake ya mwaka uliopita 2011/2012 ilitoa Maoni/Maagizo kumi na tano (15) kwa Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, Fedha,

Uchumi na Mipango ya Maendeleo, ambayo hivi punde Baraza lako Tukufu limepokea namna ya utekelezaji wake. Vile vile Mhe. Spika, Kamati ilitoa Maoni/Maaagizo saba (7) kwa Wizara ya Kilimo na Maliasili ambayo nayo hivi punde, Baraza lako tukufu limepokea namna ya utekelezaji wake.

Aidha, Mhe. Spika, Kamati yako ya Fedha, Biashara na Kilimo ilitoa Maoni/Maagizo kumi na tatu (13) kwa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ambayo nayo Waheshimiwa Wajumbe wamepokea namna ya utekelezaji wake.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa kwa ruhsa yako naomba nitoe maoni ya kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa malengo katika Wizara na taasisi tunazozisimamia ndani ya kipindi cha miezi 9 yaani Julai 2012 hadi Machi 2013.

WIZARA YA FEDHA, UCHUMI NA MIPANGO YA MAENDELEO

IDARA YA MHASIBU MKUU WA SERIKALI:

Mhe. Spika, kamati imefanyakazi ya kupitia utekelezaji wa malengo mbali mbali ya Ofisi ya Rais Fedha, kupitia Idara ya Mhasibu Mkuu ambayo imepewa majukumu ya kusimamia mapato na matumizi ya serikali sambamba na usimamizi wa mifumo ya kihasibu na ukaguzi.

Katika eneo la kada ya wahasibu na washika fedha, kamati imeona kuwa ili ufanisi na utendaji kazi wa wafanyakazi wa kada hiyo uwe endelevu ni vyema zoezi la kuwahamisha kwa mzunguko (*rotation*) katika maidara na taasisi mbali mbali za Serikali likafanyika haraka.

Aidha, kamati inashauri wizara kuharakisha uajiri wa wahasibu wengine wenye sifa kwani kamati ilipotembelea kisiwani Pemba imegunduwa kuwa kuna baadhi ya Taasisi za Serikali ambazo hazifungi hesabu za mwaka kutokana kukosekana kwa wahasibu wenye sifa. Baadhi ya Taasisi hizo ni Mabaraza ya Miji, Manispaa na baadhi ya Mashirika ya Serikali.

MAMLAKA YA KUKUZA VITEGA UCHUMI ZIPA

Mhe. Spika, Mamlaka ya Kukuza Vitega Uchumi ZIPA ni kiungo muhimu cha kukuza mapato ya serikali katika sekta ya uwekezaji vitega uchumi.

Mhe. Spika, dhana ya kukuza mapato kupitia sekta ya uwekezaji imekuwa ni kama hadithi ya alif lela ulela. Kamati yetu imeshuhudia maombi mengi yanayowasilishwa serikalini kupitia mamalaka hii kwa miradi mbali mbali ya kiuchumi ikiachwa solemba bila ya kupatiwa majibu.

Mhe. Spika, ipo miradi inayochukuwa zaidi ya hata miaka mitano imekwama utekelezaji wake kutokana na sababu mbali mbali zisizokuwa za msingi, urasimu katika sekta hii imekuwa kama ni jambo la kawaida kwao jambo linalosababisha kuikosesha mapato mengi serikali.

Suala la kuimarisha ulinzi katika maeneo ya uwekezaji hasa hasa katika sekta ya Mahoteli ni muhimu sana, kwani katika siku za hivi karibuni kumejitokeza vitendo vya uhalifu vinavyotishia

usalama wa wageni na hata wawekezaji wenyewe katika maeneo yao, jambo ambalo likiachwa liendelee linaweza kuzorotesha biashara hii ya utalii.

Mhe. Spika, dhana ya kuanzisha *"One Stop Centre"* ni jambo muhimu katika kuziwezesha zile taasisi zinazohusika na wawekezaji kuwa karibu na mamlaka ya kukuza vitega uchumi (*ZIPA*), dhana ya kuanzishwa kwa jambo hili limekuwa ni ndoto, kwani zile taasisi zilozounganishwa na *ZIPA* ama hazishiriki katika vikao au kama zitashiriki basi Wajumbe wanaoshiriki vikao hivyo hawana maamuzi juu ya jambo husika.

Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo inasikitishwa sana jambo hilo ambalo liko ndani ya uwezo wetu, lakini kwa bahati mbaya sana wahusika wanashindwa kuwajibika katika majukumu yao.

Mhe. Spika, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo inaitaka serikali kuachana kabisa na urasimu katika masuala ya uwekezaji, kwani kufanya hivyo tutakimbiwa na wawekezaji. Aidha, tunaitaka Serikali iongeze ulinzi katika maeneo ya uwekezaji hasa hasa katika maeneo ya mahoteli.

BODI YA MAPATO ZANZIBAR (*ZRB*)

Mhe. Spika, Bodi ya Mapato Zanzibar ni taasisi iliyopewa dhamana ya kukusanya mapato ya serikali. Kazi hii ya kukusanya mapato inaendelea kuimarika kadri siku zinavyoendelea. Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo inaipongeza *ZRB* katika kuhakikisha kuwa inafikia malengo ya ukusanyaji kama ilivyopangwa.

Mhe. Spika, pamoja na Bodi ya Mapato Zanzibar kufikia malengo ya ukusanyaji kama ilivyopangiwa. Lakini Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo inaamini kuwa mapato zaidi yanaweza kupatikana ikiwa taasisi hii itaachana kabisa na utaratibu huu wanaoutumia hivi sasa waukusanyaji wa mapato, yaani utaratibu wa kukusanya kodi kwa makisio.

Mhe. Spika, utaratibu wa kukusanya mapato ya serikali kwa makisio kuna ikosesha serikali mapato mengi, ambayo yangeweza kuisaidia serikali kutekeleza mipango yake mingi ya maendeleo.

Mhe. Spika, utaratibu wa kukusanya mapato kwa makisio sasa umepitwa na wakati, nchi nyingi duniani zimewezakupiga hatua za maendeleo baada ya kuachana na mtindo huo na badala yake tutumie ule mtindo wa kileo wa kukusanya mapato kihalisia.

Mapato yanayotokana na mahoteli bado hayakusanywi vizuri, kwani utaratibu wa kuingia wageni kwa njia ya makundi (*Packages*) huikosesha serikali mapato mengi, ambapo fedha zote za wageni hao hulipa kule wanakotoka. Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo inaishauri serikali iachane na mwendo huu wa kuingiza wageni kwa makundi na badala yake wageni hao walipe malipo yao hapa hapa nchini.

Mhe. Spika, moja kati ya sekta inayoipatia mapato serikali ni mapato yanayotokana na uvuvi wa bahari kuu, mapato ambayo hukusanywa na Wizara ya Mifugo, na Uvuvi. Wakati Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimko ilipofanya ziara katika Bodi ya Mapato iliarifiwa kuwa Mapato

yanayotokana na Leseni za Uvuvi wa bahari Kuu yameshuka sana ukilinganisha na mapato ya nyma, hii ni baada kuunganisha mapato ya sehemu mbili za Jamhuri ya Muungano.

Mhe. Spika, kamati yetu ilishtushwa sana na taarifa hii ya kushuka kwa mapato yanayotokana na leseni za uvuvi wa bahari Kuu kwani hiki ni kiuanzio chetu cha mapato ya nchi, hii ni changamoto kubwa kwa Bodi ya Mapato. Hivyo, tunaitaka serikali kufanya uchunguzi wa kina juu ya suala hili ili iweze kulitafutia ufumbuzi wake mara moja.

Mhe. Spika, kama kuna eneo linalovuja mapato mengi ya serikali basi ni eneo la Kiwanja cha Ndege cha Zanzibar sehemu ya utoaji wa *Visa*. Utaratibu wa utoaji wa *visa* kwa wageni unasababisha mapato mengi ya serikali kuvuja, jambo ambalo halikubaliki hata kidogo.

Mhe. Spika, hakuna hata nchi moja duniani hata ile ya Mabaabeli inayotumia utaratibu wa kugonga mihuri kwa mikono yaani njia ya (*manual*) na ukategemea fedha hizo za wananchi zikawa salama.

Kamati ya Fedha, biashara na Kilimo imejionea yenyewe wa kati ilipofanya ziara fupi katika viwanja vya ndege vya Zanzibar na kudadisi namna ya kodi zinavyokusanywa kwa ufupi Kamati haikuridhiswha na mfumo wa kugonga mihuri ya *Visa* kwa kutumia mkono, hivyo kamati inaigiza Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kufanya kila linalowezekana kulitafutia muarobaini suala hili. Aidha, ile Kamati ndogo iliyoundwa kwa ajili hiyo kupatiwa ripoti yake baada ya kukamilisha kazi iripoti mara moja.

Mhe. Spika, katika eneo linaloongeza mapato ya nchi ni eneo la kukodisha ardhi, eneo hili huongeza mapato ya nchi kwa kukodisha ardhi kwa uwekezaji, mapato haya hukusanywa na Wizara inayosimamia ardhi kwa kushirikiana na Bodi ya Mapato (ZRB)

Mhe. Spika, hakuna umakini katika kukusanya au kuweka thamani ardhi ya uwekezaji, jambo ambalo linasababisha mapato mengi ya serikali kupotea.

Mhe. Spika, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ilipotaka kujua juu ya jambo hili iligundua kuwa hakuna uwiano wa thamani kati ya mradi na mradi na ukubwa wa eneo la ardhi. Lakini pia imegundua kuwa wapo wanaomiliki ardhi ya uwekezaji na wamepatiwa *lease* a*greement*, lakini hawalipi chochote na hata katika orodha ya waliopewa *lease* hawamo kabisa. Lakini pia Mhe. Spika, wapo waliopewa msamaha wa kodi (*Grace Period*) na baadae miradi yao ikaanza kazi. Lakini lakushangaza wakapewa tena msamaha wa kulipa kodi ya ardhi wakati mradi umeshaanza kutoa huduma zake.

Kamati ya Fedha Biashara na Kilimo inaishauri serikali kulingana sana eneo hili la mapato ya Serikali na ifanye uhakiki wa kitaalamu katika maeneo yote ya ardhi ili kujua nani anatakiwa kulipa hiki, nani halipi kabisa, ili kuimarisha mapato ya serikali na kuinua uchumi wa nchi.

Mhe. Spika, misamaha ya kodi isiyodhibitiwa inasababisha serikali kupoteza mapato mengi, hivyo kamati inapendekeza kuwa Sheria ya Ardhi (*Act No.12/1992*) ifanyiwe marekebisho kwa kupunguza uwezo wa Waziri wa Ardhi kusamehe na kupunguza Kodi ya Ardhi kwa mwekezaji

na badala yake uwezo huo ubakie kwa Waziri anaeshughulikia masuala ya fedha ambaye ndie aliekabidhiwa Mfuko wa Mapato na Matumizi ya Serikali.

Mhe. Spika, ili kuongeza Mapato ya Serikali ni lazima kila mmoja wetu aweze kuchangia katika Mfuko huo, wafanyakazi wa serikali na hata wale wa sekta binafsi nao huchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali kwa kutowa kodi katika mishahara yao.

Mhe. Spika, kitendo cha Mashirika ya Serikali cha kutokuchangia mapato katika Mfuko Mkuu wa Serikali hakikubaliki kabisa. Yapo Mashirika ya Serikali ambayo yanafanya biashara kubwa tu, lakini hayachangii chochote serikalini ilihali mashirika hayo yanayo uwezo wa kuchangia chochote. Lakusikitisha zaidi Mhe. Spika ni pale wanapoingiza vifaa vyao huomba kupewa msamaha wa kodi (*Exemption*) na serikali kuwakubaliya misamaha hiyo.

Kamati ya Fedha Biashara na Kilimo inaitaka Serikali kuyalazimisha mashirika hayo kulipa aiana yoyote ya kodi inayowawajibikia ili sote kwa pamoja tuweze kuchangia hazina yetu, kwani waswahili wanasema, “Haba na haba hujaza kibaba”.

MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR (*ZSSF*)

Mhe. Spika, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (*ZSSF*) unafanya vizuri katika utekelezaji wa malengo yake.

Mhe. Spika, katika kutekeleza majukumu yake umeweza kupunguza kwa kiasi kikubwa malalamiko ya wananchi hasa katika maeneo ya vinua mgogo na hata pencheni. Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo inaupongeza Uongozi wa Mfuko huo kwa ahadi yake ya kuanza ujenzi wa kiwanja cha kufurahishia watoto cha Uhuru (Kariakoo).

Mhe. Spika, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo inaushauri Uongozi wa Mfuko kuangalia maeneo zaidi inayoweza kuwekeza hasa katika miradi mikubwa ya maendeleo hata kama itaweza kushirikiana na mashirika mengine ya kibiashara ili kukuza mfuko wake na kuongeza kasi ya maendeleo ya nchi.

Mhe. Spika, ni jambo la kusikitisha sana kuona kuwa hadi leo hii yapo Mashirika ya Serikali na Taasisi za Umma hazipeleki michango ya waajiriwa wao, ilhali michango hiyo inakatwa katika mishahara yao.

Mhe. Spika, jambo hili haliwezi kuendelea kuvumiliwa, Kamati ya Fedha Biashara na Kilimo inauagiza uongozi wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ya Zanzibar kuwachukulia hatua za kisheria waajiri wote ambao hawapeleki michango ya waajiriwa wao.

WIZARA YA KILIMO NA MALIASILI

Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo na Maliasili inajukumu kubwa la kusimamia kilimo na maliasili nchini, asilimia kubwa ya Wananchi wa Zanzibar ni wakulima, ambapo Wananchi hutegemea kilimo kama ndio ajira yao.

Kwa maana hiyo, serikali kupitia Wizara ya Kilimo inawajibu wa kuhakikisha Wakulima wote Nchini wanalima kilimo cha kisasa chenye tija, suala la kutoa elimu kwa wakulima kupitia kwa mabwana shamba na mabibi shamba haliwezi kuepukika.

Mhe. Spika, chakula kikuu cha Wananchi wa Zanzibar ni wali, ambapo asilimia kubwa hutumia mlo huo kama ni chakula chao cha kila siku. Kutokana na hali hio ni lazima serikali itilie mkazo sana kilimo cha mpunga ilikuondokana na njaa, huku mkazo zaidi ukielekezwa katika kilimo cha mpunga wa umwagiliaji maji ambacho ni cha uhakika badala ya kilimo cha kutegemea mvua ambacho hakina uhakika.

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Spika, Idara hii mbali na mambo mengine inawajibu wa kusimamia utekelezaji wa miradi na programu mbali mbali zilichini ya Wizara ya Kilimo na Maliasili. Mradi wa *ASSP* na ule wa *ASDL* ambao una lengo la kutoa huduma ya kilimo vijijini na kuanzisha skuli za wakulima, ni lazima usimamia vizuri na uendelezwe kwani mradi huu utawawezesha wakulima kujifunza kilimo cha kisasa lakini pia wakulima wengine watapata nafasi ya kujifunza kutoka kwa wenziwao.

Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ilipata nafasi ya kulitembelea baadhi ya mashamba darasa na kujionea maendeleo yao.

Mhe. Spika, mradi wa kuimarisha miundo mbinu ya masoko, uongezaji wa thamani ya mazao, huduma ya fedha vijijini bado haujaonesha mafanikio makubwa. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo na Maliasili kusimamia kwa karibu ili iweze kupata mafanikio kwani ni mradi muhimu kwa maendeleo ya nchi.

Mhe. Spika, idara ya Kilimo ina wajibu wa kusimamia huduma za kilimo kama vile matrekta, zana za kilimo, pembejeo za kilimo kama vile mbolea, dawa za magugu, huduma za matibabu ya mimea, kusambaza mitego ya kunasia nzi wa matunda ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa wakulima na kadhalika.

Mhe. Spika, kamati yako ilipata nafasi ya kuzitembelea maeneo mbali mbali ya kilimo na kujionea wenyewe maendeleo ya kilimo nchini, lakini pia ilipata nafasi ya kuzungumza na baadhi ya wakulima wa mpunga wa juu na ule wa umwagiliaji maji.

Mbali na changamoto zinazowakabili wakulima idara inajitahidi sana kutekeleza majukumu yake, imeweza kutoa huduma ya matrekta kwa wakati, mbolea, madawa ya magugu na mahitaji yote muhimu ya kilimo.
Mhe. Spika, tunaipongeza serikali kwa kupunguza huduma ya matrekta, bei ya mbolea na dawa za kuujlia magugu kwa wakulima.

IDARA YA UMWAGILIAJI MAJI

Idara hii ina jukumu la kusimamia kilimo cha umwagiliaji maji nchini ikiwa ni pamoja na kuendeleza miundombinu mipya ya umwagiliaji maji pamoja na kuifanyia ukarabati

miundombinu ya zamani, sambamba na kutoa elimu kwa wakulima wa sekta ya umwagiliaji maji nchini.

Mhe. Spika, idara hii ya umwagiliaji maji ina majukumu ya kipekee kabisa kwani aina hii ya ukulima ndio mkombozi wa wanyonge.
Mhe. Spika, kilimo cha umwagiliaji maji kiwe ndio kipa umbele hasa kutokana na mabadiliko ya tabia ya nchi. Kilimo cha umwagiliaji maji ndicho kilimo cha uhakika kuliko kile cha kutegemea maji ya mvua.

Mhe. Spika, mbali na mafanikio madogo yaliyoweza kupatikana katika sekta hii, pia kuna changamoto nyingi inayokabili sekta hii kama vile bajeti ndogo kwa kila mwaka, ucheleweshaji wa kuendeshea kazi ni baadhi tu ya changamoto inayokabili sekta hii.

Kamati yako ilipopata nafasi ya kutembelea idara hii imekuta haijaingiziwa hata senti moja katika fedha za kuendeshea kazi katika kipindi chote cha miezi sita tokeo bajeti ya idara hiyo ilipoidhinishwa na Baraza lako tukufu.
Mhe. Spika, hebu tujiulize idara hii inawezaje kufanya kazi katika mazingira kama haya.

IDARA YA UHAKIKA NA LISHE

Mhe. Spika, Idara ya Uhakika na Lishe ina jukumu la kuratibu masuala ya chakula la lishe nchini, hii ikiwa ni pamoja na kuanzisha uhifadhi wa chakula Zanzibar. Mhe. Spika, mbali na majukumu mengine iliyopewa idara hii lakini lengo kuu ni kuanzisha uhifadhi wa chakula Zanzibar ili itakapotokea hali ya ukosefu wa chakula nchini basi hifadhi hiyo iweze kusaidia wananchi kwa wakati huo.

Mhe. Spika, kamati yako haikuridhishwa kabisa na hali ya utekelezaji wa masuala ya chakula nchini. Kamati inaona kuwa bado jukumu la msingi la kuanzisha uhifadhi wa chakula halijatekelezwa na badala yake imeshuhudia fedha nyingi za serikali na wafadhili zinatumika kwa mikutano na makongamano ikiwa ni pamoja na utafiti kwa kupanda kwa bei ya mchele duniani na mafunzo kwa kamati ya chakula na lishe za wilaya. Mhe. Spika, hii ni dhihaka, tunaitaka Wizara ya Kilimo na Maliasili izirekebishe kasoro hizi mara moja.

KITUO CHA USARIFU MAZAO KIZIMBANI

Mhe. Spika, Kituo cha Usarifu Mazao Kizimbani kimejengwa kwa ufadhili wa ndugu zetu wa Korea. Lengo la kuanzishwa kwa kituo hicho ni kusaidia wakulima wetu kuelewa njia bora za usarifu wa mazao mbali mbali ya kilimo.

Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo imetembelea kituo hicho ambacho ujenzi wake umefikia katika hatua nzuri.

Kwa kuwa washirika wetu wa kilimo wa Korea waliokuwa wakiufadhili ujenzi huo umemaliza muda wao na kwa kuwa kituo hicho kimesita kumalizwa ujenzi, kufungwa vifaa ambavyo tayari vipo, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo inaitaka serikali itenge fedha katika bajeti hii ili

kukimalizia kituo hicho kwa haraka na kuepuka uharibifu wa vifaa ambavyo vipo. Hii ni kwa manufaa yetu na maendeleo ya nchi yetu kwa ujumla.

IDARA YA MISITU

Mhe. Spika, Idara ya Misitu ina jukumu kubwa la kulinda hifadhi zetu za misitu na kusimamia matumizi bora ya maeneo ya maliasili zisizorejesheka pamoja na kuendeleza zao la karafuu. Mhe. Spika, jukumu hili ni zito na linahitaji mashirikiano ya hali ya juu kati ya taasisi na Mashehe, viongozi wa Wilaya na Mikoa na wananchi kwa ujumla.

Suala la ukataji miti ovyo, uchimbaji wa mchanga, vifusi katika maeneo yasiyoruhusiwa, ujenzi wa karibu na vianzio vya maji imekuwa ni jambo la kawaida hivi sasa.

Mhe. Spika, serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Maliasili kama itaendelea kuvifumbia macho vitendo hivi hatimaye nchi yetu itageuka kuwa jangwa. Mhe. Spika, utunzaji wa maeneo ya misitu na ile yenye vyanzo vya maji ni muhimu katika ustawi wa nchi yetu. Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo hairidhishwi hata kidogo na ujenzi wa nyumba za kuishi watu karibu na vyanzo vya maji huku ikionekana kama vile imeshindikana kudhibiti hali hiyo.

Mhe. Spika, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo inaagiza Wizara ya Kilimo na Maliasili kufanya marekebisho ya sheria ya misitu ili sheria hizo ziende sambamba na hali ilivyo hivi sasa, kwani viwango vya vifungo na faini zinazotolewa haziendani na wakati wa sasa.

Mhe. Spika, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo inaipongeza Idara hii ya Misitu kwa kuweza kuotesha miche mingi ya mikarafuu na miche ya aina nyengine mbali mbali kwa ajili ya wakulima. Kamati yetu imeridhishwa na juhudi zote zinazochukuliwa na idara hii mbali na changamoto zinawakabili.

WIZARA YA BIASHARA, VIWANDA NA MASOKO

Mhe. Spika, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ina jukumu la kusimamia masuala ya biashara na maendeleo ya viwanda nchini, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha tunakuwa na masoko ya uhakika ndani na nje ya nchi.
Mhe. Spika, majukumu hayo si madogo ni makubwa kwa maendeleo ya nchi yetu na hasa ukizingatia kuwa sekta hii ya biashara na viwanda ni kichecheo kikubwa cha maendeleo ya uchumi popote pale duniani.

Mhe. Spika, Idara ya Maendeleo ya Viwanda ina wajibu wa kuimarisha mazingira ya uwekezaji katika sekta ya viwanda. Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo imeweza kufanya maeneo kadhaa yenye viwanda na kujionea namna ya uwekezaji katika sekta hii ya viwanda.

Mhe. Spika, ni ukweli usiopingika kuwa bila ya kuwa na viwanda nchini serikali haiwezi kukuza uchumi wake na kufikia kiwango kinachokubalika. Nchi zilizoendelea zimeweza kukuza uchumi wake na kufikia kiwango kinachokubalika na kuweza kukuza uchumi wao kutokana na maendeleo katika sekta ya viwanda. Hii ni pamoja na kutoa ajira kubwa kwa vijana.

Mhe. Spika, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo haikuridhishwa na kasi ya maendeleo ya viwanda nchini. Kamati inaitaka Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko iongezee kasi ya kuimarisha viwanda nchini ili ipambane na changamoto mbali mbali zinazoikabili sekta hii ili tuweze kuwa na viwanda vya kutosha kwa maendeleo ya nchi.

IDARA YA BIASHARA NA UKUZAJI MASOKO

Mhe. Spika, idara hii ina dhamana ya kusimamia masuala ya biashara na kukuza masoko. Zanzibar ni nchi ya kibiashara na wananchi wake zaidi ya asilimia 10 ni wafanyabiashaa, iwe ni biashara kubwa au biashara ndogo ndogo.

Mhe. Spika, uchumi wa Zanzibar kwa asilimia kubwa unategemea sekta hii ya biashara. Hivyo ni jukumu la wizara hii kusimamia masuala ya biashara ili kukuza uchumi sambamba na kutafuta masoko ya uhakika iwe ya ndani au nje ya nchi.

Mhe. Spika, suala la kuwa na masoko kwa ajili ya bidhaa tunazozidhalisha ni muhimu kwani kamati yako ilipopata nafasi ya kutembelea maeneo ya uzalishaji hasa maeneo ya ujasiria mali wadogo wadogo, changamoto kubwa inayowakabili wajasiriamali hao ni suala la soko la uhakika.

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Spika, Kamati yako ya Fedha, Biashara na Kilimo imepokea taarifa ya maendeleo ya kuegeuza Zanzibar kuwa ni eneo la tengefu la uchumi (*SEZ*). Mhe. Spika, wazo la kuigeuza Zanzibar eneo tengefu la kiuchumi ni wazo jema ili kuimarisha uchumi na viwanda lenye lengo la kuchangamsha biashara.

Utafiti unaonesha kuwa suala la kuigeuza Zanzibar kuwa eneo tengefu la kiuchumi lina changamoto nyingi, kwa kuwa wazo hili ni zuri na kama dhamira ya kweli ipo basi jambo hili linawezekana. Hivyo Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo inaitaka serikali ifanye kila inawezekana kupambana na changamoto ziliopo ili ifikapo mwaka 2020 Zanzibar itangazwe rasmi kuwa ni eneo tengefu la kiuchumi.

Taasisi ya Viwango Zanzibar

Mhe. Spika, Taasisi ya Viwango Zanzibar imeanzishwa kwa lengo la kupima viwango vinavyokubalika katika bidhaa mbali mbali zinazozalishwa nchini na kuangalia viwango vinavyotoka nje ya nchi na kuingia Zanzibar. Mhe. Spika, kamati yako ilipata nafasi ya kutembelea maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kuweka au maabara ya vipimo.

Kiasi ya uendelezaji wa eneo hilo bado hairidhishi na hii inatokana na ufinyu wa bajeti iliyotengwa. Mhe. Spika, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo inaishauri serikali itenge bajeti ya kutosha ili taasisi hii ianze kufanya kazi zake kwa haraka.

Mwisho Mhe. Spika, baada ya maelezo yangu naomba tena kuwashukuru Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa mashirikiano makubwa waliyonipa kwa kipindi

chote cha miaka miwili na nusu, ushirikiano ulioweza kuniongoza kwa ufanisi na kupata kazi kamati hii kwa urahisi.

Aidha ninapenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa kuniwezesha kunivumilia muda wote nilipokuwa nikitoa maoni ya kamati. Kuhusu ripoti ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi ya mwaka 2012/2013. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Mahmoud Muhamed Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuchangia mawili matatu juu ya Kamati hii ambayo na mimi ninaifanyia kazi.

Mhe. Spika, pamoja na maelezo mazuri ambayo yaliyokwisha kutolewa hapa na Waheshimiwa Mawaziri pamoja na Mwenyekiti wetu, napenda kuchukua fursa hii vile vile kuchangia baadhi ya maeneo ambayo nilihisi Mhe. Waziri alipokuwa akizungumzia masuala ya kilimo aliaghfilika kidogo.

Katika maagizo yale yaliyokuwa yametolewa kuna agizo moja suala la elimu liongezwe juu ya matumizi bora ya gesi na majiko mengine ambayo yanapunguza matumizi ya kuni. Hili ningeomba kulisawazisha kidogo ili nalo liwemo katika utaratibu.

Jengine ambalo nilikuwa naomba kutilia mkazo tu zaidi ni pale ambapo Mhe. Waziri wa Fedha alipozungumzia agizo Nam. 4. Naomba katika agizo hili Mhe. Waziri ajitahidi ili tuweze kuona tunaharakisha zaidi suala hili ili mwishoni mwa mwaka wa fedha huu na mwanzoni mwa mwaka wa fedha mwaka unaokuja tuweze kuona kwamba hili jambo linaanza kuonekana kwa vitendo na utekelezaji wake, ili tuweze kukabiliana na uhalisia ambao upo.

Jengine ilikuwa katika agizo Nam. 7 vile vile kwenye suala la TRA, aangalie sana malipo ya ushuru unatolewa ili kusiwe na malipo tofauti ushuru huo iwapo bidhaa itasafirishwa kupelekwa Tanzania Bara. Pamoja na maelekezo ambayo yapo lakini tunaomba hii kamati ambayo imeundwa isicheleweshe hizi taarifa kwa sababu hili suala ni la muda mrefu na ili tuweze kufikia pahala pazuri, tunaomba kwamba mambo haya yafanyike kwa haraka zaidi ili mwakani tusikabiliana na tatizo hili.

Jengine ni agizo Nam. 10. Katika agizo hili kulikuwa kumezungumziwa suala la mamlaka inayosimamia masuala ya utoaji wa bima. Kwa madhumuni yale yale ambayo yaliyokusa yamekusudiwa, napo vile vile tunaomba tatizo hili liweze kuharakishwa zaidi ili tuweze kuona tunafanikiwa kwa haraka zaidi.

Nikiondoka hapo nikija katika sekta ya kilimo, kuna eneo jengine vile vile sheria Nam. 1. Mhe. Spika, Mhe. Waziri alipokuwa akizungumzia hapa maagizo na utekelezaji zaidi tuliona wameingia zaidi katika sera na kanuni. Lakini tunaomba kuchukua fursa hii vile vile kumuomba Mhe. Waziri na sheria pia iangaliwe, tukiachia suala la kanuni tu na sera ili tuweze kupata nguvu ya haya masuala ambayo tunayaombea hapa.

Na mwisho katika mambo nilikusudia kuongezea ni katika ripoti hii ya Wizara ya Kilimo na Maliasili Nam. 6, wizara itayarishe maombi ya fedha serikalini mapema ili fedha hizo zipatikane kwa wakati na kwa msimu unaoendelea wa kilimo.

Tulipokutana na maelekezo ya utekelezaji hapa Mhe. Waziri alituelekeza kwamba serikali iliidhinisha shilingi bilioni moja kwa ajili ya kilimo. Mhe. Spika, tungeliomba vile vile ili mambo yetu yaweze kwenda katika kipindi kinachokuja, tunaomba pawepo na ongezeko asilimia ya 19 ya fedha ambayo zilitoka, hii haiamaanishi ule umuhimu tunaouzungumza kwamba kilimo kwanza au kilimo ni uti wa mgongo.

Tungeliomba ongezeko hili liweze kupatikana tena lipatikane kwa wakati ili wizara inayohusika iweze kufanya mambo yake kwa mujibu wa taratibu tulizojiwekea. Baada ya maelekezo hayo Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima na kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kikwajuni ninakubaliana na ripoti hii. Ahsante sana.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipa fursa ya kuweza kuchangia ripoti ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo na ripoti za utekelezaji za wizara tatu ziliopo chini ya kamati hii; Wizara ya Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, Wizara ya Kilimo na Maliasili na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Spika, ninawapongeza wote, mawaziri na mwenyekiti wa kamati kwa uwasilishaji wao na ripoti za kina. Lakini kabla sijaingia undani wa ripoti hizo Mhe. Spika, kuna jambo nimeliona naona niligusie.

Ripoti mbili Mhe. Spika, zilizowasilishwa hapa zimewasilishwa na Makaimu wa Kaimu Waziri; yaani Waziri hayupo, kuna Kaimu Waziri na Kaimu pia hayupo, kaja Kaimu wa Kaimu Waziri.

Sasa hilo ni juu ya serikali yenyewe ku-*sort out* ripoti zake kunapokuwa na Baraza, lakini hoja yangu hasa ni kwamba kuna picha inajitokeza Mhe. Spika, ambayo haileti taswira nzuri katika suala la muundo wa Serikali yetu kwamba ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye muundo wa Umoja wa Kitaifa.

Kwa kipindi fulani tulipoanza palikuwa panaonekan ni utaratibu kuona Waziri au Wizara inayoongozwa wa CCM anapoondoka Kaimu akawa ni wa *CUF* au vile vile kinyume chake kwamba wizara ambayo inayoongozwa na *CUF* anapoondoka Waziri akawa wa CCM, lakini kwa kitambo hivi tumeona kama vile wizara zimegaiwa, sasa tunashangaa katika serikali moja kwamba hata katika Kukaimu lazima mtu atoke upande ule ule, hii haitoi ishara nzuri Mhe. Spika, la sura ya taswira ya Umoja wa Kitaifa.

Nadhani ile ripoti ya kamati yako ya mwaka 2010 iliyokuwa ikiongozwa na Mhe. Ali Mzee inafaa sana pamoja na kukumbusha mara nyingi na ahadi nyingi za serikali kwamba tutapewa semina juu ya ripoti ile na kuona hatua gani zitachukuliwa, lakini sasa miaka miwili na nusu inakatika, nadhani imefika wakati wake hasa wa kupewa semina tujue hasa kwamba kulipendekezwa nini ili tuweze kuona kwamba matunda ya serikali ile yanafikia ilivyokusudiwa.

Mhe. Spika, sasa niende katika ripoti zilizoletwa hapa. Naomba nianze na Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa sababu nna nukta moja tu hapa. Mhe. Spika, katika ripoti hizi kuna suala ambalo tunalisahau ingawa hili linajitokeza katika mijadala linaulizwa suala la Kiwanda cha Sukari.

Mhe. Spika, Kiwanda cha Sukari kiliopo Mahonda wakati fulani kilisaidia sana Zanzibar kuzalisha sukari kwa mahitaji yake lakini pia kutoa ajira kwa wananchi wake, kwanza walikuwa wakifanya kazi katika shamba lile la miwa pale na pia kuchechemua maendeleo fulani ya kiuchumi katika eneo lile.

Lakini hiki kiwanda sasa hakifanyi kazi, serikali imejaribu kutafuta mwekezaji akaja tukaambiwa badala ya kuzalisha sukari akija zaidi katika kuzalisha pombe au *spirit*. Mhe. Spika, nadhani wakati sasa umefika utwambie kwamba ina mpango gani kuhusu kiwanda hiki.

Jana Mhe. Spika, nilikuwa nasoma katika mtandao katika gazeti la *Financial Times* la Uingereza linasema kwamba Afrika kwa ujumla wake Bara la Afrika, linategemea litakuwa ndio msafirishaji wa sukari kwa wingi katika kulihudumia soko la dunia. Zanzibar ilikuwa na nafasi yake hata ikiwa ndogo kiasi gani lakini tumeipoteza fursa ile wachilia mbali kusafirisha nje hata kujitosheleza sisi wenyewe kwa sababu kiwanda kile tumekisahau kabisa. Nilikuwa nadhani hapa Wizara ya Kilimo pamoja na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ambayo zinahusika wakashirkiana tukapata maelezo kwamba serikali ina mpango gani au ndio basi tu tumekiacha vile vile kiende na maji kama vilivyokwenda na maji viwanda vyengine. Hilo moja Mhe. Spika.

La pili Mhe. Spika, naomba niende katika Wizara ya Fedha. Wizara ya Fedha Mhe. Spika, katika ukurasa wa 171 wa ripoti ya kamati unazungumzia Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ. Mhe. Spika, wakati wa bajeti mwaka jana niliwahi kusimama nikasema na nakumbuka Waziri wa Fedha akatofautiana na mimi lakini bado naendelea kushikilia msimamo wangu, kwamba nikitazama kwa jumla mimi gharama za kuiendesha ofisi ile na tija inayoleta katika nchi , mimi bado sijaona kama tunazungumzia hapa thamani ya fedha zetu.

Mhe. Spika, tumetoka zamani kule tulikokuwa shughuli zilikuwa zikimalizwa Dar es Salaam kupitia ofisi hii, lakini sasa tuna Idara ya Fedha za Nje na alitueleza Mhe. Waziri wa Fedha tofauti ya shughuli hizi nakumbuka. Lakini mimi nasema hata ile kutafuta uratibu kufanya mawasiliano, ukitazama washirika wengi wa maendeleo na Mhe. Spika, wakija hasa wanatutafuta na sisi, wanafanya mawasiliano moja kwa moja kupitia Makao Makuu ya wizara ziliopo hapa Zanzibar, wanakuja wanaleta watu wao. Sasa kuendelea kuihudumia ofisi ile wakati imebakia kazi yake mawaziri wakenda Dar es Salaam kuwapokea kwa magari basi. Kwa nini tuingie gharama kubwa za kuendesha ofisi ile ambayo kazi yake hasa imekuwa haileti tija ya hivyo katika nchi yetu. Mimi nadhani kwa sababu sasa hivi mawasiliano ni makubwa basi suala lingeshughulikiwa hapa hapa.

Mhe. Spika, wakati fulani niliwahi kumshauri Waziri wa Fedha na aliwahi kuniahidi ndani ya Baraza hili kwamba serikali imekubali pendekezo langu na serikali imeshaanza mawasiliano na mwezi wa Oktoba mwaka juzi tungeanza mkutano wa mwanzo wa lile pendekezo langu kwamba tuwe na *consultative group meeting* kwa ajili ya Zanzibar, yaani mkutano kati ya washirika wa maendeleo na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kujadili maeneo ambayo tunahitaji kusaidiwa hasa katika yale maeneo yasiyokuwa ya muungano.

Na nilimwambia kutokana na mazungumzo yangu wengi hawa walikuwa tayari katika kufanya kitu hiki na serikali ilikiri na yeye mwenyewe kasema Oktoba ingeanza, Oktoba mwaka juzi imekwenda, Oktoba mwaka jana imekwenda na ninaamini Oktoba mwaka huu itapita Mhe. Spika, tutarudi pale pale kwamba pengine ile shughuli ambayo tunategemea ingefanywa na ofisi hii, inaweza kufanyika moja kwa moja kupitia vikao kama hivi lakini Mhe. Spika, kama kawaida tunakuwa na ahadi nyingi, lakini utekelezaji baadae hauonekani.

Mhe. Spika, nikiondoka kwenye Idara hiyo ya Kuratibu Shughuli za SMZ Dar es Salaam, naomba kidogo nigusie vile vile ukurasa 169 wa ripoti hii inazungumzia Idara ya Mipango ya Kitaifa, Maendeleo ya Kisekta na Kupunguza Umaskini.

Mhe. Spika, wala sitaki kuingia undani wa malengo ya programu, utekelezaji wa malengo na maoni na ushauri wa kamati, mimi nadhani hatuna haja ya kwenda kote. Mhe. Spika, ufanisi wa utendaji wa idara hii na serikali kwa jumla katika suala la kukuza uchumi na kupunguza umaskini tungekuwa tunaona katika mabadiliko ya maisha ya watu wetu.

Lakini nina kigezo kizuri Mhe. Spika, cha mipango mizuri cha ukuzaji uchumi na upunguzaji umaskini kingekuwa ni ukuaji wa uchumi, upatikanaji wa nafasi za ajira na kuongezeka kwa mapato katika nchi, kuwa serikali katika nchi maana yake *economic growth* ukuaji wa uchumi ambao unaonekana kitakwimu lakini mwananchi wa kawaida hauhisi katika mfuko wake. Ukuaji wa uchumi wa namna hiyo Mhe. Spika, haumsaidii mwananchi kama hujamuongezea kipato akajiona kuwa mwaka jana kapata hiki, mwaka huu ameongezeka, alikuwa anamiliki hiki mwaka huu ameongezeka. Hayo ndio tungeona kuna tija ya ukuaji wa uchumi.

Mimi nasema bado serikali inapaswa kujitazama katika hili. Tumeunda MKUZA ambayo tumeambiwa inatokana na dira ya 2020, lakini Mhe. Spika, bado matunda yake wananchi wake hawajayaona. Tunapaswa tujitathimini tena nadhani kamati na namuombea dua sana mwenyekiti wake Mhe. Salmin Awadh Salmi arudi tena na aiongoze kamati hii kutokana na uweledi wake, tuone basi tija ya mipango yetu Mhe. Spika.

Mhe. Spika, hatujapishana sana ambapo kipindi Zanzibar ilifikiria kuwa na dira ya 2020 na walipoanza wenzetu nchi za Mashariki ya mbali kama Malaysia. Lakini tutizame Malaysia leo ilipo Mhe. Spika, chini alipoanzisha Dr. Mahathir Mohamed vision 2020 ambayo iliwafanya nchi nyingi kwenda kuangalia wenzetu wanafanya nini. Lakini hii yetu tangu ilipoanza mpaka leo, tutizame kweli yapo mabadiliko madogo madogo lakini huoni kwamba inatokana na mipango ambayo ni centralise na inaratibiwa kwa pamoja, lakini yetu naona kama ni matokeo ya bahati mbaya tu, vinafanyika vitu kila mmoja anajifanyia tunakwenda mbele lakini huoni ile mipangilio kama ile ya wenzetu Mhe. Spika, nadhani hili tunahitaji kulitazama kwa kina.

Mhe. Spika, hapo hapo kuna suala halikuguswa humu, naomba vile vile niliseme kwa jumla. Mhe. Spika, Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, ndio inayosimamia katika ile miradi mikubwa ambayo tunapata mikopo kutoka nje. Mimi naendelea kutahadharisha, sitochoka kwa sababu kumbukumbu zitabakia na iko siku tutakuja kunukuu *hansard*, kama tunavyonukuu za watu wengine na sisi waje waone kama tulitahadharisha.

Mhe. Spika, mimi bado nina wasi wasi mkubwa sana na mikopo hii ambayo tunaishabikia sana kutoka katika Benki ya Exim ya China. Tumeliona suala la mradi ule, kila wakati tunalizungumza la uwanja wa ndege. Tumetahadharisha humu kuhusu walivyokuza gharama za mradi ambao umepelekwa huko wa Bandari na juzi Waziri wa Fedha katupa uhakikisho kwamba wanajitahidi ili kuhakikisha kwamba masuala haya hayatotokea tena. Mimi nilikuwa nadhani hebu badala ya kuingia katika mikopo na madeni makubwa ambayo yanakua mzigo kwa wananchi kwa miaka mingi inayokuja.

Kwa nini bado tunashindwa kutafuta njia za kutafuta kuendesha miradi yetu kupitia mpango wa *PPP* yaani *Public Private Partnership*, ambapo serikali inagharimika kidogo na wanaingia wawekezaji, mnaendesha mradi katika wale ambao wanajilipa wanaochangia na nyinyi mnapata, lakini hakuna ule mzigo mkubwa wa madeni kwa miaka mingi, ni ule mradi unaozalisha ndio unaopelekea kujilipa ule mradi wenyewe, badala ya kuwa na riba na vitu vyengine kama hivyo. Mhe. Spika, nilikuwa nadhani suala hili tulitizame sana katika mipango yetu.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 168 wa ripoti ya Kamati unazungumzia Mhasibu Mkuu, hapa nina suala moja tu. Namkumbusha tena Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, kwamba nilitoa hoja na yeye akaikubali na akaniambia wamo mbioni kuleta sheria juu ya kuanzisha Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa ndani wa Hesabu za Serikali, *Internal Auditor General*. Kasema mambo mengi haya ambayo yanaonekana hayapatiwi ufumbuzi kupitia kwa mkaguzi wa nje, pengine angeanzia kupata ufumbuzi kwa Mkaguzi Mkuu wa ndani *Internal Auditor General.* Nilikuwa nataka maelezo Waziri akija, suala hili limefikia wapi tulizungumza pia hapa.

Mhe. Spika, nikisema hivyo nataka kusema kwamba nadhani imefika pahala hizi ripoti za Kamati zinapofanya majumuisho na michango yetu iwe inazingatiwa. Kwa sababu tunaona ripoti zinapokuja za utekelezaji, ni yale yale ambayo Kamati imeandika katika ripoti yake. Sasa imekua kama ile michango ya Wajumbe tunayoitoa yote hii inakuwa imemalizika hivi hivi. Nadhani yale maeneo ambayo tunaongezea basi yaingizwe katika ripoti ili tupate maelezo yake, badala ya kuwa tunakumbushia hayo kwa hayo kila wakati Mhe. Spika.

Mhe. Spika, sasa niende katika suala la mwisho ambalo kidogo lina nchi nyingi hili, narudi pale pale. Katika Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo suala la vianzio vyetu vya mapato vinavyohusika na suala la Muungano.

Mhe. Spika, asubuhi nilihoji hapa na Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano hakunijibu na mimi sikusimama kumkumbusha, kwa sababu huu umekuwa ndio utaratibu wetu. Niliuliza vyanzo vyetu vya mapato kutoka katika *TCRA, TCAA, TPC, TTCL* haya yako katika Wizara ya Mawasiliano, kwa Zanzibar uko wapi mgao wetu. Halina majibu, yaani Mhe. Spika, kila tukiuliza hatupewi majibu ya uhakika.

Sasa humu Mhe. Spika, katika Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, tumetajiwa kwamba suala la kodi ya *payee* kuwa hatimaye limepatiwa ufumbuzi angalau kwa sasa tutapata bilioni 1.75 kwa kila mwezi, tunashukuru na tunapongeza hatua zilizochukuliwa.

Mhe. Spika, na hili la *Visa* pia ambalo liko nambari 2 katika maagizo Mhe. Spika, naomba lisiishie katika kuzungumzia suala la baina ya muhuri na stempu, lakini pia suala la mgao wa Zanzibar kwa wale watalii au wageni ambao wanachukulia *Visa* zao kutoka Ofisi za Kibalozi za Tanzania zilizoko nchi za nje wanaokuja Zanzibar, tulilizungumza mara nyingi kwamba mgao ule urudi Zanzibar. Wengi wanakuja katika sekta ya utalii ambao ndio sekta tegemeo kwa uchumi wetu tunapata nini Mhe. Spika. Hilo bado halijapa majibu.

Mhe. Spika, lakini katika hilo hilo la vyanzo vya mapato ripoti ya mwaka jana ya kamati, katika ukurasa wa 14, ilizungumzia tume ya pamoja ya fedha, ili kuokoa muda sitaki kuisoma. Lakini nakumbusha tu ilikuwa ukurasa wa 14, lakini mwaka huu haikugusiwa. Nilikuwa nadhani Mhe. Spika, pia tuambiwe zile danadana zimefikia wapi za serikali hizi mbili, kwamba Zanzibar imeshafanya maamuzi na imeshaajiri Mshauri Muelekezi kuja kushauri, lakini baada ya hapo hakuna kilichoendelea.

Mhe. Spika, najua unaangalia saa nimalizie katika maeneo hayo ya Muungano. Bado naomba kusaidiwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Tunafaidika na nini kutokana na taasisi za Muungano kama Benki Kuu ya Tanzania, Mamlaka ya Kodi na Waziri wa fedha ambaye kajitwika jukumu la kuwa yeye ndiye muamuzi wa masuala mengi ya kodi haya katika uchumi wetu sisi Wazanzibari. Tumesema mara nyingi uchumi wetu sisi ni wa huduma ni *Service Oriented Economy*, ni tofauti na uchumi wa rasilimali *Resource Based Economy*. Vyombo hivi viwili vinapopanga sera zake vinazingatia kiasi gani uchumi wa Zanzibar Mhe. Spika. Tunaahidiwa lakini hatupati maelezo, kila siku tunaambiwa mazungumzo tu.

Mhe. Spika, kulikuwa na maeneo mengi ambayo Zanzibar ilianzisha, leo wenzetu walituekea buti wakatuzuia tusiende mbele. Lakini leo wanafanya kwao. Suala la eneo tengefu la uchumi *Exclusive Economic Zone,* suala la maeneo huru *Free Economic Zone,* suala la Bandari Huru Mhe. Spika, suala la kuwa na *Offshore Bank* na *Offshore Company Center Zanzibar*. Yote haya Mhe. Spika, yalianzia Zanzibar katika miaka ya 1980 na 1990, tukawekewa guu na wenzetu tumezuiwa, lakini leo tunasikia yanaendelezwa kule, kunajengwa Bandari ya Bagamoyo ya kushughulikia mambo kama hayo, kunajengwa maeneo ya utengefu ya Benjamin William Mkapa na vitu vingine.

Mhe. Spika, kwa nini Zanzibar tuendelee kudhalilika katika mfumo huu ambao unatukwamisha, wenzetu wanatupiga teke kurudisha nyuma na wao wanasonga mbele kwa mawazo ambayo yameanzishwa hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, nimuombe sana Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, aitafute ripoti ya mshauri mmoja muelekezi anayeitwa *Casmin Blackman*. Ambapo nadhani alipokuwa yeye Katibu Mkuu, sijui kama ilikuwa mipango wakati ule, nadhani atakuwa anaikumbuka, huyu aliajiriwa wakati wa utawala wa awamu ya tano wa Dk. Salmin Amour. Ripoti yake Mhe. Spika, tunayo sisi wengine. Hii imetaja mambo mengi kabisa ya msingi ambapo Zanzibar ingeweza kujikwamua katika mambo haya yanayohusu uendeshaji wa mambo ya Muungano.

Mhe. Spika, kusema kweli mambo haya yanaudhi kwamba kila siku tunaendelea kuyakariri, wala sio kwamba tunapenda kila siku kuja kusema hayo kwa hayo, lakini tunaendelea kuyakariri kwa sababu wananchi wa Zanzibar wanataka kuona kwamba mambo haya yanapatiwa ufumbuzi.

Mhe. Spika, hapa ninayo nakala ya *declassified document* ya mwaka 1975 Ubalozi wa Marekani kama kawaida wanaripoti kwao juu ya kazi ya Balozi wao hapa, wanazungumzia haya tunayozungumzia leo Mhe. Spika, tunaambiwa tusubiri eti kuna mazungumzo yenye nia njema. Mazungumzo hayo tangu miaka ya 1975 yanazungumzwa hayana ufumbuzi. Mhe. Spika, hii 1975 sitaki kusoma kwa sababu ni refu. Lakini hii inazungumzia barua ambayo Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Mhe. Hassan Nassor Moyo yu hai Mwenyezi Mungu ampe umri mrefu, ampe afya. Aliandika barua kwa Clopa Msuya akiwa Waziri wa Fedha katika Serikali ya Muungano, kuwa maelekezo aliyopewa Rais wa Zanzibar, Sheikh Aboud Jumbe kulalamikia juu ya masuala ya misaada ambayo Serikali ya Muungano, ilikwenda kufanya mazungumzo, wakati huo ilikuwa hakuna Muungano wa Ulaya, kulikuwa na Jumuiya ya Uchumi wa Ulaya yaani *European Economic Community*, bila ya kuishirikisha Zanzibar wala bila ya kufikiria miradi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, yule mwakilishi mkaazi wa *EEC* Dar es Salaam ndiye ambaye aliwasiliana na Ofisi ya Rais wa Zanzibar, Sheikh Aboud Jumbe kutaka ipelekwe *input* ya Zanzibar. Lakini wenzetu ndugu zetu wa damu walitusahau sisi Zanzibar. Hii hadithi Mhe. Spika, inaendelea 1975, 1985, 1995, 2005, itafika mwaka 2015. Mhe. Spika, kama hatujaamua kurejesha mamlaka kamili ndani ya Zanzibar, basi mambo haya ya kudhalilishwa Zanzibar na kuwekwa nyuma kiuchumi, wakati wenzetu wakitumia fursa ambazo tumezianzisha sisi yataendelea.

Mhe. Spika, nitamsaidia baadae Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo aione hii, ili ajiridhishe kwamba haya mambo tunayoyazungumza hayakuanza jana na leo, lakini maafa yale yamefika Mhe. Spika. Serikali tunapotoa maelezo haya basi itupe majibu ya kina na ifanye maamuzi Mheshimiwa. Wananchi wa Zanzibar wanategemea maslahi yao, hayatolindwa Tanganyika, yatalindwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar walioichagua kuiweka madarakani ili kutunza maslahi yao.

Mhe. Spika, haya tunayoyasema tunayasema kwa sababu sisi tumeletwa kwa lengo la kuwatetea wananchi wetu. Naomba sana serikali ituambie kwamba hivi maeneo haya yote ya uchumi ambayo katika mfumo wa sasa, hatukwamuki, tumekwama. Nini mpango wake wa kutukwamua hapa. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi asubuhi hii kuweza kuchangia taarifa za Kamati za kudumu. Mhe. Spika, mimi niende katika Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ambayo ndio wizara kubwa katika nchi hii ambayo ndio muweza wa kuwasaidia wanyonge katika masuala ya kuondoa umaskini.

Mhe. Spika, niende katika agizo la Kamati kuhusu suala ambalo wale askari wastaafu ambalo mara nyingi sana tulisema hapa, kwamba jamani hebu hizi fedha tuzichukue huku zipitishiwe huku Zanzibar, tulipiga kelele sana lakini kwa bahati mbaya bado tunaletewa hakuna ukamilifu wa kuwa hili suala limepata muelekezo mzuri, ndio kwanza tunatafuta njia.

Mhe. Spika, tukiwapa *ZRB* ni pahala pake kabisa na wameonesha jinsi gani jitihada zao ambazo ni za kutukomboa kwa umaskini Zanzibar katika ukusanyaji wa kodi, ambao una fani nzuri, kila siku kukicha wanazidi kuulimbikiza na kukusanya fedha nyingi sana. Hilo ni moja ambalo ni kigezo tosha kwa *ZRB* wanaweza kukusanya kodi kwa hapa kwetu Zanzibar. Sio vibaya tukasema kuwa *TRA* wakae kando ili *ZRB* wawe mbele kwa hilo, hiyo itakuwa sio vibaya na wala sio dhambi wana jitihada zao.

Mhe. Spika, katika suala jengine suala la kupotosha masuala ya magendo ya mambo ya mafuta. Mhe. Spika, kamati yangu iliita kikao cha wahusika wote wadau pale, tuliwaita Jeshi la Ulinzi, Polisi na watu wengine na tulikaa nao pamoja na wahusika wenyewe wa Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ili kulitafutia njia ya utatuzi. Tukafikia pahala pazuri na tukapanga mkakati wa kutoa ripoti ya makisio ya fedha ambayo yangeweza kuonesha jitihada za kuondoa suala hili. Lakini mpaka tunaingia hapa leo sijapata taarifa yoyote ya kuwa tumefikia wapi makisio yale. Tusione hasara kwa sababu fedha zile pengine mnatoa nyinyi basi tungeokoa zaidi kuliko zile. Kwa hivyo, mimi naomba sana hili suala tuliangalie kwa makini sana na kuweza kulisaidia ili kupata ufumbuzi mwengine.

Mhe. Spika, nikiendelea na michango yangu. Mimi mara nyingi sana nimeona ripoti huku katika buku kuu ni jinsi gani *ZRB* wanavyokusanya zile fedha ni nyingi sana kusema kweli Mhe. Spika, kwa kuonesha kuwa hali ya uchumi ya nchi yetu unakua. Lakini ushauri wangu ambao nautoa ni kwamba mara nyingi sana tunatumia fedha nyingi kuliko kiwango ambacho tulichokuwa tunakikusanya. Ingekuwa katika muelekeo wa bajeti basi ningeomba tutafute mradi mmoja au miwili ili fedha nyengine tukaweza kufanya maendeleo mengine ambayo ni ya saizi ya kati ya kutafuta dawa na kadhalika.

Kwa maoni yangu hilo mimi nimeona litatusaidia sana kuliko kujilimbikizia miradi mingi, hatimaye kwenye ripoti mwisho wake hauleti maana, tunaambiwa ndio kesho, mradi huu haujafikia na huu uko hivi. Kwa hivyo, naomba sana hili suala tuliangalie kwa kina kabisa, tuwe na *plan* ya kuwa na mradi mmoja tu, ili tuuendeleze na mpaka kufika pahala tuumalize, na fedha nyengine kuweza kuzifanyia shughuli nyengine. Suala hili ni moja ambalo nimeliona katika mawazo yangu kuweza kusaidia Kamati yangu pamoja na Wizara.

Mhe. Spika, Waziri naamini kwamba ndiye Mwenyekiti wa miradi mikuu ya kitaifa Zanzibar. Kwa hivyo, ningeomba sana Mhe. Spika, kama wewe ndio Mwenyekiti hasa na ni mtu ambaye naamini wazi kuwa unapenda maendeleo katika nchi yetu. Tuna miradi ambayo kuna wawekezaji wakubwa sana katika nchi hii ambao wanataka kuja kuwekeza. Hivi Mhe. Waziri utakuja kunieleza ni wangapi ambao tayari wamekwishakukubalika katika serikali yetu kuwekeza hapa kwa kuwaondolea watu umaskini.

Mhe. Spika, nitoe mfano, hivi karibuni tu kuna wafadhili wamekuja kutaka kuwekeza masuala ya kutumia mradi wa takataka na kutoondolea hili zogo la uchafu katika nchi yetu. Mimi naamini ingekuwa mradi huu umekubalika, basi leo Mhe. Mwenyekiti wa Wenyeviti Mhe. Hamza Hassan Juma alisema sana kuhusu suala la ukusanyaji wa taka na alikemea sana kuwa Waziri anashindwa kutafuta magari kwa kuyaazima magari ya wizara nyengine ili kuondolea taka. Lakini naamini ungekuwa mradi huu umekubalika haraka sana na serikali umepitishwa, basi hili zogo tusingekuwa tunapiga kelele hata kidogo. Ingekuwa sasa hivi chupa adimu zinatafutwa,

ingekuwa betri zinatafutwa zimekuwa adimu, ingekuwa *oil* uchafu huo unatafutwa umekuwa ni adimu. Kwa sababu ni hivi vitu kwa mradi huu wa *SECRONA* unafanya vitu vyote hivi vya masuala ya umeme haibakishi kitu, unavyouona huu uchafu basi ndio umeme kwao.

Mhe. Spika, wenzetu wa Marekani wanatumia umeme wa aina hiyo na wanatumia pia umeme wa karatasi. Seuze sisi Wazanzibari kwa nini tushindwe na mataka tunayo mengi sana. Kwa hivyo, mimi naomba sana kwamba kwanza utatusaidia kuondosha uchafu, utatusaidia ajira itaweza kupatikana na utatusaidia hizo kodi ambazo zinakusanywa zitapatikana kwa wingi. Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Spika, na hivi sio vibaya wala sio dhambi kuniambia mradi huu serikali hivi sasa inatamka nini, naomba sana nijue kuwa tamko la serikali kuhusu mradi huu uko vipi. Naamini hilo unaweza kunisaidia kunifikisha pahala pazuri.

Vile vile Mhe. Spika, nije kwenye *ZIPA. ZIPA* mpaka sasa hivi wanashughulikia vizuri na wanapanga vizuri katika miradi yao. Lakini ningeomba sana kuna matatizo ambayo hutokezea kwa Wawekezaji ndani ya uwekezaji. Hebu suala hili naomba sana wajaribu kulifuatilia na kulitolea suluhu haraka sana na kusitokezee tatizo ni mahodari wanapenda sana kujaribu. Kwa hivyo, naomba sana na kuna malalamiko mengi, tumeshajaribu kuwasaidia na sisi Wawakilishi kuwapelekea. Tunawaomba wafanye haraka kuyatatua ili tuendelee na miradi yetu, tusije kupewa dhana potofu ya kauli mbaya ya kuondolewa jina la *Zanzibar njema atakaye aje*. Naomba sana kwa jitihada hizo wazidi kwa upeo wao wa kuweka suluhisho katika miradi yao ambayo wanasimamia.

Pia Mhe. Spika, nikubaliane na suala la uwekezaji wa mahoteli. Mhe. Spika, nakubaliana na Kamati ni kweli. Hivi karibuni nimeshuhudia *OCD* wa Kaskazini B, aliingia mwenyewe katika operesheni ya kuondosha matatizo haya ya kuvamiwa, ni jambo la faraja kubwa kuwa *OCD* mwenyewe alijijumuisha katika suala hilo. Lakini bado askari wetu wako kidogo, vituo vyetu bado zana hawajapewa ni kidogo, gari mpaka itoke sehemu nyengine ndio iweze kuja kuunga mkono. Hawa Wawekezaji na wao tuwape fursa ya ulinzi, serikali haijawa *serious* katika usimamizi huo. Mimi naomba sana hili suala tulitilie maanani kuweza kulisaidia ili kupata ufanisi mzuri sana na wateja wetu wa mahotelini wasipate bughudha ya hapa na pale.

Mhe. Spika, nije katika masuala ya ukusanyaji wa mapato ya utalii. Masuala ya ukusanyaji mapato ya utalii kwa kweli hatujawa *serious* kabisa, hii ni nchi ndogo kabisa, kweli tunashindwa kusimamia kukusanya kodi zetu, hili ni suala ambalo hatujawa *serious*, kila siku tunapiga kelele tu tukiondoka hapa. Mhe. Spika, watizame wenzetu wa nchi kama Unganda na nyengineo wameshafikia malengo makubwa, wanatushinda sasa hivi kwa utalii wao. Pia Zimbabwe, Kenya na sehemu nyengine. Hebu tutafute njia hasa madhubuti ya kitaalamu ambayo inaweza ikakusanya mapato yetu kwa kupitia utalii na tuone kama sisi tutakuwa maskini. Kama tutakuwa *serious* basi naamini hivyo, kama masuala ya *Visa* yamezungumzwa hapa, utakuta wanaingia kila leo.

Lakini suala hili la *Visa* ningeomba Mhe. Spika, kwa kuwa tuna ushindani wa kibiashara ya utalii katika nchi za Kiafrika na sisi tuweze kupunguza kidogo ili tuweze kupata wateja wengi wa kitalii. Suala hili la *Visa* wanalipigia kelele sana huko wanasema Zanzibar *Visa* iko juu katika utoaji wake. Kwa hivyo, naomba suala hili tuliangalie kwa umakini kabisa.

Mhe. Spika, nikienda katika suala la kilimo. Suala hili la kilimo, mimi mara nyingi husema hata zile sheria za misitu nyengine zinakuwa sijui zimepitwa na wakati, zinahitaji marekebisho. Lakini bado tutafute sheria mbadala sasa hivi, niseme kuwa iliyokuwa kali kabisa ya udhibiti kabisa. Mhe. Spika, misitu yetu inakwenda na maji, watu wanakata kiholela, miongoni mwa sisi wakubwa gari zetu zikikamatwa tunakwenda kusema zitolewe, hili sio siri tukubaliane wakubwa na sisi vile vile magari yetu yanayokwenda kupakia kuni haramu za mwituni zinazokatwa hizo, nalo hili tuliseme tulikemee.

Wengine Mhe. Spika, waliwahi kuninunia kuhusu masuala hayo. Lakini ndio mambo na ndio utendaji, sikubali mali yangu iharibiwe mimi kwa kumuona mtu kwa makusudi, hilo mimi sikubaliani nalo. Kwani ukisemwa ndio umeumia, sikuogopa Mhe. Spika, nilishirikiana na Wakurugenzi waliokuwa misitu, kwa kusema *maneno sio mkuki* kabisa, maneno ya jirani yangu hapa.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, nasema kuwa na sisi Waheshimiwa kuna mambo mengine madogo madogo tujilinde nayo, tusiwaachie hawa watu wetu kuwapa magari wakaenda kwenye misitu yetu yakatuharibia, halafu baadae unakuta wewe Mheshimiwa unakwenda kulalamika na kumuona Mkurugenzi mbaya au adui, kwa kuwa nini kaikamata gari yako. Mkurugenzi timiza wajibu wako kamata gari, mpige faini wala usiziache na hizi sheria tuzione ni jinsi gani zinaweza kurekebishwa.

Mhe. Spika, kwenye suala hili la kilimo, kwa kweli mara nyingi sana tunachelewa kwa nyakati za kulima, na kwa sababu tunakuwa zile nyenzo zenyewe hatuna, hasa matrekta. Mimi ningeomba sana Mhe. Spika, kuwa haya matrekta mabovu basi tushushiwe sisi kule majimboni tutaweza kuyatengeneza, wala msione tabu, tushushieni sisi matrekta mabovu kwenye majimbo yetu tutayatengeneza na tutasaidia, na hili suala limefanyika, nimewahi kulifanya mimi kuisaidia serikali kutengeneza trekta la wananchi wakalimia, sio tatizo tunaomba sana watushushie chini, tutawasaidia ili kuweza kuokoa wakati ule kuweza kuupata vizuri muda wa kilimo, kwa sababu Zanzibar wengi tunapenda kula wali na hilo sio siri kabisa, kwa sababu wali mtamu, hakuna asiyejua kuwa wali ni mtamu. Kwa hivyo, ni lazima Mhe. Spika, tupatiwe nyenzo kwa wakati. Ndio maana nikasema kwamba serikali sasa iamue itafute mradi mmoja mkubwa na kuweza kuwekeza, ikifanya hivyo basi mimi naamini kuwa tutaweza kulima kwa wakati na wananchi wataweza kupata mazao ya msingi na sisi.

Mhe. Spika, nije katika Kiwanda cha Sukari, mwenzangu karashia tu, lakini mimi niingie ndani. Mwanasheria tunaye huyu hapa, Mwanasheria anatakiwa aangalie ni jinsi gani serikali inaingia mikataba na hawa wawekezaji kama wa viwanda, ardhi na mambo chungu nzima. Lakini mimi inanipa shida sana. Sheria ya mwanzo mwekezaji huyu alipewa siku 48 za kuangaliwa. Siku 48 zimepita hatukuona chochote.

Vile vile mwekezaji huyu tunaona kuwa kila siku badala ya kwenda mbele yeye bado anaturudisha nyuma, sidhani kama hata hii kodi ya ardhi analipa. Naamini kuwa dakika za mwisho niliacha kuwa kodi ya mapato ya ardhi halipi. Nilikuwa nazo *data* hizo, lakini kwa bahati nzuri *briefcase* yangu imepotea tu sikujua nimeiweka wapi. Lakini nilizipata hizo *data* kuwa halipi kodi zetu, isitoshe anadaiwa na watu wa umeme wanamdai makodi yao halipi. Sasa

sijui tunatafuta sheria gani ya kuweza kumuambia bwana sasa tuachie kiwanda chetu tuweze kufanya sisi wenyewe.

Mhe. Spika, nakumbuka miaka ya nyuma alipokuwa China mwenyewe katika kiwanda kile, kilituokoa watu wengi sana kabisa, watu walipata kazi na tulikuwa tunasafirisha sukari nje na ilikuwa ya daraja la juu kabisa, *spirit* daraja la juu na mambo mengine. Leo Mhe. Spika, unakuta tuna kiwanda jina tu. Mhe. Ismail Jussa kasema *East Africa* hapo ndio ilitegemewa hivyo, na ni kweli kwa sababu sisi peke yetu hapa tukitoa sukari inakuwa ni sukari nzuri tena tamu.

Mimi nashangaa sana Mhe. Spika, kuwa bado serikali ipo inapigwa danadana tu, maana yake inahadithiwa tu. Bora tuwaachie wenyewe wananchi walime. Hebu fikiria wewe ukilima mpunga pale unapata mpunga mzuri tena mwingi sana. Haiwi mua kila siku unapandwa tu kesho unapandwa, hatuelewi upandaji huo ukoje. Mimi naomba sana hili suala tuweze kusaidiwa. Mhe. Mwanasheria kama mtu ameshashindwa muondoeni bwana, hakuna haja ya kumuweka tu, anawadhalilisha wananchi kila siku ugomvi tu, mwananchi na yeye ana njaa anaona mabonde yapo matupu, akienda kulima yeye anaingia na kitrekta chake.

Vile vile Mhe. Spika, nije kwenye sehemu ya biashara, tusione tabu kusema, sheria bado imewabana sana watu wetu, kwa sababu sheria ya nchi kwa mujibu wa sheria ya Muungano, sheria yetu sisi hapa hawezi huyu kuleta kampuni kubwa za viwanda hapa, hili tusidanganyane tuambizane ukweli. Ingekuwa sheria hiyo iko wazi, basi naamini viwanda vikubwa vingekuwa vimeshakuja kuwekwa hapa, suala hili tuseme ukweli ulivyo. Basi tuangalie njia nyengine mbadala ya kuwaambia wenzetu kuwa turuhusuni kuweka viwanda vikubwa huku, tusione tabu kumwambia yule mtu.

Mhe. Spika, nirudi tena kidogo karibu namalizia, kuna suala la wafanyabiashara. Suala la wafanyabiashara Mhe. Spika, umesema ndio kwanza kuna tume ambayo imeundwa. Mimi ninakuomba, umesema kuna tume ya *ZRB* na watu wengine imeundwa ili kufuatilia suala hili la magari la kulipa *defense* iliyobakia. Mimi ningeomba, ushauri wangu hebu washirikisheni na Waheshimiwa humu ndani, japo wawili au watatu tu lakini washirikiane katika kamati yenu. Ikiwa mimi, au Mhe. Jussa, au Mhe. Hamza au Mhe. Salmin na Waheshimiwa wengine, angalau watatu tu tuone kama hili suala halitokwisha. Mimi naomba Mhe. Spika, nakuomba sana kaka yangu hebu fanya ujivuwe na wewe hili tatizo, nakuhakikishia watakapokwenda hawa wataleta jibu zuri na mambo yatafanikiwa.

Kwa kumalizia nije kwenye *ZSSF*. Mhe. Spika, leo Mhe. Hamza Hassan katupa vitu vikubwa sana hapa, amesema kuna makampuni ambayo yanataka kuwekeza hapa nchini, muoneni, Mhe. Hamza yuko wazi kabisa hana ofisi, ofisi yake wakati wowote iko wazi tu, *breafcase office,* lakini wakati wowote anafanya kazi, ukimuita anakuja, wamshirikishe na wao wamuite. Hawa watu wanaotaka kuwekeza hebu tuambie tusaidie vipi, lakini fedha zinakaa tu, tusiende katika miradi midogo midogo. Mimi naomba sana Mhe. Waziri hebu tutafuteni sisi tuliokuwa na vichwa, tuliokuwa na makampuni makubwa makubwa hapa nchini, ili tulete huo ufanisi na watu waweze kuondokana na umaskini. Jambo hili nawaombeni sana tuweze kulimaliza, tuweze kupata ufanisi mzuri. Vyengine vyovyote tutakwenda na maji.

Mhe. Spika, kwa kumalizia, kama nilivyokuambia Wizara hii hasa sina mchango mkubwa sana. Nimalizie kwa kusema kuwa ninaomba sana miradi isimamie na tupewe jibu haraka sana. Wawekezaji wa mahoteli wako wengi, lakini maeneo wananyang'anywa. Ushauri wangu, kutana wewe na Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili na ukutane na Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati mlimalize hili suala. Wawekezaji waje jamani ili tumalizie hii shughuli, tusikae hapa tukasema bajeti ndogo sijui tutafute wafadhili gani.

Mhe. Spika, bajeti kama tutasimamia vizuri, kodi za mapato tutakusanya vizuri, masuala ya *lands* na tukisimamia mambo ya utalii basi naamini sisi hatutotaka kukopa kwa mtu, wala hatutofanya bajeti tegemezi. Mimi naamini hivyo, lakini kama tutakuwa kila siku omba omba, mara leo bilioni 20 za elimu ya juu huna, mara sijui nini. Mimi naomba sana Mhe. Spika, ahsante sana najali wakati wako. Naunga mkono ripoti ya Kamati hii, ikiongozwa na Mwenyekiti, mwenyewe Mhe. Salmin Awadh, ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Asaa Othman Hamad: Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, nikushukuru na wewe Mhe. Spika kwa kunipa nafasi ya kutoa maoni au mchango mdogo kwenye sekta hizi zilizoko mbele.

Mhe. Spika, kwanza niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri wa wizara hizi, pamoja na watendaji wao. Pia niwapongeze kwa dhati kabisa Waheshimiwa waliotangulia kuchangia tokea mwanzo jioni hii. Kama Mhe. Spika, kanuni ingeruhusu nadhani maudhui wamekamilisha yote tuliyokusudia.

Mhe. Spika, kwa upande wa Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, nimshukuru na kumpongeza sana mwenzetu kwa kazi nzuri ya kilio cha muda mrefu cha Wajumbe wa Baraza hili, kwa kile tulichokuwa tukikisubiri, ile kodi inapofika mahali wakaona hakuna kinachoendelea, basi wanatoa majina wanayoyaona yatafaa, sasa yanatusibu sote.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo nimeliona kwenye makusanyo, kuhusu kodi za mahoteli bado Mhe. Waziri analalamika na kusema hili zoezi litakamilika baada ya kutiwa madaraja ya mahoteli yetu. Mhe. Spika, madaraja nadhani ni shughuli ya kitaalamu hiyo na sijui kama itahitaji uchungu au upembuzi yakinifu na sijui kitatajwa nini hapa mpaka tuzipate hizo nyota za mahoteli.

Kwa hiyo, nimuombe Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba suala hili aliharakishe nalo litusaidie, kwa sababu hali yetu si nzuri katika suala hili. *(Makofi)*

Mhe. Spika, jengine ni kuhusu kodi za wafanyabiashara wetu kutozwa mara mbili. Kwa kweli haifai, haijuzu, haipendezi, inakera na ni maudhi makubwa sasa na hili ni kero, kwa sababu Mhe. Spika wala wananchi hivi sasa hawatuamini katika hili, na haiwezekani watu wazima kama wanakaa na kuzungumza jambo kwa maslahi ya wananchi wao likachukua karne haiwezekani, nadhani hapa kuna jambo katikati. *(Makofi)*

Mhe. Spika, SMT na SMZ wanakutana na hili ugumu wake ni upi, vikao hivi sasa tutie na buhuri, maana labda kuja jini anatafutwa hajaja akaja kusema anachotaka, kwa sababu hakuna

jibu. Kutokana na hali hii inaoneshwa kwamba hakuna nia safi katika hili isipokuwa tunadanganyana.

Kwa mfano, ukienda *TRA* na mwenzetu mmoja hapa Mheshimiwa Mjumbe mmoja hapa amepeleka gari Dar-es-Salaam na Mhe. Waziri wa Fedha hili analifahamu, yaani tayari ameshalipa hapa na anafika Dar-es-Salaam anaambiwa alipe mara tatu ya kile alicholipa hapa. Sasa kufananishwa sisi Mhe. Spika kwamba kodi yao kwao inafanana na walivyonavyo na sisi hatuna, hivyo sisi tutalipa kodi kutokana na mazingira yetu na chumi tuliyonayo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, niliposema hapana nia njema na wala sibahatishi. Niliwahi kuwa Mjumbe wa Kamati ya Fedha kuhusu dai letu la Benki Kuu wanatuambia wala hawatasumbuka na Zanzibar kutafuta chumi mbili katika nchi moja, hadi pale Zanzibar itakapopinda mgongo kufuata huo mkondo wanaoutaka wao. *(Makofi)*

Sasa katika hili Mhe. Spika, ndipo niliposema hakuna nia njema SMT na SMZ katika vikao vyao linalohusu suala hili tunadanganyana.

Mhe. Spika, suala jengine ni pale kamati ilipoiagiza wizara kutoa kipaumbele kwenye miundombinu katika maeneo yetu ya uchumi, ambayo ni maeneo huru. Mhe. Spika, tokea yatangazwe maeneo huru ni muda mrefu sana sasa na maeneo huru haya tukasema Fumba na kule kwetu Micheweni katika ile sura iliopo bado tutaendelea kuyataja tu bila ya mafanikio.

Kwa hivyo, lazima serikali kwa namna moja au nyengine basi angalau ianze, kwa sababu miundombinu ni umeme, barabara, maji yatampa matumaini huyu mwekezaji. Lakini katika sura ile iliopo sasa haji mtu kutuanzia sisi na wala hana shida hiyo.

Mhe. Spika, naomba kutoa ushauri wangu wa bure katika Serikali yangu ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar. Mhe. Waziri wapo watu ambao wako tayari na fedha wanazo, basi waiteni na wala hakuna jambo la mtu peke yake, waje hapa na jambo litakalotugharimu ni makubaliano namna gani waweze kuyaendeleza maeneo haya na faida kwao na maslahi ni kwetu.

Nadhani isiwe ni joka la mdimu hatufaidiki sisi wala wenzetu ina maana gani, labda kwa sababu ya shida tulizonazo, basi watu wetu wanayaharibu maeneo yale, yaani watu wanachimba miamba kwa ajili ya kutafuta matofali na tafrani moja kwa moja, ndio hivyo tena yameambiwa huru kwa tafsiri pana. Kutokana na hali hiyo, ni vyema tuwaite wenzetu na tuwajengee mazingira ambayo yatakuwa na faida kwao, lakini na sisi watu wetu pamoja na taifa hili likaweza kufaidika na isiwe hali ile ilioko.

Mhe. Spika, nataka nimalizie kwenye Wizara ya Kilimo na Maliasili, bado asilimia kubwa maisha yetu tunategemea kilimo. Kwa kweli mengi yameshasemwa kama vile Kilimo ni Uti wa Mgongo, Kilimo Kwanza, Chakula ni Uhai, lakini bado kilimo chetu hakijakuwa na tija.

Mhe. Spika, ni ukweli usiofichika kilimo Zanzibar na ili kilete tija kwa Wazanzibari ni lazima kiwe cha sayansi, lakini kilimo alicholima babu na bibi yangu hakitatusaidia hata kidogo isipokuwa kitatugharimu tu kwa sasa, eneo kubwa linakwenda zake na bahari na wala hatuna uwezo wa kuikinga bahari kuila visiwa hivi. Mhe. Spika, rutuba ya ardhi yetu inamalizika kwa

nguvu sana, lakini idadi ya watu inaongezeka, mahitaji ya ardhi yanaongezeka, ufujifu wa ardhi yenyewe unaongezeka na hakuna usimamizi shamba la bibi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ni aibu kubwa akina sisi kuona kwamba yale maeneo mazuri ya kilimo ndio sisi tunakwenda kujenga makasri kuwaonesha wenzetu kwamba tunaweza kuharibu na wala tusingetarajia hali hii. Mhe. Spika, kama nia haijawa njema, basi Mwenyezi Mungu anaziona nafsi zetu, kwa sababu Mwenyezi Mungu ni mjuzi wa siri na tutaimba mdomoni nafsi zinatusuta hatwendi mbele, ardhi tunaiharibu na haina tena rutuba.

Mhe. Spika, juzi Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati alitoa *statement* kama tuliibeba kwa uzito wake basi tunayo hali ngumu sana, tena mbaya. Mhe. Spika, muda umefika sasa serikali kwa makusudi, kitaifa, kimkoa, wilaya, jimbo, masheha asijekuharibu ardhi tu, isipokuwa wapewe majukumu kuhakikisha ardhi inalindwa na inatunzwa. Kwa maana hiyo, lazima kuwe na *evaluation* ifanyike, Siku ya Misitu, Siku ya Uhai wa Wanyama na kadhalika ardhi inakwenda hii Mhe. Spika na wala hatutapata hata pa kupanda mche. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kilimo bora ni kuwa na ardhi bora, matumizi mazuri ya ardhi na wataalamu wapo wa kutosha Zanzibar. Lakini tuwe na mbegu bora na wala hatutaipata mbegu kwa mtindo huu wa kuwaambia JKU limeni hakuna utaratibu huo. JKU mbegu tutapata huku, kwa kweli JKU atazalisha mpunga sio mbegu, kwa sababu mbegu zitazalishwa kuna vyombo vya utafiti ndio watoe mbegu, yaani mbegu bora ni Vituo vya Utafiti na kazi ifanywe huko tupate kilimo bora tunachokitaka Mhe. Spika.

Sasa baada ya kupata mbegu taaluma ambayo hiyo si tatizo. Nashukuru sana Mwenyezi Mungu ametujaalia Chuo cha Kizimbani sasa kinafanya kazi nzuri na kinatoa vijana na tumebahatika sasa mpaka *Degree* ruhusa ipo na wamekubali huko *NACTE*, kwa hiyo tunayo nafasi ya kuwapeleka mpaka hapo. Lakini Mhe. Spika, kazi kubwa iliyotukabili ni vipi mazingira tutayatunza, yote haya ninayoyazungumza na Mhe. Waziri ametuthibitishia kwamba maji ni tatizo, na bila ya kuwa na kilimo cha umwagiliaji na wala kabisa hatujaingia katika hilo ninalosema. *(Makofi)*

Kwa kweli umwagiliaji wetu Zanzibar tunategemea visima na huko visimani Mhe. Waziri ametuambia maji hayako, je kama ya kunywa leo ni tatizo tutaweza kuyatoa ya baharini na hiyo ndio changamoto yetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mengi tunaweza tukayakabili wenyewe kama tutakuwa *serious* katika kusimamia maeneo yetu ya mapato. Kwa hivyo, vijana wenye ujuzi wataalamu wa shughuli hizo za kifedha na kiuchumi tunao vijana wa taalamu ya kilimo wapo. Sasa nadhani nitoe serikali ikisema kwamba sasa tunaanza na yaliyopita yamepita na yaliyopita si ndwele tugange yajayo.

Baada ya haya machache sana Mhe. Spika, ilikuwa niweze kutoa na mimi kile kilichokiona kwamba kitaweza kusaidia kwa serikali na Baraza hili tukufu. Mhe. Spika, nikushukuru ahsante sana Wazanzibari wamenisikia na yale yanayowagusa, basi nina imani nimeweza kuyawakilisha kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, muda wetu unatukwaza mno ninao wachangiaji wawili, basi niwaombe wanisaidie kuchangia haraka haraka, ili tuweze kuendelea na hatua iliyobaki. Mhe. Hamza Hassan Juma jaribu sana utumie muda mfupi na baadaye Mhe. Abdalla Juma Abdalla.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na nitajitahidi kutumia muda mchache sana.

Kwanza nataka niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri pamoja na Mhe. Mwenyekiti wa Kamati kwa ripoti yake nzito kabisa na kimsingi sina matatizo wala pingamizi nayo, naunga mkono kabisa Ripoti ya Mhe. Mwenyekiti wa Kamati hii ya Fedha, Kilimo, Biashara na Utalii.

Mhe. Spika, nataka nianze alipogusia Mhe. Mwenyekiti kuhusu suala zima la urasimu hasa katika kuwapokea Wawekezaji wetu. Mhe. Spika, ni kweli kuna maeneo mengi wanakuja wenzetu hasa kutokana na wanaposikia sifa ya Zanzibar utulivu wake, wanakuja kutaka kuwekeza, lakini tunachukua muda mrefu.

Nakumbuka kuna mradi wa kujenga mji Fumba, yaani mji karibu meli tano tena wa kisasa kabisa, ambao utakuwa na *facilities* zote za kibiashara, makaazi pamoja na mahoteli, lakini mradi huu umechukua muda mrefu. Mhe. Spika, niliwahi kuzungumza na Mkurugenzi wa *ZIPA*, kwamba mradi huu umekwama kiasi gani, aliniambia kwamba tumo mbioni na mradi huu serikalini tayari tumeshafanya hizo *process*, lakini mpaka leo mradi huu umelala njiani.

Kutokana na hali hiyo, bado narejea kusema kwa kujenga nyumba moja moja mji wetu utakuwa haupendezi hebu tuwatafuteni au tuwakaribishe hawa wawekezaji ambao watakaoweza kutujengea miji angalau mtu akisema anaye rafiki yake anataka kwenda kumtembeza Zanzibar basi apate sehemu ya kwenda kumuonesha katika mji fulani.

Mhe. Spika, nataka niendelee hapa katika eneo la *ZIPA.* Mhe. Spika, nataka niseme kitu kimoja, bado narejea kauli yangu kwamba Baraza la Wawakilishi tunajitahidi sana kutunga sheria tena ambazo ni nzuri sana, lakini bado katika utekelezaji wa sheria hizi kwa kweli wenzetu wanakuwa hawako makini.

Kwa mfano, Mhe. Spika limezungumzwa sana na wenzangu hapa kuhusu suala la wawekezaji kuja kupatiwa ardhi na serikali halafu wakanyang'anywa ardhi bila ya utaratibu. Katika suala ambalo linasikitisha tena ni aibu kwa nchi yetu basi ni suala hili, tukiangalia Sheria ya *ZIPA* kuhusu Uwekezaji, Mhe. Spika kwanza mtu anapotaka kupewa lile eneo la uwekezaji kabla ya kuanza ujenzi inabidi lazima anapewa ile *Entering Certificate* kwa ajili ya ule ujenzi wake. Mhe. Spika, leo inafikaje eneo linafutwa anapewa mtu mwengine na kama eneo linafutwa ina maana kile kibali cha *ZIPA* kinakuweko wapi.

Mhe. Spika, ninao ushahidi kuna wawekezaji ambao *document* ya *ZIPA* wanayo ndani ya ule muda wa utekelezaji wa sharti ya *ZIPA* wanayo, lakini eneo lile Wizara ya Ardhi imelifuta na inampa mtu mwengine, sasa hii ni migogoro ya makusudi kwa sababu sheria zipo na kwa nini tuzikiuke hizi sheria.

Kikao kilichopita Mhe. Spika, nililizungumzia suala moja la Muyuni Matemwe na mpaka leo sijapata jawabu, labda ndio lipo kwenye ile Kamati Teule ya Ardhi. Kwa kweli eneo lile limefutwa kwa yule mwekezaji wa mwanzo na anataka kupewa mwekezaji wa pili. Kwa kweli mimi nawashukuru sana *ZIPA* na wamegoma na kusema hili eneo mpaka hivi sasa sisi yule tuliyempa mwanzo kibali cha ujenzi bado hatujamfutia, sasa leo inakuwaje apewe mtu mwengine na mambo haya yanatutia aibu sana.

Vile vile kuna eneo jengine hivi karibuni tumeshapata taarifa kuna mwekezaji kama sikosei ni Mfaransa ameshapeleka taarifa mpaka kwao analalamika, kuhusu suala zima kwamba tayari ameshapewa eneo na ameshatafuta *funds* kwa ajili ya kujenga na leo hati yake inafutwa kinyume na utaratibu. Sasa jamani hizi sheria tunazozitunga hapa, ina maana sisi tukishatunga kazi yetu imemaliza na watu wakafanye wanavyotaka.

Mhe. Spika, nadhani tuanze kubadilika angalau twende na wakati, lakini suala hili ni aibu sana. Kwa mfano, ukiangalia hivi sasa katika ripoti kuna kipindi kimoja iliwahi kutoka haya mashirika ya Kimataifa walitoa ripoti wakaeleza katika eneo ambalo lina matatizo katika uwekezaji hasa kwenye maeneo ya ardhi ni Zanzibar, hali hii ni aibu sana.

Suala jengine kuhusu *ZIPA* kwenye masuala ya uwekezaji, bado hawawasaidii wananchi wetu *ZIPA* sijui kama kuna mwekezaji mmoja tulikwenda kule akasema au *ZIPA* kawaweka mkononi na wengine kawaweka mkononi ile Hoteli ya *Cristal*, yaani wote anasema amewaweka mkononi.

Lakini ukiangalia yale matendo anayoyafanya Mhe. Spika hakuna wasi wasi kwamba amewaweka mkononi, kwa sababu kile kibali walichopewa na *ZIPA* kwa ajili ya ujenzi wa hoteli yao, yaani uwekezaji wao amekiuka masharti yote na *ZIPA* wapo wanamtizama, kama hajawaweka mkononi amefanya nini. Mhe. Spika, hii ni aibu kwa taasisi yetu hii.

Mhe. Spika, kama nilivyosema mwekezaji yeyote anapowekeza kwa mujibu wa masharti ya *ZIPA* kabla ya kuanza ule mradi wake anatakiwa kama kulikuwa na suala la kulipa fidia kwa wananchi basi awe tayari ameshalipa fidia ndipo aanze mradi wake.

Kutokana na hali hii Mhe. Spika nasikitika tena na niliomba katika ripoti yangu ya Kamati naomba nizidi kukumbusha, kwamba Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ifuatilie wale wananchi wa Michamvi waliodhulumiwa fedha zao shilingi milioni 26. Mhe. Spika, fedha zile yule mwekezaji alikiri kweli ni haki ya wananchi akachukua eneo lake akakata miti yao na eneo lake hivi sasa anazalisha mali anaingiza wageni anapata fedha na wananchi wanadhalilika.

Kwa kweli wananchi wale wameshapanda na kushuka ndani ya ukumbi wako wa Baraza la Wawakilishi katika ofisi zako wameshakuja na tumeonana nao na kuzungumza nao, pia *ZIPA* tumezungumza nao na mpaka leo hakuna hatua yoyote inayochukuliwa. Sasa kama *ZIPA* wanashindwa kuwalipa wananchi, basi acha wazuie ile *certificate* yao na suala litakuwepo wapi, itakuwa limemalizika. Mhe. Spika, kwa kweli ni kitu ambacho kinatusikitisha sana.

Mhe. Spika, nikija katika suala zima la uhalifu katika uwekezaji. Sisi hivi sasa katika uchumi wetu tunategemea utalii, ndio sehemu ya mapato yetu katika nchi yetu ya Zanzibar. Lakini jambo

la kushangaza Mhe. Spika kesi za kupigwa mapanga wageni wetu zimekuwa nyingi, unyang'anyi umekuwa mwingi.

Kwa kweli Mhe. Spika kosa hili ni letu, kwa sababu uchumi wa nchi yetu unatakiwa ulinde mwenyewe, leo tuangalie kampuni za Ulinzi ni za kigeni, sasa kampuni za kigeni basi watashirikiana na watu watakuja watafanya uhalifu na baadaye wakimbie. Kwa hivyo, uchumi wetu bado hatujaulinda, naomba sana uhalifu katika ukanda wa maeneo ya utalii umekuwa mkubwa.

Tunashukuru serikali imeanzisha utaratibu wa Sera ya Utalii kwa Wote. Mhe. Spika, kazi hii naomba sana wananchi wahamasishwe, ili kuweza kujilinda wenyewe. Lakini je kama leo tutawahamasisha wananchi utalii kwa wote, lakini wanaolinda utalii ni wageni na wao wenyewe wanakuwa watazamaji watashiriki vipi katika utalii kwa wote.

Nadhani Mhe. Spika, tuangalie *priority* hasa kwa mahoteli mapya walazimishwe Makampuni ya Ulinzi ya Zanzibar yaweze kupeleka *Security Guard* katika maeneo haya.

Nikiendelea na mchango wangu sasa nakuja kwenye masula ya malipo ya *visa*. Mhe. Spika, kweli nakubaliana na ripoti ya Mwenyekiti wa Kamati na nimeisoma hapa, kwa kweli mapato yetu mengi yanapotea uwanja wa ndege.

Sasa utaratibu Mhe. Spika, nafikiri hivi sasa kuna ukarabati wa uwanja wa ndege, basi pangeliwekwa pale ofisi ndogo, yaani benki ndogo na sio benki ya wananchi kwenda kuweka fedha uwanja wa ndege sio hivyo, isipokuwa yale mapato ya *visa* yanapokuja pale yalipwe *through* benki, nadhani hapa ndio njia pekee ya kuweza kuzuia mapato yale. Lakini kwa utaratibu tunaokwenda nao hivi sasa kwa kweli mapato yataendelea kuvuja na tutaweza kukosa hayo matarajio tunayoyataka.

Vile vile kuna suala la misamaha ya kodi. Mhe. Spika, misamaha ya kodi hasa katika maeneo ya utalii, na mwaka jana nilizungumza hapa kwamba kuna punguzo lilijitokeza ambapo *ZRB* walikuwa wameshaliingiza katika bajeti yao, wawekezaji wale wa Hoteli ya *Resident*. Kwa kweli walipunguziwa fedha nyingi sana na mpaka leo bado hatujapata jawabu, kwamba fedha zile maana yake kwanza punguzo lenyewe halikuwa halali kwa sababu bajeti ilikuwa tayari imeshapita na katika malengo yalikuwa yameshakuwa tayari, hatukujua fedha zile ziliamuliwa zirejeshwe serikalini au vipi.

Kwa hiyo, Mhe. Spika, hii misamaha ya kodi katika ripoti kwa haraka wametembelea katika hoteli tatu, zote kuna ukwepaji maana yake huwezi kusema ni msamaha, kwa sababu msamaha ungelikuwemo kwenye sheria, lakini huu ni ukwepaji kwa makusudi, yaani ule muda wa msamaha umeshapita anaongezewa muda mwengine na yale ndio mapato yenyewe ya serikali.

Jambo jengine Mhe. Spika, kuna mwenzangu mmoja Mhe. Asaa Othman Hamad hapa alilizungumza suala la kodi katika mitandao ya simu. Mhe. Spika, wenzetu hivi sasa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nimemsikia Waziri wa Sayansi na Teknolojia, walizungumza kwamba hivi sasa kuna mapato mengi ya serikali yanapotea hasa katika kodi za *airtime* hii tunayopigiana simu na *message* na hapa kuna fedha nyingi zinakosekana.

Kutokana na hali hiyo, wenzetu Wizara ya Sayansi na Teknolojia ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanataka kuanzisha utaratibu wa kulipisha kodi hizi kama alivyosema mwenzangu kwamba lazima tujiandae na sisi kodi hizi tuzipate, kwa sababu suala la mawasiliano ni jambo la Muungano kwa hiyo lazima tuweze kupata lile gawio letu.

Mhe. Spika masuala haya kama hayakuingia katika ile sheria itakayopitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hapa kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge wetu wapo akina Mhe. Jaku Hashim Ayoub na Mhe. Asaa Othman Hamad basi waende wakatusemee hili kwamba kuna kodi ambayo inataka kuanzishwa kwa ajili ya *airtime* na fedha hizi ni nyingi sana. Kwa kweli katika nchi ambayo inatumia simu kwa wingi Afrika, basi Tanzania sijui kama si nchi ya pili. *(Makofi)*

Kwa hivyo, kuna fedha nyingi zitatengenezewa sheria ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, basi tunaomba katika sheria ile itakayopita gawio letu tuweze kulijua mapama, vyenginevyo tutakuja kuambiwa gawio hili sisi hatukufikia, kwa kuwa tumeshaanza kujua mapema, basi tunaomba suala hilo lizingatiwe.

Mhe. Spika, huku nimeangalia katika eneo la Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, wanasema wamo katika utafiti wa kuifanya Zanzibar kuwa eneo tengefu la biashara. Mhe. Spika, tumeshachelewa, kwa sababu unapoweka eneo tengefu *at least* iwe wewe unajitengezea mazingira, ili zile nchi zilizokuzunguka za jirani yako wao waweze kuja kupata *service* yako. Lakini hivi sasa katika Jumuia ya Afrika ya Mashariki Kenya na wao wanataka kutengeneza huu utaratibu wa *Special Economic Zone*.

Kwa hiyo, naomba sana Mhe. Spika, kwamba Zanzibar suala la kuifanya eneo tengefu la kibiashara, kwa kweli limeshazungumzwa muda mrefu nadhani tujitahidi sana angalau tuweze kukamilisha hayo masharti na kutokana na mazingira ya Zanzibar yalivyo, yaani hapa tumekuwa sawa sawa kama kwenye kopa sisi tuko kwenye mkia wa kopa, kwa kweli Afrika ya Mashariki yote tukinyanyua mikono yote tumeikata ni soko kubwa sana katika Jumuia yetu ya Afrika ya Mashariki. Sasa hili Mhe. Spika, naliomba sana.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, unazo dakika mbili.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, dakika mbili sawa. Sasa nataka kuzungumzia suala la kuhusu kodi bado nataka kusema Mhe. Spika, nafikiri watakaokwenda katika Bunge la Katiba, ndio sisi humu na ndio tutakaokwenda kupitisha maamuzi hasa katika masuala ya kodi. Suala la kodi Mhe. Spika kwa kuweka kodi moja kwa nchi mbili tofauti zenye uchumi mbili tofauti Mhe. Spika tunajidanganya.

Kwa kweli Mhe. Spika, ulitupa ruhusa na umetupeleka China na tumekwenda kujifunza, yaani wenzetu ndani ya China moja kuna kodi za aina tofauti, kwa mfano ukienda *Guangzhou* kuna kodi yake ukenda *Zhong bong* kuna kodi yake. Mhe. Spika, kila sehemu na wameweka vipi, yaani kila eneo wanaloweka eneo tengefu la kiuchumi wanapunguza kodi wanaweka masharti maalum, ili kuweza kufanya masuala ya uwekezaji. *(Makofi)*

Baada ya hayo Mhe. Spika, sasa namuomba Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba kwenye bajeti tumepitisha fungu la bilioni moja kwa ajili ya kuimalizia barabara ya *Mkapa Road* na leo Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano hakunielewa, kwa sababu amenijibu kwamba amepata fedha za Mfuko wa Barabara.

Kwa hivyo, mimi nasema fedha tulizozipitisha bilioni 1 kwa ajili ya kuimaliza barabara ya Amani (Mkapa *road*), fedha hizi mpaka leo Mhe. Waziri anasema hajapewa, na fedha alizozipata ni za Mfuko wa Barabara za *compensation* ndio wamejengea barabara.

Sasa naomba sana Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba amsaidie Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, ili tuje tumpitishie bajeti yake kwa vizuri muingizie fedha bilioni moja, ili aweze kukamilisha barabara ya Mkapa *road*. Mhe. Spika, barabara ile tulisaidiwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni aibu kuja Mhe. Rais Kikwete akaja akaikuta barabara mpaka leo imejaa matope bado hatujaimaliza.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache nakushukuru kwa kuweza kunistahamilia, pia namshukuru Mwenyekiti wa Kamati na naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tunaye mchangiaji mmoja Mhe. Abdalla Juma Abdalla. Sasa kesho tunayo shughuli moja kubwa ya Kamati ya *PAC*, ambayo kwa mujibu wa Kanuni chini ya ibara ya 108(15), ambayo labda ningeisoma, ili tukaona nini kinahitajika kwa ajili ya kukubaliana muongozo juu ya shughuli ya kesho ambayo itakuwa ni shughuli ndefu sana kuliko zote.

Kanuni ya Baraza la Wawakilishi ibara ya 108(15) kinaeleza hivi:-

> “Kila wizara itapaswa kuwasilisha mbele ya Baraza Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati za Kudumu za Baraza na ripoti za kamati hizo kuhusiana na Wizara husika mara moja kwa mwaka katika mkutano wa mwezi wa Machi. Mara hii kwa bahati nzuri tumeanza Aprili, isipokuwa ripoti ya utekelezaji ya maagizo ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika, itawasilishwa na Wizara inayohusika na Fedha.

Sasa kwa kawaida Ripoti ya *PAC* ina mambo mengi ni pamoja na masuala yanayohusu matumizi ya fedha kwa mujibu wa sheria na kanuni zake. Lakini pia kuna na matumizi yasiyofuata utaratibu wa bajeti iliyoidhinishwa na chombo hiki ambapo kila Wizara inaweza ikawa imetokea baadhi ya mambo ambayo kwa kweli Wizara ya Fedha inawezekana kabisa ikawa hawafahamu.

Kwa sababu tatizo la matumizi mabaya yanawezekana yakawa kwa wizara nyengine bila ya Waziri anayehusiana na masuala ya fedha kufahamu jambo hilo. Hii maana yake nini? Katika maeneo yale ambayo matumizi mabaya yamefanyika katika Wizara Fulani, Waziri wa Fedha yeye hataweza kutoa majibu. Sasa inabidi kila Wizara ambayo itakuwa imeguswa na ripoti ya *PAC* kwamba kuna jambo Fulani halikukamilika vizuri kama tulivyokuwa tunafanya huko

nyuma, basi Waziri wanayehusika atoe maelezo juu ya jambo lile ambalo ripoti hii imesema na yeye katika ripoti za nyuma kulikuwa na jambo gani nilielekezwa sasa alitoe.

Tatizo linakuja kwamba jambo hili halikuwahi kuelekezwa mapema na kama kuna maagizo hayo kila Wizara ikatengeneza kibango kitita chake cha utekelezaji ambayo maana yake vibango vitita hivi vitakuwa kwa mujibu wa Wizara, na kama kutakuwa kuna maagizo kwa kila Wizara kutokana na Kamati ya *PAC* itakuwa kwa idadi ya Wizara ziliopo. Sasa hili ni tatizo katika muda huu hatuwezi na si rahisi kutengeneza hivyo vijibango kitita zaidi ya bango kitita, yale mambo yanayohusu sera na taratibu za sheria ambazo Waziri wa Fedha atakuwa anazungumza kwa ujumla kuhusiana na Wizara mbali mbali juu ya masuala hayo.

Hivyo niwaombe kwanza Waheshimiwa Mawaziri kwamba kesho tujitahidi tuwepo sote ili pale ambapo ripoti ya Kamati inasomwa lakini pia kama kulikuwa na maelekezo kwenye ripoti iliyopita, basi tupate maelezo angalau hivi hivi tu bila ya kile kibango kitita mbali mbali ambavyo itakuwa ni vigumu kuvitengeneza kwa muda wa kuanzia sasa hivi hadi kutwa nzima ya kesho.

Hivyo nitoe muongozo kwamba Mawaziri mtaoguswa na ripoti na kama kulikuwa na maelekezo fulani yanahitaji majibu kujitayarisha angalau kutoa maelezo hayo kwa mdomo tu bila pengine kuwa na kitu cha kuwasilisha kwa mfano wa bango kitita kama hivi tulivyofanya. Ili tukamilishe shughuli hiyo kwa kesho ambayo itakuwa ni shughuli ndefu sana. Inawezekana kabisa pengine tukamaliza au tusimalize, lakini muda utakuwa ni mrefu mno kwa ajili ya Kamati ya *PAC*, kama tunavyoelewa *PAC* inagusa serikali nzima.

Basi nilitaka niseme hayo na kwa sababu ya maneno hayo umuhimu wa kumalizika shughuli hii pamoja na machofu tuliyonayo inaonekana ni lazima. Niwaombe basi Waheshimiwa Wajumbe baada ya kupitisha utaratibu kikawaida, ambapo nitamuomba Mhe. Waziri wa Nchi afanye kazi hiyo tukubaliane kazi hii tuimalize ambapo imani yangu ni kwamba Mawaziri wale wanaohusika kuja kutoa majumuisho pamoja na Mwenyekiti wa Kamati, hawatatumia muda mkubwa kwa hivyo ziada ya muda sitegemei kama itakuwa muda mkubwa sana. Na pia Mhe. Abdalla Juma naye hatatumia muda mkubwa kwa kuwa michango mingi imeshaguswa na hatapenda kurejea rejea kwa mujibu wa taratibu za kanuni.

KUONGEZWA MUDA WA BARAZA

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa shughuli iliyo mbele yetu bado haijamalizika, na kwa kuwa kuna umuhimu wa kuimaliza kutokana na ratiba yetu. Hivyo Mhe. Spika, naliomba Baraza lako liridhie kuweka kando kanuni ya muda ili tuwezeshe kumaliza shughuli iliyo mbele yetu leo hii na kesho tuweze kuanza na shughuli nyengine.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja hii ya kuongeza muda wa Baraza wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ambayo nilikusudia kusema maneno machache katika kuunga mkono ripoti ya Kamati hii ya Fedha, lakini kwa sababu muda umekimbia mno, na kwa sababu Mhe. Spika, yale niliyoyapanga kuyasema yote yamesemwa na Wajumbe wenzangu humu, tena wameyasema katika kile kiwango ambacho ningefikia mimi kukisema, kwa hivyo naomba niungane nao kwa yale waliyochangia akiwemo Mhe. Asaa katika masuala ya kuhifadhi misitu, Mhe. Hamza katika masuala ya kodi nadhani nikubaliane na michango yao Mhe. Spika, na nisiendelee kupoteza muda. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwanza kabisa na mimi nataka niwashukuru wale wote waliochangia pamoja nimshukuru vile vile Mwenyekiti kwa kutuwasilishia vizuri hotuba yake. Michango ilikuwa mingi nilikuwa najiuliza hii michango inaonekana kama michango ya kibajeti. Mhe. Spika, kama nitasema niijibu michango yote hii nadhani huo muda hautonitosha isipokuwa nataka niseme tu kwamba michango nimeipokea, nitaifanyia kazi na tutaweza kuja na majibu muafaka wakati wa bajeti. Lakini nataka niseme niyachangie yale ya msingi haraka haraka.

Kwanza nikianza na Mwenyekiti aligusia na suala zima la kuwahamisha Wahasibu Wakuu, nadhani katika Wizara zetu 16 na Taasisi zetu nathubutu kusema zaidi ya asilimia 50 ya Wahasibu Wakuu tumeshawahamisha, na hao ambao waliopo sasa hivi tayari programu zao za kuwahamisha tumeshaziandaa tunasubiri wamalize maandalizi ya bajeti. Lengo letu ni kuwazungusha ingawa sheria yetu na Mwanasheria yupo hapa inampa nguvu Mhasibu Mkuu kuwahamisha lakini haitangazi kwa kipindi gani. Hapa ndio yeye anaangalia baada ya miaka 2, baada ya miaka 3 nani wa kumhamisha, nani aendelee lakini tunafikiria kwamba ni vyema hasa tukaja na maamuzi thabiti angalau basi jinsi ya kuifanyia marekebisho ile sheria ya fedha.

Amezungumzia kwamba tuwaajiri Wahasibu wenye sifa hasa kwa kutilia maanani kwenda Pemba kuna haja hiyo na mimi nakubaliana na Mwenyekiti na Kamati, kwamba kuna haja hiyo bila ya kuwa na Mhasibu mwenye sifa hili litajitokeza kuwa tatizo hawataweza kufanya kazi kwa ufanisi. Nakubaliana na wewe hivyo na tutajaribu sana iwezekanavyo katika kipindi hiki tuweze kuangalia yale maeneo ambayo hayana Wahasibu wenye sifa ili tuweze kuwapelekea wahasibu wenye sifa na kuwaajiri wengine ambao wenye sifa.

Suala la urasimu Mhe. Spika, limezungumzwa sana na mimi nataka niseme tu kwamba Waheshimiwa Wawakilishi ni wajibu wenu kuzungumzia urasimu. Urasimu hautusaidii katika maendeleo hautusaidii kabisa, tutaliangalia hili suala na pale ambapo pana urasimu bila ya sababu nitawaomba sana ndugu zangu wa *ZIPA* hasa *ZIPA* ndio waliozungumziwa. Lakini urasimu mwengine *time* nyengine inatokakana kwamba kuna matatizo ya ardhi inabidi wachukue muda ku-*solve* lile tatizo la ardhi, *time* nyengine mradi wenyewe ambao uliopendekezwa

haujafikiwa viwango inabidi kuwe na urasimu wa kwenda rudi kwa muwekezaji, lakini kama urasimu ambao si wa lazima basi nitawashauri wenzangu sana wa *ZIPA* wasiwe na urasimu kwa sababu tunapoteza mapato ya serikali na mapato ya nchi.

Ulinzi katika maeneo ya Utalii, nataka nithubutu kusema kwamba tayari serikali imelipokea kwa nguvu zote na tayari serikali Mhe. Rais amefanya mkutano na Wawekezaji katika maeneo ya utalii pamoja na serikali, nilikuweko mimi, Mhe. Dr. Mwinyihaji alikuwepo, Mhe. Waziri wa Habari katika kikao hicho tayari serikali inaunda kikosi maalum kwa ajili ya ulinzi katika maeneo yetu ya Utalii. Ni kweli nakubaliana na Waheshimiwa Wawakilishi kwamba tukiterereka katika eneo hili, uchumi wetu na mapato yetu yanaweza kuterereka, kwa hivyo ni dhahir kwamba lazima tuyalinde maeneo haya ili *concern* yenu Waheshimiwa Wawakilishi nadhani na serikali nayo inakubaliana na nyinyi na hili ni *urgent* kwa ajili ya maelekezo ya Mhe. Rais ametuelekeza *very urgent* hili suala tuweze kulikamilisha na tuko katika hatua nzuri sasa hivi la kuweza kulikamilisha.

Mhe. Mwenyekiti amezungumzia dhana ya *one stop centre*, tuna tatizo kwamba wale tuliowapeleka pale ZIPA baadhi yao hawana *decision* na mimi baada ya kuona kwamba kuna baadhi ya maeneo *ZIPA* yanahitajia *decision making* hata bodi yangu niliyoiunda sasa hivi iko tofauti kidogo. Nimempeleka Katibu Mkuu wa Ardhi kama Mjumbe wa Bodi kwa sababu nilijua hakuna *decision* ya ardhi, kwa hivyo huyu akiwemo mle ndani ataweza kutusaidia. Nimeelewa kwamba kuna matatizo kwenye Tawala za Mikoa nikampeleka Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Tawala za Mikoa kama ni Mjumbe wa bodi amalize hayo matatizo badala ya kuzunguka. Kwa hivyo hizi *decision* za *one stop centre* ni kwamba wale watendaji tuliowapeleka pale wengine hawana *decision* ni watendaji wadogo sana. Nadhani sasa hivi tufikirie kuibadilisha kidogo wawe wajumbe wake ni wale wenye *decision* zaidi.

Suala jengine ambalo Mwenyekiti amelizungumzia ni suala la makisio katika kutafuta kodi. Mimi nadhani kuna haja Mhe. Mwenyekiti, hivi unavyozungumza na wanavyozungumza leo wataalamu nadhani mnapishana pahala. Mimi nitaandaa kikao cha pamoja baina yako Mwenyekiti na mimi nitakuwepo na wataalamu wetu wa kodi tulizungumzie tulifahamu sote hasa nadharia unayoizungumzia ni ipi ili tuweze kufikia muafaka, na hili jambo kama unavyosema mwenyewe unataka liwe historia kama wenzetu wanavyofanya basi liwe historia.

Kwa wenzetu ukienda Singapore pale, Singapore ukienda pale huonani na mtoza kodi kila kitu kipo *computerized* ni *electronic* wewe unazungumza na mashine unatia *bills* zako mle ndani twende kodi inatoka unafanyiwa *assessment* basi unalipa kodi tena unalipa benki halafu kule unapeleka risiti yako tu tena ni *electronic* unatia ile namba ya risiti basi umemaliza. Mimi nadhani Mhe. Mwenyekiti kwa hili nimeli-*note* tutakutana na wewe ili tupate hasa nini tunachokizungumza hapa tuweze kufahamu kwa pamoja.

Mapato yanayotokana na hoteli bado hayakusanywi vizuri na mimi nataka nikubaliane na wewe kwamba bado kunahitajia juhudi kubwa sana, lakini nataka niwapongeze ndugu zangu wa *ZRB*, niwapongeze ndugu zangu wa *ZRB* ambao wao ndio wenye dhamana ya kukusanya mapato ya hoteli. Tulipoingia hapa *ZRB* mwaka 2010 ilikuwa inakusanya karibu bilioni nane, bilioni saba kwa mwezi lakini sasa hivi nataka niwapongeze sana wanakusanya karibu bilioni 12, 13 kwa

mwezi, wanaongeza *effort*. Na Kama nilivyosema kwamba *once* wakishakubadilisha madaraja yale wakishakuyaweka ya mahoteli zile *rate* zinawekwa kwa mujibu wa daraja lako la hoteli.

Kwa hivyo itakuwa hakuna kukimbizana. Hili nadhani tutalifanyia kazi kama ilivyosemwa kwamba tulifanyie kazi kwa haraka zaidi na tutalisimamia liweze kukamilika kwa haraka zaidi tukishirikiana na Kamisheni ya Utalii. Suala la kuingia wageni kwa Makundi Mhe. Mwenyekiti wageni wataingia tu, wataingia kwa makundi wataingia mmoja mmoja ndio wageni. La msingi kuangalia mapato yetu yatakavyoweza kuyapata kwa ufanisi na kwa ukamilifu. Tutalifanyia kazi hili na ninakuahidi kwamba lengo letu hasa ni kupata mapato yetu ni haki yetu.

Suala jengine Mhe. Mwenyekiti umelizungumzia ni suala la kufanya uchunguzi wa kina juu ya leseni za uvuvi kushuka, tutashirikiana na watu wa uvuvi, tutashirikiana na watu wenzetu wa *ZRB* tutakaa pamoja, tutaangalia sababu za msingi jinsi zilizopelekea kushuka, *is it* zimeshuka kwa sababu meli kule zimepungua? Maana yake mapato haya ni ya leseni za meli zinazovua katika Bahari Kuu. Au zimeshuka tu kwa sababu tu kuna mambo mengine meli ziko idadi ile ile, tutajaribu kuyaangalia hayo na nadhani *from time to time* tutakuwa tunatoa taarifa kwenye Baraza lako tukufu Mhe. Spika.

Visa nimeeleza hii *revenue* sasa hivi tunavyotaka kuifanya tokea mtalii anaingia anaonekana anakwenda wapi anachangia kiasi gani kwenye *visa* hii ndio itakayotuokoa na tuko katika hatua nzuri sasa tunajaribu kukamilisha *feasibility study*, na wakati wowote tunaweza tukaanza kuitafutia pesa ili iweze kutuokoa katika mapato ya *visa*. *Visa* tusimlaumu mtalii, mtalii hawezi kuingia bila ya kulipa *visa I doubt it, visa* ni sisi wenyewe mapato yetu. Ni sisi wenyewe ndugu zetu, kaka zetu, dada zetu, mama zetu, wajomba zetu ni sisi wenyewe ambao *part* ya sehemu labda inaondoka tu sitaki ni- *accuse* mtu, lakini *under any circumstances* mtalii hawezi kuingia ndani ya nchi yako akakwepa *visa* ya dola 100 au dola 50. Kwa hivyo hili nalo tutaliangalia ili kila mmoja aweze kuchangia na mapato yale ya *visa* yaweze kupatikana.

Mhe. Spika, alizungumzia suala la kugongewa *visa*, ni kweli sasa hivi hakuna utaratibu ule wa kugonga kwa muhuri, pale ndio mapotevu yanapotokea kwa wingi sana, *visa* zote sasa hivi ni *stamp*. Unajua ume-*issue visa* ngapi unaziona kwa mujibu wa *serial number*. Lakini unapopiga muhuri tu, pale yatapotea tu lazima tukubali yatapotea tu. Kwa hivyo hili ni suala la kisera Mhe. Spika, na huko nyuma tulikuwa tunafanya sijui nani aliyeli-*stop* ikaja mambo ya mihuri mihuri. Kwa hivyo hili nalo tutakaa na wenzetu wa uhamiaji tupate hasa nini kinachoficha katika eneo hili. Umetaka vile vile Mhe. Mwenyekiti kwamba tulipatie muarubaini, mimi nasema si muarubaini peke yake mimi nasema tutalipatia muarubaini, muhamsini lakini hili limalizike kabisa.

Suala la ardhi umelizungumzia sana linapoteza mapato yetu na umetutaka tubadilishe sheria, mimi nadhani chombo hiki ndio chenye mamlaka ya kubadilisha sheria kimesikia hichi chombo dhamana apewe Waziri wa Fedha badala ya kupewa Waziri wa Ardhi. Ni kweli duniani kote katika masuala mbali mbali masuala ya fedha anakabidhiwa Waziri wa Fedha. Hili sijui Baraza hili limepitishaje likaenda kwa Waziri wa Ardhi, mmeona matatizo yake, inawezekana Waziri siye mwenye matatizo lakini jamii yenyewe ndio yenye matatizo.

Kwa hivyo kama mlivyoeleza kwamba tulifanyie marekebisho Mwanasheria Mkuu yupo anaweza akaleta *miscellaneous* katika kikao cha bajeti kana ni *urgent* akarekebisha baadhi ya hizi sheria ndogo ndogo ili tukenda samba samba. Kama muwekezaji amefikia umri wa kuanzisha shughuli zake basi anapaswa kulipa kodi ya ardhi sasa hakuna suala la kusema kwamba hapa anakuwa tena *grace period* hapa ndio penye utata, tutalifanyia kazi ili tuweze kuibadilisha hiyo sheria twende sambamba na matakwa ya Kamati.

Mhe. Spika, eneo jengine ambalo Mhe. Mwenyekiti ametaka mashirika yachangie katika Mfuko Mkuu wa Serikali hicho ndio kilio changu na mimi ninalia siku zote sisemi mashirika yote kwa sababu mashirika mengine sasa hivi yapo *ICU*. Tunajaribu kuyafanyia mapitio kama yataweza ku-*survive* ushindani yataendelea, kama hayawezi ku-*survive* bora yakafungwa kuliko kupoteza fedha za serikali. Kuna mashirika sasa hivi ni aibu mashirika kama hayo hayawezi kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Ni aibu lakini tumeanza sasa hiyo People's Bank of Zanzibar ameshaanza kutoa gawio kwa serikali, Bima nayo sasa hivi itatoa gawio kwa serikali, tunalitizama Shirika la Bandari na Shirika la Umeme. Lakini hata kama hatuwezi kutoa gawio kwa serikali, ripoti imesema humu Mhe. Spika, basi hata kodi za serikali wanapewa *exemption* kwa miradi mikubwa mikubwa mimi nakubali. Lakini anaingiza gari mtu anaomba *exemption* ya gari milioni mbili anashindwa kulipa milioni mbili tunayalea vibaya. Mimi nitasema siku zote mashirika haya tutayalea vibaya. Lakini tukiyaambia yafanye kazi yalipe na kodi ndio watafanya kazi. Kwa hivyo Mhe. Spika, hili tumelichukua na tutalifanyia kazi.

Jengine umeipongeza sana *ZSSF* na mimi nachukua pongezi zako kuzipeleka kwao kwa ujenzi wa uwanja wa watoto wa Uhuru Kariakoo. Ni matarajio yetu kwamba uwanja huu utamalizika haraka iwezekanavyo na utakuwa ni uwanja wetu mzuri wa kisasa kabisa ili watoto wetu nao wapate maeneo ya kuchezea. Umewataka vile vile watafute maeneo ya ziada ya kuweza kuwekeza, mmetushauri tuonane na Mhe. Hamza tutaonana nae Mhe. Hamza. Tutaonana na wengine na wengine kama wapo vile vile ili watupatie hizo anuani na *e-mails* za hao wawekezaji na tutazungumza nao ili tuje tuone kama ni kiasi gani wanaweza kusaidiana na sisi katika kusaidiana na *ZSSF* katika kuwekeza katika miradi mbali mbali mikubwa.

Vile vile umesema kwamba kuna baadhi ya mashirika na Taasisi haziwalipii michango waajiri wao, hilo ni kosa. Mimi nasema *ZSSF* wana sheria, kama wataona kama kuna Taasisi ya binafsi au ya serikali haiwalipii waajiri wao na yeye akanyamaza kimya bila ya kuwachukulia hatua, mimi nadhani Mkurugenzi Muendeshaji ndio anatakiwa kuchukuliwa hatua basi. Kwa sababu sheria unayo na hawa unaowaona wewe hawachangii basi ni kuwachukulia hatua kwa mujibu wa sheria na taratibu zipo. Mimi nadhani nitamkumbusha Mkurugenzi Muendeshaji wa Mfuko wa Jamii ili aweze kulisimamia hili na wale ambao hawalipi michango aweze kuwachukulia hatua kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Mahmoud ametutaka tu kwamba suala hili la tofauti ya ushuru kati ya Tanzania Bara na Zanzibar tuliharakishe. Na mimi kwa kweli ninaliharakisha sana kwa sababu ilikuwa mwezi huu tukutane na Dr. Mgimwa ili ile Kamati itupatie taarifa wamefikia wapi na tufanye maamuzi. Lakini kwa bahati mwenzangu anasoma bajeti kwa hivyo akawa yupo kwenye bajeti. Kwa hivyo

nadhani baada ya muda mfupi nitamuomba tena muda wake ili tuweze kukutana kupata ile taarifa.

Suala la *TRA* tutaliharakisha vile vile, wakati Fulani niliomwita Mkuu yule wa Mamlaka ya *TRA* kwa bahati nzuri na yeye alikuwepo safari ili tuje tulizungumze hili suala kwa sababu na sisi tunataka likamilike vile vile kwa manufaa na faida ya wananchi wetu.

Mhe. Ismail Jussa ameuliza masuali mengi Mhe. Spika, lakini mengine hasa ni ya kibajeti si ya Kamati lakini nitasaidia bado. Mhe. Jussa mimi ninavutika na Kamati yetu ya Fedha na Uchumi ilikwenda na kuzungumza na Idara hii Dar es Salaam na wakaleta taarifa yao nzuri tu, mimi nitaomba sana ile taarifa ya hii Kamati kuhusu Idara hii Mhe. Jussa apatiwe, asome na yeye ataridhika. Kama sisi wenyewe hatuitumii ile Idara sio sababu ya kwamba ile Idara isiwepo, lakini kwa kweli Idara ina majukumu mazuri, makubwa na wanayafanya. Nitaomba sana Mhe. Dr. Salmin ile ripoti mliyonileta mimi mpatieni na Mhe. Jussa.

Mhe. Jussa suala la *consultative meeting* tumelizungumza na sio kwamba hatukuchukua hatua, tumechukua hatua sana Mhe. Jussa. Tumeshatayarisha sasa hivi nini tunataka kuyazungumzia tuna *document* kama hivi hatukuwa tumelala tuko tunaifanyia kazi. Unajua huwezi ukaenda kuzungumza na *donor community* halafu unaanza kujiramba midomo aa maana yake. Huna kitu *tangible* cha kuweza kuwapa donors ndio tumekifanyia kazi hicho kitu ili tuje tuwape *donor community*. Na sasa hivi tumepata *blessing* nzuri tu kwamba wenzetu wanataka kuitisha mpaka Jumuiya ya *Arab leagues* waje hapa tuzungumze na wao vile vile katika kutusaidia. Kwa hivyo mimi nakuomba sana ingawa ume-*quote* Oktoba imepita, Oktoba nyengine imepita usishughulike mambo mazuri hayataki haraka Mhe. Jussa.

Suala la kukuza uchumi na kupunguza umaskini, Mhe. Jussa ukuaji wa uchumi ukitaka kuutazama hasa *theoretical part* yake ni kubwa sana. Unaweza uchumi ukakua katika *national level* lakini katika *individual level* wasiweze kuona kwa haraka. Lakini ile *effect* yake inakwenda taratibu kama maradhi ya *cancer*. Inakwenda taratibu mpakamwisho ikafikia pahala utakuta na hawa sasa wanaweza kuiona. Na umekizungumza kitu kizuri sana *I am stand to be corrected* Mhe. Spika.

Tumetengeneza dira hapa mwaka 1995 dira ile tumeitengeneza miaka 20 mpaka 2020 *implementation* imeanza 2000, leo tuku mwaka 2012 *impact* ya dira hatuwezi kuiona hatuwezi kuiona katika miaka 10 ya mwanzo. Kwa sababu *political* tulianza kuvutana wenyewe kwa wenyewe badala ya kujenga uchumi tukaanza kuhasimiana Wazanzibari tukapoteza muda wote wa miaka 7 mizima hakuna kitu kilichokuwa kinakwenda Zanzibar na huu ndio ukweli. Sitaki nimlaumu *CUF* sitaki nimlaumu CCM. Nasema sisi wenyewe Wazanzibari tumefikia hatua hiyo. Kwa hivyo miaka ile 7 tumeipoteza kuvutanavutana usitoe hiki usiwape hawa basi.

Sasa serikali yetu ya Umoja wa Kitaifa, mshikamano wetu Wazanzibari mimi niko *very positive* uchumi wetu utakua na wananchi wetu wataanza kuona matunda kukua kwa uchumi. Kwa sababu kila mmoja sasa hivi ana *concentrate* katika kujituma na kujenga uchumi, pale kila mmoja alikuwa ana-*concentrate* kumhujumu mwenziwe tu. *CUF* amhujumu CCM, CCM amhujumu *CUF* ndio lengo lililokuwepo hatukutaka kujituma tumepoteza muda tu sasa hivi tusirudi huko Mhe. Jussa. Na mimi naamini kwamba ajira zitapatikana, wananchi wataona

mapato, tufungue sekta hizi mpya, sekta ya uvuvi tumesema sasa hivi tunaiwekea na uwezashaji, tukizifungua basi. Tutakuja kuchangia zaidi wakati wa bajeti.

Wasiwasi wa mikopo kwa Exim China, mimi nataka nikwambie Mhe. Jussa hizi *Exim* ziko nyingi. Kuna *Exim* China, kuna *Exim* US, kuna Exim India, kuna *Exim* Tanzania. Na wala isikupe wasiwasi mkopo unatoka kwenye *Exim* wasiwasi msimamizi. Mimi nasema siku zote wasiwasi usimamizi, hawa wenzetu wanatupatia *concessional loan* ni mkopo nafuu ambao riba yake hauzidi asilimia 2 huwezi ukaupata mkopo huo. Lakini tunapopewa mikopo je tunasimamia? Hatusimamii ndio mambo yetu yanakwenda yanaharibika tunakuja hapa lakini mimi nasema kwamba wazo la pili ambalo ulilozungumza kwamba twende kwenye *PPP* mimi *I am supporting you*. *PPP* ni *option* nyengine ambayo ni *quick option* katika maendeleo. Tutafanya hivyo tutajitahidi twende hivyo.

Umezungumzia nilete sheria ya Mkaguzi Mkuu wa ndani *Internal Auditor General*, nadhani Mhe. Mwanasheria Mkuu *by professional* si Mwanasheria. Mhe. Mwanasheria Mkuu amelisikia hili tumeanza lakini kuliangalia na nadhani tutakutana Ofisi ya Mwanasheria Mkuu tuwape *extent* tunaweza tukai-*fast track* hii sheria na tukaja nayo hapa kwa faida yetu sote.

Mapato yetu kutoka vyanzo vya Muungano hili nimelisikia. Lakini nataka nimwambie tu Mhe. Jussa kwamba tunavyokwenda tunakwenda katika *right pace*, mkikamata kila pato mnaanza kupiga piga kwa pamoja hamfiki mbali, kamata moja, kamua, piga lifanikiwe twende jengine. *Payee* tushafanikiwa sasa tunakwenda mengine, tutakwenda tu, yatakwisha tu haya.

Kwa sababu ninachokiona mimi wenzetu hawa hawataki nguvu za hoja wanataka majadiliano sio maguvu, tukae tujadiliane tutengeneze *point* zetu za ku-*reason out*, basi tunakwenda nao vizuri. Tume-*reason out* hoja yetu tumekwenda vizuri *payee* sasa inakuja 1.75 kila mwezi *something is better than nothing*. Tume ya pamoja tumefikia wapi, kwa kweli kwetu sisi tumekamilisha SMZ, tunasubiri wenzetu *cabinet* yao ikae wapitishe yale mashauri yaliyotolewa na Tume ya Pamoja tuanze kazi. Na mimi sina mamlaka ya kwenda kui-*push cabinet* ya Muungano ikae ipitishe ile *paper*. Sina mamlaka hayo, mamlaka yangu yako hapa tu.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk ameondoka lakini ndio namalizia. Magendo ya mafuta kwa kweli tumefanya kazi nzuri sana yamepungua, kwa sababu wanakuja watu wanalia ofisini kwangu dola laki moja za mafuta kazifanyia magendo mafuta yake yamechukuliwa kwa mujibu wa sheria ya *ZRB*, mafuta yale yanauzwa na sehemu ya pesa ile tunasaidia vikosi vyetu ili kufanya kazi vizuri zaidi, yamepungua magendo ya mafuta.

Mimi marafiki zangu wenyewe wamekuja wanalia mafuta yao yamekamatwa, nikawaambia kwa hilo hakuna sumile kabisa. Kwa hivyo, magendo ya mafuta yamepungua na kama tunavyosema tutajitahidi yaondoke kabisa kwa sababu sio biashara nzuri.

Tuwe na miradi michache, mimi nakubaliana na yeye kwamba tuwe na miradi michache na hilo ndilo lengo letu ili hiyo michache tuweze kuikamilisha. Mradi wa uzalishaji umeme kutumia takataka huu mradi uko mbali sana Mhe. Spika. Mradi huu unatumia takataka zetu tulizonazo Zanzibar nzima kwa siku ni kama tani mia sita na kitu, tani mia sita na kitu zinazalisha baina ya 5 *to* 10 MW *only*. Tatizo ni moja, walipokuja na *power purchase agreement* bei yao ilikuwa ni

kubwa kuliko wanayonunua *ZECO* kutoka *TANESCO* ya sasa, sasa ukisema huu mradi ukae kwa bei hiyo maana yake unawauwa wananchi wako.

Kwa hivyo, tukasema *no, the power purchase agreement* lazima bei iwe chini ya *TANESCO* kwa sababu *TANESCO* ameongeza *services* ambazo yeye hazifanyii, hizi *services* zinafanyhiwa na *ZECO*. Kwa hivyo hilo ndilo tulilowaambia nadhani wataendelea tena wakishindwa kufikiana na *ZECO* tunayo *negotiating teams*, *The National Negotiating Team* ambayo inaongozwa nadhani na Mwanasheria Mkuu, tutawapeleka huko wakakae waka-*negotiate*, lakini hatuwezi kuleta miradi kama hii ambayo hatimae inakuja kuwauwa wananchi.

Pia anasema bado hatuko *serious* katika kukusanya mapato yanayotokana na utalii. Namwambia tuko *serious* na akitaka aangalie jinsi zile *vote* za makusanyo zinavyoongezeka.

Mhe. Asaa Othman Hamad *payee* nimeshazungumzia, suala la mapato ya utalii nimeshazungumzia, daraja nishazungumzia, kodi nimeshazungumzia serikali ianze kujenga miundombinu. Hilo ndio nia yetu katika maeneo huru nishalizungumzia.

Mhe. Hamza Hassan urasimu nimeuzungumzia, uhalifu nimezungumzia, mapato ya *Visa* nimezungumzia, misamaha ya kodi ya ardhi nimeshazungumzia, kodi za mitandao ya simu. Hili Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano amelisikia ataanza negosiation katika *sector level* na waziri mwenzake. Itakapofika katika sekta ya fedha mimi na Dr. William Mgimwa (Waziri wa Fedha Tanzania) kazi yetu ni kumaliza tu basi, wataanza wao kuzungumza utaratibu mzima wa kuweza kutoza kodi katika eneo hili.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo namalizia kwa kuwashukuruni sana Waheshimiwa Wawakilishi kwa kunisikiliza ahsanteni sana.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kuna jambo moja dogo, kuna fedha tuliyoipitisha shilingi bilioni moja kwa barabara ya Amani ya Mkapa. Sasa ile anamkwamisha shughuli zake Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano. Hebu atupe kidogo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, labda niseme tu taratibu ili Waheshimiwa Wajumbe waweze kufahamu. Tunapotoa fedha za mishahara kinachofuatia ni fedha za pencheni, tukimaliza kutoa pencheni kinachofuatia *development*. Sisi Hazina Mhe. Spika, hatuwapangii sekta wazipeleke wapi, sekta wanaleta wao kwamba jamani sisi tunahitaji mfano shilingi bilioni mbili, kwa mujibu wa keki iliyopo tunasema nyinyi tutakupeni shilingi bilioni moja si jukumu la Waziri wa Fedha wala Katibu Mkuu Fedha kukwambia peleka wapi, peleka wapi, unapanga mwenyewe.

Sasa hili ni jukumu la Waziri wa Miundombinu atakapopata pesa za *development* mwezi huu wa April afikirie kupeleka barabara ya Amani – Mtoni si jukumu langu mimi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (Kny. Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Spika, kwanza nikushukuru wewe pia nichukue nafasi hii kuwashukuru Wajumbe kwa maelezo na michango mizuri ili kutuwezesha kuendelea kufanya shughuli zile

ambazo zimepangwa kwa manufa ya watu wetu. Mhe. Spika, na ushauri wako wa kutumia muda mfupi sana nitaupa kipaumbele.

Mhe. Spika, ni kweli kabisa Waheshimiwa walizungumzia suala la kilimo kwamba ndio tegemeo la wananchi wa Zanzibar. Na mimi nakubaliana nao mia kwa mia na hiyo ndio dhana ya serikali, tunaelewa kwamba kilimo ni tegemeo kubwa kwa wananchi wetu na ndio maana tunafanya kila jitihada ya kuhakikisha tunaleta mabadiliko makubwa katika suala la kilimo. Na tunaelewa kwamba kilimo ni mbegu bora, kilimo ni pembejeo, kilimo ni utafiti, kilimo nmi taaluma kwa maana ya kuwafunza wakulima wetu na kilimo ni maji na mambo yote hayo yamepewa kipaumbele. Yote haya Mhe. Spika, tungependa tuyafanye vizuri zaidi kuliko tunavyoyafanya, lakini kama tulivyosema inategemea sana na uwezo wetu wa ndani ya kifedha. Kadiri tutakavyoweza kufanikiwa katika kuimarisha mapato yetu ndivyo tutakavyoimarisha kutoa huduma zetu.

Hivi sasa kwa kiasi kikubwa huduma hizi za mbolea, pembejeo na madawa, serikali kwa karibu asilimia 75 inajaribu kutoa ruzuku kwa wananchi wake kwa msingi wa kuimarisha kilicho chetu kiende vizuri. Kwa hivyo, yale mengi ambayo Waheshimiwa walisema wamekusudia kutushauri na sisi tuseme kwamba ushauri tunaupokea na kwenda kuufanyia kazi kama ambavyo maelekezo yametoka.

Kuhusu kukipa kipaummbele kilimo cha umwagiliaji. Mhe. Spika, hiyo ndio dhamira ya serikali, hivi sasa tunafanya jitihada ya kukarabati miundombinu na vile vile kujenga miundombinu mwengine mipya. Hivi sasa tumepata ufadhili kutoka *Exim Bank* ya Korea watatusaidia kwenye kilimo cha umwagiliaji katika hekta kama 2,100 na vile vile kwenye *Federal Future* ya USA watatusaidia kama hekta 1,200 lakini na GASP *Fund* nao watatusaidia kama hekta 1,200. Kwa hivyo, ukitizama kwa hatua fulani kwenye eneo hili tunaanza kupiga hatua nzuri hasa ukilinganisha na yale mahitaji yote ya kilimo cha umwagiliaji maji hapa Zanzibar. Hivyo jitihada zinachukuliwa na tunaendelea kupokea ushauri na kufanya kazi kwa karibu.

Suala la kuendeleza *Farmer Field Schools* hilo halina mjadala nia ni hiyo na tunaenelea nazo kwa nia ile ile ya kuelimisha wananchi wetu. Kuhusu suala la uongezaji thamani wa bidhaa zetu hilo limepewa kipaumbele na wizara na serikali kwa jumla kwa msingi wa ufahamu kwamba, kwa kadri tutakavyoweza kuzisarifu bidhaa zetu na kuzifanya ziwe bidhaa kamilifu kwanza zinaongeza kipato lakini vile vile zinapunguza lile tatizo kubwa la uharibifu au upoteaji wa bidhaa kwenye utaratibu mzima wa kilimo. Kwa hivyo, suala zima la kuongeza thamani ya bidhaa limepewa kipaumbele na linafanyiwa kazi.

Kuhusu kuimarisha huduma za matrekta na ziwe kwa wakati. Hivi sasa kama nilivyosema asubuhi leo kwamba, wana mradi wa kufanyia matengenezo zile trekta za zamani, lakini pia serikali imeweka kipaumbele kunua trekta nyengine mpya na vifaa vyengine vya kilimo. Kwa hivyo, masuala haya yanapewa kipaumbele na nataka nihakikishe kwamba tutafanya kila jitihada suala la matrekta na pembejeo muhimu zitatolewa kwa wakati, kadiri ya uwezo wa serikali utakavyowezekana. Lakini nia ni kwenda na wakati ili wananchi wetu waweze kuitumia kwa mujibu wa msimu na iweze kutoa tija kwao.

Kuhusu suala la kuongezwa bajeti ya Wizara ya Kilimo. Ushauri tunaupokea lakini kama maelezo yalivyotoka na Waziri wa Nchi hapa ameeleza kuwa suala ni kwamba nia na madhumuni makubwa ya serikali ni kuhakikisha kila sekta inapata yale mahitaji yake kwa ukamilifu, lakini kutokana na ukubwa wa keki yenyewe ya kipato ndio hicho unachokipata. Lakini bado tutaendelea kuzungumza ndani ya serikali ili tuzidi kuendelea kutoa kipaumbele kwa bajeti ya kilimo ili iweze kukidhi mahitaji zaidi.

Mhe. Spika, kuhusu uhifadhi wa chakula nia ya serikali tokea mwanzo imekusudia na ina mpango huu wa kuweka uhifadhi wa chakula. Hivi sasa tulikuwa tumo katika kufanya utafiti ili kuona mradi wenyewe uwe endelevu na uwe unakidhi ile haja ya malengo yaliyokusudiwa.

Kuhusu mradi wa kusarifu mazao ya kilimo ni kwamba ndugu zetu wa Korea walianza kusaidia lakini nataka niwahakikishie kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itachukua hatua ya kuhakikisha kwamba inakamilisha mradi ule ili hatua nyengine zifuate za kutoa huduma kwa wananchi wetu.

Uhifadhi wa misitu hilo siku zote linapewa kipaumbele na hivi sasa kutokana na sera yetu ile basi taratibu za kanuni na sheria zitaboreshwa ili ihakikishwe kwamba hatua kali zinachukuliwa kwa wale waharibifu wa mazingira hasa kwa upande wa ukataji miti, uchimbaji mchanga, ujenzi wa kiholela na vile vile kwenye suala zima la kulinda vianzio vya maji. Kwa hivyo, taratibu zetu hizi tutahakikisha kwamba sheria zinakwenda kwa wakati wa sasa ili ikipigwa faini basi iweze kumuwezesha mtu ajue siku ya pili asirudie makosa kama haya, na hata ikiwa ni kifungo basi sasa sheria yetu itatizama kwa mujibu wa hali ya wakati ulivyo kuhakikisha kwamba mambo haya yanaheshimiwa na yanapewa kipaumbele kwa sababu naamini kabisa kulindwa kwa mazingira ndio kulinda kwa uhai wa leo na kesho.

Mhe. Spika, kuhusu kwenda kwenye kilimo cha kisasa na chenye tija hilo ndio lengo letu na ushauri tumeupokea. Kuimarisha huduma za kilimo vijijini ndio lengo la serikali kwa hivyo ushauri tunaupokea. Kurekebisha kasoro zinazojitokeza katika wizara ili kuweza kutoa huduma bora kwa manufaa ya wananchi wetu ushauri tunaupokea na tunaufanyia kazi.

Kuhusu kutoa elimu kwa wananchi hasa juu ya umuhimu wa kutumia gesi na majiko sanifu. Jambo hili Mhe. Spika, ni jambo zuri kwa sababu tunapotumia gesi maana yake tunapunguza kwa kiasi kikubwa kutumia nishati ya miti ambayo kwa njia moja au nyengine tunapunguza ukataji miti. Kwa hivyo, jambo hili limepewa kipaumbele na kuna mradi huu ambao unashughulikiwa au unasaidiwa na ndugu zetu wa Norway kupitia Shirika la *Care International* kwa masuala mazima ya kuwezesha watu kuweza kutumia matumizi ya gesi. Nia na lengo ilikuwa ni kuwezesha kaya 7,000, hivi sasa tayari jitihada zimechukuliwa na kaya 2,300 zimeshapatiwa uwezeshaji huo na kadiri ya uwezo utavyojitokeza basi hali hiyo itaendelezwa ili kuhakikisha kwamba matumizi ya gesi yanafanikiwa zaidi katika nchi yetu ili kupunguza ukataji wa miti.

Vile vile Mhe. Spika, limejitokeza suala la Kiwanda cha Mahonda jambo hilo liko ZIPA linafanyiwa kazi. Kuna kamati maalum ya Baraza la Mapinduzi ambayo inalifanyia kazi jambo hili. Kwa hivyo, mimi sina shaka yoyote majibu mazuri kuhusu Kiwanda cha Mahonda yatakuja na kwa maslahi ya wananchi wetu na nchi kwa jumla. Hivyo naomba Waheshimiwa wazidi

kuvuta subira wakati jambo hili linashughulikiwa kwa kina chake na ni hivi karibuni tu majibu yatapatikana.

Mwisho nimalizie kwa hili Mhe. Jussa ambalo alilizungumza sana kuhusu Kaimu na kukaimu na kadhalika. Mhe. Spika, ni utaratibu wa serikali pale ambapo waziri mmoja hayupo basi serikali ina utaratibu wa shughuli zake ziendelee huteuliwa waziri mwengine kukaimu hiyo wizara. Ni utaratibu wa kawaida katika serikali. na kwa utaratibu wetu wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa sasa tumeweka utaratibu anapoondoka waziri anayetokana na *CUF* basi upande wa *CUF* huwa anamkaimu mwenzake na ni vile vile kwa upande wa CCM hilo. Sasa ikiwa jambo hilo haliridhishi wananchi basi tutazidi kuliangalia, lakini tumeliweka vile kwa msingi ambao upo sasa wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Mara nyingi mawaziri hutakiwa wawepo wakati wa shughuli muhimu hizi za kibaraza, lakini yanapotokea majukumu mengine ambayo huwa hayazuiliki Mhe. Spika, ndio hufanyika vile.

Mhe. Spika, la mwisho niseme hili la kutetea maslahi ya Zanzibar, tusiwe na sura ya kufikiri kwamba ni serikali peke yake ndio inayo wajibu huo, hili ni jambo la Wazanzibari wote, kila Mzanzibari anayepata nafasi ya kutetea maslahi ya Zanzibar anafanya hivyo. Sasa kuna baadhi ya Waheshimiwa ambao ni Wabunge hapa, wanatuwakilisha ambao ni Wawakilishi wamo katika Bunge la Jamhuri ya Muungano Mhe. Spika, nafikiri wana *forum* nzuri, yanapotokea mambo muhimu ya kutetea maslahi ya Zanzibar pale wayaeleze na waseme. Kwa sababu wanaposema hapa peke yake na mimi huwa siwasikii kuyasema haya wanayoyasema humu ndani. Kwa hivyo, hiyo ni *challenge* yetu kwa pamnoja, maslahi ya Zanzibar yatetewe na kila Mzanzibari kadiri ya nafasi aliyonayo mahali alipo.

Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe tusiendelee sana kulaumiana ni wajibu wetu sote na kila mmoja afanye wajibu wake kwa mujibu wa taratibu na nafasi aliyonayo pale alipo.

Mhe. Spika, baada ya hayo nakushukuru nawashukuru Wajumbe wote. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Afya (Kny. Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko): Mhe. Spika, nashukuru na mimi umenipa nafasi nifanye majumuisho madogo kwa sababu kwa mujibu wa waliochangia nadhani tumetajwa sehemu moja tu au mbili. Lakini wote waliochangia tunawashukuru na kukushukuru wewe pamoja na Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ametuagiza mambo fulani ambayo yote tutayachukua, tutayafanyia kazi kama vile inavyostahiki.

Lakini Mhe. Spika, kabla ya kuanza kuna jambo moja hapa naona kama tumelisahau hatulisemi na ni tukio muhimu. Mchana tulipewa taarifa ya kufariki kwa Msanii wetu ambaye ni mmoja katika aliyetujengea sifa sana Zanzibar. Wengine walikuwa hawaijui hata Zanzibar ni nini wameweza kujua kutokana na mchango wa marehemu Bi Kidude. Naomba kwa ruhusa yako tumpe pole Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa msiba uliomfika pamoja na Wazanzibari wote.

Mhe. Spika, kulikuwa na kama mambo mawili matatu niliyotaka kusema, mengine kama nilivyosema tutayashughulikia sina haja ya kuchukua mud asana. Moja kulitajwa suala la

viwanda. Mhe. Makame Mshimba alisema kwamba, aa, wale hawaturuhusu bwana kuanzisha viwanda vikubwa, sijui wale nani. Sisi ni serikali hata kiwe kiwanda kikubwa kama mbuyu, ikishakuwa ni *feasible* na kitatuletea faida ruhusa ya kufanya tunayo kama serikali na kama Wizara ya Biashara. Isipokuwa suala la msingi ni kwamba, zamani kulikotengwa maeneo ya viwanda lakini mpaka sasa yameshageuka miji, inabidi sasa liteuliwe eneo jengine jipya la kufanya hivyo viwanda.

Kwa sababu kwa kawaida viwanda hutakiwa vijitenge na mawasiliano yameshafanyika na Wizara ya Ardhi ili waweze kututengea eneo kwa ajili ya viwanda tukajimwage huko. Viwanda kuwa mjini na chini ya majumba si vizuri, tunaona makero ya magereji yanavyowapa watu matatizo.

Katika kujiandaa hatua tuliofikia sio mbaya, tumeeleza tulipokuwa tunajibu bangokitita kwamba hatua mbili tayari, *action plan* imeshafanywa, ripoti ya ushindani tayari imebakia kutayarishwa sera kwa mujibu wa hali ya wakati na mikakati. Na hivyo navyo viko katika hatua ya utekelezaji vitakapokuwa tayari aidha vitaelezwa kwenye bajeti ya wizara yetu au kwenye maelezo yatakayotakiwa. Hilo ndio moja katika lililotajwa kwetu.

La pili lililotajwa ni suala la eneo la *trade fair* kule Fumba na kwamba Mhe. Hamza Hassan alisema kuwa tumechelewa kidogo, mana faida tuliyonayo ni kubwa kwa hivyo tunahitaji haraka.

Kwa taarifa ya Baraza la Wawakilishi ni kwamba hatua zote zinazohusu utafiti tayari, ile ripoti ya utafiti imeshafikishwa kwa wadau na ndio desturi ya siku hizi unachokifanya lazima na wenzako wakisikie. Kilichobaki ni kuifikisha ripoti ile serikalini yaani kwenye *cabinet* ili kupewa muongozo na kupata idhini ya serikali kwa sababu jambo lenyewe ni kubwa. Bila shaka eneo lililokuwepo zamani lakini kwa kweli ilikuwa linahitaji kufanyiwa kitu kilichokuwa na utaalamu. Lakini bado tunahimizwa tatizo na hili liko pande zote mbili, lazima kuwe na hakika ya umeme, Mwenyezi Mungu amejaalia hatutegemei tena kwamba umeme utakatikakatika ingawa hata leo asubuhi ulikatika hapa ni mambo ya kawaida.

Sasa tunategemea umeme utakuwa ni wa uhakika, tuliohimizwa ni barabara zinazokwenda huko kwenye eneo lazima ziwe nzuri, lakini siu barabara tu, tunapotaka tuwe na *International Trade Fair* lazima tuwe na bandari iliyo nzuri inayoweza kupokea na kutoa mali za wale ambao tunataka wawe na nini na suala la mawasiliano. Suala la mawasiliano ya simu nadhani sio baya sana linaruhusu hivyo. Lakini tumehimizwa basi wekezeni hivyo, yaani *Infrastructure* ili tupate hilo suala litimize linavyotakiwa.

Suala la tatu ambalo nililotaka ku-*comment* Mheshimiwa ni kumshukuru Mwenyekiti kwa kuona umuhimu wa *ZBS* nakwamba alisema walikwenda kwenye eneo hawakuridhika vile lilivyo. Ni kweli eneo ni dogo tunahitaji eneo lile liwe kubwa, lakini la msingi ambalo kaliona ni kwamba hakuna bajeti, bajeti ni finyu na ametia msisitizo kwamba mara hii bajeti inayokuja na naomba atakapokuja kuchangia Wizara ya Biashara alisisitize kwamba tupewe bajeti ili tukamilishe ile kazi ya *Zanzibar Bureau of Standard*. Lakini kwa taarifa ya Baraza hili Mkurugenzi tayari ameshateuliwa na hivi sasa kuna kitu tunaita *induction course* yaani anafanya *orientation*

kutembelea zile *tbs* za Muungano na nchi nyengine kujifunza ajitayarishe kwa masuala ya baadae.

Mhe. Spika, kitu cha mwisho ambacho nisingependa kukisema sana limezungumzwa suala la eneo tengefu. Mimi sina hakika kwamba *vocabulary* hii ya tengefu inajulikana na kila mtu, labda kina Maalim Haroun watusaidie. Nadhani ndio hizi *economic zone*. Eneo tengefu ni mtambuka inahusu wizara nyingi sana si suala ambalo liko katika wizara moja, linaihusu Wizara ya Fedha, Wizara ya Biashara, Wizara ya Ardhi na bado tunashirikiana katika kufanya kazi hiyo kwa pamoja. Si kazi ndogo kwa sababu tunataka Zanzibar yote iwe eneo tengefu. Kuna masuala ya kiuchumi, ya kisiasa, ya kiulinzi na mambo mengine.

Lakini ni kweli Mhe. Hamza kwamba faida tuliyonayo Zanzibar hata kama na wale wenzetu watakuwa wametutangulia faida ya Zanzibar kuwa eneo tengefu wale wataalamu wa uchumi wanasema ni *strategic* kama ni mlango wa kuingilia kwenye Bara zima la Afrika na *accessibility* yetu sisi ni *the best* kuliko mote. Kwa hivyo, kunaweza kukawa kuna maeneo tengefu Mombasa, kukawa na maeneo tengefu Tanzania Bara, lakini kama tutakitayarisha kisiwa chetu basi ni rahisi zaidi kuweza kufika huko tunakokwenda na kuna mahali nakumbuka wakati ule tuko serikali ilikuwa badala ya sisi kwenda kuchukua bidhaa upande wa pili ilikuwa mpaka Zambia, Congo, wapi wanakuja hapa kwa sababu ya urahisi wa kupafika na urahisi wa mambo yetu, Mwenyezi Mungu atusaidie tufike huko.

Mhe. Spika, sikutaka kuchukua muda zaidi tunawashukuru wote, tunayachukua mapendekezo yale, tutayafanyia kazi na wakati ukifika tutarudi kueleza pale tulipofikia.

Mhe. Spika, nashukuru sana.

Mhe. Salmin Awadh Salmin (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ndogo sana nikaweza kufanya majumuisho ya mwisho juu ya ripoti mbali mbali za wizara pamoja na michango ambayo imeweza kutolewa.

Mhe. Spika, kwanza nitumie nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri pamoja na watendaji wao; mawaziri wa wizara tatu kwa kuweza kutekeleza asilimia kubwa maagizo ya kamati katika ripoti yetu iliyopita. Kwa kweli Mhe. Spika, wizara zote tatu zimeweza kutekeleza vizuri maagizo yaliyoweza kutolewa na ufafanuzi juu ya maagizo hayo yameeleweka vizuri.

Tunawashukuru sana na tunawapongeza.
Mhe. Spika, ripoti hii imebahatika kuchangiwa na Waheshimwa Wajumbe kama sita hivi na kwa bahati nzuri nadhani ni vyema kwa kuwa sio wengi, basi ni vyema tukawatambua kwa majina.

Wachangiaji walikuwa ni hawa wafuatao:-

1. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa

2. Mhe. Ismail Jussa Ladhu

3. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk

4. Mhe. Asaa Othman Hamad

5. Mhe. Hamza Hassan Juma

6. Mhe. Abdalla Juma Abdalla

Mhe. Spika, tunawapongeza walioweza kupata nafasi ya kuchangia hotuba ya zetu. Naamini kama muda ungekuwepo basi karibu wajumbe wangeweza kuchangia, na hii inatokana hasa na umuhimu wa wizara hizi; Wizara ya Fedha, Wizara ya Biashara, Wizara ya Kilimo, zote ni wizara za uchumi. Kwa hivyo ni wizara ambazo zinasimamia zaidi masuala ya uchumi na ni mihimili mikubwa ya uchumi wa nchi yetu.

Mhe. Spika, wajumbe wengi wameipongeza kamati yetu juu ya ripoti yake na mimi kwa niaba ya kamati tunazipokea pongezi hizo na tunawashukuru sana.
Lakini pia kwa niaba ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo nitumie nafasi hii kwanza kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri kwa ufafanuzi mzuri walioutoa juu ya hoja mbali ambali ambazo zimewasilishwa na Waheshimiwa Wajumbe. Kwa kweli Mhe. Spika, usingetemea kwa haraka haraka ile kwamba Waheshimiwa Mawaziri wangeweza kujibu hoja za Waheshimiwa Wajumbe vizuri na kwa uhakika. Kwa hivyo tunawapongeza kwa ujasiri wao wa kuweza kufanya shughuli hiyo kwa haraka haraka, na mimi ninaamini Waheshimiwa Wajumbe wengi wameridhika juu ya ufafanuzi wa hoja mbali mbali ambazo zimetolewa.

Lakini Mhe. Spika, mimi nitazungumzia kidogo na kutoa ufafanuzi juu ya mambo kama sita hivi kwa haraka haraka.

Kuhusu suala la kukaimu mawaziri ambalo hoja hii imewasilishwa na Mhe. Jussa na ikatolewa na Mhe. Waziri anayekaimu kilimo. Mhe. Spika, jambo hili pamoja na kwamba ni la kawaida na serikali imekuwa ikilitumia katika utekelezaji wa shughuli zake za kila siku. Lakini moja kati ya watu wasiofurahishwa na suala hili la kukaimu hasa wakati kama huu wa session za Baraza na mambo muhimu ambayo yanazungumzwa hapa ni mimi. (*Makofi*).

Mara nyingi huwa sisiti kulisema hili pengine hata kuna watu haliwafurahishi lakini na mimi huwa sifurahishwi. Kwa kuwa na mimi halinifurahishi na mimi nina wajibu wa kulisema, maana kusema ndio kazi yangu.

Mhe. Spika, kukaimu ni kukaimu. Kukaimu ni tofauti ya mwenyewe kuwepo na kwa sababu wewe ndio mwenye dhamana ya kushughulikia wizara ile, tofauti na kusikia kwa mtu mwengine. Kwa hivyo tunapenda sana Mhe. Spika, Waheshimiwa Mawaziri wetu wawe au waone umuhimu wa kuwepo katika vikao kama hivi. (*Makofi*).

Mhe. Spika, mimi ninampongeza sana Mhe. Waziri wa Fedha. Mhe. Waziri wa Fedha alikuwa na safari huyu ya Marekani, safari ya zaidi ya siku kumi lakini amethubutu kuahirisha safari yake na akawapeleka wenziwe kwa sababu ya kuona umuhimu wa jambo hili.

Sasa nadhani Waheshimiwa Mawaziri pale ambapo hakuna ulazima wa kwenda nje wakati kama huu wa vikao basi ni vyema na wao wakafuata mfano kama huo wa Mhe. Waziri wa Fedha ili wenyewe wawepo, waweze kutoa ufafanuzi wa mambo mbali mbali wenyewe. Na wenyewe kama kuna maagizo basi wapokee wenyewe. Hilo ni jambo zuri. (*Makofi*).

Mhe. Spika, kuhusu vianzio vya mapato vya visa. Jambo hili Mhe. Spika, tumekuwa tukilizungumza sana na tunalilisitiza sana. Vianzio vya mapato ya visa hasa katika maeneo ya viwanja vya ndege. Mimi nimuombe sana Mhe. Waziri wa Fedha, fedha ile pamoja na kwamba inakusanywa na wenzetu wa Idara ya Uhamiaji lakini asilimia 50 ya fedha ile ni mapato ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Na inasaidia katika kuimarisha mapato na ni kianzio kizuri sana. Kuna kila aina ya ushahidi unaonesha kwamba fedha pale inapotea na kwa utaratibu unaotumika. Kwa hivyo jambo hili linahitaji kufanyiwa kazi kwa nguvu zote na kuhakikisha kwamba mapato ya visa yanayolipwa kwenye viwanja vya ndege yanapatikana kwa manufaa ya wananchi wa Zanzibar. (*Makofi*).

Sisi tumetoa mpaka ushauri wa kufungua tawi la Benki pale ya Zanzibar ili watalii wanapokuja pale basi waweze kwenda pale na kulipa benki na wanachukua ile *slip* wanayopewa pale wanaipeleka kwa ajili ya kwenda kugongewa visa.

Utaratibu ninaona hauna matatizo na upo ndani ya uwezo wetu. Pamoja na kwamba Mamlaka ya Viwanja vya Ndege wanasema hawana nafasi pale ya kujenga benki. Juzi kamati yangu ilipokwenda wanasema maana yake hatuna nafasi, maana yake tutasababisha msongamano. Sisi hatusemi kwamba benki ile ihudumie watu wote kama benki ya kawaida. Benki ile ni maalum kwa ajili ya wageni wanaokwenda kulipa visa pale.

Sasa sijui huo msongamano huo utatokea wapi. Leo pale pana maduka hayana maana yoyote; maduka ya vipodozi, matiki. Hivi leo tukose nafasi pale japo ndogo ya kuwaweka wenzetu wa Benki ya Watu Zanzibar na wageni kuweza kwenda kulipa pale.

Ninadhani Mhe.Waziri hilo ulichukulie umuhimu sana ili limalizike tuweze kuzungumza vyengine. Na huo utaratibu ambao nimeueleza basi tutaendelea nao lakini kwa *first stage* basi basi tufanye hivyo na kwa vile mapato mengi ya serikali yanavuja pale.

Jengine Mhe. Spika, ni kuhusu urasimu katika uwekezaji. Hili nalo Mhe. Waziri unatakiwa ulichukulie hatua za haraka haraka. Kuna urasimu mkubwa katika maeneo ya uwekezaji. Kuna wawekezaji wengi wanakuja hapa kutaka kuekeza, lakini kutokana na urasimu tuliokuwa nao wanashindwa kuekeza.

Juzi Mhe. Spika, wakati wa *session* hii ya vikao tulipata kidogo kupenya na kamati yangu kwenda katika maeneo ya Michamvi, kwenda kuangalia eneo la mradi ambao ulikuwa umeshaanza kulipa. Taarifa tulizokuwa nazo kutoka *ZRBA*, umeshaanza kulipa kodi, wameshapewa *grace period*, wameshaanza ku-*operate* lakini baadae wamepewa tena period ili waendelee kupata msamaha.

Lakini matokeo yake Mhe.Spika, tulipofika pale tulikuta hakuna hoteli, hakuna chochote lakini mwekezaji yupo. Tumekwenda na suala jengine lakini tumekuta jengine. Anasema kwamba mimi sijapata kibali, sasa zaidi ya miaka mitano sijapata kibali, watu wa Idara ya Mazingira kila siku kesho, keshokutwa mradi umeombewa zaidi ya miaka mitano haujaweza kupata kibali kutoka katika Idara inayohusika na *ZIPA*. *ZIPA* wanasema hawawezi kumpa kibali mpaka tupate ripoti ya mazingira.

Ni mradi wa hoteli, ni mradi wa dola milioni 15 ambapo mwekezaji amekuja na fedha zake kwa ajili ya kuekeza hapa. Sasa tuufikirie ni namna gani ambapo mradi ule kama ungekuwa umeshamalizika, ungeweza kusaidia mapato katika nchi hii, kutoa ajira kwa watu wetu.

Miradi ya aina hii Mhe. Spika, ipo mingi, huo ni mmoja kwa bahati mbaya tumemgundua lakini miradi hii ipo mingi ambayo haisaidiwi, watu wana fedha zao wanataka kuekeza matokeo yake wanashindwa. Sasa hili eneo Mhe. Waziri wa Fedha unayeshughulikia masuala ya uwekezaji ni eneo muhimu, kwa sababu masuala ya uwekezaji yatatusaidia katika kuinua uchumi wetu na kuweza kufanya shughuli zetu za maendeleo.

Mhe. Spika, kuhusu Mamlaka ya Mapato kukusanya kodi kwa makisio. Hili nalo ni eneo ambalo tunalizungumza. Tunapozungumzia kodi kwa makisio tunakusudia kwamba hakuna ule utaratibu wa kileo wa kukusanya mapato ya realistic ile yaani ya ukweli, ambapo mtu anakisia. Mfanyabiashara anafanya biashara yake kwa mwezi, akifika mwisho wa mwezi anataka kupeleka *return ZRB* anajiuliza nikalipe kiasi gani, mwezi huu nilipe kiasi gani.

Sasa anachoamua kulipa maana yake ndicho anachokwenda kulipa katika Mamlaka ya Mapato. Hiyo ni ukusanyaji wa mapato kwa njia ya makisio. Lakini makisio yanayokwenda na wakati ni yale yanayolipwa kwa njia ya *electronic machine*, unakwenda katika taasisi inayohusika unalipa unapewa risiti *return*, wewe unakwenda zako katika taasisi ya kukusanya mapato unakuta hesabu yako tayari ipo kwamba unatakiwa ulipe hiki kutokana na *return* ambayo umefanya hivi.

Sasa hii ni kodi ya uhakika ambayo tayari wenzetu wa Jamhuri ya Kenya wanaitumia. Mhe. Waziri nadhani tayari umeshafika na umeshaona. Huwezi kupata huduma yoyote bila ya kupewa risiti na ndio maana leo Kenya wamepiga hatua kubwa sana za kiuchumi katika nchi za Afrika ya Mashariki na hii ni kutokana na *seriousness* yao waliyo nayo ya ukusanyaji wa mapato. Kwa hivyo hili nalo ni jambo muhimu linahitaji kuangaliwa kwa umakini.

Jengine Mhe. Spika, kuhusu utalii kwa utaratibu wa *package tour*. Mhe. Spika, utalii huu ni utalii ambao tumeuzoea. Lakini ni utalii ambao unapoteza fedha nyingi za wananchi. Watalii wanaochukua *package tour* wanalipa fedha zao zote nje ya nchi. Kwa maana hiyo serikali inaweza ikakosa pesa nyingi kutokana na watalii hawa. Utafiti unaonesha hivyo. Kwa hivyo utalii wa *package tour* kwa kweli unahitaji kuangaliwa kwa umakini, unatupotezea pesa nyingi. Hivi karibuni tumezungumza na wataalamu wanaohusiana na mambo ya utalii na wameeleza juu ya jambo hili, kwamba hamuwezi kuendelea katika hali hii ya utalii wa aina hii. Kwa hivyo hili nalo linahitaji kuangaliwa na kupatiwa maamuzi juu ya maamuzi ya jambo hili.

La mwisho Mhe. Spika, ni hili ambalo Mhe. Waziri wa Biashara amelizungumza kuhusu eneo la Zanzibar kulifanya kuwa ni eneo la tengefu. Amesema kwamba lugha hii ya eneo tengefu pengine ina tafsiri nyingi na kwa ufafanuzi wake Mhe. Waziri inaonekana ni kweli neno hili ni geni kwake. Lakini hili tumelipata kutoka wizarani kwake kwenye Wizara ya Biashara. Lengo la kuifanya Zanzibar kuwa eneo tengefu, maana yake kwamba eneo lote la Zanzibar linakuwa ni eneo huru la uchumi, badala ya kuchagua vipande vipande kama ilivyo sasa kwamba tumechagua Fumba, Micheweni na Amani katika viwanda vidogo vidogo.

Sasa kuifanya Zanzibar kuwa ni eneo tengefu, maana yake ni Zanzibar nzima. Wenzetu hawa Wizara ya Biashara tayari wameshafanya *research* wameshamtafuta *consultant* amekuja amefanya uchunguzi na akatoa hoja zake nyingi, katoa changamoto nyingi sana. Lakini kama ripoti yangu ilivyosema kama changamoto ambazo amezieleza kama kweli tutakuwa tupo tayari basi suala la kuifanya Zanzibar kuwa ni eneo tengefu ni suala zuri na linaweza likatutoa katika hapa tulipo hapa likatuweka katika *position* nzuri zaidi kuliko hii tuliyo.

Lakini kwa kweli lina changamoto nyingi. Sisi kama Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo tumeelezewa juu ya suala hili na tumeona, na tumeona changamoto ziliopo lakini tumeona pia na faida yake itakayopatikana hapo baadae.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, nikushukuru sana, niwashukuru wote wajumbe wote wa Baraza hili kwa mashirikiano yote waliyotupa na kuwezesha kuwasilisha ripoti hii na hatimaye kumaliza kwa salama na amani.
Mhe. Spika, naomba kuwashukuru.(*Makofi*).

Mhe. Spika: Mhe. Mwenyekiti tunakushukuru na sasa kazi iliyobaki basi ni kupokea taarifa hizi. Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubali na kupokea ripoti za utekelezaji pamoja na ripoti mpya ya kamati wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Saa 2.50 usiku Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 18/04/2013 saa 3.00 subuhi)